



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA  
MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI  
  
KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA  
UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2017

**SERIKALI KUU**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA  
MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA  
UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2017

SERIKALI KUU





JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 16 Barabara ya Samora Machel, S.L.P. 9080, 11101 Dar es Salaam.

Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527, Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz), tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)

Unapojuibu tafadhali taja:

Kumb. Na.FA.27/249/01/2016/2017

31 Machi 2018

Mh. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
S.L.P. 9120, Ikulu,  
Barabara ya Baraka Obama,  
**11400 DAR ES SALAAM.**

Barua

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA  
MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI JUU YA TAARIFA  
ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE  
30 JUNI, 2017**

Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) inanipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha za Serikali na kuripoti kwa Bunge. Kulinganga na mamlaka hayo, ninayo heshima kubwa kuwasilisha kwako ripoti yangu ya Ukaguzi wa Serikali kuu kwa mwaka wa fedha 2016/17 kwa ajili ya hatua zaidi.

Wako mwaminifu;

Prof. Mussa Juma Assad  
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## YALIYOMO

YALIYOMO.....	I
ORODHA YA VIAMBATISHO.....	III
ORODHA YA MAJEDWALI .....	V
ORODHA YA VIELELEZO .....	IX
MAMLAKA YA OFISI.....	XI
DIBAJI.....	XIII
SHUKRANI.....	XV
MUHTASARI .....	XVI
SURA YA KWANZA.....	1
<b>1.0      MAELEZO YA AWALI.....</b>	<b>1</b>
SURA YA PILI.....	10
<b>2.0      HATI ZA UKAGUZI.....</b>	<b>10</b>
SURA YA TATU.....	16
<b>3.0      UFUAMILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI NA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA HESABU ZA SERIKALI KWA MIAKA ILIYOPITA .....</b>	<b>16</b>
SURA YA NNE .....	27
<b>4.0      USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA .....</b>	<b>27</b>
SURA YA TANO .....	50
<b>5.0      HESABU JUMUIFU ZA TAIFA .....</b>	<b>50</b>
SURA YA SITA .....	111
<b>6.0      TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA .....</b>	<b>111</b>
SURA YA SABA.....	124
<b>7.0      USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA .....</b>	<b>124</b>
SURA YA NANE .....	138

<b>8.0</b>	<b>UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE .....</b>	<b>138</b>
	SURA YA TISA .....	178
<b>9.0</b>	<b>MANUNUZI NA USIMAMIZI WA MIKATABA .....</b>	<b>178</b>
	SURA YA KUMI .....	199
<b>10.0</b>	<b>USIMAMIZI WA MATUMIZI .....</b>	<b>199</b>
	SURA YA KUMI NA MOJA.....	223
<b>11.0</b>	<b>USIMAMIZI WA MALI NA MADENI .....</b>	<b>223</b>
	SURA YA KUMI NA MBILI.....	237
<b>12.0</b>	<b>KAGUZI MAALUM NA UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA.....</b>	<b>237</b>
	SURA YA KUMI NA TATU .....	270
<b>13.0</b>	<b>HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>270</b>
	VIAMBATISHO .....	283

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 2.1: Orodha ya taasisi na aina ya hati zilizotolewa .....	283
Kiambatisho Na. 2.2: Taasisi zenye hati yenye shaka na msingi wa hati hiyo .....	291
Kiambatisho Na. 2.3: Sababu zilizosababisha Taasisi kupata Hati Isiyoridhisha .....	296
Kiambatisho Na. 2.4: Taasisi na Mambo yaliyopelekea Kupata Hati mbaya .....	299
Kiambatisho Na. 3.1: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita katika Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa CAG.....	302
Kiambatisho Na. 4.1: Fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa.....	351
Kiambatisho Na. 4.2: fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo zikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa .....	353
Kiambatisho Na. 5.1:.....	355
Kiambatisho Na. 5.2: Hesabu zilizojumuishwa kwenye hesabu jumuifu bila kusainiwa/kutolewa na mamlaka husika .....	362
<b>Kiambatisho Na. 5.3: Mchanganuo wa makusanyo yaliyofanya na TRA kwa niaba ya taasisi zingine Julai 2016-Juni 2017 (Tarakimu ni katika mamilioni ya shilingi za kitanzania).....</b>	<b>363</b>
Kiambatisho Na. 6.1:Taasisi zenye upungufu kwenye ukaguzi wa ndani ..	364
Kiambatisho Na. 6.2:Taasisi Zenye Mapungufu Kwenye Kamati ya Ukaguzi .....	365
Kiambatisho Na. 6.3: Taasisi Zenye Mapungufu Kwenye Usimamizi wa Vihatarishi .....	368
Kiambatisho Na. 6.4:Taasisi Zenye Mapungufu Kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) .....	370
Kiambatisho Na. 6.5: Sheria mbalimbali zinazohusiana na kuzuia mali ..	375
Kiambatisho Na. 7.1:.....	378
Kiambatisho Na. 7.2: Taasisi zenye upungufu wa watumishi .....	379
Kiambatisho Na. 8.1: Mlinganisho wa uwezo wa Makusanyo ya ndani kufanikisha bajeti matumizi ya kawaida na maendeleo ya wakala wa serikali .....	383
Kiambatisho Na. 8.2: Mchanganua wa Makasio yaliyopitishwa na kiasi cha fedha kilichotolewa .....	384
Kiambatisho Na. 8.3: Mchanganuo wa Makusanyo Halisi na Makisio ya Mapato ya Ndani.....	385
Kiambatisho Na. 8.4: Orodha Ya Taasisi Za Serikali Zenye Madeni Shilingi 1,312,983,248,513.....	386
Kiambatisho Na. 8.5: Orodha ya Taasisi za serikali zenye madai Shilingi 657,992,846,515 .....	389

Kiambatisho Na. 8.6: Mapungufu katika ukaguzi wa Matumizi .....	390
Kiambatisho Na. 9.1: Manunuzi Yaliyofanyika bila Ushindanishi .....	393
Kiambatisho Na. 9.2: Manunuzi ya Bidhaa, Huduma na Ujenzi bila ya Mikataba .....	395
Kiambatisho Na. 9.3: (a) Mapungufu Yaliyobainika katika Usimamizi wa Mikataba na Miradi .....	397
Kiambatisho Na. 9.4: Mapokezi ya vifaa visivyofanyika Uguzi .....	406
Kiambatisho Na. 9.5: Vifaa na huduma zilizolipiwa hazikupokelewa .....	408
Kiambatisho Na. 9.6: Miradi ya ujenzi iliyochelewa kukamilika .....	409
Kiambatisho Na. 9.7: Manunuzi kwa kutumia Masurufu/Fedha Taslimu..	413
Kiambatisho Na. 9.8: Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikingizwa katika vitabu .....	414
Kiambatisho Na. 9.9 (a): Hoja Zitokanazo na Uhakiki wa Mali za Serikali, Mapungufu katika Manunuzi na Utunzaji wa Bohari/Stoo kwa Mwaka wa Fedha Unaoshia 30 June, 2017.....	416
Kiambatisho Na. 9.10: Ripoti ya Mhakiki Mali wa Serikali Iliyo Wasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 .....	419
Kiambatisho Na. 10.1: Fedha Kutumika kwa Shughuli Zisizokusudiwa Shilingi 6,810,775,133 .....	424
Kiambatisho Na. 10.2: Taasisi Zilizofanya Malipo yenyé Hati za Malipo Yenyé Nyaraka Pungufu.....	426
Kiambatisho Na. 10.3: Malipo Yaliyofanyika bila Kudai Risiti za Kielektroniki (EFD) -Shilingi 1,551,184,131 .....	427
Kiambatisho Na. 10.4: Taasisi za Umma zisizotoza kodi ya Zuio-Shilingi 109,163,824. ....	428
Kiambatisho Na. 10.5: Fedha zilizokopwa ndani ya Taasisi bila kurejeshwa-shilingi 2,113,764,574.....	428
Kiambatisho Na. 11.1: Orodha ya taasisi za Serikali ambazo zina madeni .....	430

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Maoni ya Ugazusi .....	xvi
Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa taasisi za Serikali Kuu zilizokaguliwa .....	2
Jedwali Na. 3: Kaguzi maalum zilizoombwa katika mwaka husika .....	3
Jedwali Na. 4: Uchambuzi wa maoni ya ugazusi yaliyotolewa kwa mwaka 2016/17 .....	14
Jedwali Na. 5: Maana ya maneno yaliyotumika kutathmini hali ya utekelezaji .....	17
Jedwali Na. 6: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa kila Mkaguliwa .....	18
Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo kuanzia 2013/14 hadi 2015/16 .....	19
Jedwali Na. 8: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ugazusi wa CAG wa miaka iliyopita .....	20
Jedwali Na. 9: Muhtasari wa Utekelezaji wa maagizo ya PAC kwa miaka iliyopita juu ya Ripoti kuu ya CAG ya Mwaka .....	22
Jedwali Na. 10: Muhtasari wa utekelezaji wa maagizo ya PAC wa miaka ya nyuma .....	24
Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa kwa mwaka 2014/15 na 2015/16.....	25
Jedwali Na. 12: Mchanganuo wa Bajeti ya Makusanyo .....	28
Jedwali Na. 13: Bajeti na Matumizi Halisi kwa miaka miwili .....	30
Jedwali Na. 14: Makisio ya Mapato na Matumizi yaliyoidhinishwa .....	33
Jedwali Na. 15: Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana kutoka vyanzo visivyo vya kodi na asilimia ya ufanisi wake kwa miaka miwili ( <i>Kiasi katika Shilingi bilioni</i> ) .....	42
Jedwali Na. 16: Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa miaka minne ( <i>Kiasi katika Shilingi bilioni</i> ) .....	42
Jedwali Na. 17: Balozi zilizokusanya Maduhuli pasipokuyarejesha kwenye Mfuko Mkuu.....	47
Jedwali Na. 18: Mitambo ya kuchenjua madini bila kuwa na leseni .....	49
Jedwali Na. 19: Muda wa kuiva dhamana za serikali.....	54
Jedwali Na. 20: Madeni ya serikali kwenye mifuko ya pensheni.....	65
Jedwali Na. 21: Muhtasari wa dhamana zilizokiukwa masharti mnamo Juni 2017 .....	66
Jedwali Na. 22: Mafaili ya wastaafu yaliyokaguliwa 2015/2016 .....	71
Jedwali Na. 23: Makosa katika ukokokotozi wa mafao ya hitimisho la akazi .....	72
Jedwali Na. 24: Idadi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa miaka iliyopita ..	76
Jedwali Na. 25: Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita ..	76

Jedwali Na. 26: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2016/17 kiidara (Shilingi kwa mamilioni) .....	78
Jedwali Na. 27: Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa Tanzania na nchi za Afrika Mashariki, 2013 - 2017 (Shilingi kwa milioni) .....	79
Jedwali Na. 28: Kesi za Rufaa ya Kodi ambazo Bado Kuamuliwa .....	85
Jedwali Na. 29: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2012-2017 (Shilingi kwa mamilioni) .....	89
Jedwali Na. 30: Bidhaa ambazo hazikupatikana kwenye maghala binafsi ya forodha.....	92
Jedwali Na. 31: Magari yaliyoingia nchini kwa muda maalum lakini hayakutoka nje ya Tanzania .....	93
Jedwali Na. 32: Kodi iliyokokotolewa na kutokukusanya (Kiasi katika Mamilioni) .....	98
Jedwali Na. 33: Muhtasari wa mapato yaliyokusanya na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine .....	100
Jedwali Na. 34: Uondoshaji usiokamilika wa miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa shilingi bilioni 359.....	104
Jedwali Na. 35: Uondoshaji usiokamilika wa miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa shilingi bilioni 359.....	106
Jedwali Na. 36: Uwekezaji wa mtaji wa biashara uliothaminishwa kwa gharama ya awali shilingi bilioni 549 .....	107
Jedwali Na. 37: kutotambua dhima tarajiwa baada ya kuamuliwa shilingi430,500,000.....	108
Jedwali Na. 38: uwekezaji hasi .....	109
Jedwali Na. 39:Mlinganisho wa Tathmini ya Udhibiti wa Ndani .....	112
Jedwali Na. 40: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi .....	113
Jedwali Na. 41: Tathmini katika usimamizi wa vihatarishi.....	115
Jedwali Na. 42: Wakala zisizokuwa na Bodi Ya ushauri.....	119
Jedwali Na. 43: Taasisi ambazo hazikufanya mikutano ya baraza la Watumishi .....	125
Jedwali Na. 44: Taasisi zilizochelewa kutuma makato ya kisheria.....	127
Jedwali Na. 45: Taasisi zilizopata adhabu kwa kuchelewa kupeleka makato .....	127
Jedwali Na. 46: Malipo ya Watumishi ambao hawapo kazini.....	128
Jedwali Na. 47: Taasisi ambazo hazikufanya tathmini na kupima watumishi .....	130
Jedwali Na. 48: Taasisi zenyne watumishi wanaokaimu zaidi ya miezi sita .....	132
Jedwali Na. 49: Taasisi ambazo stahili za watumishi hazijalipwa.....	134
Jedwali Na. 50: Taasisi zenyne watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango .....	136

Jedwali Na. 51: Ulingenifu wa Bajeti kuu na makusanyo ya fedha kutumia vyanzo vya ndani .....	139
Jedwali Na. 52: Ulingenifu wa Fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha iliyotolewa .....	140
Jedwali Na. 53: Ulingenifu wa Fedha za maendeleo ziliyoidhinishwa na fedha iliyotolewa .....	141
Jedwali Na. 54: Ukusanyaji wa Maduhuli kutumia vyanzo vya ndani ....	142
Jedwali Na. 55: Malipo ya ziada kutokana na madabiliko ya bei katika mikataba.....	143
Jedwali Na. 56: Malipo ya fedha za kukaimu bila idhini .....	145
Jedwali Na. 57: Malipo yasiyo na tija kwa Serikali Shilingi 587,226,56; .	145
Jedwali Na. 58: Mapungufu katika kukata makato ya kisheria na uwasilishwaji wake.....	147
Jedwali Na. 59: Mapungufu katika Makubaliano ya Ubia .....	149
Jedwali Na. 60: Mauzo ya Matrekta na vifaa vyake vya kilimo kwa mkopo .....	153
Jedwali Na. 61: Mapungufu yaliyojitekeza katika ukaguzi wa miradi ya umeme vijijini .....	154
Jedwali Na. 62: Malipo yaliyofanywa bila ya kuwepo kwa mikataba ....	156
Jedwali Na. 63: Utolewaji pungufu wa fedha .....	157
Jedwali Na. 64: Mkopo kwenda Wizara ya Maji .....	158
Jedwali Na. 65: fedha zilizolipwa kama VAT hazijarudishwa .....	159
Jedwali Na. 66: Mchango wa maendeleo ya madini haujaulipwa na Acacia Ltd TZS 732,631,200 .....	164
Jedwali Na. 67: Mapungufu katika mradi wa ufugaji Nyuki .....	166
Jedwali Na. 68: Fedha ambazo hazijarejeshwa na Katibu tawala-Dar Es Salaam .....	168
Jedwali Na. 69: Madeni yasiolipika .....	170
Jedwali Na. 70: Madai yasiokusanywa .....	171
Jedwali Na. 71: Taasisi za Serikali zisizokuwa na hati Miliki ya Ardhi ....	174
Jedwali Na. 72: Malipo yasiyokuwa na risiti za kielektroniki-EFD .....	175
Jedwali Na. 73: Manunuzi Yaliyofanyika bila Idhini ya Bodi ya Zabuni ....	179
Jedwali Na. 74: Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa .....	183
Jedwali Na. 75: Manunuzi yenze Mapungufu katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.....	186
Jedwali Na. 76: Taasisi zilizotakiwa kufanyiwa uchunguzi na PPRA .....	194
Jedwali Na. 77: Matumizi Yasiyokuwa na Manufaa - Shilingi 61,793,117 .	201
Jedwali Na. 78: Taasisi zenye madai yaliyokataliwa na NHIF .....	202
Jedwali Na. 79: Taasisi zilizolipa zaidi ya malipo ya stahiki .....	204
Jedwali Na. 80: Taasisi zenye malipo yasiyo na hati za malipo .....	206

Jedwali Na. 81: Orodha ya Taasisi zilizolipa katika vifungu nya bajeti visivystahili .....	212
Jedwali Na. 82: Taasisi zilizofanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa	214
Jedwali Na. 83: Taasisi zenyenye masurufu ya muda mrefu .....	216
Jedwali Na. 84: Taasisi zenyenye madeni yasiyoonyeshwa.....	221
Jedwali Na. 85: Jedwali la hapo chini linaonyesha taasisi hizo:.....	228
Jedwali Na. 86: <i>Taasisi zenyenye madai yasiyokusanywa .....</i>	230
Jedwali Na. 87: Malipo yasiyo na nyaraka .....	257
Jedwali Na. 88: Malipo yenye nyaraka pungufu.....	265

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Chati inayoonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa mwaka wa fedha 2015/2016.....	18
Kielelezo Na. 2: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti kuu ya CAG .....	20
Kielelezo Na. 3: Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa maagizo ya PAC ya miaka iliyopita juu ya Ripoti kuu ya Mwaka ya Ukaguzi .....	23
Kielelezo Na. 4: Hali ya utekelezaji wa Maagizo ya PAC kwa ulinganisho wa miaka miwili.....	26
Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Makisio ya Serikali kwa miaka minne ....	31
Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa Mapato ya Serikali kwa miaka minne ....	32
Kielelezo Na. 7: Mwenendo wa Mapato ya Serikali kwa miaka minne ikilinganishwa na Bajeti iliyodhinishwa.....	32
Kielelezo Na. 8: Fedha za Matumizi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2016/17 .....	35
Kielelezo Na. 9: Mwenendo wa makisio ya Bajeti kwa miaka mitatu .....	35
Kielelezo Na. 10: Mwenendo wa makusanyo ya mapato kwa miaka mitatu	36
Kielelezo Na. 11: Makisio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi kwa miaka minne .....	38
Kielelezo Na. 12: Makisio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi kwa miaka minne .....	40
Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara/Idara za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Balozi ( <i>Kiasi katika Shilingi bilioni</i> ) .....	43
Kielelezo Na. 14: Mapto yasiyotokana na Kodi Kwa Sekretarieti za Mikoa	44
Kielelezo Na. 15: Mapato yasiyotokana na Kodi kwa Balozi .....	45
Kielelezo Na. 16: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano .....	51
Kielelezo Na. 17: Vyanzo vya deni la Nje hadi tarehe 30 Juni 2017 .....	52
Kielelezo Na. 18: Kuhuishwa kwa hati fungani na Malipo ya Riba, 2015 hadi 2017 .....	55
Kielelezo Na. 19: Mwenendo wa soko la hati fungani za muda mrefu .....	56
Kielelezo Na. 20: Chati ya Mwenendo wa Malipo ya Mishahara Hewa ....	129
Kielelezo Na. 21: Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za Kielektronik.....	176
Kielelezo Na. 22: Miamala ya uhamisho wa Fedha kutoka Akaunti ya Amama kwa ubadhirifu .....	200
Kielelezo Na. 23: Mwenendo wa miaka minne (4) wa malipo yasiyokuwa na manufaa .....	201
Kielelezo Na. 24: Mwenendo wa miaka saba (7) wa malipo zaidi ya Stahiki .....	205
Kielelezo Na. 25: Mwenendo wa malipo ambayo Hati zake za Malipo zilikosekana na Taasisi zake: .....	207

Kielelezo Na. 26: Chati ya Ulingenifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka 5 iliyopita :	209
Kielelezo Na. 27: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu .....	210
Kielelezo Na. 28: Mwenendo wa Kukosekana kwa EFD Stakabadhi kwa miaka 5 .....	211
Kielelezo Na. 29: Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili.....	213
Kielelezo Na. 30: Mwenendo wa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa .....	215
Kielelezo Na. 31: Mwenendo wa Masurufu yasiyorejeshwa.....	217
Kielelezo Na. 32: Mwenendo wa Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za Mapokezi.....	219
Kielelezo Na. 33: Mtiririko wa malipo bila kutoa kodi ya zuio kwa miaka mitatu iliyopita .....	220

## MAMLAKA YA OFISI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi Taifa ya Ukaguzi,  
(Imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyofanyiwa marekebisho mara ya mwisho mwaka 2005) kama yalivyoafanuliwa zaidi na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 (iliyofanyiwa marekebisho) na Kanunu za Ukaguzi wa Umma ya za Mwaka 2009.

### Dira ya Ofisi

**Kuwa Taasisi ya Hali ya Juu katika ukaguzi wa sekta ya Umma.**

#### Dhamira

Kutoa Huduma za Ukaguzi wa Sekta ya Umma Zenye ubora wa Hali ya Juu Zinazoimarisha utendaji, Uwajibikaji na Uwazi Katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma

#### Misingi ya Maadili

<b>Uadilifu</b>	Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo
<b>Ubora</b>	Sisi ni wanataluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi.
<b>Uaminifu</b>	Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia Utawala wa sheria.
<b>Kuwalenga watu</b>	Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
<b>Ubunifu</b>	Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
<b>Kujielekeza kwenye matokeo</b>	Sisi ni taasisi inayojikita kwenye mafanikio kulingana na malengo tuliojiwekea
<b>Kufanya Kazi kwa Kushirikiana</b>	Tunafanya kazi pamoja kama timu, kujadiliana kitaalamu na kubadilishana maarifa, mawazo na uzoefu.

## VIFUPISHO

<b>ACGEN</b>	<b>Mhasibu Mkuu wa Serikali</b>
<b>ADEM</b>	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu
<b>AFRM</b>	Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika
<b>AGITF</b>	Mfuko wa Pembejeo za Kilimo
<b>AO</b>	Afisa Masuuli
<b>APP</b>	Mpango wa Manunuzi wa Mwaka
<b>ASA</b>	Wakala wa Mbegu za Kilimo
<b>BOQ</b>	Mchanganuo wa Gharama za Ujenzi
<b>BoT</b>	Benki Kuu ya Tanzania
<b>CAG</b>	Mdibiti na Mkaguzi Mkuu
<b>CDF</b>	Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi
<b>CG</b>	Serikali Kuu
<b>CTA</b>	Kibali cha Kazi cha Muda Mfupi
<b>DART</b>	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam
<b>DDCA</b>	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa
<b>EFD</b>	Mashine za Kielekroniki
<b>ETD</b>	Hati za Dharura za Kusafiria
<b>FETA</b>	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo
<b>FRF</b>	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
<b>GCLA</b>	Wakala wa Maabara za Serikali
<b>GN</b>	Tangazo la Serikali
<b>GoT</b>	Serikali ya Tanzania
<b>GPSA</b>	Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi
<b>GST</b>	Wakala wa Utafiti wa Miamba
<b>HESLB</b>	Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu
<b>HQ</b>	Makao Makuu
<b>IFMS</b>	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha
<b>IJA</b>	Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA)
<b>IPSAS</b>	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma

## DIBAJI

Kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebisha 2005) na kama ilivyofafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008; kwa mara nyingine tena ninafurahi kuwasilisha kwa Mh. Rais ripoti ya ukaguzi kwa taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2017. Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inanitaka kuwasilisha kwa Mh. Rais ripoti kuu ya ukaguzi kufikia tarehe 31 Machi kila mwaka kisha kuwasilishwa bungeni kwa maelekezo ya Rais kupitia kwa Waziri husika (Waziri wa Fedha na Mipango).



Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali Kuu kwenye tathmini na ukaguzi wa taarifa za fedha pamoja na nyaraka husika, mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu na mchakato wa manunuzia na uzingatifu wa Sheria na Kanuni mbalimbali. Pia inajumuisha matokeo ya kaguzi maalumu zilizofanyika kwa mwaka 2016/17, hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka ya nyuma na utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Fedha ya Bunge (PAC).

Nimefanya jumla ya kaguzi 241 zinazohusisha; Wizara zote, Idara za Serikali zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa yote, Balozi, Wakala wa Serikali, Mifuko Maalumu, Bodi za Mabonde ya Maji, pamoja na taasisi nyingine za Serikali. Kufuatia kukamilika kwa kaguzi hizo nimetoa hati za ukaguzi kwa kila taasisi kuhusiana na taarifa za fedha zilizoandaliwa kama zinaonesha hali halisi ya shughuli zilizofanywa kulingana na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha usiofuata misingi ya fedha taslimu (IPSAS Accrual basis of accounting).

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs)<sup>1</sup> vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC) ambavyo ni mahsus kwa ukaguzi wa sekta ya umma. Ofisi yangu imekuwa ikitimiza majukumu yake kitaalamu ili kuonyesha umuhimu na uhalisia wake kwa wananchi, Bunge na wadau wengine.

<sup>1</sup> International Standards of Supreme Audit Institutions

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ofisi yangu imepanga kufanya yafuatayo kwenye ukaguzi wa 2017/18;

- Kufanya ukaguzi wa kina na wa kitaalamu kwenye maeneo yenye uwekezaji mkubwa wa serikali kama vile: ujenzi wa barabara, ujenzi wa reli za kisasa ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, miradi ya nishati (umeme) na miradi ya mafuta na gesi;
- Kufanya ukaguzi wa kina kuhusiana na usimamizi wa masurufu (imprests), hasa kwenye taasisi ambazo zina bakaa kubwa na ambazo zimekaa kwa muda mrefu bila kurejeshwa; vilevile, taasisi ambazo zimekuwa zikitoa masurufu mapya kabla ya kurejeshwa yaliyotolewa awali;
- Kitengo cha Ukaguzi wa kiforensiki kitajikita zaidi kufanya chunguzi zilizopo kwenye mpango wake na kupunguza kaguzi ambazo zinaombwa na wadau wengine. Kwa mwaka 2017/18 kitengo hicho kitafanya ukaguzi wa kiuchunguzi kwenye maeneo yenye viharishi, hasa kwenye utaratibu na mchakato wa manunuvi, wizi wa fedha pamoja na matumizi mabaya ya mali za serikali.
- Kwa kuwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itafaidika na mpango wa DFID ambao utashughulikia masuala ya rushwa na udanganyifu kupitia mchakato wa kutengeneza mazingira ya kupunguza matukio ya udanganyifu. Ofisi inatarajia kupendekeza kuanzishwa kwa mapitio ya matukio ya udanganyifu kila mwaka (*Annual Fraud Survey*), ambapo jamii katika ngazi zote itatoa taarifa ya maeneo na taasisi/ofisi zinazojihusisha na udanganyifu na rushwa na kiasi cha udanganyifu na rushwa kilichohusika. Hii itaenda sambamba na uanzishwaji wa mtandao wa intaneti, ambapo jamii itakuwa inatoa taarifa kuhusiana na matukio ya rushwa na undanganyifu. Pia itaendana na pendeleko la 11 la mkutano wa 16 wa INCOSAI uliofanyika nchini Uruguay mwaka 1998 ambao mada yake ilikuwa ni 'Jukumu la Taasisi Kuu za Ukaguzi katika kupambana na rushwa'.

Naamini kuwa, kama matokeo na mapendekezo yaliyopo kwenye ripoti hii na yatakayojitokeza kwenye maeneo yaliyopangwa kukaguliwa kwa mwaka 2017/18 yatakelezwu kikamilifu, yataboresha kwa kiasi kikubwa utendaji wa serikali na taasisi katika utoaji wa huduma; hivyo kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uaminifu.

Prof. Mussa Juma Assad,

**Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

## SHUKRANI

Sina budi nianze na neno la shukrani kwa Ofisi mbalimbali, watu binafsi na wafanyakazi ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa sana katika kufanikisha kutimiza majukumu yangu ya kikatiba ya kuwasilisha ripoti yangu ya mwaka ya Serikali Kuu kwa Mh. Rais kabla ya mwisho wa mwezi Machi kila mwaka.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kuendelea kuiunga mkono na kuwa na imani na Ofisi yangu.

Rasilimali fedha na rasilimali watu ni nyenzo muhimu sana katika jitihada za taasisi yoyote, hivyo natoa shukrani zangu za dhati kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kamati zake kwa kutimiza majukumu yake ya kuhakikisha rasilimali fedha kwa ajili ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi zinapatikana kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa vyovyote, vile mafanikio ya ofisi yangu yasingepatikana kama sio juhudi, ushirikiano na uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango, hivyo naishukuru sana.

Pia, nashukuru Menejimenti za taasisi zilizokaguliwa kwa ushirikiano mkubwa walionipatia wakati wote wa ukaguzi.

Mwisho, natambua jitihada kubwa zinazofanywa na wafanyakazi wa Ofisi yangu katika ngazi zote. Nimeweza kusimama kifua mbele na kuzungumzia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu tu wao walijitahidi kutimiza majukumu yao; na wakati mwingine, katika mazingira magumu sana, walifanya kazi yao kwa kiwango cha hali ya juu sana na kutoa ripoti zao kwa wakati.

Prof. Mussa Juma Assad,  
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

## MUHTASARI

### Utangulizi

Sehemu hii ya taarifa ya ukaguzi wa jumla wa Serikali kuu inatoa muhtasari mfupi wa matokeo makubwa, hitimisho na mapendekezo ya Ukaguzi. Ripoti hii imejumuisha ukaguzi wa Mafungu 65 ya Wizara na Idara ya Serikali, Wakala za Serikali 35, Mifuko Maalum ya Fedha 17, Taasisi Nyingine za Serikali 38, vyama vya siasa 10; Sekretarieti za Mikoa 26, Balozi 39, Bodi za Maji ya Bonde 13. Pia taarifa hii inajumuisha ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, Akaunti ya Jumla, ukaguzi wa awali wa Taarifa za Pensheni na ukaguzi maalum.

### Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kati ya taasisi 241 zilizokaguliwa Taasisi 237 zimekaguliwa na kupewa hati ya Ukaguzi wa hesabu waliozo andaa. Balozi za Tanzania 4 hazikupata hati za Ukaguzi kwa sababu ndio kwanza zimeanzishwa. Mlinganisho wa hati za ukaguzi kwa miaka mitatu iliyopita ni kama ionekanavyo hapo chini

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Maoni ya Ukaguzi

Mwaka wa Fedha	Hati Inayoridhish a		Hati zenye Mashaka		Hati isiyo ridhisha		Hati Mbaya		Jum la
	Na.	%	Na	%	Na	%	Na	%	
2016-17	204	86	22	9	4	2	7	3	237
2015-16	190	86	24	11	3	1	5	2	222
2014-15	181	91	17	9	1	1	0	0	199

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kumekuwa na ongezeko la ripoti za ukaguzi kutoka ripoti 199 zilizotolewa mwaka 2014/2015 hadi ripoti 244 mwaka 2016/2017. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa taasisi mpya.

Pia kumekuwa na maboresho ya hati za ukaguzi kwa kila mwaka. Matokeo ya ukaguzi kwa 2016/17 yamekuwa mazuri sana licha ya kuwa Serikali Kuu imeanza kufuga kikamilifu hesabu zake kwa

kutumia viwango vya kimataifa visivozingatia pesa taslim (full IPSAS accrual). Matokeo kamili ya hati za ukaguzi zilizotolewa yameanishwa kwenye **Sura ya Pili** ya ripoti hii.

### **Ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya PAC**

Nilipitia hali ya utekelezaji wa mapendekezo yangu na kubaini kuwa kati ya mapendekezo 4,108 ya ukaguzi 1,543 (37.57%) yaliopendekezwa yametekelvezwa, 1,454 (35.39%) yalikuwa katika utekelezaji, 721 (17.55%) hayakutekelezwa na 390 yalikuwa yamepitwa na wakati. Pia nashukuru kwa jithada zilizofanya na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57) kuwasilisha hati zote za malipo za kiasi cha Shilingi 91,261,040,310 ambazo hazikuwasilishwa wakati wa ukaguzi mwaka jana. Hati hizo za malipo zote zilihakikiwa na ripoti ilitolewa.

Kwa ripoti kuu yangu ya mwaka 2015/2016, mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi mpaka mwisho wa mwaka wa fedha 30 Juni, 2016 ambayo yalihitaji kujibiwa na Serikali yamebungua kutoka 102 hadi 85. Kati ya mapendekezo 85 ambayo yalikuwa hayajashughulikiwa, 14 (16.5%) yalitekelezwa, 51 (60.0%) yalikuwa katika utekelezwaji, 9 (10.6%) hayakutekelezwa na 11 (12.6%) yalikuwa yamepitwa na mwakati.

Kwa maagizo ya PAC juu ya ripoti kuu ya ukaguzi, kulikuwa na maagizo 16 ambayo yalikuwa hayajafanyiwa kazi. Kati ya maagizo 16 ambayo yalikuwa hayajafanyiwa kazi, 1 (6%) lilitekelezwa, 10 (63%) yako katika utekelezaji, 3 (19%) hayajatekelezwa na 2 (12%) yamepitwa na wakati.

Kwa maagizo ya PAC kwa kila Mkaguliwa, PAC ilifanya vikao na Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na kutoa baadhi ya maagizo kwa ajili ya utekelezaji. Kwahiyio, jumla ya utekelezaji kwa kila Mkaguliwa yamejumuisha maagizo yale za miaka iliyopita na ya mwaka huu. Nimefanya ufuatiliaji wa utekelezwaji wa maagizo ya PAC kwa kila mkaguliwa ambapo maagizo 106 (39%) yaliyotolewa na PAC yalitekelezwa, 106 (39%) yalikuwa katika utekelezaji, 54 (17%) hayakutekelezwa na 9 (3%) yalikuwa

yamepitwa na wakati. Maelezo zaidi ya utekelezaji huu ipo katika Sura ya Tatu

### **Usimamizi wa Fedha za Umma**

Ili kugharamia bajeti ya 2016/17, Serikali ilipanga kukusanya Shilingi bilioni 29,539.6 hii ni sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 7,044.10 ikilinganishwa na makadirio yaliyopangwa ya Shilingi bilioni 22,495.5 kwa mwaka 2015/16.

Mapato halisi yaliyokusanywa kutoka kwenye vyanzo vinyavyotambulika yalifikia Shilingi bilioni 25,307.48. Hii inaonyesha Serikali ilikusanya chini ya makadirio kwa kiasi cha Shilingi bilioni 4,232.12 sawa na asilimia 14.33.

Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Mapato yaliyotokana na kodi yalikuwa Shilingi bilioni 14,271.30 sawa na asilimia 94.48 ya bajeti, hii ni sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 1,807.47 (asilimia 14.5) ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanywa mwaka 2015/16.

Mapato yasiotokana na kodi bado yanaendelea kukusanywa chini ya makadirio ambapo mwaka huu wa fedha kiasi cha Shilingi bilioni 2,072.9 kimekusanywa ukilinganisha na makadirio ya Shilingi bilioni 3,358.4 sawa na asilimia 61.72 ukilinganisha na mwaka 2015/16.

Mapato yanayotokana na Mikopo ya Ndani ambayo ni kwa ajili ya bajeti na kulipa amana za Serikali zilizoiva yalikuwa Shilingi bilioni 5,915.85 ambayo ni kubwa kuliko makadirio kwa asilimia 10.08 na kubwa zaidi kwa asilimia 11.52 ikilinganishwa na mapato ya 2015/16.

Mapato yanayotokana na kukopa Nje, Misaada ya Wahisani na Wadau wa Maendeleo iliyopokelewa kwa Mwaka wa Fedha 2016/17 ilikuwa Shilingi bilioni 3,047.43 sawa na asilimia 53.45 dhidi ya makadirio yaliyopitishwa ya Shilingi bilioni 5,701.80. Kiasi cha Shilingi bilioni 2,654.37 sawa na asilimia 46.55 hakikupokelewa kama ilivyopangwa.

Bajeti ya matumizi ilipangwa Shilingi bilioni 29,546.84 sawa na ongezeko la Shilingi 7,051.34 bilioni ukilinganisha na Shilingi bilioni 22,495.5 zilizokadiriwa mwaka 2015/16. Shilingi bilioni 18,084.56 zilielekezwa kwenye matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 11,462.28 zilielekezwa kwenye matumizi ya maendeleo ambapo ilipelekea ongezeko la Shilingi bilioni 1,510 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 5,541.18 kwa matumizi ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo imeongezeka mara mbili zaidi kutoka Shilingi bilioni 5,921.1 na kufikia Shilingi bilioni 11,462.28 na matumizi ni Shilingi bilioni 4,184.26.

Shilingi bilioni 219.47 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kulipa madeni, ambapo Shilingi bilioni 184.10 kwa ajili ya madeni ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 35 kwa ajili ya madeni ya matumizi ya maendeleo. Selikali imeendelea kulipa madeni ya yaliyohakikiwa ya Wazabuni, Wakandarasi, Watumishi na Watoa Huduma mbalimbali kwa kutegemea upatikanaji wa fedha, kwa maoni yangu kutumia mapato ya mwaka kulipia madeni kunaathiri utekelezaji wa bajeti.

Ukaguzi wangu wa leseni za uchenjuaji madini kwa migodi iliyoko Mwanza, Kahama na Shinyanga ulionesha mitambo ya kuchenjulia madini 8, 25 na 51 mtalia ilikuwa ikiendeshwa bila kuwepo kwa leseni hivyo kusababisha hasara ya upotevu wa maduhuli ya Dola za Kimarekani 104,400, sawa na Shilingi milioni 231.66 kwa mwaka.

Jumla ya Shilingi bilioni 14.55 zilikusanya na balozi zetu nje ya nchi ikiwa ni mapato yasiyotokana na kodi kwa mwaka 2016/17, hata hivyo kiasi hicho cha fedha hakikupelekwa mfuko mkuu wa Serikali; na kusababisha Serikali kushindwa kutumia fedha hizo. Vilevile, fedha hizo zaweza kutumika isivyokusudiwa. Maelezo zaidi ya yanapatikana katika **Sura ya Nne**

#### **Usimamizi wa Mapato Yatokanayo na Kodi**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ya Mapato, Tanzania ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 14,249.25 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya Shilingi bilioni 15,261.5. Hali hii

inaonesha upungufu wa makusanyo kwa Shilingi bilioni 1,012.1 ambazo ni sawa na asilimia 6.63 ya malengo. Jumla ya makusanyo hayo haikujumlisha Shilingi bilioni 22.13 ambazo ni misamaha ya kodi iliyotolewa na serikali. Hivyo, makusanyo halisi ya mwaka 2016/17 ni Shilingi bilioni 14,271.38.

### **Kesi za muda mrefu katika mamlaka za rufaa za kodi zikisubiri hukumu**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina kesi nyingi za kodi zilizokwama kwa muda mrefu katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya rufaa. Kesi hizi zinazosubiri maamuzi zina kodi yenye thamani ya Shilingi trilioni 4.44.

Nilibaini kuwa, Taasisi hizi zina ufanisi mdogo unaochangiwa na upungufu wa makamu wenye viti na wajumbe wa bodi zake, upungufu huu unapelekea kushindwa kufanyika kwa vikao vya kutosha kwa ajili kusikiliza na kuamua kesi za kodi.

### **Mapungufu katika kushughulikia pingamizi za kodi**

Katika mwaka 2016/17 nilibaini kuwa Mamlaka ya Mapato ina pingamizi za kodi ambazo bado hazijashughulikiwa zenye thamani ya jumla ya Shilingi 738,619,739,113.48. Mlundikano wa pingamizi za kodi ambazo hazijashughulikiwi kwa wakati unachangiwa na uwezo na ufanisi hafifu wa kitengo cha ukaguzi wa kodi na kitengo cha ufundi katika Mamlaka ya Mapato.

Pia, suala hili limesababishwa na upungufu wa wafanyakazi wenyewe weledi na uzoefu wa kutosha kushughulikia mapingamizi ya kodi ikilinganishwa na idadi kubwa ya mapingamizi yanayowasilishwa na walipa kodi.

Kadhalika, Mamlaka haikukusanya kodi yenye thamani ya Shilingi 1,558,116,225,302.76 iliyotakana na mapingamizi ya kodi ambayo yalikuwa yameshughulikiwa na kukamilishwa, na kodi ya Shilingi 269,612,850,131.28 haikukusanya kwa mapingamizi yaliyokataliwa na Kamishna kwa sababu mapingamizi hayo hayakukidhi vigezo vya kisheria.

Pia, Mamlaka ilipokea mapingamizi ya kodi yene thamani ya Shilingi 296,099,930,972.27 bila kukusanya amana za mapingamizi hayo; pia hapakuwa na kibali cha msamaha wa amana kutoka kwa Kamishna. Mapungufu haya ni kinyume na matakwa ya sheria, na yanaweza kuhamasisha walipa kodi wasio waaminifu kuleta mapingizi mengi yasiyofuata misingi ya kisheria na kupelekeea ukwepaji kodi.

**Udhibiti wa misamaha ya kodi za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji wa madini**

Nilibaini kuwa malori 94 yalikuwa yamebeba mafuta lita 3,147,289 yene kodi ya Shilingi 2,083,246,836.00 kutoka Dar es Salaam kwenda migodi ya dhahabu minne (Buzwagi, Bulyanhulu, North Mara na Geita) kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Juni 2017, lakini hapakuwa na nyaraka zinazothibitisha kuwa mafuta hayo yalipokelewa na makampuni hayo manne huko migodini. Kukosekana kwa nyaraka hizo kunaashiria kwamba mafuta hayo hayakutumika kwa shughuli zilizokusudiwa za uchimbaji wa madini, hivyo kuisababishia Serikali hasara ya ukosefu wa mapato.

Kadhalika, nilibaini kuwa mafuta yene msamaha wa kodi ya Shilingi 11,052,806,957.20 yaliyolengwa kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji madini yalitumiwa na wakandarasi na watu wengine ambao sio wanufaika wa msahama huo wa kodi katika kipindi cha mwezi Januari 2016 hadi Juni 2017.

**Mifumo isiyoridhisha ya udhibiti wa mafuta na mizigo inayoingizwa nchini, inayopita kwenda nchi nyingine katika ukadiriaji wa kodi**

Nilipitia taarifa za mafuta yaliyoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani na kulinganisha na taarifa za mafuta zilizoingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kukadiria na kulipiwa kodi. Nilibaini kuwa mafuta lita 31,254,211 yene kodi ya Shilingi 14,749,404,154.26 ambayo yaliingizwa kupitia nyaraka 73 za kuagizia bidhaa nje ya nchi (bills of lading) za makampuni ya mafuta 22 hayakuingizwa kwenye mfumo wa

TANCIS kwa ajili ya kukadiriwa na kulipiwa kodi. Kitendo hiki ni kinyume cha matakwa ya taratibu za Mamlaka.

Mafuta kutokuingizwa kwenye mfumo wa kodi (TANCIS) kunamaanisha kuwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia nyaraka hizi hayakulipiwa kodi, na hivyo, kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Kadhalika, katika ukaguzi wa mafuta na mizigo inayopita nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine nilibaini lita 21,228,114.50 za mafuta na mizigo 68 yenye kodi ya Shilingi bilioni 14.75 haikusafirishwa kwenda nchi zilizokusudiwa. Mapungufu haya yanamaanisha kuwa mizigo na mafuta haya yaliuzwa na kutumika ndani ya nchi bila kulipia kodi.

#### **Usimamizi na ufuutiliaji usioridhisha wa makusanyo ya madeni ya kodi**

Mwaka huu wa ukaguzi Mamlaka inadai kodi ya Shilingi 262,293,791,682 kutoka kwa walipakodi. Kuwapo kwa madeni ya kodi kunasababishwa na mifumo na mikakati isiyoridhisha kwenye ukusanyaji wa madeni ya kodi hasa katika ofisi za mikoa. Kadhalika, nilibaini makadirio ya kodi yaliyokuwa pungufu kwa kiasi cha Shilingi 9,363,346,393.23. Makadirio pungufu yalisababishwa na mapitio na uchambuzi hafifu wa taarifa za walipakodi.

#### **Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine lakini hayakuwasilishwa kwenye Taasisi husika**

Mamlaka ilikusanya Shilingi 1,671,096,919,536.3 kama tozo na ushuru uliokusanywa kwa niaba ya Taasisi nyingine. Makusanyo hayo yanahusu tozo za barabara, tozo ya petroli, ada ya maendeleo ya maji, tozo ya maendeleo ya reli na tozo ya bandari; Lakini nilibaini kwamba, kati ya makusanyo yote, kiasi cha Shilingi 410,448,166,098.44 hakikuwasilishwa kwenye taasisi husika, swala ambalo ni kinyume na matakwa ya sheria.

Kuchelewa kuwasilisha makusanyo haya kwenda kwenye Taasisi husika kunaathiri utoaji wa huduma na utekelezwaji wa mipango ya Taasisi hizo.

## **Tathimini ya Deni la Taifa**

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2017 lilikuwa Shilingi bilioni 46,081.43 ambapo deni la ndani lilikuwa Shilingi bilioni 13,335.65 na deni la nje Shilingi bilioni 32,745.78 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 5,042.05 sawa na asilimia 12 ikilinganishwa na deni la Shilingi bilioni 41,039.39 liloripotiwa tarehe 30 Juni 2016.

Katika ukaguzi wangu nilibaini masuala ya msingi yafuatyo kuhusu deni la taifa na usimamizi wake;

Kushushwa Kiwango cha Deni la Taifa kwa Kiasi cha Shilingi Bilioni 4,588.39 kutokana na kutojumuishwa kwa madeni ya mifuko ya pensheni na dhamana zilizokiukwa masharti, Ukuaji hafifu wa dhamana za Serikali katika soko la mtaji, Mikopo iliyosainiwa mikataba lakini haijapokelewa, Shilingi bilioni 2,367, Mapungufu katika utaratibu wa kuingiza kumbukumbu za mapokezi ya mikopo, Usimamizi usioridhisha wa mikataba ya mikopo iliyofaulishwa ‘on-lending contracts’ na kutapanywa kwa shughuli za ofisi ya mbele, kati na ya nyuma kunakoongeza changamoto katika kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa sahihi zinazohusu deni la taifa; tatizo hili limekuwa ndio chanzo kikuu cha changamoto nyingi kwenye deni la taifa. Kwa maelezo zaidi ya kodi na deni la taifa tazama **Sura ya Tano**

## **Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na utawala bora**

Utekelezaji wa udhibiti wa mfumo wa ndani ni jukumu la menejimenti ya Taasisi husika.

Tathmini yangu katika mifumo ya udhibiti wa ndani nilibaini mapungufu mbalimbali kwenye Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani katika Wizara 3 na Sekretariati za Mikoa 15 .Vilevile, katika tathmini yangu ya kamati za ukaguzi, nilibaini mapungufu katika taasisi 27 ikijumuisha Wizara 6, Sekretarieti za Mikoa 18 na Wakala za Serikali 3. Pia, tathmini yangu ya vihatarishi nilibaini Taasisi 16 zenye mapungufu ambazo ni Wizara 4, Sekretariati 11 na balozi 1.

Katika kupitia tathmini ya Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) nilibaini kuwa Wizara 5, Sekretarieti za Mikoa 13, na Balozi 13 zinamapungufu ya TEHAM. Katika masuala ya utawala kulikuwa na Wizara 1 yenye mapungufu. Katika tathmini yangu nilibaini Ubalozi mmoja wenyewe miamala ya udanganyifu. Mbali hayo, nimejumuisha changamoto zilizobainishwa katika usimamizi wa mali zilizotaifishwa na sheria yake. Maelezo ya kina yanapatikana katika **Sura ya Sita**

### **Usimamizi wa Rasilimali watu na Mishahara**

Ingawa katika miaka ya hivi karibuni Serikali imefanya mabadiliko makubwa ya kusafisha na kuboresha taarifa na kumbukumbu za watumishi ambayo imesababisha maboresho muhimu, lakini bado baadhi ya maeneo yanahitaji hatua zaidi. Kwa mwaka huu nimebaini mapungufu katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara kama ifuatavyo;

Kushindwa kufanya mikutano ya baraza watumishi, kutokamilika kwa taarifa za watumishi katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za watumishi kama vile tarehe za kuzaliwa, watumishi waliohamishwa, waliostaafu na walioacha kazi hawajaondolewa katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu na kutokuonesha kama watumishi waliohibitishwa kazini.

Pia nimebaini makato ya Kisheria kutowasilishwa kwa wakati kwenye mifuko ya pensheni, kulipa mishahara watumishi wasiokuwepo katika utumishi wa umma kiasi cha Shilingi 31,296,376, kushindwa kufanya tathmini na upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi, watumishi kukaimu katika nafasi za kazi kwa zaidi ya miezi sita, stahiki za watumishi ambazo hazijalipwa kiasi cha Shilingi 4,604,984,054.64, ukosefu wa watumishi katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Ofisi za Balozi na watumishi kupokea mshahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria. Taarifa zaidi ya masuala haya inapatikana **Sura ya Saba**

Katika **Sura ya Nane**, nimebainisha masuala yote yaliyoibuliwa wakati wa ukaguzi wa Wakala za serikali 33, Mifuko Maalamu ya

Fedha 17, Taasisi nyingine za Serikali 38 na Bodi za Mabonde ya maji 13.

### **Mapungufu yaliojitokeza katika Ukaguzi wa Wakala za Serikali**

Nimebaini Wakala za Serikali kuendelea kutegemea fedha za Serikali kuijidesha; Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa mapato yatokananyo na vyanzo vya mapato ya ndani kwa Wakala za serikali yana uwezo wa kutekeleza bajeti za Wakala kwa asilimia 16 tu ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, hivyo taasisi hizi hutegemea fedha za Serikali kuu kwa asilimia 84 ili kutekeleza bajeti zao. Pia, nilibaini kuwa kuna kushuka kwa makusanyo ya mapato ya ndani kwa asilimia 24 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka uliopita.

### **Uzingatiaji wa Sheria za Kodi kwa Wakala wa serikali**

Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa baadhi ya Wakala wa Serikali hawazingatii sheria za Kodi. Katika suala hili nimebaini taasisi tano ambazo zimefanya malipo bila ya kuchukua stakabadhi za kieletroniki kutoka kwa watoa huduma katika manunuzi ya Shilingi 41,830,706,134. Kiasi hiki ni ongezeko la Shilingi 38,854,212,890 sawa na asilimia 93 ukilinganisha na manunuzi kama hayo yaliofanyika mwaka uliopita.

### **Mapugufu Katika Ukaguzi wa Manunuzi na Utekelezaji wa Mikataba**

Katika ukaguzi wa mikataba ilioingiwa na wakala za Serikali nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania amefanya malipo zaidi ya Shilingi 1,177,740,226 kimakosa yatokanayo na mabadiriko ya bei.

Pia, katika ukaguzi huu nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Nchini pamoja na Wakala wa Majengo Nchini kwa ujumla walilipa kiasi cha Shilingi 587,226,567 kama adhabu itokanayo na ucheleweshwaji wa kulipa madai ya Wakandarasi na marejesho ya mkopo.

## **Mapungufu yaliobainika katika utekelezaji wa bajeti za wakala na taasisi nyingine**

Katika ukaguzi wa utekelezaji wa bajeti za wakala wa serikali, nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 18,780,000 kilifanyika nje ya bajeti, kiasi cha Shilingi 89,473,398 kilifanyika bila kuzingatia vifungu sahihi vya bajeti, na kiasi cha Shilingi 173,889,382 kimefanyika nje ya utaratibu na mfumo wa kibajeti.

Pia, katika ukaguzi huu nilibaini kuwepo kwa matumizi ya Shilingi 529,296,700 kwa wakala saba za serikali bila kuwepo na nyaraka za kutosha. Nimebaini pia kuna wakala nyingine nne ambazo zilikuwa na masurufu ambayo hayajarejeshwa yenyе jumla ya Shilingi 118,134,300.

## **Mapungufu niliyobaini katika ukaguzi wa shughuli za uwekezaji wa Mashirika ya Majeshi ya Ulinzi.**

Katika ukaguzi wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa, SUMA (JKT) nilibaini kuwa kuna madai ya muda mrefu yasiokusanywa kutoka kwa wakulima waliokopeshwa kiasi cha Shilingi 40,047,937,000 kwa kukopeshwa matrekta na vifaa vya kilimo.

Pia, nilibaini kuwa SUMA JKT ina kukopeshwa pampu za umwagiliaji zenye thamani ya Shilingi 2,912,369,000 ambazo haziuziki. Pampu hizi zimekaa muda mrefu hivyo hazina hali nzuri ya kuuzika

Katika ukaguzi huu wa Uwekezaji wa mashirika haya ya jeshi, nilibaini kuwepo kwa mashine mpya za kusagia nafaka zenye thamani ya Shilingi 148,135,000 ambazo zimetelekezwa kwa muda wa miaka mine hazitumiki. Pia nimebaini kuwa kuna matrekta 11 yametelekezwa na Shirika hili bila kutengenezwa. mapungufu haya yameelezewa kwa kina katika **Sura ya Nane**

## **Mapungufu katika ukaguzi wa Bodi za Mabonde ya Maji**

Katika ukaguzi hu nimepaini kuwa katiaka bodi za bonde la maji, nilibaini kiasi cha shillingi 42,889,557,718 kutoka katika mradi wa

maendeleo katika sekta ya maji hazikutolewa kutekeleza bajeti ya bodi hizi.

Pia katika ukaguzi huu nilibaini kuwa kuna kiasi cha Shilingi 110,702,495 kilikopeshwa kwa wizata ya maji na umwagiliaji ambazo hazijarejeshwa mpaka wakati wa ukaguzi. Kiasi hiki kilitakiwa kutekeleza bajeti ya Bodi hizi.

Katika matumizi ya Bodi za Bonde la Maji kwa kutumia pesa za Mradi wa Maendeleo katika Sekta ya Maji (WSDP) nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 251,437,021 kililipwa kama kodi ya ongezeko la thamani. Kwa mujibu wa makubaliano baina Serikali na WSDP pesa za mradi huu hazitakiwi kulipa kodi aina yoyote ile. Kiasi hili kinatakiwa kirejeshwe na Mamlaka ya kodi.

Pia, nilibaini uchepushwaji wa Shilingi 333,790,806 zilizokuwa zinatakiwa kukarabati mabwawa ya maji. Mapungufu haya yameelezewa kwa kina katika **Sura ya Nane**

#### **Mapungufu yaliobainika katika ukaguzi wa Mifuko ya fedha za serikali**

Katika ukaguzi wa Mifuko maalum ya Fedha za Serikali, nilibaini kuwa kuna mifuko inayotoa mikopo kwa wananchi lakini mifuko hiyo haijafanya jitihada za kutosha kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inarejeshwa kwa wakati. Katika mikopo hiyo nimebaini kuwa kiasi cha Shilingi 1,141,590,806 kilikopeshwa na Mfuko wa ufadhili wa Pembejeo za Kilimo, Kiasi cha mkopo wa Shilingi 510,572,419 kilitolewa na Mfuko wa Ufadhilli wa Rais, na jumla ya Shilingi 1,085,430,924 kilikopeshwa na mfuko wa maendeleo ya Wanawake.

Pia wakati wa Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Madini, nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 732,631,200 kilitakiwa kutolewa na Kampuni ya Buzwagi Gold Mine (ACACIA Ltd) lakini kiasi hiki hakijatolewa na Mgodi huu kama ilivyokubalika katika Mkataba wa uzalishaji.

Katika Ukaguzi wa Mfuko wa Maafa, nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 206,318,360 kilitakiwa kurejeshwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar Es Salaam kutokana na salio la fedha zilizotumika

katika maafa ya Gongolamboto. Kiasi hiki cha pesa hakijareshwa na katibu Tawala. Mapungufu haya yameelezewa kwa kina katika **Sura ya Nane**

### **Mapungufu katika Ukaguzi wa Manunuzi**

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2017, niliweza kubaini mapungufu kadhaa katika Taasisi za Serikali kutokuweza kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi.

Katika Taasisi za Serikali Kuu nane (8) nilizokagua, nilibaini manunuzi ya vifaa na huduma yenye thamani ya Shilingi 52,678,585,370 vilivyoagizwa na kulipiwa lakini havikupokelewa. Mwaka jana hoja kama hii ilikuwa inajumla ya Shilingi 3,452,112,838 hivyo imeongezeka Shilingi 49,226,472,532,] na kufikia Shilingi 52,678,785,370. Ongezeko hili limetokana na ununuzi wa ndege aina ya Q400 Bombardier yenye thamani ya Shilingi bilioni 51.838

Nilibaini kuwa, Taasisi kumi na moja (11) zilinunua bidhaa, na huduma za za ujenzi za Shilingi bilioni 1.453 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila ya kuwa na mikataba. Kufanya hivyo ni kinyume na kanuni ya 10(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Kwa kutokuwapo mikataba kati ya Serikali na watoa huduma ikitokea mmojapo anashindwa kutimiza makubaliano hatua za kisheria hazitaweza kuchukuliwa dhidi yake.

Taasisi za Umma saba (7) zilibainika kufanya manunuzi ya Shilingi bilioni 2.997 bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

Jumla ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kumi na tatu (13) ziliingia katika makubaliano ya Mikataba na Wakandarasi katika ujenzi wa miradi mbalimbali. Nilibaini kuchelewa kukamilika kwa miradi hii yenye thamani ya Sh. 21.877 bilioni, kinyume na muda ulivyoainishwa kwenye mikataba. Kuchelewa kukamilika kwa

miradi/mikataba kunaweza kusababisha Serikali kuingia ghamra zisizo za lazima zinazotokana na mfumuko wa bei pamoja na kuongezeka kwa ghamra za vifaa.

Ilibainka kuwa Taasisi kumi na nne (14) zilizokaguliwa zilinunua na kupokea bidhaa na huduma zenyet thamani ya Shilingi bilioni. 1.689 bila ya kukaguliwa na kamati zinazohusika na ukaguzi na upokeaji wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa, hii ni kinyume na matakwa Kanuni 244(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Kupokea mali na huduma bila kukaguliwa na kamati kunaweza kutengeneza mianya ya manunuzi ya bidhaa au huduma hafifu.

Taarifa ya kina ya mapungufu haya iko katika **Sura ya Tisa**.

#### **Mapungufu yaliojitokeza katika Usimamizi wa Matumizi**

Sura ya kumi ya taarifa hii inahusu matokeo ya ukaguzi wa fedha za matumizi za Wizara, Idara na Balozi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Baadhi ya Mapungufu ya msingi niliyoyabaini katika ukaguzi huu na ushauri wangu ni kama ifuatavyo: Kuna ubadhirifu wa Shilingi milioni 332.86 uliotoka katika Ubalozi wa Tanzania Nchini Maputo; Matumizi ya Shilingi milioni 61.79 yasio na tija kwa serikali; Hasara ya Shilingi milioni 343.62 iliyotokana na NHIF kutozilipa hospitali zenyet madai ya bima ya afya yenye dosari; Malipo zaidi ya kiasi stahiki ya Shilingi milioni 306.38; Hati za Malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi za Shilingi milioni 243.846, fedha zilizochepushwa kutekeleza shughuli nje madhumuni yaliyokusudiwa za Shilingi milioni 6,810.78.

Pia kuna malipo yasiokuwa na nyaraka za kutosha ya Shilingi milioni 4,508.13; Malipo yasiokuwa na Stakabadhi za Kieletroniki ya Shilingi 1,551.18; Malipo yaliofanyika bila kuzingatia vifungu stahiki ya Shilingi milioni 751.94; Malipo yaliofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa ya Shilingi milioni 3,044.07; Masurufu yasiorejeshwa kwa kipindi kirefu ya Shilingi milioni 135.77; Malipo yasiokuwa na stakabadhi ya Shilingi milioni 2,142.96; Malipo yaliyofanywa bila kutozwa kodi ya zuio ya Shilingi milioni

109.16; Ulipaji wa madeni ya nyuma ambayo hayakwemo kwenye hesabu za mwaka uliopita ya Shilingi milioni 23.18; na Malipo yaliyokopwa kutoka idara moja kwenda nyingine bila kurejeshwa ya Shilingi milioni 2,113.76.

Ni maoni kwamba, mapungufu kwenye usimamizi wa matumizi yanasaababishwa na uwepo wa madhaifu yafuatayo; kutoandaliwa na kuwasiliswa kwa nyaraka kamilifu kwa ajili ya ukaguzi, mapungufu kwenye mfumo wa udhibiti wa ndani (interanal controls) kama vile kutoandaliwa Taarifa za Usuluhihi wa Kibenki, Kutokuwepo Mgawanyo wa Majukumu, na kukosekana kwa udhibiti wa matumizi kwa mujibu wa bajeti na kutosanifiwa vyema kwa mfumo EPICOR unaozingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa Mfumo usio Taslimu (IPSAS accrual) . Maelezo ya kina ya mapungufu haya yapo **Sura ya Kumi**

#### **Mapungufu katika usimamizi wa Mali**

Usimamizi wa mali na utoaji wa ripoti ya mali ni mojawapo ya maeneo yenye changamoto nyingi hasa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa visivyo vya Msingi wa Taslimu (IPSAS accrual) hivyo zinahitaji mikakati thabiti ya kufanya ili kufikia malengo.

Mapitio yangu ya usimamizi wa mali mbalimbali na utoaji wa taarifa ya mali uliofanywa na Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Sekretarieti za mikoa umeonyesha madhaifu kadhaa ikiwa ni pamoja na; kuripoti ardhi na majengo kama kitu kimoja cha mali, mali ambayo haitumuki, mali iliyosajiliwa kwenye rejista bila kuonyesha eneo ilipo, mali isiyo na nambari za utambulisho, mali isiyohamishika isiyo kwenye rejista, taarifa katika rejista haijaboreshwa, na mali zilizoandikwa katika rejista bila kuonyeshwa thamani yake.

Ukaguzi pia ulibainisha makosa ya hesabu kama vile kutokuthaminisha ardhi na mali nyingine, na kutokutambuliwa kwa uchakavu wa mali kwa miaka kadhaa. Matokeo ya kina yameonyeshwa katika **Sura ya Kumi na Moja** ya taarifa hii

## Mapungufu katika usimamizi wa madeni

Nilibaini kiasi kikubwa cha madeni kinachofikia Shilingi trilioni 2.68 kiasi ambacho ni ongezeko la Shilingi trilioni 0.793 sawa na asilimia 36 kulingana na salio la Shilingi trilioni 1.979 kwa mwaka unaoishia 30 Juni 2016.

Pia nilibaini ongezeko kubwa la deni la gharama za matibabu nje ya nchi kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika hospitali za India kutoka kiasi cha Shilingi 28,609,803,615.40 klchoripotiwa tarehe 30 Juni 2017 hadi kiasi cha Shilingi 45,731,070,267.31 kufikia tarehe 31 Desemba, 2017.

Pia, nilibaini Taasisi 10 zilikuwa na kesi zenye madai ya Shilingi 135,598,347,446 na yanashiria maamuzi ya mahakama dhidi ya makampuni na watu binafsi. Maelezo ya kina yako **Sura ya Kumi na Moja** ya taarifa hii.

## Ukaguzi wa Vyama vyा Siasa

Nilikagua taarifa za fedha za vyama vyा siasa na niliona udhaifu mkubwa katika vyama vingi vyा siasa kama vile kutokuwepo kwa mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha; Kwa mwaka huu wa fedha vyama vyा siasa tisa (9) havikuwasilisha kabisa taarifa za fedha za kila mwaka wa ajili ya ukaguzi. Ufanuzi wa kina umeelezewa kwenye **Sura ya 12** ya Ripoti hii.

Kutokana na udhibiti mdogo wa ndani katika vyama hivi, nilibaini vyama vitatu (3) vyा siasa kati ya vyama kumi (10) vilivyokaguliwa villikuwa na malipo yasiyo na viambatisho yaliyofikia kiasi cha Shilingi 735,978,559. Nilibaini kuwa vyama vinne (4) havina regista ya mali za kudumu.

Pia, niliona kwamba usuluhishi kati ya kitabu cha fedha taslimu na mizania ya benki haikufanyika katika vyama vitano (5) vyा siasa. Ufanuzi wa kina umeelezewa kwenye **Sura ya 12** ya Ripoti hii.

## **Ukaguzi Maalum juu ya Ukusanyaji Maduhuli/Mapato na Ununuzi wa Kiwanja Katika Idara ya Uhamiaji**

Ukaguzi ulikuwa na lengo la kuangalia ukweli wa tuhuma zilizotolewa kwa Menejimenti ya Idara ya Uhamiaji kuhusiana na matumizi mabaya ya fedha na ununuzi wa kiwanja Mbeya. Katika uchunguzi maalum umeonyesha kuwa manunuvi ya kiwanja Na. 622 kilichopo Kasumulu katika wilaya ya Kyela mkoani Mbeya gharama zake zilikuwa zimeongezwa kwa Sh 132,365,604.

Nilibaini jumla ya makusanyo kiasi cha Dola za marekani 127,184 sawa na Shilingi milioni 205 hayakupelekwa benki na wahasibu wanne (4) mpaka tarehe 31 Januari, 2013. Ufafanuzi wa kina umeelezewa kwenye **Sura ya 12** ya Ripoti hii.

### **Ukaguzi Maalum wa Chama cha Walimu (CWT)**

Ukaguzi huu maalum ulifanyika kutokana na tuhuma kwa menejimenti juu ya matumizi mabaya ya fedha za Chama cha Walimu.

Uchunguzi wangu ulibaini kwamba menejimenti ya Chama cha Walimu, Bodi ya Wadhamini, na menejimenti ya kampuni ya TDCL wamefanya ubadhilifu wa mali na fedha za Chama cha Walimu kwa kipindi hicho.

Mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani ulichangia sehemu kubwa katika mfumo mbaya wa kuhifadhi kumbukumbu za kutosha wa wanachama, mkanganyiko wa sheria juu ya usimamizi wa mali za Chama chini ya Bodi ya Wadhamini, uwepo wa malipo yenye nyaraka pungufu kiasi cha Shilingi 11,924,250,620.13 na malipo yaliyolipwa nje ya bajeti Sh.26,857,334,119.

zaidi ya hayo, nilibainisha usimamizi usiofaa wa miradi ya Uwekezaji ya Chama cha Walimu hasa Benki ya Walimu (MCBL) na Mwalimu House na pia nilibaini nyaraka zilizogushiwa juu ya uanzishwaji wa kampuni ya Mwalimu (TDCL). Ufafanuzi wa kina umeelezewa kwenye **Sura ya 12** ya Ripoti hii.

## **Ukaguzi Maalum Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

Nilibaini kuwa menejimenti ya NIDA kwa kushirikiana na mwenye nyumba, na kampuni ya Gotham International Limited (GIL) wote walishiriki katika udanganyifu wa fedha za Serikali katika kukodisha jengo la ofisi Shilingi 402,210,885.

Pia, nilibainisha kuwa malipo yalifanywa katika Shilingi za kitanzania kwa viwango vya kubadilishana vilivyoonyeshwa na Mabenki ya Biashara badala ya viwango vya ubadilishaji vilivyoainishwa na zinavyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania Sh.167,445,671.96 na ukaguzi wangu maalum umeonesha malipo mara mbili kwa utoaji wa Huduma za Ushauri kiasi cha Sh. 899,935,494.

## **Ukaguzi Maalum Katika Utekelezaji wa Mradi wa Vituo Vya Polisi vya Mfano Tanzania Chini ya Mpango wa STACA**

Ukaguzi huu maalum unalenga kutoa ukweli kutokana na utekelezaji wa Mpango kazi wa ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Mfano (MPS) na kutoa ripoti juu ya usahihi wa masuala ya kifedha na kuzingatia sheria za ujenzi / ukarabati wa Vituo vya Polisi vya Mfano.

Masuala makuu yaliyotajwa katika ukaguzi huu ni udhaifu juu ya mfumo wa udhibiti wa ndani uliosababisha, Wafadhili wa DFID kusitisha utoaji wa Paundi za Uingereza (GBP) 320,000 kutokana na Menejimenti ya Polisi kushindwa kuzingatia makubaliano (MoU) na kutokumaliza ujenzi wa vituo vilivyojengwa katika mikoa mbalimbali

### **Masuala mengine yaliyojitokeza yamefupishwa kama ifuatavyo:-**

Nilibaini matumizi juu ya kiasi kilichopangwa kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Mfano Sh. 365,756,625 tangu 2012-2015. Jumla ya Sh.1,052,020,000 zilipangwa kwa Vituo vya Polisi vya Mfano thelathini na tano (35) lakini vibanda kumi na sita tu (16) vilikarabatiwa/ kujengwa kwa gharama ambazo zilizidi fedha zilizoidhinishwa kwa Shilingi 365,756,625 na kuacha vituo kumi na tisa (19) ambavyo havikujengwa, kati ya vituo vilivyokarabatiwa/ jengwa vituo sita (6) havikukamilika ina

maana kuwa kutakuwa na fedha zaidi zinazohitajika ili kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo.

Pia, kinyume na kanuni 73 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma 2013 nilibainisha kugawanywa kwa makusudi kazi za ujenzi zilizotolewa kwa M/s Posh Alliance Ltd katika Kituo cha Polisi cha Lushoto zenyeharama ya Shilingi 515,233,760

#### **Ukaguzi Maalum wa Fedha za Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT)**

Ukaguzi ulikuwa na lengo la kujua ukweli juu ya madai kuhusu kuweka fedha za ALAT kwenye akaunti binafsi na wafanyakazi kufanya kazi bila mikataba kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2017

Nilibaini kuwa menejimenti ya ALAT ilitumia fedha kiasi cha Shilingi 284,599,600 kwa matumizi ya kawaida bila kupata kibali kutoka Mkutano Mkuu wa Mwaka. Mbali na hilo jumla ya Sh. 3,769,667,891.27 zililipwa kwa shughuli mbalimbali bila kuwa na viambatisho stahiki na pia kulikuwa na nyaraka na miamala ya benki iliyogushiwa.

Nilibaini kuwa fedha za ALAT zimebekwa kwenye akaunti ya binafsi ya M/S Vision Investment kiasi cha Shilingi 150,000,000 bila kibali kutoka kwa menejimenti

Menejimenti ya ALAT imeshindwa kuwasilisha viambatanisho vya malipo yenye thamani ya Sh.3,567,766,421,72. zaidi ya hayo, nilibaini udanganyifu kwa malipo ya TZS 76,666,835 na makusanyo ya mapato mbayo hayakupelekwa benki ya TZS 14,330,000. Tazama zaidi kwenye **Sura ya 12** ya Ripoti hii.

#### **Ukaguzi Maalum juu ya Ujenzi wa Mtando wa Usambazaji Umeme kwa ajili ya Mradi wa Mtwara (MEP)**

Ukaguzi huu maalum una lengo la kuhakiki uhalali na usahihi wa gharama za kurejesha zilizotumika wakati wa ujenzi wa mtando wa usambazaji umeme Mtwara (MEP).

Mapungufu yaliyojitokeza katika usimamizi wa mikataba yalipelekea M/S Wentworth Gas Limited pamoja na kampuni zake

ndogo (M/S Umoja Light Company) kufanya kazi zake bila kuzingatia masharti ya mikataba ya Tariff Equalisation Fund na MICRA, pia ununuzi wa mitambo ya umeme ulifanyika bila kumshirikisha Mthamini Mkuu wa Serikali.

zaidi ya hayo, Ukaguzi wangu maalum unahitimisha kwamba Serikali inapaswa kurejeshewa kutoka kwa Kampuni ya Wentworth Gas Limited (Umoja Light Co Ltd) kiasi cha Dola za Marekani 8,426,819.33 kati ya madai yanayodaiwa ya Dola za Marekani 8,121,058. Kwa maelezo ya kina ya kaguzi hizi, **tazama Sura ya Kumi na Mbili ya Ripoti hii.**

### **Ukaguzi wa CCM**

Katika ukaguzi huu nilibaini Chama cha Mapinduzi (CCM) kilitoa Mikopo ya Maendeleo kwa makampuni isiyo na faida, mikopo ya maendeleo haikuwa na viambatisho vya kutosha na mikopo iliyotolewa hajarejeshwa. Tazama **Sura ya Kumi na Mbili**

### **Mapendekezo ya Ujumla ya ukaguzi**

Ili kuwa na Uwazi, Uwajibikaji, Utawala Bora, Usimamizi na kufuata sheria na kanuni ambazo hatimaye huhakikisha matumizi bora ya rasilimali za Umma, inakuwa muhimu sana kutekeleza mapendekezo ya CAG na maelekezo ya PAC na hivyo kufanya jukumu la CAG na uwajibikaji kwa PAC kuwa na maana.

Katika kuitia utekelezaji wa katika mapendekezo yangu ya mwaka uliopita na maagizo ya PAC, nimebainisha kuwa kuna maboresho kwa kutekeleza mapendekezo yangu na maagizo yaliyotolewa na PAC. Hata hivyo, mapendekezo mengi na maagizo bado yapo katika hatua ya utekelezaji.

Ninawahimiza Maafisa Masuuli kuhakikisha maagizo yaliyo katika hatua ya utekelezaji yanatekelezwa kikamilifu. Vivyo hivyo jitihada nyingi zinahitajika ili kuhakikisha mapendekezo na maelekezo yote yanatekelezwa.

Kwa hiyo, ninawashauri Maafisa Masuuli kubora kitengo cha kujibu na kufuatili utekelezaji wa hoja za ukaguzi. Hii iendane na

kuimarisha kwa mifumo ya Udhibiti wa Ndani ambayo ni sababu inayochangia madhaifu katika usimamizi.

Serikali inahimizwa kuchunguza vyanzo vingine vya ndani vya mapato au kutafuta njia bora ya kutumia, ushirikiano wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kama njia ya kuhamisha baadhi ya majukumu ya sekta binafsi na kupunguza gharama ya uendeshaji wa bajeti kwa kutumia mikopo na Misaada. Shughuli nyingi za maendeleo zinapaswa kufanyika kwa ushirikiano wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya Umma ambayo itasababisha upatikanaji wa kazi kwa urahisi na ubora; na itasaidia kuongeza kiwango cha maisha ya wananchi na kutengeneza fursa nyingi za ajira.

Naishauri Serikali ihakikishe mamlaka za rufaa za kodi zina idadi kamili ya makamu wenyeviti na wajumbe itayowezesha mamlaka hizo kufanya vikao vya kutosha ili kuendana na wingi wa kesi za kodi. Pia Serikali iongeze wafanyakazi wenyewe uwezo, uzoefu na weledi wa kutosha ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato kushughulikia mapingamizi ya kodi kwa wakati. Kadhalika Serikali iongeze ukaguzi na udhibiti wa bidhaa za mafuta zinazoingia kwa matumizi ya hapa nchini, zinazotumika migodini na zinazokwenda nchi nyingine ili kuhakikisha kuwa hazitumiki bila kulipa kodi stahiki. Madeni ya kodi pia yanatakiwa kukusanya kwa wakati ili kuiongezea serikali mapato, kwa upande wa ada na tozo zinazokusanya na Mamlaka kwa niaba ya taasisi nyingine, ni vema ada na tozo hizo zikawalishwa kwa wakati kwenda kwa taasisi husika.

### **Tathmini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani na Utawala Bora**

Katika Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Utawala Bora nilizingatia katika Tathmini ya Kamati za Ukaguzi, Kazi za Ukaguzi wa Ndani, mchakato wa Udhibiti wa Vihatarishi, TEHAMA, uhakiki wa kutambua udanganyifu na kuzuia udanganyifu, changamoto katika utekelezaji wa sheria za kunyanganya na kurejesha pamoja na masuala ya Utawala Bora . Kuna mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini zote kwa maelezo zaidi rejea sura ya sita.

Ninashauri Serikali kuendelea kufuatilia na kuboresha mfumo wa Udhibiti wa Ndani kwa kuja na utaratibu wa udhibiti ambao unasaidia ufanisi na ilikupunguza mapungufu ambayo hujitokeza.

Ninazishauri menejimenti za MDA kuweka udhibiti madhubuti wa kuangalia vikwazo hivi katika mfumo wa udhibiti wa ndani na kuhakikisha kuwa hali hiyo inakaa sawa.

Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi zimeendelea kuwa na udhaifu katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara, udhaifu ulioendelea kujitokeza ni kama - mapungufu katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za watumishi na mishahara, mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao hawapo katika utumishi wa umma, kushindwa kufanya tathmini na upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi, kuchelewesha kuwasilisha kwa makato ya kisheria kwenye mifuko ya pensheni, watumishi kupokea mishahara chini ya kiwango kilichokubalika na idadi kubwa ya ukosefu wa watumishi katika Taasisi nyingi na mikutano ya kisheria ya watumishi kutokufanyika.

Kwahiyu napendekeza Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menijimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kuhakikisha dosari zote zilizoonekana katika ripoti hii zinatafutiwa ufumbuzi na zoezi la usafishaji na uboreshaji wa taarifa za watumishi katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za watumishi linakuwa zoezi endelevu katika Taasisi zote. Vile vile Kanuni na Sheria lazima zizingatiwe katika kuongoza na kusimamia rasilimali watu.

Nashauri Wakala za Serikali kuboresha utoaji wa huduma zao, kuangalia upya tozo wanazotoza katika huduma zao, kutumia njia mpya za kisasa za kibiashara katika utoaji wa huduma na kubuni njia mpya za kuongeza mapato yao ili Wakala hizi ziweze kuijendesha na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

Nasisitiza kwa Watendaji wakuu wote wa Serikali kutekeleza shughuli zao kulingana na kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2013, Sheria ya Fedha ya Umma 2001 (iliyorejewa 2004) pamoja na

Sheria za kodi, pamoja na kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani ilikudhibiti mapungufu yaliojitokeza.

Nazishauri Wakala na Taasisi zote za Serikali kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kilipa Madeni ya Serikali kuzuia kulipa adhabu zinazotokana na madeni hayo.

#### **Nashauri menejimenti ya kila Taasisi ya Umma;**

Kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 35 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, nashauri menejimenti za Taasisi husika zizingatie kikamilifu ushiriki wa Bodi ya Zabuni katika kuidhinisha manunuzi ili kuepuka manunuzi yasiyo kuwa na tija au mikataba isiyo tekelezeka

Kuhakikisha inazingatia Kanuni ya 114 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 na kusimamia kikamilifu mikataba inayoendelea ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati bila kuchelewa.

Nashauri kwamba menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu zijitahidi kufuatilia uletwaji wa vifaa vyote. Na inaposhindikana zihakikishe fedha zilizolipwa zinarejeshwa kutoka kwa Wazabuni na Wakandarasi, na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale walioshindwa kuleta vifaa na huduma.

Ziendelee kufanya juhudhi za ufuatiliaji rasilimali fedha kutoka Hazina ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa katika bajeti

miradi yenye fedha kidogo itekelezwe kwa hatua ili kurahisisha usimamizi wa miradi na ulipaji wake

Vile vile, zihakikishe hakuna cheti cha malipo kwa kazi iliyothibitika kuwa imekamilika kinachobakia bila kulipwa.

#### **Nashauri uongozi wa Taasisi za Serikali kuu;**

Kubadilisha mtazamo katika kusimamia miradi na mikataba mbalimbali kwa kuangalia mashariti yaliyomo katika mikataba na kuangalia na kusimamia utekelezaji wake ipasavyo.

Kutambua kuwa TBA ni Taasisi ya Umma ila imepewe uwezo wa kujenga majengo ya Serikali, lakini siyo kwamba yenewewe

imeruhusiwa kutozingatia mashariti yanayowekwa katika mikataba iliyosainiwa au kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013.

Ninawahimiza Maafisa Masuhuri Wizara, Idara na Balozi kuendelea kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani wa taaasis zao ikiwa ni pamoja na kujewanga uwezo watumishi wao. Mbali na hayo, nyaraka zinapaswa kuboreshwa na kufuata kanuni za kifedha zilizowekwa.

Ninashauri kuwa Mhasibu Mkuu kwa kushirikiana na menejimenti za Wizara, Idara pamoja na benki Kuu kuondokana na vikwazo vilivyomo ambavyo vinazuia Wahasibu Mkuu wa Wizara na katibu Tawala kuwa na uwezo wa kuzipata taarifa zao benki za akaunti zao jambao hili linapelekea ugumu kwao kufanya upatanisho wa benki.

Ninapendekeza Serikali kuwa na mipango mazuri ya mafunzo ilioandaliwa mahsusini kwa kuwapa mafunzo wafanyakazi wanaofanya kazi ya usimamizi wa Mali za Kudumu, kutafakari upya taratibu za usimamizi wa Mali za Kudumu na kufanya kazi kwa moduli ya Mali za Kudumu iliyopo katika mfumo wa EPICOR-IFMS.

Ninapendekeza kwa Menegimenti za taasisi mbalimbali kuchukua hatua muhimu ili kusimamia kwa ufanisi madeni na kuhakikisha yanalipwa kwa ukamilifu, hasa madeni ya matibabu.

Naishauri Serikali ihamasishe kila taasisi yake iwe na mikakati thabiti ya usimamizi wa madeni kulingana na mazingira yao kwa ajili ya kuhakikisha hatari zilizopo katika taasisi zao zinajumuishwa na kupunguzwa mpaka kufikia kiwango cha kudhibitiwa.

Kuhusiana na madeni ya matibabu ya nje ya nchi naishauri Serikali ifanye yafuatayo: (i) ije na Mpango Mkakati wa kina katika Sekta ya Afya ili kujijengea uwezo wa matibabu kwa Watanzania ndani ya Nchi ili kuhudumia idadi kubwa ya watu na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni; Ishirikiane na wadau

wote kuhamasisha ukusanywaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na mahitaji ya wafanyakazi.

Naishauri menejimenti za Vyama vya Siasa zihakikishe inazingatia Miongozo ya fedha ili kuhamasisha ushindani na uwazi katika manunuzi kwa ajili ya kupata thamani ya fedha ya bidhaa au huduma inayonunuliwa.

Menejimenti ya Vyama vya Siasa ihakikishe kuwa inaweka utaratibu wa kufanya usuluhishi wa kibenki na maafisa husika wanapitia vizuri na kuhakiki miamala ya benki na vitabu vya hesabu ili kurekebisha makosa katika hatua za mwanzo.

Namkumbusha Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kushirikiana na wadau wa vyama vya siasa kukamilisha kuandaa muundo wa uandaaji wa hesabu za vyama. Kuwa na mfumo mmoja wa muundo wa uandaaji hesabu utakaopelekea kuwa na muendelezo unaofanana na usawa kwa kuandika miamala na maandalizi ya uandaaji wa hesabu za vyama.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA AWALI

### 1.1 Utangulizi

Kama nilivytangulia kusema katika muhtasari, ripoti hii inatoa maelezo ya kina ya matokeo ya ukaguzi, mapendekezo na hitimisho kutokana na ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu<sup>2</sup> kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2017. Ripoti hii inatoa pia matokeo ya kaguzi maalum zilizofanyika katika mwaka 2016/17. Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 143(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005.

### 1.2 Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya kaguzi hizi ni kuweza kutoa maoni huru ya ukaguzi kwamba hesabu kwa ujumla wake na nyaraka zilizotumika wakati wa kuziandaa hazikuwa na makosa makubwa ambayo yanatokana na udanganyifu au makosa wakati wa maandalizi na iwapo ziliandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya uhasibu visivyo vya Misingi ya Taslimu pia iwapo Sheria nyingine pamoja na Kanuni zake zinazohitajika wakati wa kuandaa hesabu zilifuatwa.

### 1.3 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyikwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Asasi Kuu za Ukaguzi na taratibu nyingine kama zilivyoonekana zinafaa kutokana na mazingira.

Katika ukaguzi wa mwaka 2016/17, Jumla ya taasisi 241 za Serikali Kuu zilikaguliwa na kutolewa taarifa kati ya taasisi 256 zilizotakiwa kukaguliwa kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini;

<sup>2</sup> Serikali Kuu inajumuisha Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali, Sekretariati za Mikoa, Balozi, Mifuko, Mabonde ya Maji, Vyama vya Siasa na Taasisi nyingine zinazoangukia Serikali Kuu

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa taasisi za Serikali Kuu  
zilizokaguliwa**

SN	Taasisi	Jumla ya Taasisi	Maoni
1	Wizara	65	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ikjumuisha Mamlaka ya Mapato (Matumizi) na TRA (Mapato) na Taarifa Jumuifu za Serikali.</li> <li>➤ Fungu 11 - Tume ya Ushauri Gesi na Mafuta ambayo ilianzishwa na kuripotiwa katika kipindi hiki.</li> </ul>
2	Wakala wa Serikali	35	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kati ya wakala 37, wakala 35 zilikaguliwa ambapo wakala wawili taarifa zao zimejumuishwa kwenye ripoti ya jumla ya mashirika ya umma<sup>3</sup>.</li> <li>➤ Kama ilivyokuwa katika kipindi cha nyuma, Mamlaka ya Kuendeleza Kigamboni haikuwasilisha hesabu zake hivyo haikukaguliwa.</li> <li>➤ Wakala wa Ukaguzi wa Migodi ilifungwa katika mwaka wa ukaguzi.</li> </ul>
3	Balozi	39	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Balozi saba zilifunguliwa katika mwaka huu wa ukaguzi na kufanya jumla ya balozi kufika 41;</li> <li>➤ Kati ya balozi saba, balozi tano zilikaguliwa ila ni ubalozi mmoja tu uliweza kupewa hati. Nyingine nne zilikaguliwa tu kwa kuangalia tu mfumo wa ndani. Hazikuweza kuandaa hesabu maana hazikua na mhasibu kulikua na balozi peke yake.</li> <li>➤ Balozi mbili hazikukaguliwa kabisa kwa sababu ndio tu zilikuwa zimeanza kufanya kazi.</li> </ul>
4	Sekretariati za Mikoa	26	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Sekretariati za Mikoa zote zilikaguliwa</li> </ul>
5	Mifuko	17	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Ukaguzi wa Mifuko miwili ulikua unaendelea wakati wa uandaaji wa ripoti hii.<sup>4</sup></li> </ul>
6	Vyama vyaa Siasa	10	<ul style="list-style-type: none"> <li>➤ Kati ya vyama 19 vyaa Siasa, 9 havikukaguliwa kwa sababu</li> </ul>

Sura ya Kwanza

<sup>3</sup> Tume ya Taifa ya Takwimu na Wakala wa Chakula na Dawa wa Taifa

<sup>4</sup> Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mfuko wa Huduma za Afya

			hawakuandaa hesabu zake na kuziwasilisha kwa ukaguzi <sup>5</sup>
7	Mabonde ya Maji	9	➤ Mabonde ya Maji yote yalikaguliwa
8	Mamlaka za Maji safi na Maji taka	4	➤ Zote zilikaguliwa
9	Taasisi Nyingine	38	
<b>JUMLA</b>		243**	

Jumla ya kaguzi maalum sita zilifanyika katika mwaka husika wa ukaguzi zilizoombwa na wadau mbali mbali kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini. Matokeo ya kaguzi hizi yanapatikana katika **Sura ya Kumi na Mbili ya ripoti hii.**

#### **Jedwali Na. 3: Kaguzi maalum zilizoombwa katika mwaka husika**

<b>Na.</b>	<b>Ukaguzi Maalum</b>	<b>Aliyeomba</b>	<b>Maelezo</b>
1	Chama cha Serikali za Mitaa	Mwenyekiti wa ALAT	Umekamilika
2	Ukaguzi maalum kwenye ukusanyaji wa mapato na ununuazi wa vitalu (Idara ya Uhamiaji)	Wizara ya Mambo ya Ndani	Umekamilika
3	Uhakiki wa madai yaliyotolewa na Wentworth Gas Limited juu ya ujenzi wa mtandao wa maambukizi na usambazaji wa Mradi wa Nishati ya Mtwara (Umoja Light Company)	Wizara ya Nishati na Madini	Umekamilika
4	Ukaguzi maalum juu ya utekelezaji wa vituo vya polisi vya Mfano (MPS) ndani ya Jeshi la Polisi la Tanzania chini ya mpango wa STACA (Jeshi la Polisi la Tanzania)	STACA-PCO	Umekamilika
5	Ukaguzi maalum wa Umoja wa Walimu wa Tanzania (CWT)	Ofisi ya Rais Ikulu	Umekamilika
6	Ukaguzi maalum katika Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (NIDA)	Mamlaka ya Uchunguzi	Umekamilika

<sup>5</sup> 1). TADEA, 2). NCCR MAGEUZI, 3). UDP, 4). CUF, 5). APPT, 6). ACT Wazalendo, 7). NRA, 8). UPDP and 9). CHAUMA

\*\* Wakala wawili wa Serikali wameripotiwa kwenye Ripoti ya Mashirika ya Umma

Ripoti hii inajumuisha ukaguzi wa awali wa mafaili ya wastaafu ambapo mafaili 3,694 yalifanyiwa ukaguzi wa awali. Matokeo ya ukaguzi huo yanapatikana katika sura ya tano ya ripoti hii.

Katika ngazi ya taasisi, ukaguzi ulifanyika kwa sampuli; hivyo matokeo ya ukaguzi yalikuwa ni kutokana na nyaraka zilizopitiwa na maelezo yaliyoombwa na kutolewa kwa ukaguzi.

Ukaguzi ulipangwa kufanyika kwa kufuata njia ambayo itatoa uhakika pasipo shaka, kama kungekua na makosa makubwa au hesabu zingekuwa zimekosewa kwa sehemu kubwa ikijumuisha udanganyifu au makosa ya kutokukusudia yangeonekana. Ni jukumu la menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu kugundua na kuzuia makosa mbalimbali ikiwamo udanganyifu na kutengeneza mfumo wa ndani madhubuti katika sehemu zao za kazi.

Ripoti hii inajumuisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo kutoka katika maeneo yafuatayo;

- a) Tathimini ya mifumo ya ndani ya taasisi;
- b) Maandalizi ya bajeti na utekelezaji wake;
- c) Menejimenti ya rasilimali watu na usimamizi wa mishahara;
- d) Manunuzi na utunzaji wa Mikataba;
- e) Usimamizi wa Matumizi;
- f) Usimamizi wa Mali za Kudumu na Madeni;
- g) Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma na maelekezo ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali Kuu;
- h) Kupima ufanisi wa wakala wa Serikali, Taasisi nyingine, Mifuko na Bodi za Mabonde ya Maji.

#### **1.4 Mchakato wa Ukaguzi**

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa mwanachama wa asasi za kitaaluma; INTOSAI<sup>6</sup>, AFROSAI na AFROSAI - E; inatumia viwango na miongozo inayotolewa na asasi

<sup>6</sup> Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi; ushirikiano duniani kote wa vyombo vya serikali na Umoja wa Mataifa

hizi. INTOSAI inatoa viwango vya wakaguzi wa nje (ISSAI)<sup>7</sup> kwa ajili ya sekta za Umma na Umoja wa Mataifa. Viwango hivi vinamtaka mkaguzi kufuata uadilifu katika kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata uhakika pasipo shaka kwamba hesabu zilizokaguliwa hazina makosa makubwa yanayotokana na udanganyifu au makosa ya kutokukusudia.

Hivyo basi, ukaguzi ulipangwa na kufanyika kwa uhakika. Ukaguzi wa Hesabu ulijumuisha; kutekeleza taratibu za tathmini ya kutambua maeneo ya hatari kama sehemu ya mchakato wa mpango wa ukaguzi. Kupata ushahidi sahihi wa kutosha kwamba hakuna makosa makubwa kwa kupanga na kutekeleza matokeo ya tathimini ya maeneo ya hatari yaliyotambuliwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya miaka ya nyuma na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali na kuhakikisha hatua stahiki zimechukuliwa.

### **1.5 Mchakato wa Kuripoti**

Mchakato wa ukaguzi unatumia mbinu shirikishi, ambapo taasisi inayokaguliwa inashirikishwa kikamilifu katika mchakato. Inajumuisha Afisa Masuuli, viongozi waandamizi, Kamati ya Ukaguzi na kitengo cha Mkaguzi wa Ndani, maana tunaamini viongozi waliokasimiwa madaraka wana nafasi nzuri ya kutueleza iwapo hesabu zilizoandaliwa ni sahihi na nyaraka nyingine zilizotolewa kwa ajili ya ukaguzi zimezingatia Sheria na Kanuni.

Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yamezingatia; vigezo vilivyowekwa au mazoea bora, athari na mapendekezo ya maboresho ya baadaye kwa menejimenti yametolewa kuititia barua za udhaifu kwa menejimenti. Pia tumetoa hati za ukaguzi zinazojumuisha matokeo ya nyenzo kwenye hesabu zilizokaguliwa, pamoja na mapungufu makubwa yaliyoonekana katika udhibiti wa ndani.

Kama inavyotakiwa na Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

<sup>7</sup> Viwango vya Kimataifa vya Asasi Kuu za Ukaguzi

Serikali anapeleka kwa Rais kila ripoti anayoiandaa kufuatia maelezo ya ibara ndogo ya (2) ya ibara tajwa. Pia Kanunii ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inaelezea kuwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawasilisha ripoti yake ya jumla kwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka ambayo itapelekwa Bungeni kupitia Waziri mwenye dhamana (Waziri wa Fedha na Mipango). Kwa hiyo ripoti hii ya jumla inafanya msingi wa hitaji hili.

### **1.6 Msingi wa maandalizi ya Hesabu**

Fungu A2 na A3<sup>8</sup> la Viwango vya Kimataifa ya Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) 1210 limeweka mahitaji ya ukaguzi yanayokubalika (masharti ya awali ya ukaguzi - mfumo unaokubalika wa taarifa za fedha). Hivi ndivyo vipaumbele vya maandalizi ya Hesabu kwa menejimenti na ndivyo vigezo anavyotumia mkaguzi kukagua na kutoa hati ya ukaguzi. Bila kuwepo kwa vigezo vinavyokubalika kuandaa hesabu, menejimenti haitakua na msingi mahsusini wa maandalizi ya hesabu na wakaguzi hawatakuwa vigezo mahsusini vya kukagua hesabu.

Fungu la 7 la Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inamtaka Mhasibu Mkuu kutoa maagizo kuhusiana na misingi ya uhasibu itakayotumika na uainishaji utakaotumika kuandaa Hesabu. Pia, Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma kinataka Hesabu zote zilizoandaliwa na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ziandaliwe kwa kuzingatia Misingi ya Jumla ya Kihasibu iliyokubalika pamoja na maagizo mengine yaliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kuthibitishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha; yakieleza misingi itakayotumika kuandaa Hesabu na kutambua kama kuna ikikuwaji na sababu ya kukiuka.

Serikali Kuu ilihamia kwenye Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu visivyo vya Misingi ya Taslimu kama misingi ya kuandaa Hesabu zake rasmi kuanzia Julai 1, 2012 na kupita katika kipindi cha

<sup>8</sup> Maombi na vifaa vingine vya maelezo

mpito kama kinavyotolewa na viwango husika; hivyo mwaka huu imemaliza kipindi cha mpito kimekwisha na wameanza kuandaa Hesabu kwa kufuata viwango hivyo kwa ukamilifu katika mwaka wa fedha 2016/17. Hesabu zote zimeandaliwa kwa katika msingi endelevu; hata hivyo kuna mapungufu mengi yamejitekeza kwa baadhi ya Taasisi katika matumizi ya sera za kihasibu hasa katika kutolea taarifa mali za kudumu na mitambo. Serikali ilichagua kutumia modali ya gharama halisi wakati baadhi ya Taasisi zimetumia mtindo wa kurekebisha thamani ya mali na mitambo ambazo zina madhara kwenye kuandaa hesabu jumuifu za Taifa.

### **1.7 Kuwasilisha Hesabu**

Kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebishwa 2004) na Kanuni ya 71 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, 2009 inamtaka Afisa Masuuli kutengeneza Hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha husika kuisha.

Tunaipongeza Serikali kwa jitihada zake za dhati zilizowezesha kuandaa na kuwasilisha hesabu zilizokidhi vigezo vyta viwango vyta kimataifa vyta kuandaa hesabu za umma visivyo vyta misingi ya taslimu. Viwango vyta uhasibu visivyo vyta misingi ya taslimu vinaitaka taasisi kutambua matumizi pale yanapotumika na maduhuli pale yanapopatikana sio lazima pale hela inapolipwa au inapopokelewa. Pia inataka kuonesha kwa ukamilifu thamani ya mali za kudumu, kama vile vifaa na mitambo, na madeni kama madeni ya watumishi ambayo hayakuweka kama sehemu ya hesabu hapo kabla.

Licha ya mafanikio yaliyofikiwa na Serikali ya kutoa hesabu zilizozingatia kwa ukamilifu viwango vyta kimataifa vyta uhasibu visivyo vyta misingi ya taslimu, viwango vyta uzinngatiaji vinatofautiana baina ya taasisi moja na nyingine. Kumekuwapo changamoto katika kutambua, kupima na kuonesha mali za kudumu za Serikali kama ifuatavyo;

- a) Uchakavu wa mali za kudumu kwa mwaka, uchakavu wa mali zisizoshikika na hasara ya kushuka kwa thamani ya mali (Kila taasisi inatakiwa kufanya tathimini ya uchakavu huo na kuona kama kuna viashiria nya mali za kudumu kushuka thamani) pamoja limbikizo la uchavu na limbikizo la kushuka kwa thamani ya mali hazikutolewa taarifa ingawa mali hizo za kudumu zipo tangu mwaka 2012 hadi sasa.
- b) Mali zote zisizo za muda mfupi zilifanyiwa uchakavu kama vile zilinunuliwa mwaka 2012 wakati zilikuwepo kabla ya hapo.
- c) Baadhi ya taasisi zina mali za kudumu ambazo hazitumiki kwa kuwa zimeharibika kupitiliza lakini hazikufanyiwa tathimini ya kushuka kwa thamani ya mali kama inavyotakiwa na IPSAS 17 na 21 badala yake zimeripotiwa katika thamani yake ya awali kutoka mwaka 2012/13 hadi 2016/17 na zimeoneshwa kwa thamani yake ya kwenye vitabu.
- d) Kulikuwa na maoni tofauti juu ya matumizi ya Para 42 ya IPSAS 17 (Jinsi ya utambuzi wa awali na kupima mali za kudumu za Serikali). Kulingana na sera ya Serikali, imechagua mtindo wa għarama kama sera yake ya uhasibu; hata hivyo, baadhi ya vyombo vimetumia mfumo wa kurekebisha ambayo ilipingana na sera ya Serikali. Baadhi ya Taasisi zimekuja na thamani mpya ya mali zao hata zile zilizoripotiwa kwa għarama wakati wa maandalizi ya Utangulizi wa Ufunguzi wa mizania ya hesabu na nyongeza zao baadae mnamo Juni 30, 2017 na bado kuchukuliwa kwa thamani mpya kama hesabu ambayo kwa kweli ilikuwa uhakiki kama uamuzi uliosababisha ziada ya upungufu / upungufu. Għarama zilizohesabiwa zimewekwa kama tarehe 30 Juni 2017 hata mali zilizo na għarama za awali na zile zilizopatikana kwa għarama ndogo ikilinganishwa na għarama halisi ilipaswa kupimwa kwa thamani ya halisi wakati wa ununu.
- e) Thamani za mali za kudumu zinatofautiana kati ya thamani zilizoandikwa kwenye daftari la mali za kudumu na zilizooneshwa kwenye hesabu.

Changamoto hizi zimesababisha kuwepo na mijadala mirefu kati ya wakaguzi na wakaguliwa ambapo taasisi nyingi zilibadilisha hesabu zao ambazo tayari zilikua zimeshawasilishwa. Hesabu zilizorekebishwa ziliwasilishwa tena tarehe 6 Februari 2018 na bado baadhi na Wizara, Idara za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Wakala wa Serikali zilishindwa kuwasilisha hesabu zao zilizorekebishwa hivyo kusababisha kupata hati zenye mashaka.

## **Ufanisi katika utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya uhasibu visivyo vya misingi ya taslimu**

Wakati tukipongeza kazi kubwa iliyofanyika na mafanikio yaliyofikiwa ya kuzalisha hesabu zilizotengenezwa kwa viwango vya IPSAS; uwekezaji wa ziada unachukuliwa kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu ya kutosha kwa utekelezaji wa ufanisi wa mfumo wa IPSAS. Uwekezaji unapaswa kuzingatia zaidi kuwa na; mfumo jumuishi wa usimamizi wa fedha (ERP) unaounga mkono kikamilifu ujuzi wa IPSAS, kuimarisha ujuzi wa usimamizi wa kifedha na uwezo, kuunganisha sera za uhasibu kwa kufuata mahitaji ya ziada ya IPSAS na marekebisho ya sheria na kanuni ambazo zina athari ya moja kwa moja juu ya utekelezaji wa msingi wa malipo ya IPSAS.

Tunakumbuka kuwa, serikali sasa inatumia mfumo wa uhasibu wa Epicor ambayo ina uwezo wa kuunganishwa na programu nyingine, lakini kwa sasa; mfumo huo hauwezi kuunga mkono kikamilifu utekelezaji wa IPSAS. Kwa mfano; Epicor ina moduli ya mali za kudumu lakini haifanyi kazi matokeo hakuna njia thabiti ya kurekodi mali za kudumu na kusimamia mienendo yake; moduli ya madeni pia haifanyi kazi. Moduli ya usimamizi wa manunuvi (moduli ya ununuvi) haitumiwi kikamilifu kama inaruhusu tu utaratibu wa malipo, taratibu zote za manunuvi hazifanyiki kwenye mfumo.

Vile vile, Serikali inatumia Mfumo wa malipo wa kibenki (TISS), japo kuwa huo mfumo haujaunganishwa na mfumo wa malipo (Epicor) matokeo yake Taasisi haziwezi kufanya usuluhisho wa hesabu.

Menejimenti inapaswa kuchunguza ufanisi wa mfumo wa Epicor ili kuweza kufikia mahitaji ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu za umma (IPSAS) na pia kwa kuzingatia vigezo vya nje ambavyo zinaathiri ufanisi. Kwa mfano ukuwaji wa haraka wa teknolojia katika sekta za kibenki ambao unahitaji mfumo wa kihasibu kuunganishwa moja kwa moja na mfumo wa kibenki.

## SURA YA PILI

### 2.0 HATI ZA UKAGUZI

#### 2.1 Utangulizi

Kama ilivyoelezwa katika sura zilizopita, madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kupata uhakika kama Taarifa za Fedha kwa ujumla ni huru kutokana na kukosewa au udanganyifu na kutoa ripoti ya ukaguzi ambayo itakuwa na hati ya ukaguzi. Nimefanya ukaguzi wangu kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma (ISSAIs). Ninatoa uhakika wa hali ya juu lakini sio dhamana kuwa ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia viwango hivyo utatambua mapungufu yote yaliyopo. Mapungufu yanaweza kutokana na makosa au udanganyifu na yanaonekana kuwa makubwa kama likiwa moja au ukiyakusanya kwa ujumla wake yanaweza kuathiri maamuzi ya kiuchumi ya watumiaji wa taarifa za fedha.

Ninaamini kuwa ushahidi wa ukaguzi nilioupata ni wa uhakika na wakutosha kuweza kupata msingi wa kutoa maoni. Katika utoaji wa hati za ukaguzi nilikuwa huru kwa Taasisi zilizokaguliwa kama inavyotakiwa na Bodi ya Kimataifa ya Maadili kwa Kanuni za Maadili ya Wahasibu (Kanuni ya IESBA) pamoja na mahitaji ya kimaadili ambayo yanafaa kwa ukaguzi wangu wa taarifa za Fedha nchini Tanzania.

Kati ya kaguzi 243 zilizofanyika mwaka huu (hati 2 zimejumuishwa katika ripoti za Mashirika ya Umma), zifuatazo ni aina za hati zilizotolewa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma namba 1700<sup>9</sup> na 1705<sup>10</sup>

---

<sup>9</sup> Kutoa hati na kuripoti taarifa za fedha

<sup>10</sup> Marekebisho ya maoni katika ripoti ya mkaguzi

## 2.2 Aina na misingi ya hati za ukaguzi

### 2.2.1 Hati inayoridhisha

Hii inatokea pale mkaguzi anahitimisha kuwa taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa uandaaji wa hesabu<sup>11</sup>. Hii inamaanisha kuwa taarifa za fedha ni huru na hazina makosa au udanganyifu, japo kutolewa kwa hati inayoridhisha hakutoi uhakika wa asilimia mia kuwa Taasisi ni fanisi na fasaha katika mifumo yake ya ndani ila inaamanisha kuwa hakuna chochote alichokiona mkaguzi ambacho angeweza kutoa hati yenye mashaka.

### 2.2.2 Hati yenye shaka

Hii ni hati ambayo mkaguzi anahitimisha kuwa taarifa za fedha zinamakosa makubwa lakini makosa hayo sio muhimu<sup>12</sup>. Hii inamaanisha kuwa, kuna kikwazo au kutokubaliana kwenye eneo fulani lakini sehemu nyingine za taarifa za fedha zinaonyesha ukweli na uhalisia.

### 2.2.3 Hati isiyoridhisha

Hii ni hati ambayo mkaguzi anahitimisha kuwa makosa ambayo aidha moja moja au kwa ujumla wake ni makubwa na ya muhimu<sup>13</sup>. Hii inamaanisha kuwa kutokukubaliana na menejimenti kutokana na mapungufu ya kutokuonyesha njia sahihi za kihasibu zinazoathiri ripoti za fedha.

### 2.2.4 Hati mbaya

Hii ni hati ambayo mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi sahihi na wakutosha ambao angeweza kuutumia kutoa hati, hivyo

<sup>11</sup> ISSAI 1700.16 (iliyorekebishwa)

<sup>12</sup> ISSAI 1705.7 (iliyorekebishwa)

<sup>13</sup> Makosa ya muhimu ni yale ambayo; hayajafungwa katika sehemu ya akaunti au sehemu ya hesabu na kama imefungamanishwa inaweza kusababisha sehemu kubwa ya hesabu

mkaguzi anahitimisha kuwa hii inaweza kusababisha kutokutambua makosa ambayo ni makubwa na ya muhimu<sup>14</sup>.

### **2.3 Mambo mengine ya kuripoti**

Wakati wa kutoa taarifa, tumetumia muongozo mpya uliotolewa na viwango vya kimataifa vya ukaguzi, ISSAIs 1701; pamoja na ISSAIs 1706 na 1720 iliyorekebishwa ambayo kwa pamoja inamtaka mkaguzi kutoa taarifa za ziada katika ripoti ya ukaguzi ili kuweza kutoa meezezo mengine kwa watumiaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa. Hii inafanyika wakati wakuonyesha aya inayohusiana na: mambo muhimu ya ukaguzi (ISSAI 1701), kusisitiza baadhi ya mambo (ISSAI 1706 iliyorekebishwa) na taarifa nyingine (ISSAI 1720 iliyorekebishwa).

#### **2.3.1 Masuala ya Msisitizo**

Aya ya masuala yenye msisitizo inaonyeshwa katika report moja moja ili kuwaonyesha watumiaji wa taarifa mambo muhimu japo yamaeonyeshwa na kuripotiwa vizuri katika taarifa za fedha lakini yanasisitizwa kuwa ni muhimu kwa watumiaji ili kuelewa tarifa za fedha<sup>15</sup>.

#### **2.3.2 Mambo muhimu**

Aya hii inaonyeshwa katika ripoti ya ukaguzi ili kuonyesha mambo muhimu ukiacha yale yalonyeshwa katika tarifa za fedha ambayo yanaonekana ni muhimu kwa watumiaji ili kuelewa ukaguzi, majukumu ya mkaguzi au ripoti za ukaguzi.<sup>16</sup>

#### **2.3.3 Mambo muhimu ya Ukaguzi**

Mambo yanayajiri kama vile aya ya mambo muhimu ya ukaguzi yameingizwa katika ripoti moja moja, ili kuongeza uwazi katika ukaguzi na kuwaelezea watumiaji wa ripoti za fedha maeneo yenye viatarishi zaidi kwa makosa na wote waliohusika katika kufanya maamuzi na tahadhari muhimu ya mkaguzi.

<sup>14</sup> ISSAI 1705.9

<sup>15</sup> ISSAI 706.8 (iliyorekebishwa)

<sup>16</sup> ISSAI 706.10 (iliyorekebishwa)

Jambo hili limeelekezwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha kama moja ya kutoa hati ya ukaguzi. Hakuna hati tofauti ya ukaguzi itakayotolewa katika mambo muhimu.

#### **2.3.4 Maelezo mengine**

Viwango vya kimataifa vya ukaguzi namba 1720 (ISSAI 1720 - imerekebisa) inahitaji ripoti ya ukaguzi kuonyesha aya ya maelezo mengine. Maelezo mengine imekusanya ripoti ya wakurugenzi (taarifa ya Waheshimiwa mawaziri, taarifa ya Katibu Mkuu, taarifa ya Mwenyekiti wa bodi ya ushauri) na tamko la wakuu wa idara ya uhasibu kuonyeshwa katika taarifa za fedha. Menijementi ya Taasisi zinazokaguliwa wanajukumu la kutoa maelezo mengine. Mkaguzi anahitajika kusoma maelezo mengine na kuhakikisha kuwa haitofautiani kwa kiwango kikubwa na taarifa za fedha au kwa uelewa nilioupata katika ukaguzi, ina makosa makubwa na kuripoti inavyotakiwa. Maoni yangu ya ukaguzi hayajumuishi taarifa nyengine zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha na sitatoa hati kwenye taarifa nyengine.

#### **2.3.5 Tathmini za Kisheria na matakwa ya Udhibiti**

Kifungu namba 1700.43 cha Viwango vya kimataifa vya ukaguzi (ISSAI 1700.43- imerekebishwa) imetoa muongozo kwa wakaguzi katika kuelezea mambo mengine ya kuripoti. Kifungu namba 48(3) cha sheria ya Manunuvi ya Umma namba 7 ya 2011 inanihitaji kuelezea katika ripoti yangu ya mwaka kwamba Taasisi zilizokaguliwa zimezingatia sheria na miongozo ya manunuvi. Katika mwaka wa ukaguzi, nimepitia shughuli za manunuvi nikiwa na lengo la kupima utekezaji wa sheria za manunuvi za mwaka 2011 (imerekebishwa mwaka 2016) na kanuni zake za 2013. Matokeo ya tathmini hii yameelezewa katika sura ya tisa ya ripoti hii.

### **2.4 Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka 2016/2017**

Kati ya kaguzi 241 zilizofanyika kipindi hiki, balozi nne (4) hazikutolewa maoni kwa sababu wakati wa ukaguzi ndio zilikuwa zimeanzishwa. Matokeo ya ukaguzi kwa taasisi 237 zilizobaki kwa

mwaka 2016/2017 ni kama ilivyochambuliwa katika jedwali hapa chini ikilinganishwa na matokeo ya ukaguzi wa mwaka jana.

**Jedwali Na. 4: Uchambuzi wa maoni ya ukaguzi yaliyotolewa kwa mwaka 2016/17**

Aina ya Taasisi	Maoni	hati inayoridhisha		Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo/masuala mengine		Hati yenye shaka		Hati Isiyoridhisha		Hati mbaya	
		2017	2016	2017	2016	2017	2016	2017	2016	2017	2016
Mwaka wa fedha											
Wizara		52	46	6	11	6	9	1	1	0	1
Idara za Serikali		27	24	2	7	3	2	1	0	0	0
Balozi		32	28	1	5	2	1	0	0	0	0
Sekretarieti za Mikoa		23	14	2	6	1	0	0	1	0	0
Vyama vya Siasa		0	0	0	0	3	0	0	0	7	4
BWB/NWSSA		9	12	0	0	4	0	0	0	0	0
Mifuko ya kijamii		14	11	3	1	0	0	0	0	0	0
Taasisi zingine		31	22	2	3	3	12	2	1	0	0
Jumla		188	157	16	33	22	24	4	3	7	5

Ikilinganishwa na mwaka jana kumekuwa na ongezeko la idadi ya ripoti za ukaguzi zilizotolewa kutoka 222 hadi 241 mwaka 2016/17. Vivyo hivyo, licha ya kuwa, Serikali Kuu iliandaa hesabu zake kwa mara ya kwanza kwa mujibu wa viwango vya hesabu vya kimataifa vya sekta ya umma vizivyozingatia fedha taslim (IPSAS accrual) kipindi hiki cha 2016/17 kumekuwa na maboresho katika hati za ukaguzi ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Taasisi 19 zimeboresha taarifa zao kutoka hati yenye shaka mwaka jana na kupata hati inayoridhisha kwa mwaka 2016/17. wakati, taasisi moja (1) taarifa yake iliimarika kutoka hati isiyoridhisha na kupata hati inayoridhisha. Taasisi mbili (2) ziliboresha taarifa zao kutoka hati mbaya na kuwa hati ya mashaka na taasisi moja (1) iliboreshwu kutoka hati isiyoridhisha kuwa hati yenye mashaka. Taasisi 167 zimeendelea kuwa na hati inayoridhisha, wakati huo taasisi saba (7) zilianzishwa na taasisi saba (7) ambazo hazikukaguliwa kwa mwaka uliopita zilipata hati iinayoridhisha.

Taasisi 17 zilishuka kutoka hati inayoridhisha na kupata hati yenye shaka; taasisi tatu (3) zilitoka kwenye hati yenye shaka na kupata hati isiyoridhisha. Taasisi nne (4) zimeendelea kupata

hati zenyenye mashaka na taasisi nyingine nne (4) ziliendelea na hati mbaya. Taasisi tatu (3) ambazo hazikukaguliwa kwa mwaka uliopita, mwaka huu zimepata hati mbaya. Orodha ya kina ya taasisi na Hati za Ukaguzi husika kwa mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na a mwaka uliopita imeunganishwa na ripoti hii kama **Kiambatisho 2.1**.

Taasisi zenyenye hati yenye shaka na msingi wa hati hiyo zimeambatishwa katika ripoti hii katika **Kiambatisho 2.2**, zenyenye hati isiyoridhisha na msingi wake imeonyeshwa katika kiambatisho 2.3, na wakati huo taasisi zenyenye hati mbaya zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 2.4** cha ripoti hii.

## SURA YA TATU

### **3.0 UFUAMILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI NA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA HESABU ZA SERIKALI KWA MIAKA ILIYOPITA**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inawasilisha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita ya ukaguzi wa CAG kwa ripoti mojamoja, ripoti kuu na ufuamiliaji wa utekelezaji wa maagizo ya PAC.

Hii ni kuzingatia kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 (iliyorekebishwa 2013) kinachonitaka kujumuisha mipango ya utekelezaji kutoka kwa Maafisa Masuuli na majibu jumuifu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) katika Ripoti kuu ya mwaka ya ukaguzi.

Ili mapendekezo yangu na maagizo ya PAC kuwa na maana, inapaswa kuwa na umuhimu sawa katika kuhakikisha kuwa mapendekezo yanatekelezwa ipasavyo, kwa ufasaha na kuzaa matokeo yaliyokusudiwa.

Utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na maagizo ya PAC huonesha dhamira ya Wakaguliwa na Serikali kwa ujumla katika kuimarishe Uwazi, Uwajibikaji, Utawala bora, Uangalizi na Kuboresha usimamizi bora wa fedha na rasilimali katika ngazi zote.Kwahiylo, kutotekeliza au kuchelewa kutekeleza mapandekezo ya CAG na maagizo ya PAC kunaweza kusababisha usimamizi mbaya wa mapato ya Serikali, Matumizi na Mali na hivyo kufanya uaminifu na ukamilifu wa mifumo na taratibu kutoaminika.

Baadhi ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali hawajafanya jitihada za kutekeleza mapendekezo ya CAG.Mtazamo huu wa kutoshughulikia mapungufu na kasoro kunaweza kupelekea kujirudia katika miaka ijayo.Hii pia ni ishara ya kutokuwa makini na kukosa dhamira kwa Maafisa Masuulii na menejimenti za Wizara, Idara na Wakala wa serikali husika

Vigezo vyetu vilivyotumika kutathmini hali ya utekelezaji vimeoneshwa kwenye jedwali hapo chini

**Jedwali Na. 5: Maana ya maneno yaliyotumika kutathmini hali ya utekelezaji**

Vigezo vilivyotumika kwenye tathmini	Maana ya maneno husika
<b>Yaliyotekelawa</b>	Mapendekezo na Maagizo yametekelawa kikamilifu na Mkaguliwa aidha, kama ilivyoelawa kwenye taarifa au katika namna ambayo jambo limetatuliwa
<b>Yaliyo katika utekelezaji</b>	Mkaguliwa ana mipango mahususi ya kuanza nayo au ameshaanza kutekeleza na amedhamiria kutekeleza pendekozo kikamilifu au ametekelawa sehemu ya pendekozo na maagizo
<b>Yasiyotekelawa</b>	Mkaguliwa hajatekeleza pendekozo na inaonesha hatafanya hivyo
<b>Yaliyopitwa na wakati</b>	Mkaguliwa amejitahidi kwa kiasi kikubwa kwamba mapungufu ya nyuma hayatokei tena katika mwaka (Miaka) ujayo (ijayo) au mapendekezo na maagizo siyo ya muhimu tena kutekeleza au utekelezaji wake hauwezekani au siyo muhimu kwa sababu ya mabadiliko ya sheria, vipaumbele vya serikali, maagizo na miongozo.

### 3.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa CAG wa miaka iliyopita kwa kila Mkaguliwa

Wakati wa kupitia hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG tumebaini kuwa kati ya mapendekezo ya ukaguzi 4,108, 1,543(37.57%) yalitekelawa, 1,454(35.41%) yalikuwa katika hatua mbalimbali ya utekelezaji 721(15.5%) hayakutekeleza na 390(9.49%) yalikuwa yamepitwa na wakati. Hali ya utekelezaji imeelezwa katika **Jedwali Na 6** na **Kielelezo Na 1**

**Angalizo:** Maelezo ya hali ya utekelezaji imeelezwa kwa kina kwenye barua za mapungufu kwa kila Mkaguliwa.


**Jedwali Na. 6: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa kila Mkaguliwa**

Taasisi Utekelezaji	Mafungu(Wizar a na Idara)	Wakala	Balozi	Taasisi nyine	Sekretariati za mikoa	Vyama vya Siasa	Mifuko	Mabonde ya Maji	Jumla
Yaliyotekelzwa	411	266	154	195	402	22	58	35	1,543
Yaliyo katika utekelezaji	439	213	189	206	240	11	92	64	1,454
Ambayo hayajatekelezwa	125	61	144	118	173	37	15	48	721
Yaliyopitwa na wakati	78	6	45	73	171	2	13	2	390
Jumla	1053	546	532	592	986	72	178	149	4,108

*Chanzo: Barua ya mapungufu kwa kila Mkaguliwa kwa mwaka 2016/17*

Hitimisho la jedwali hapo juu linaonesha mapendekezo yaliyokuwa yamesalia yametekelezwa kwa 37.57% % na 35.39% ama sehemu yake imetekelezwa au yako katika utekelezaji. Kwahiyoo naendelea kusisitiza juu ya utekelezaji wa 17.55% ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa na Wizara, Idara na Wakala wa Serikali.

**Kielelezo Na. 1: Chati inayoonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa mwaka wa fedha 2015/2016**



*Chanzo:*

*Barua za mapungufu kwa kila Mkaguliwa 2016/17*

### 3.3 Mwenendo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa CAG kwa kila Mkaguliwa kwa miaka miwili mfululizo

Jedwali la hapo chini linaonesha mwenendo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG wa miaka ya nyuma kuanzia 2013/14 hadi 2015/16 kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 7 na Kielelezo Na. 2 hapo chini;

**Jedwali Na. 7: Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo kuanzia 2013/14 hadi 2015/16**

Aina	Mwaka wa fedha	Yaliyotekelzwa		Yaliyo katika utekelezaji		Ambayo hayajatekelzwa		Yaliyopitwa na wakati		Jumla
		Na.	%	Na.	%	Na	%	Na.	%	
<b>Mafungu, Balozi na Tawala za Mikoa</b>	2013/14	803	38	666	32	444	21	188	9	2101
	2014/15	883	35	866	35	570	23	183	7	2502
	2015/16	967	38	868	34	442	17	294	11	2571
<b>Wakala</b>	2013/14	132	35	168	45	65	17	11	3	376
	2014/15	372	47	291	37	114	14	15	2	792
	2015/16	266	49	213	39	61	11	6	1	546
<b>Taasisi nyingine</b>	2013/14	93	51	57	31	28	15	5	3	183
	2014/15	197	32	197	32	158	26	58	10	610
	2015/16	305	31	369	38	216	22	88	9	978

**Chanzo:** Barua za mapungufu kwa kila Mkaguliwa kuanzia 2014/15 hadi 2016/17

**Angalizo:** Taasisi nyiginezinajumuisha Taasisi, Mifuko, Vyama vyा Siasa, Mabonde ya Maji na Mifumo ya Taifa ya Usambazaji wa Maji safi na Taka

### 3.4 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa na CAG kwenye Ripoti ya Jumla

Majibu ya Serikali kwa Ripoti ya jumla ya 2015/16 yaliwasilishwa Kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuititia barua yenye kumb.Na CHA.114/474/01/78 ya tarehe 10/7/2017.Natambua jitihada za Maafisa Masuulii, Mlipaji Mkuu wa Serikali na Serikali

kwa Ujumla kwa kuifanya kazi yangu ya kikatiba na kisheria kuwa na maana, Hivyo naendelea kusisitiza juu ya utekelezaji kamili wa mapendekezo yangu ili kuzuia kujirudia kwa mapungufu yaleyale kwa miaka ijayo.


Katika Ripoti zangu kuu za miaka iliyopita,kulikuwa na limbikizo la mapendekezo ambayo hayajashughulikiwa mpaka tarehe 30 Juni,2016 yaliyohitaji kujibiwa na serikali yamepungua kutoka 102 hadi 85.

Kati ya mapendekezo 85 ambayo yalikuwa hayajashughulikiwa,14(16.5%) yametekelezwa, 51(60.0%) yako katika utekelezaji, 9(10.6%) hayakutekelezwa na 11(12.9%) yaliyalikuwa yamepitwa na wakati.Hali ya utekelezaji wa mapendekezo imetolewa kwenye **Jedwali Na. 8, Kielelezo Na. 2 na kiambatisho 3.1**

#### **Jedwali Na. 8: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa CAG wa miaka iliyopita**

Mwaka wa Fedha Utekelezaji	2014/2015		2015/2016	
	No.	%	No.	%
Yaliyotekelvezwa	19	19	14	16.5
Yaliyo katika utekelezaji	53	52	51	60.0
Ambayo hayajatekelezwa	20	20	9	10.6
Yaliyopitwa na wakati	10	9	11	12.9
Jumla	102	100	85	100

#### **Kielelezo Na. 2: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti kuu ya CAG**



Kwa ujumla, Kutokana na **Jedwali Na. 8** na **kielelezo Na. 2** ni ishara kuwa kuna maboresho katika utekelezaji wa mapendekezo ya CAG ambapo mapendekezo ambayo hayatajekelezwa yamepungua kutoka 20% hadi 10.6%. Mapendekezo mengi ambayo yalikuwa hayajashughulikiwa yako katika hatua za utekelezwaji kwa 60.0% kwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na 52% kwa mwaka 2014/15. Jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha kutekeleza kikamilifu mapendekezo yaliyo katika hatua ya utekelezwaji. Vilevile, bado nasisitiza utekelezaji wa 10.6% ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa licha ya maboresho muhimu ya kupungua kwa mapandekezo ambayo hayajatekelezwa kutoka 20% mpaka asilimia 10.6% ikilinganishwa na mwaka jana. Hii itasaidia Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kuwajibika katika matumizi ya rasilimali za Umma.

### **3.5 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo ya PAC kwenye Ripoti kuu ya mwaka**

Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ni chombo cha juu kabisa cha usimamizi wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 117(15) cha Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Majukumu ya Kamati yameelezwa kwa kina chini ya kifungu cha 14 na 16 cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo Ripoti za CAG huwa nguzo muhimu katika kujenga misingi ya shughuli za PAC.

Kwa sababu ya umuhimu wa kimuundo, utekelezwaji wa maagizo yaliyotolewa yanapaswa kushughulikiwa ipasavyo na Maafisa Masuulii husika. Utekelezaji wa maagizo ya PAC ni muhimu ili kuhakikisha shughuli zinafanyika kwa utaratibu unaokubalika, kuzingatia maadili, ufanisi, ufasaha wa maendeleo ya kiuchumi, Uangalizi na uwajibikaji unazingatiwa, sheria na kanuni zilizopo zinazingatiwa na Rasilimali zinasimamiwa dhidi ya upotevu, matumizi mabaya na uharibifu. Hivyo ni muhimu mambo yote yaliyoibuliwa na PAC yanashughulikiwa vizuri na maagizo yote yanatekelezwa ipasavyo.

Kwahiyoo, naendelea kushukuru PAC na Bunge zima juu ya mwendelezo wa msaada wa kupitia ripoti ya CAG na

mapendekezo na kufanya majukumu yangu ya kisheria kuwa muhimu na ya manufaa,

Katika ripoti iliyopita kulikuwa na maagizo 16 yaliyopaswa kutekelewa na Serikali. Kati ya maagizo 16 ya utekelezaji, Agizo 1(6%) lilitekelezwa, 10(63%) yako katika utekelezaji, 3(19%) hayakutekelezwa na 2(12%) yamepitwa na wakati. Maelezo ya hali ya utekelezaji yametolewa chini ya **Jedwali Na 9** na **Kiambatisho 3.1**

**Jedwali Na. 9: Muhtasari wa Utekelezaji wa maagizo ya PAC kwa miaka iliyopita juu ya Ripoti kuu ya CAG ya Mwaka**


Utekelezaji	Mwaka wa Fedha		2011/12		2012/13		2013/14[1]		2014/15		2015/16	
	No	%	No	%	No	%	No	%	No	%	No	%
Yaliyotekelawa	0	0	1	33	0	0	0	0	0	1	6	
Yaliyo katika utekelezaji	4	80	2	67	0	0	4	57	10	63		
Ambayo hayajatekelezwa	0	0	0	0	0	0	2	29	3	19		
Yaliyopitwa na wakati	1	20	0	0	0	0	1	14	2	12		
Jumla	5	100	3	100	0	0	7	100	16	100		

*Chanzo: Majibu ya PMG juu ya maagizo ya PAC*

[1] NB: Kwa mwaka wa fedha 2013/14 hakuwa na maagizo ya PAC kwa kuwa kamati haikujadili ripoti ya CAG kutokana na kukamilisha katiba ya bunge la mwaka 2015

Kutokana na Jedwali hapo juu, hali ya utekelezaji imeoneshwa na **Kielelezo Na.3**

### Kielelezo Na. 3: Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa maagizo ya PAC ya miaka iliyopita juu ya Ripoti kuu ya Mwaka ya Ukaguzi



Kutokana na jedwali Na.9 na Kielelezo Na.3 hapo juu, Hitimisho linaonesha maagizo mengi bado yako katika hatua ya utekelezaji ikimaanisha kuwa jitihada zaidi zinatakiwa kuhakikisha maagizo ambayo hayajatekelezwa kikamilifu (63%) yanatekelezwa. Vilevile maagizo ambayo hayajatekelezwa sawa na 16% yanapaswa kutekelezwa ili Maagizo ya PAC kuwa yenye tija

### 3.6 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo ya PAC ya miaka iliyopita juu ya Ripoti za kila Mkaguliwa

Katika mwaka huu uliokaguliwa, Wajumbe wa PAC walifanya vikao na Wizara, Idara, na Wakala wa Serikali 15 na kutoa maagizo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji. Kwahiyu hali ya utekelezaji inajumuisha maagizo ya mwaka huu na yale ya miaka iliyopita. Nimefanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa Maagizo ya PAC kutoka kwa Wakaguliwa ambapo 106 (39%) ya mapendekezo yaliyotolewa na PAC yalitekelezwa, 106 (39%) yako katika utekelezaji, 54(17%) hayakutekelezwa na 9(5%) yamepitwa na wakati. Hali ya utekelezaji wa maagizo imetolea katika Jedwali Na.10 na Kiambatisho 3.2

**Angalizo:** Maelezo ya kina ya utekelezaji wa maagizo ya PAC yametolewa kwenye barua za mapungufu za Kila Mkaguliwa

**Jedwali Na. 10: Muhtasari wa utekelezaji wa maagizo ya PAC wa miaka ya nyuma**

Wakaguliwa Utekelezaji	Mafungu	Wakala	Balozi	Taasisi nyingine	Sekretarieti za Mikoa	Vyama vy'a Siasa	Mifuko	Mabonde	Jumla	Asilimia
Yaliyotekelawa	58	8	0	5	35	0	0	0	106	39
Yaliyo katika utekelezaji	63	8	0	3	32	0	0	0	106	39
Yaliyotekelawa	23	0	0	12	19	0	0	0	54	17
Yaliyopitwa na wakati	9	0	0	0	0	0	0	0	9	5
<b>Jumla</b>	<b>153</b>	<b>16</b>	<b>0</b>	<b>20</b>	<b>86</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>275</b>	<b>100</b>

*Chanzo: Barua za mapungufu kwa kila Mkaguliwa 2015/16*

Nawasihi sana Maafisa Masuuli kutekeleza kikamilifu maagizo yote ya PAC ambayo yametekelawa kiasi (39%) na yale ambayo hayajatekelawa (17%) ili kupata manufaa yanayotokana na maagizo ya PAC

### 3.7 Mwenendo wa hali ya utekelezaji wa maagizo ya PAC ya miaka iliyopita juu ya ripoti za kila Mkaguliwa kwa miaka miwili mfululizo

Jedwali hapo chini linaonesha mwenendo wa hali ya utekelezaji wa maagizo ya PAC kwa miaka miwili kuanzia 2014/15 na 2015/16 kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kama ilivyooneshwa na **Jedwali 11** na **Kielelezo Na. 4** hapo chini:


**Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa hali ya utekelezaji wa maagizo  
yaliyotolewa kwa mwaka 2014/15 na 2015/16**

<b>Hali</b> <b>Mkaguliwa</b>	<b>Mafungu,Balozi na Sekretariati za Mikoa</b>		<b>Wakala</b>		<b>Taasisi nyngine</b>		<b>Jumla</b>		<b>Asilimia</b>	
	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>	<b>2015</b>	<b>2016</b>
<b>Mwaka wa fedha</b>										
Yaliyotekelawa	91	93	7	8	4	5	102	106	35	39
Yaliyo katika utekelezwaji	75	95	10	8	2	3	87	106	30	39
Ambayo hayajatekelawa	85	42	0	0	0	12	85	54	29	20
Yaliyopitwa na wakati	16	9	0	0	0	0	16	9	6	3
<b>Jumla</b>	<b>267</b>	<b>239</b>	<b>17</b>	<b>16</b>	<b>6</b>	<b>20</b>	<b>290</b>	<b>275</b>	<b>100</b>	<b>100</b>

*Chanzo: Barua za mapungufu za kila Mkaguliwa kwa mwaka 2014/15 ,2015/16 na 2016/17*

Kutokana na Jedwali hapo juu,hali ya utekelezaji inaweza kuoneshwa na **Kielelezo Na. 4** hapo chini

#### Kielelezo Na. 4: Hali ya utekelezaji wa Maagizo ya PAC kwa ulinganisho wa miaka miwili



Kutokana na Jedwali Na. 11 na Kielelezo Na.4 hapo juu ni ishara kwamba kuna maboresho katika utekelezaji wa maagizo kutoka 35% hadi 39% Maagizo mengi ambayo yalikuwa hayajatekelezwa 39% kwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na 30% ya mwaka 2014/15 bado yako katika utekelezaji.Jitihada zaidi zinahitajika ili kutekeleza kikamilifu maagizo ambayo yalikuwa bado hayajatekelezwa.Vilevile, Naendelea kusisitiza juu ya utekelezaji wa 20% ya maagizo ambayo hayajatekelezwa licha ya maboresho muhimu ya utekelezaji kutoka 29% hadi 20% ikilinganishwa na mwaka uliopita.

## SURA YA NNE

### **4.0 USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA**

#### **4.1 UTANGULIZI**

Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilielekezwa katika kuhakikisha kuwa kila raia anafaidika kutokana na rasilimali za Taifa. Ilisisitiza juu ya umuhimu wa kukabiliana na changamoto pamoja na matatizo yanayowakabili wananchi hasa wa kipato cha chini. Mkazo huo umetangazwa na kauli mbiu ya Rais ya '*Hapa kazi tu*' iliopangwa kubadili mtazamo wa watu katika utendaji kazi. Msingi wa bajeti ya 2016/17 ulijengwa katika "Ukuaji wa viwanda na uongezaji wa ajira".

#### **4.2 Muelekeo wa Bajeti ya mwaka 2016/17**

Bajeti ya mwaka 2016/17 ilijielekeza katika vipaumbele vingi mionganoni mwavyo ni: -

- □Mikakati ya kukuza uchumi na viwanda;
- □Kuunganisha maendeleo ya kiuchumi na rasilimali watu;
- □ Kuwezesha mazingira ya biashara;

Sura hii inatoa taswira ya vipengele vifuatavyo: Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge ikiwa ni makisio ya mapato na matumizi, fedha halisi zilizokusanywa na kutolewa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ikilinganishwa na makisio na mwenendo wa mapato pamoja na matumizi katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2017.

#### **4.3 Muonekano wa Jumla wa Bajeti**

Katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali iliweka sera na miongozo mbalimbali ya kuwezesha utekelezaji mzuri wa bajeti yake.

Kati ya miongozo na sera zilizowekwa ni zile zitakazoondoa mianya ya upotevu wa maduhuli, kuimarisha ukusanyaji wa kodi katika vituo vyote vya kukusanya kodi, kurasimisha biashara zisizokuwa rasmi, kukusanya kodi kwa uwezo wake wote na mirabaha, na kuhamasisha matumizi ya vifaa vya kieletroniki katika ukusanyaji wa maduhuli.

Mikakati ya matumizi inahusisha kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja kufuata sheria, kanuni na taratibu za fedha pamoja na miongozo. Lengo likiwa ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwenye matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutumia kumbi za serikali kwa ajili ya mikutano, warsha, mafunzo na semina mbalimbali za kiserikali, kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa matumizi ya umma katika miradi ya maendeleo, kuunganisha Halmashauri zote kwa kutumia Mfumo wa Kieletroniki wa kuhamisha Fedha (EFTS) nk.

Katika mwaka wa Fedha 2016/17, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha Shilingi bilioni 29,539.6 ikiwa ni ongezeko la kiasi cha Shilingi bilioni 7,044.10 sawa na asilimia 31 ikilinganishwa na kiasi cha makisio ya Shilingi bilioni 22,495.5 kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Jedwali hapa chini linaonesha makisio ya mapato ya Serikali kwa vyanzo vilivyotambuliwa na asilimia ya kuiwezesha bajeti;

**Jedwali Na. 12: Mchanganuo wa Bajeti ya Makusanyo**

VYANZO	Kiasi katika Shilingi Bilioni	Asilimia ya makisio kwa kila chanzo
<b>Kodi</b>	<b>15,105.10</b>	<b>51.14</b>
<b>Yasiyo ya Kodi</b>	<b>3,358.40</b>	<b>11.37</b>
<b>Mikopo ya Ndani</b>	<b>5,374.30</b>	<b>18.19</b>
<b>Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani</b>	<b>5,701.80</b>	<b>19.30</b>
<b>Jumla</b>	<b>29,539.60</b>	<b>100</b>

Chanzo: Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, 2016/17

Bajeti ya matumizi iliyofanyiwa marekebisho ya mwaka 2016/17 ilikuwa Shilingi bilioni 29,546.84<sup>17</sup>, ongezeko la Shilingi bilioni 7,051.34 (31.35%) ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa ya Shilingi bilioni 22,495.50 kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kutoka katika bajeti iliyorekebishwa, Shilingi bilioni 18,084.56 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 1,510 (9.11%) ikilinganishwa na Shilingi bilioni 16,574.40 zilizotengwa mwaka wa fedha 2015/16 na matumizi halisi yalikuwa kiasi cha Shilingi bilioni 17,294 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 1,324 (8.29%) ikilinganishwa na Shilingi bilioni 15,970 zilizotumika kwa matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2015/16.

Shilingi bilioni 11,462.28 zilitengwa kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 5,541.18 (94%) ikilinganishwa na Shilingi bilioni 5,921.1 zilizotengwa mwaka wa fedha 2015/16. Shilingi bilioni 6,498.3 zilikuwa matumizi halisi kwa ajili ya Maendeleo, sawa na asilimia 57 ya bajeti iliyorekebishwa; hili ni ongezeko la Shilingi bilioni 2,447.47 (60.42%) ikilinganishwa na matumizi halisi ya Shilingi bilioni 4,050.83 yaliyotumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/16. Maeleo zaidi yanapatikana katika Jedwali Na. 13 hapo chini kwa muhtasari.

<sup>17</sup> Hii hesabu imepatikana katika Taarifa ya Robo ya nne ya Utekelezaji wa Bajeti 2017

**Jedwali Na. 13: Bajeti na Matumizi Halisi kwa miaka miwili**

Maelezo	2016/2017		2015/2016		Asilimia ya kubadilika Bajeti	Asilimia ya kubadilika halisi
	Bajeti Iliyorekebishwa	Matumizi Halisi	Bajeti Iliyorekebishwa	Matumizi Halisi		
Matumizi ya Kawaida	18,084.56	17,294.00	16,574.40	15,970.00	9.11	8.29
Matumizi ya Maendeleo	11,462.28	6,498.30	5,921.10	4,050.83	93.58	60.42
Jumla	29,546.84	23,792.30	22,495.50	20,020.83	31.35	18.84

*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti robo ya nne, 2017*

#### **4.4 Muhtasari wa Ukusanyaji wa Mapato na fedha zilizotolewa**

Mapato halisi yaliyokusanya kutoka kwa vyanzo vinavyotambuliwa yalifikia Shilingi bilioni 25,307.48 na kushindwa kufikia lengo kusudiwa kwa kiasi cha Shilingi billioni 4,232.12 sawa na asilimia 14.33 ya makisio.

##### **Mapato kutokana na kodi**

Makusanyiko ya kodi yalikuwa Shilingi bilioni 14,271 sawa na 94.48% ya makisio hivyo kutofikia lengo kwa asilimia 5.52. Ikilinganishwa na mapato halisi kutokana kodi yaliyopotiwa mwaka wa fedha 2015/16 kumekuwa na ongezeko la Shilingi bilioni 1,807.77 sawa na asilimia 14.50 ambayo ambayo inaonesha matokeo chanya.

##### **Mapato Yasiyotokana na Kodi**

Mapato yasiyotokana ya kodi yalikuwa Shilingi bilioni 2,072.9 dhidi ya lengo la Shilingi bilioni 3,358.4 sawa na asilimia 61.72. Ikilinganishwa na ukusanyaji wa 2015/16 kuna ongezeko la asilimia 28.43. TZS 1,285.5 bilioni hazikukusanya sawa na asilimia 38.28 ya makadirio yaliyothibitishwa.

##### **Mikopo ya Ndani**

Mikopo ya Ndani ambayo hasa ni kwa ajili kugharamia bajeti pamoja na amana za Serikali zilizoiva ilikua Shilingi bilioni 5,915,85 ambayo ni ya juu kuliko makadirio kwa asilimia 10.08


na asilimia 11.52 juu ikilinganishwa na mapato kutoka mwaka 2015/16.

### **Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani na Misaada ya Washirika wa Maendeleo**


Mapato yaliyotokana na Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani yenye masharti nafuu na Misaada ya Washirika wa Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2016/17 yalifikia Shilingi bilioni 3,047.43 sawa na asilimia 53.45 dhidi ya makadirio yaliyopitishwa ya Shilingi bilioni 5,701.80. Shilingi bilioni 2,654.37 sawa na asilimia 46.55 a malengo yaliyothibitishwa hazikupokelewa. Maeleo zaidi kuhusu mikopo ya Ndani na Nje pamoja na misaada ya wahisani imeelezewa katika sura ya tano ya ripoti hii.

Makadirio ya mapato ya Serikali na mwenendo wa makusanyo kwa miaka minne mfululizo ni iliyotolewa katika kielelezo hapa chini;

#### **Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Makisio ya Serikali kwa miaka minne**




### Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa Mapato ya Serikali kwa miaka minne



Sura ya Nine

### Kielelezo Na. 7: Mwenendo wa Mapato ya Serikali kwa miaka minne ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa



*Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti*

**Jedwali Na. 14: Makisio ya Mapato na Matumizi yaliyoidhinishwa**

2016/2017						
Aina ya Mapato	Makisio katika shilingi bilioni	Halisi katika shilingi bilioni	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Asilimia iliyozidi/ Kupungua kulingana makisio	Asilimia ya Ongezeko/Punguzo na ikilinganishwa na mwaka jana	
Kodi	15,105.10	14,271.30	(833.80)	(5.52)	14.50	
Yasiyotokana na Kodi	3,358.40	2,072.90	(1,285.50)	(38.28)	28.43	
Mikopo ya Ndani	5,374.30	5,915.85	541.55	10.08	11.52	
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	5,701.80	3,047.43	(2,654.37)	(46.55)	76.52	
<b>JUMLA</b>	<b>29,539.60</b>	<b>25,307.48</b>	<b>(4,232.12)</b>	<b>(14.33)</b>	<b>19.89</b>	
2015/2016						
Aina ya Mapato	Makisio katika shilingi bilioni	Halisi katika shilingi bilioni	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Asilimia iliyozidi/ Kupungua kulingana makisio	Asilimia ya Ongezeko/Punguzo na ikilinganishwa na mwaka jana	
Kodi	12,362.96	12,463.53	100.57	0.81	15.69	
Yasiyotokana na Kodi	1,634.56	1,613.99	(20.57)	(1.26)	113.05	
Mikopo ya Ndani	6,175.45	5,304.94	(870.51)	(14.10)	33.33	
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	2,322.53	1,726.40	(596.13)	(25.67)	(52.07)	
<b>JUMLA</b>	<b>22,495.50</b>	<b>21,108.86</b>	<b>(1,386.64)</b>	<b>(6.16)</b>	<b>10.45</b>	
2014/2015						
Aina ya Mapato	Makisio katika shilingi bilioni	Halisi katika shilingi bilioni	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Asilimia iliyozidi/ Kupungua kulingana makisio	Asilimia ya Ongezeko/Punguzo na ikilinganishwa na mwaka jana	
Kodi	11,318.20	10,773.22	(544.98)	(4.82)	15.98	
Yasiyotokana na Kodi	1,318.30	757.57	(560.73)	(42.53)	18.19	
Mikopo ya Ndani	2,955.20	3,978.95	1,023.75	34.64	20.96	
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	4,261.60	3,601.95	(659.65)	(15.48)	16.76	
<b>JUMLA</b>	<b>19,853.30</b>	<b>19,111.68</b>	<b>(741.62)</b>	<b>(3.74)</b>	<b>17.22</b>	
2013/2014						
Aina ya Mapato	Makisio katika shilingi bilioni	Halisi katika shilingi bilioni	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Asilimia iliyozidi/ Kupungua kulingana makisio	Asilimia ya Ongezeko/Punguzo na ikilinganishwa na mwaka jana	
Kodi	10,412.95	9,289.00	(1,123.95)	(10.79)	15.36	
Yasiyotokana na Kodi	763.43	640.95	(122.48)	(16.04)	33.21	
Mikopo ya Ndani	1,699.87	3,289.41	1,589.54	93.51	31.96	
Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani	5,011.60	3,084.93	(1,926.67)	(38.44)	(22.73)	
<b>JUMLA</b>	<b>17,887.85</b>	<b>16,304.29</b>	<b>(1,583.56)</b>	<b>(8.85)</b>	<b>8.56</b>	

*Vyanzo: Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti, Taarifa ya fedha ya Mamlaka ya Mapato  
iliyokaguliwa na taarifa ya Wizara ya Fedha*

#### **4.5 Uchanganuzi wa makadirio ya mapato kugharamia matumizi**


Katika mwaka huu unaopitiwa, sehemu ya bajeti iliyogharamiwa na kodi na yasiyotokana na kodi ilikuwa Shilingi bilioni 18,463.5 sawa na asilimia 62.50 ya bajeti iliyoidhinishwa ya Shilingi bilioni 29,539.60 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 4,465.98 sawa na asilimia 31.91 ikilinganishwa na sehemu ya bajeti ambayo ilifadhiliwa na kodi mwaka 2015/16. Makusanyo halisi ya fedha kwa matumizi ya kodi yalifikia Shilingi bilioni 16,344.20 sawa na asilimia 64.58 ya bajeti ikioneshaa ongezeko la uwiano wa bajeti iliyogharamiwa kwa kutumia kodi kwa Shilingi bilioni 2,266.68 sawa na asilimia 16.10 ikilinganishwa fedha zilizopatikana kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha Shilingi bilioni 11,076.10 sawa na asilimia 37.5 ya makadirio yaliyoidhinishwa kutoka katika vyanzo vya mikopo ya Ndani na Nje na Misaada ya Wahisani na Washirika wa Maendeleo. Kiasi halisi kilichopatikana kutokana na chanzo hiki ni Shilingi bilioni 8,963.28 sawa na asilimia 35.42 ya mapato halisi.

Kati ya Shilingi bilioni 25,307.48 zilizokusanywa, Shilingi bilioni 23,792.30 zilitolewa kwa ajili ya mishahara ya watumishi, matumizi mengine, matumizi ya maendeleo na fedha kwa ajili ya kulipa madeni yatokanayo na amana za Serikali pamoja na riba.


Kielelezo cha hapo chini kinaonesha fedha za matumizi katika mwaka wa fedha 2016/17

### Kielelezo Na. 8: Fedha za Matumizi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2016/17




*Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa bajeti 2017, Hesabu zilizokaguliwa na taarifa za miamala toka Hazina*

### Kielelezo Na. 9: Mwenendo wa makisio ya Bajeti kwa miaka mitatu



**Kielelezo Na. 10: Mwenendo wa makusanyo ya mapato kwa miaka mitatu**



Kuendelea kukopa ndani kumeongezeka kila mwaka; na kwa mwaka huu unaotolewa taarifa yake Serikali ilikopa Ndani zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa asilimia 10.08. Wakopeshaji wa Serikali kwa sehemu kubwa ni mabenki ya kibiashara ambayo kwa upande mwingine ina athari kwa wakopaji wengine, kwani sehemu kubwa ya mtaji wa mabenki unakuwa umefungwa kwenye fedha walizokopesha Serikali kwa muda mfupi na muda mrefu; na matokeo yake, riba ya kukopesha kwa watu binafsi inakuwa kubwa na gharama ya maisha inakuwa juu.

**4.6 (a) Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa**

Makadirio ya matumizi ya kawaida yaliyoidhinishwa katika mwaka uliopitiwa kwa Wizara/Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yalikuwa Shilingi bilioni 13,882.04; hili ni ongezeko la Shilingi bilioni 977.28 sawa na asilimia 7.57 ikilinganishwa na bajeti ya 2015/16 ya Shilingi bilioni 12,904,75.

Mapitio yangu ya taarifa za fedha kwa Wizara/Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yilibainisha kuwa Shilingi bilioni 13,159.75 zilitolewa kama matumizi ya kawaida sawa na asilimia 94.80 ya

makadirio ya yaliyopitishwa, hivyo Shilingi bilioni 722.29 sawa na asilimia 5.20 ya makadirio yaliyoidhinishwa hazikutolewa.

Pia, kuna ongezeko la fedha zilizotolewa kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1,094.53 sawa na asilimia 9.07 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka wa fedha 2015/16. Fedha zilizotolewa katika Mwaka wa Fedha 2015/16 zilikuwa Shilingi bilioni 12,065.22.

Ni dhahiri kuwa fedha ambazo hazikutolewa pamoja zile zilizotolewa kwa kuchelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilizuia utekelezaji mzuri wa shughuli za Serikali. Maelezo zaidi ya fedha zilizoidhinishwa pamoja na fedha zilizotolewa kama zilivyooneshwa katika **kiambatisho 4.1** kwa kila taasisi iliyokaguliwa.

**(b) Uwiano wa fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa na matumizi halisi**


Kuna ongezeko katika matumizi ya kawaida kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1,366.93 sawa na asilimia 11.35 kwa mwaka wa fedha 2016/17 ikilinganishwa na matumizi halisi ya katika mwaka 2015/16.

Matumizi halisi kwa mwaka fedha 2016/17 yalikuwa kiasi cha Shilingi bilioni 13,413.69 dhidi ya fedha zilizotolewa kiasi cha Shilingi bilioni 13,159.75. Kiasi cha Shilingi bilioni 144 kati ya fedha zilizotolewa hakikutumika; na kiasi cha Shilingi bilioni 104.02 kati ya fedha ambazo hazikutumika zilirudishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Matumizi yaliyozidi fedha zilizotolewa husababisha kuzaliwa kwa madeni ambayo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka ama kutokana na fedha kutotolewa kwa wakati au kutolewa kwa kutozingatia bajeti iliyoidhinishwa. Maelezo zaidi kuhusu madeni yanayozalishwa kila mwaka inapatikana katika sura ya kumi na moja ya ripoti hii.

Nilibaini kuwa kuna baadhi ya Wizara/Idara za Serikali zimetumia zaidi ya fedha zilizoinishwa kwa matumizi ya kawaida kwa kiasi cha Shilingi bilioni 397.23. Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya robo ya nne ya mwaka 2017 ilionesha baadhi ya Idara za Serikali zilizotumia zaidi ya bajeti zao ikiwa ni pamoja na Idara za Deni

la Taifa na Huduma za Kijamii kwa asilimia 101, Waziri Mkuu asilimia 115, Tume ya Uchaguzi asilimia 192 na Uhamiaji asilimia 143. Maelezo zaidi kuhusu fedha zilizotolewa na matumizi halisi kwa kila Wizara/Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yanapatikana katika **kiambatisho 4.1.**

#### Kielelezo Na. 11: Makisio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi kwa miaka minne



#### 4.7 (a) Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo zikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Makisio yaliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha husika kwa shughuli za maendeleo kwa Serikali kuu yalikuwa kiasi cha Shilingi bilioni 10,235.41likiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 5,266.55 sawa na asilimia 106 ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ambazo ni kiasi cha Shilingi bilioni 4,968.86.

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara, Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yilibaini kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 6,939 zilitolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 67.79 ya makisio yaliyoidhinishwa, hivyo kuonesha kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 3,296.46 sawa na asilimia 32.21 hazikutolewa. Hata hivyo, kuna ongezeko katika fedha

zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo kwa kiasi cha Shilingi bilioni 3,170.40 sawa na asilimia 84.13 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka 2015/16 za Shilingi bilioni 3,768.59. Kutotolewa kwa fedha za maendeleo kama zilivyooidhinishwa katika bajeti kunasababisha kutokamilika kwa miradi ya maendeleo iliyopangwa kufanyika, hivyo kukwamisha miradi ya maendeleo. Maelezo zaidi ya fedha zilizoidhinishwa pamoja na fedha zilizotolewa kama zilivyooneshwa katika **kiambatisho 4.2** kwa kila taasisi iliyokaguliwa.


**(b) Uwiano wa fedha za matumizi ya maendeleo zilizotolewa na matumizi halisi**

Fedha zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/17 zilikuwa Shilingi bilioni 6,939 ikiwa ni ongezeko la asilimia 84.13 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2015/16. Matumizi halisi yalikuwa Shilingi bilioni 6,045.81 sawa na asilimia 87.13 ya fedha zilizotolewa, hivyo kusababisha bakaa la Shilingi bilioni 892.60 sawa na asilimia 12.87 ya fedha zilizotolewa na kiasi cha Shilingi bilioni 80.77 ya fedha ambazo hazikutumika zilirejeshwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali mwishoni mwa mwaka.

Kuna ongezeko katika matumizi halisi katika mwaka wa fedha 2016/17 kwa Shilingi bilioni 2,316.63 sawa na asilimia 62.11 ikilinganishwa na fedha zilizotumika katika mwaka wa fedha 2015/16 ya Shilingi bilioni 3,729.72. Maelezo zaidi kuhusu fedha zilizotolewa na matumizi halisi kwa kila Wizara/Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yanapatikana katika **kiambatisho 4.2**.

Kielelezo cha hapo chini kinaonesha mwenendo wa makisio, fedha zilizotolewa na matumizi halisi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka minne.

**Kielelezo Na. 12: Makisio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi kwa miaka minne**



*Chanzo: Hesabu za Wizara/Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa zilizokaguliwa*

Kuwepo kwa bakaa kunamaanisha kwamba baadhi ya shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa ama kutokana na fedha kutotolewa kwa wakati au uwezo wa utekelezaji wa taasisi husika. Kiasi cha Shilingi bilioni 6,543.90 sawa na asilimia 27.5 ya Shilingi bilioni 23,792 ya fedha zilizotolewa, zilitolewa katika robo ya mwisho wa mwaka 2017, wakati kiasi cha Shilingi bilioni 3,511.97 sawa na asilimia 14.76 ya Shilingi bilioni 23,792.30 zilitolewa mwezi Juni 2017 ikionesa kulikuwa na ucheleweshaji wa kutolewa fedha.

#### **4.8 Fedha zilizotolewa kwa ajili ya kulipa madeni ya miaka ya nyuma Shilingi bilioni 219.47**

Wakati napitia hesabu za Wizara/Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 219.47 zilitolewa kwa ajili ya kulipa madeni ya miaka ya nyuma. Kiasi cha Shilingi bilioni 184.10 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyotokana na matumizi ya kawaida wakati kiasi cha Shilingi bilioni 35 kilikuwa ni kwa ajili ya madeni yaliyotokana na shughuli za maendeleo.

Matumizi haya hayakuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika, hivyo kupelekea matumizi nje ya bajeti na kuathiri utekelezaji wa bajeti ya mwaka husika, hatimaye kuendelea kuzalisha madeni mengine. Matokeo yake ni kuwa, Serikali itaendelea kulipa madeni ya ndani ya wazabuni, wahandisi na watumishi kwani bajeti haitekelezwi kama ilivyoidhinishwa.

#### **4.9 Mapato yasiyotokana na Kodi na bajeti iliyoidhinishwa**

Bajeti iliyoidhinishwa ya mapato yasiyotokana na kodi iliyoidhinishwa kwa Wizara, Sekretariati za Mikoa na Balozi kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilikuwa kiasi cha Shilingi bilioni 365.94, Shilingi bilioni 0.086 na Shilingi bilioni 24.56 mtawalia. Makusanyo halisi yalikuwa kiasi cha Shilingi bilioni 473.27, Shilingi bilioni 0.077 na Shilingi bilioni 27.85 kwa Wizara/Idara, Sekretariati za Mikoa na Balozi mtawalia.

Wizara na Idara za Serikali ziliweza kuvuka lengo kwa kusanya Shilingi bilioni 107.32 sawa na asilimia 29.3, Balozi zilivuka lengo kwa Shilingi bilioni 3.29 wakati Sekretariati za Mikoa zilishindwa kufikia lengo kwa Shilingi bilioni 0.01 sawa na asilimia 10.4 ya makisio yaliyoidhinishwa.

Hata hivyo taarifa ya robo ya nne ya utekelezaji wa bajeti robo ya nne ya mwaka 2017 inaonesha kwamba mapato yaliyokusanywa kutoka katika vyanzo visivyo vya kodi yalichanganuliwa kwa asilimia kwa kuzingatia ufanisi wake ambapo Gawio kutoka mashirika ya umma ilitoa asilimia 93 ilinganishwa na asilimia 80 ya mwaka uliopita, Kerejesha Mitaji ya ziada asilimia 35, Wizara na Mikoa asilimia 80 ikilinganishwa na 39 ya mwaka jana na Mamlaka ya Mapato ilikusanya maduhuli yasiyotokana na kodi kwa asilimia 279 ikilinganishwa na 207 ya mwaka 2015/16. Matokeo yake ni kwamba mapato yasiyotokana na kodi yalifikia asilimia 76 ikilinganishwa na asilimia 71 iliyofikiwa mwaka 2015/16. Muhtasari ni kama unavyoonekana hapa chini.

## Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti

### Jedwali Na. 15: Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana kutoka vyanzo visivyo vya kodi na asilimia ya ufanisi wake kwa miaka miwili (*Kiasi katika Shilingi bilioni*)

	Makisio 2016/17	Makusanyo Halisi 2016/17	Asilimia ya Makisio	Makusanyo Halisi 2015/16	Ongezeko/P ungufu	Asilimia ya Badiliko mwaka kwa mwaka
Gawio la Mashirika ya Umma	756.60	701.20	93%	388.60	312.60	80%
Marejesho Mitaji ya Ziada	549.90	192.80	35%	-	192.80	0%
Wizara na Mikoa	1,386.50	1,107.70	80%	799.40	308.30	39%
Mamlaka ya Mapato	25.60	71.30	279%	23.20	48.10	207%

*Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa bajeti robo ya nne 2017*


### Jedwali Na. 16: Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa miaka minne (*Kiasi katika Shilingi bilioni*)

Mwaka wa Fedha	Maelezo	Makisio	Makusanyo Halisi	(Pungufu)/ Zaidi ya Makusanyo	% ya Halisi Dhidi ya Makisio	% ya Makisio dhidi ya Kisichokusanywa
2016/17	Wizara/Idara za Serikali	366	473	107	129	29
	Sekretariati za Mikoa	0.09	0.08	(0)	90	(10)
	Balozi	25	28	3	113	13
2015/16	Wizara/Idara za Serikali	692	727	36	105	5
	Sekretariati za Mikoa	26	0.047	(26)	0	(100)
	Balozi	18	22	4	122	22
2014/15	Wizara/Idara za Serikali	702	598	(104)	85	(15)
	Sekretariati za Mikoa	40	89	49	225	125
	Balozi	16	19	4	123	23
2013/14	Wizara/Idara za Serikali	640	532	(107)	83	(17)
	Sekretariati za Mikoa	0	14	14	28,571	28,471
	Balozi	17	21	4	123	23

*Chanzo: Hesabu za Wizara/Idara za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Balozi*


**Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara/Idara za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Balozi  
(Kiasi katika Shilingi bilioni)**

Mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara na Idara za Serikali




*Chanzo: Hesabu zilizokaguliwa za Wizara na Idara za Serikali*

Mwenendo wa mapato yasiyotokana na Kodi kwa Wizara na Idara za Serikali yanaonesha kuwa makadirio na makusanyo halisi yameongezeka katika kipindi cha miaka miwili; na kwa mwaka husika yalishuka ukilinganisha na mwaka uliopita. Licha ya kuwapo kwa ongezeko katika makusanyo, baadhi ya Wizara na Idara za Serikali zimekuwa haziweki makisio ya mapato yasiyotokana na kodi ingawa wamekuwa wakikusanya. Hii inaonesha kuwa kuna upungufu wa makisio ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Wizara na Idara za Serikali.

**Kielelezo Na. 14: Mapto yasiyotokana na Kodi Kwa Sekretarieti za Mikoa***Chanzo: Hesabu zilizokaguliwa za Sekretariati za Mikoa*

Kumekuwa na hali ya kupanda na kushuka kwa makisio na makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Sekretarieti za Mikoa. Baada ya kuitia taarifa za fedha za Sekretariati za Mikoa nimebaini kuwa wengi walikusanya ingawa walikuwa hawana makisio. Ninashauri Sekretariati za Mikoa kuweka makisio ya mapato yasiyotokana na kodi na kuongeza bidii katika kufikia malengo watakayokuwa wamejiwekea.

## Kielelezo Na. 15: Mapato yasiyotokana na Kodi kwa Balozi



*Chanzo: Hesabu za Balozi zilizokaguliwa*

Mwenendo wa mapato yasiyotokana na kodi kwa balozi yanaonesha matokeo chanya; baadhi ya balozi zimekusanya zaidi ya malengo waliyojiwekea wakati nyingine zikishindwa kufikia malengo waliyojiwekea. Kati ya hesabu za balozi 39 nilizopitia, balozi 23 zimekusanya zaidi ya makisio yao wakati balozi 16 hazikuweza kufikia malengo waliyokuwa wamejiwekea.

#### 4.10 Fedha za Ushuru wa Maendeleo ya Utalii ambazo hazikuletwa kiasi cha Shilingi 8,248,083,588

Kanuni ya 4(2) ya Kanuni ya Tozo za Maendeleo ya Utalii, 2013 inamtaka Mkurugenzi wa Utalii kupeleka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) orodha ya wote waliosajiliwa kuhusika na maswala ya malazi ya watalii na ambao wanapaswa kulipa tozo ya kulala. Fedha zote zitumwe kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika mwaka wa fedha husika na baadaye kuwekwa katika akaunti ya Tozo za Maendeleo ya Utalii kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 9 (1).

Katika mwaka wa ukaguzi, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya kiasi cha Shilingi 8,248,083,588 kama ilivyokuwa katika taarifa ya makusanyo ya kila mwezi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi mwezi Juni 30, 2017 fedha hizo zilizokuwa zimekusanywa hazikuwa zimehamishiwa kwenye akaunti ya Tozo za Maendeleo ya Utalii kama inavyotakiwa na Kanuni husika. Katika mwaka wa Fedha 2015/16 kiasi cha Shilingi bilioni 6,357,529,854 kilichokusanywa na Mamlaka ya Mapato kwa tozo za Maendeleo ya Utalii hazikutolewa kwa Wizara ya Malisasili, niliandika kwenye taarifa yangu iliyopita.

Kushindwa kuwasilisha makusanyo kama inavyotakiwa na kanuni husika kunazuia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Utalii ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa bidhaa za utalii, kukuza masoko ya utalii, kujenga uwezo kwa watumishi wa sekta ya utalii, utafiti wa utalii na shughuli nyingine yoyote kwa ajili ya maendeleo na kuboresha sekta ya utalii kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 10 (a-e) cha Kanuni ya Tozo za Maendeleo ya Utalii, Kanuni, 2013.

Kwa minajili hiyo, ni maoni yangu kuwa madhumuni ya mfuko yanaweza yasifikasiwe.

#### **4.11 Mapato yasiyotokana na Kodi ambayo hayakuwasilishwa Mfuko Mkuu Shilingi 14,546,473,045**

Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2001, “kinataka maduhuli au fedha nyingine zozote zinazokusanywa au kupokelewa kwa ajili ya Serikali ziwekwe katika Mfuko Mkuu isipokuwa pale tu ambapo fedha zilizokusanywa zinapelekwa katika mifuko mingine iliyoanzishwa kisheria kwa madhumuni maalumu au kubakizwa katika mamlaka iliyozipokea kwa ajili ya kulipia gharama za mamlaka hiyo kama inavyotakiwa na Sheria maalumu”.

Ukaguzi wangu kwenye ofisi za ng'ambo ya nchi ulibaini kuwapo kwa maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa tarehe 5 Julai 2016 wenye

namba ya kumbukumbu CA 441/527/01 kukataza balozi zetu kutotumia fedha wanazokusanya katika kuendesha shughuli zake kama walivyokuwa wakifanya hapo awali.

Hivyo basi fedha zilizokusanya sизizotokana na kodi katika balozi zetu 21 kwenye mwaka wa fedha 2016/17 kiasi cha Shilingi 14,546,473,045 hakikuwasilishwa katika Mfuko Mkoo kinyume na Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2001; badala yake, kiasi hicho kilibaki katika akaunti za Balozi zetu bila kutumika kwa muda mrefu. Mchanganuo wake ni kama unavyoonekana katika jedwali hapo chini;

**Jedwali Na. 17: Balozi zilizokusanya Maduhuli pasipokuyarejesha kwenye Mfuko Mkoo**

<b>SN</b>	<b>Jina la Ubalozi</b>	<b>Shilingi</b>
1	Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa	146,072,597
2	Ubalozi wa Tanzania Brasilia	118,680,839
3	Ubalozi wa Tanzania Cairo	45,124,511
4	Ubalozi wa Tanzania Muscat	2,130,432,332
5	Ubalozi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa NY	1,009,255,443
6	Ubalozi wa Tanzania Nairobi	202,560,365
7	Ubalozi wa Tanzania Ottawa	167,044,974
8	Ubalozi wa Tanzania Kinshasa	65,041,096
9	Ubalozi wa Tanzania Abuja	1,169,441,535
10	Ubalozi wa Tanzania London	2,706,569,324
11	Ubalozi wa Tanzania Maputo	23,160,143
12	Ubalozi wa Tanzania New Delhi	870,325,189
13	Ubalozi wa Tanzania Tokyo	1,303,086,457
14	Ubalozi wa Tanzania Washington DC	3,842,107,471
15	Ubalozi wa Tanzania Kampala	154,940,892
16	Ubalozi wa Tanzania Pretoria	102,644,739
17	Ubalozi wa Tanzania Kigali	45,610,667
18	Ubalozi wa Tanzania Bujumbura	45,712,430
19	Ubalozi wa Tanzania Kuala Lumpur	86,588,539
20	Ubalozi wa Tanzania Moroni	247,294,670
21	Ubalozi wa Tanzania Kuwait	64,778,832
	<b>JUMLA</b>	<b>14,546,473,045</b>

*Chanzo: Hesabu za Balozi zilizokaguliwa*

Ni mtazamo wangu kuwa, kutopeleka fedha zilizokusanya kiasi cha Shilingi 14,546,473,044 kama inavyotakiwa na Sheria ya

Fedha za Umma sio tu kumezuia Serikali fursa ya kutumia fedha hizo bali pia imeongeza shaka ya fedha hizo kutumika bila utaratibu.

Nashauri menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashakiri kuhakikisha kuwa fedha zilizokusanywa zimeripotiwa ipasavyo kama inavyotakiwa na Kifungu cha 11 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 na kupunguza shaka ya fedha hizo kutumika bila utaratibu maalumu ikiwa ni pamoja na kupunguza gherama za benki katika kutunza bakaa.

**4.12 Uendeshaji wa Mitambo ya Kuchenjua Madini bila kuwapo kwa leseni hivyo kupelekea upotevu wa maduhuli kiasi cha Shilingi 158,436,600 na Dola za Kimarekani 71,400**

Kifungu cha 60(1) cha Sheria ya Madini Na.14 ya Mwaka 2010 kinasema “mtu ambaye hana haki ya kuchenjua madini mahali popote ndani au nje ya eneo la madini anaweza akaomba leseni ya kuchenjua madini”. Kifungu kidogo cha tatu cha kifungu hicho hicho inasema “Kamishina atamwandikisha mwombaji na kutoa leseni baada ya kukidhi vigezo na masharti kama yalivyoolezewa katika leseni”.

Kanuni ya 3(2) ya Kanuni ya Madini ya mwaka 2010 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2012) imeweka bayana kwamba leseni ya kuchenjua madini gherama yake ni dola za kimarekani 200, ada ya kaandaa leseni ni dola za kimarekani 200 na ada ya kila mwaka kwa leseni ni dola za kimarekani 1000 kama ilivyo katika jedwali la kwanza la Kanuni ya Madini ya mwaka 2001 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2012).

Ukaguzi wangu wa leseni za kuchenjua madini kwa Mikoa ya Mwanza, Kahama na Shinyanga ulionesha kuwa mitambo ya kuchenjua madini 8, 25 na 51 mtawalia huo ilikuwa inatumika bila kuwa na leseni halali za uendeshaji kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini;

**Jedwali Na. 18: Mitambo ya kuchenjua madini bila kuwa na leseni**

Maelezo	Mwanza	Kahama	Shinyanga	Jumla
Mitambo ya Kuchenjulia madini inayoendeshwa bila kuomba kibali na hivyo kutokua na leseni	8	2	41	51
Mitambo ya kuchenjulia madini inayoendeshwa bila kuwa na leseni ingawa wametuma maombi yao kwa Kamshina wa Madini	-	23	10	33
Jumla	8	25	51	84

Kutokana na kutokuwapo kwa leseni za mitambo ya kuchenjulia madini 51, Serikali imepata hasara ya dola za Kimarekani 71,400 sawa na Shilingi 158,436,600<sup>18</sup> kwa mwaka (Mitambo 51x (USD 200 ada ya matayarisho ya leseni + USD 200 ada ya maombi ya leseni + USD 1000 ada ya leseni kwa mwaka)). Pia kuendesha mitambo ya kuchenjulia madini bila leseni ni kosa la kisheria ambalo limepelekea upotevu wa kodi ya pango na ada ya maombi kwa mwaka.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa mitambo 33 ilikuwa ikiendeshwa bila kuwa na leseni ingawa tayari waendeshaji walikuwa wameomba leseni kwa Kamishina wa Madini, matokeo yake ni kuwa Serikali ilipoteza kiasi cha dola za Kimarekani 33,000 sawa na Shilingi 73,227,000 kama ada ya leseni kwa mwaka.

Ninapendekeza kuwa Wizara ya Madini ihakikishe watu wote wanaojihusisha na mitambo ya kuchenjulia madini wanatekeleza Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake. Kushindwa kufanya hivyo ni kosa; na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wakiukaji. Pamoja na hayo, ufuatiliaji wa hatua za kurejesha fedha ambazo hazijakusanywa ufanyike mara moja na Wizara husika.

<sup>18</sup> Dola moja ya Marekani kwa shilingi 2,219 za Tanzania

## SURA YA TANO

### 5.0 HESABU JUMUIFU ZA TAIFA

#### 5.1 Ukaguzi na Usimamizi wa Deni la Taifa

##### 5.1.1 Utangulizi


Deni la Taifa linajumuisha madeni inayodaiwa Serikali Kuu na Taasisi zake kama inavyoelezwa katika Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebisha 2004). Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali, 1974 Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali.

##### 5.1.2 Mseto wa Deni la Taifa

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2017 lilikuwa Shilingi bilioni 46,081.43 ambapo deni la ndani lilikuwa Shilingi bilioni 13,335.65 na deni la nje Shilingi bilioni 32,745.78 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 5,042.05 sawa na asilimia 12 ikilinganishwa na deni la Shilingi bilioni 41,039.39 lililoripotiwa tarehe 30 Juni 2016.

Deni la taifa limekuwa likiendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwapo kwa nakisi ya mapato ya serikali na matumizi, ubadilishwaji wa hati za ukwasi kugharamia bajeti ya serikali, ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo pamoja na hasara katika kubadilisha fedha za kigeni ikisababishwa na kushuka kwa thamani ya Shilingi ikilinganishwa na fedha nyingine za kigeni ambazo ni imara. Chati hapo chini kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa miaka mitano iliyopita;

### Kielelezo Na. 16: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano



#### 5.1.3 Mseto wa Deni la Ndani


Mseto wa deni la ndani unajumuisha dhamana zinazouzwa sokoni, na zisizouzwa zenye ukomo tofauti kama vile dhamana za muda mrefu na hati fungani. Hadi kufikia 30 Juni 2017, Deni la ndani lilifikia Shilingi 13,335.65 bilioni ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi bilioni 11,193.39 zilizofikiwa mwishoni mwa Juni, 2016. Deni la ndani limeongezeka kwa Shilingi bilioni 2,142.27 sawa na asilimia 19 ya deni la ndani lilorekodiwa mwaka jana.

#### 5.1.4 Mseto wa Deni la Nje

Deni la nje linahusisha mikopo kutoka, Taasisi za Kimataifa na Washirika wa Maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni 2016 Deni la nje lilikuwa Shilingi bilioni 32,745.78 sawa na asilimia 71 ya deni la Taifa. Deni hili limeongezeka kwa Shilingi bilioni 2,899.78 sawa na asilimia 10 ya deni la nje la Shilingi bilioni 29,846.00 liloripotiwa mwaka 2015/16. Mlinganisho wa Madeni ya nje kwa

aina tofauti ya vyanzo ni kama ilivyo katika **Kielelezo Na. 2** hapa chini;

**Kielelezo Na. 17: Vyanzo vya deni la Nje hadi tarehe 30 Juni 2017**



Ukaguzi wangu umebaini kwamba, ongezeko la deni la nje limechangiwa na ukopaji kutoka katika Mashirika ya Kimataifa kama vile Shirika la Maendeleo la Kimaitaifa (IDA) ambapo tumepokea jumla ya Shilingi bilioni 995.7 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo na kijamii ikiwa ni pamoja na Mradi wa uvezeshaji wa uzalishaji katika kaya maskini (Shilingi bilioni 205.9), Mradi wa Kuboresha Biashara na Usafirishaji Kusini mwa Afrika (Shilingi bilioni 168.3), Programu ya Kuboresha Miji na Serikali za Mitaa (Shilingi bilioni 95.2), Programu ya Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu (Shilingi bilioni 52.3), Mradi Na. II wa Miji ya Kimkakati Tanzania (Shilingi bilioni 51.8).

Vilevile, Serikali ilipokea fedha kutoka nchi wahisani (Ufaransa, Saudi Arabia na Japan) Shilingi bilioni 181.3, Mikopo yenye Masharti ya Kibashara (ENCB) katika mfumo wa Mpangilio wa

Mkopo wa nje kiasi cha Shilingi bilioni 372.7. Mikopo kutoka ENCB ambayo hutolewa za Benki ya Korea, China na India zilielekezwa kwenye miradi muhimu kama vile Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa kwa ajili ya Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa (Shilingi bilioni 28.2), Awamu ya Kwanza ya Ujenzi wa Kituo cha Afya kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Afya Muhibili (Shilingi bilioni 17.1), Mradi wa Gesi Asilia wa Mnazi Bay na Songsongo (Shilingi bilioni 15.0), Mradi wa Usambazaji Maji Dar es Salaam na Chalinze (Shilingi bilioni 61.4), na Awamu ya Tatu ya Mradi wa Taifa wa TEHAMA (Shilingi bilioni 41.3).

Pia, Serikali ilipokea fedha kutoka Benki za biashara kiasi cha Shilingi bilioni 978.0 ikiwemo Shilingi bilioni 887.6 kutoka Benki ya Credit Suisse AG (UK) ikiwa ya masharti nafuu, na Shilingi bilioni 74.2 kutoka Benki ya Hong Kong Shanghai kwa ajili Ujenzi wa Jengo Na. III la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Benki ya ING N.V. Corp. Serv. Amsterdam ilitoa Shilingi bilioni 16.1 kwa ajili ya Ukarabati na Uboreshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. **Kiambatisho 5.1** kinaonesha mchanganuo wa miradi iliyowezeshwa na mikopo mipyä iliyotolewa kwa Serikali kwa mwaka 2016/17.

Ingawa ukopaji wa kibiashara ni muhimu kiuchumi hasa katika miaka ya karibuni ambapo serikali inashughulikia miradi mikubwa ya miundombinu, ninaona kuwa ukuaji mkubwa wa deni la taifa kupitia mikopo ya nje unapaswa kutazamwa kwa makini na tahadhari ili kupunguza ukuaji wake pamoja na madhara ya baadaye.

### **5.1.5 Mkakati wa Usimamizi wa Deni la Taifa**

#### **5.1.5.1 Kasi ndogo ya ukuaji wa soko la hati fungani za serikali**

Uchambuzi wangu wa muda wa kuiva kwa dhamana za serikali kufikia 30 Juni, 2017 ulibaini kwamba asilimia 72 ya dhamana hizo zinaivaa ndani ya kipindi cha miaka mitano ikilinganishwa na asilimia 59 katika kipindi hicho hicho mwaka 2015/16 kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

## Jedwali Na. 19: Muda wa kuiva dhamana za serikali

Kipindi kabla ya kuiva	2016/17	Muundo	2015/16	Muundo
	Kiasi katika Sh.TZ bilioni	%	Kiasi katika Sh.TZ bilioni	%
Siku 35 hadi siku 364	4,948.20	42%	679	11%
>1 hadi miaka 3	2,011.90	17%	1,197.20	19%
>3 hadi miaka 5	1,460.90	12%	1,826.70	29%
>5 hadi miaka 10	2,323.40	20%	2,036.20	32%
Zaidi ya miaka 10	963.7	8%	569.9	9%
Total	11,708.10	100%	6,309.00	100%


*Chanzo: Mpango wa Uuzaji Hati Fungani*

Jedwali la hapo juu linaonesha dhahiri kuwa hati fungani za muda mfupi zinatawala sehemu kubwa ya soko la dhamana zikiwa na asilimia 42 zikifuatiwa na hati fungani zinazoiva kati ya miaka miwili na mitano zikiwa na asilimia 29. Uchambuzi huu unaonesha pia kwamba, soko la dhamana za miaka kumi au zaidi lipo katika kiwango cha chini; hivyo, kufanya wawekezaji wa muda mrefu kushindwa kuvutiwa kushiriki katika soko hilo.

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa katika kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na ongezeko kubwa la kuhuisha hati fungani za muda mfupi na kiwango kikubwa cha riba katika dhamana za serikali.

**Kielelezo Na. 18** hapa chini kinaonesha:

**Kielelezo Na. 18: Kuhuishwa kwa hati fungani na Malipo ya Riba,  
2015 hadi 2017**



Uchambuzi wa hapo juu unaonesha kuwa hati fungani za muda mfupi zimeendelea kutawala soko la dhamana za Serikali kitu ambacho kwa mtazamo wangu kinavuruga mkakati wa Serikali wa kupunguza madai yatokanayo na mikopo inayoiva ndani ya muda mfupi. Hivyo ni muhimu kwa Serikali kuupa kipaumbele kinachostahili mkakati wake wa kupata fedha ili kumudu vihatarishi vitokanazo na kuhuisha dhamana za Serikali pale inapolazimu.

*Kwa kuzingatia hayo, napendekeza yafuatayo kwa Serikali: (i) Itenge sehemu ya mapato ya ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la ndani ili kupunguza kiwango kinachohuishwa kila mwaka; na (ii) Iweke juhudini zaidi katika kuhakikisha kuwa mseto wa deni la taifa unakuwa katika mizania, na kuwezesha maendeleo ya soko la dhamana za Serikali za muda mrefu.*

#### 5.1.5.2 Ukuaji hafifu wa dhamana za Serikali katika soko la mtaji

Uchambuzi wangu wa taarifa za fedha za Fungu 22 na Mpango wa Ukopaji wa Ndani kwa kipindi cha miaka mitatu, kuanzia 2014/15 mpaka 2016/17, ulibaini kwamba soko la dhamana za Serikali za muda mrefu limekuwa halifikii malengo yaliyokusudiwa. Hapa

chini kinaonesha mwenendo wa soko la hati fungani za muda mrefu kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

#### Kielelezo Na. 19: Mwenendo wa soko la hati fungani za muda mrefu



*Chanzo: Mpango wa Ukopaji wa Ndani na hesabu za Fungu 22*

Kielelezo cha hapo juu kinaonesha kuwa hati fungani za muda mrefu zilizowekwa sokoni hazikufikia malengo yaliyokusudiwa. Kiwango kilichokusudiwa kukopwa Kikilinganishwa na kiwango halisi kilichopatikana ni wazi kuwa soko la mtaji halikufikia malengo.

zaidi ya hapo, ilifahamika kwamba katika mwaka 2016/17 Serikali ilikopa Shilingi bilioni 2,420 kutoka soko la mtaji ikilinganishwa na Shilingi bilioni 2,670.7 iliyokusudiwa katika Mpango wa Ukopaji wa ndani. Hata hivyo, uchambuzi wa kina wa mwenendo wa kukopa ulibaini kuwa soko la dhamana za muda mrefu liliwezesha kupatikana kwa Shilingi bilioni 2,420 mwaka 2016/17 [2015/16: Bilioni 1,076.80] ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 125. Kwa mtazamo wangu, huu ni mwelekeo mzuri katika kuendeleza soko la dhamana za serikali za muda mrefu ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Ingawa mipango na mikakati ya Serikali inaweza kuwa imechangia katika kuboresha soko la dhamana za Serikali, nina mashaka na ukuaji hafifu wa soko la dhamana hapa nchini

ukihusishwa na jinsi Serikali inavyoendelea kuchagua kuhuisha hati fungani za muda mfupi ili kutimiza mahitaji yake ya kifedha.

*Napendekeza Serikali ifanye yafuatayo ili kuboresha soko la mtaji: (i) Kuzingatia kufungua soko la mtaji kuruhusu wakazi wasio wa nchi za Afrika Mashariki kushiriki, (ii) Kupunguza vikwazo vya kushiriki katika soko la mtaji kitu ambacho kinapunguza kasi ya ushiriki<sup>19</sup>, (iii) Kuendelea kuboresha sheria na kanuni zilizopo kuruhusu mtiririko wa mitaji nje na ndani ya soko pamoja na kuboresha soko la hati fungani za muda mrefu; na (iv) Kufanya uelimishaji wa jamii juu ya soko la mtaji kwa lengo la kuliboresha.*

#### **5.1.5.3 Kukopa Ndani ya Nchi Kupita Kiwango Kilichowekwa Katika Mpango wa Ukopaji wa Ndani kwa asilimia 7.2**

Mapitio yangu ya Mpango wa Ukopaji wa Ndani kwa mwaka 2016/17 ulibaini kwamba Serikali ilipanga kukopa Shilingi bilioni 6,480 kwa kuza hati fungani za muda mfupi na muda mrefu. Hata hivyo, Serikali ilikopa Shilingi bilioni 6,944.99 kinyume Mpango wa Ukopaji wa Ndani.

Pia, niligundua kuwepo kwa deni (overdraft) katika akaunti za serikali za benki kuu lililofikia Shilingi bilioni 1,546.56 mnamo 30 Juni, 2017 [2015/16: Shilingi bilioni 1,188.09]. Matokeo yake, riba iliongezeka kwa asilimia 269 kutoka Shilingi bilioni 42.57 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 157.22 mwaka 2016/17. Kama Serikali ingetekeleza matumizi ya akaunti moja ya hazina (Treasury Single Account), naamini kwamba riba itokanayo na deni hilo ingepungua kwa kiwango kikubwa; na fedha hizo kuelekezwa katika maeneo mengine.

*Hivyo, nashauri Serikali ifanye yafuatayo: (i) Kuharakisha utekelezaji wa akaunti moja ya hazina (Treasury Single Account) na maandalizi ya utekelezaji wa Makubaliano ya Jumuiya ya*

---

<sup>19</sup> Serikali ifikirie kuanzisha hati fungani za muda mrefu zaidi (miaka 20 na miaka 30) katika soko la dhamana ili kufanikiwa katika malengo yake na iendeleee kuboresha na kudumisha soko la hati fungani za miaka 15.

*Afrika Mashariki katika masuala ya Kifedha; na (ii) Kufuata Mpango wa Ukopaji wa Ndani inapokopa ndani ya nchi.*

#### **5.1.5.4 Dhamana za Serikali kusababisha msongamano wa sekta binafsi**

Katika kipindi cha mwaka 2016/17, Serikali iliuza hati fungani za muda mfupi za Shilingi bilioni 4,524.71. Hii ni kinyume na Mpango wa Ukopaji wa Ndani, ambapo ilipanga kuuza dhamana za Shilingi bilioni 3,594.76 kiwango ambacho ni zaidi kwa asilimia 26 ya mpango.

Hali hii ilidhihirika pia nilipopitia taarifa za minada 10 ya hati fungani za muda mfupi iliyofanyika kati ya februari na juni 2017, ambapo Serikali iliweka sokoni dhamana za Shilingi bilioni 1,393.40 kati ya Shilingi bilioni 1,382.60 iliyojipangia na kufanikiwa kuuza dhamana za thamani ya Shilingi bilioni 1,637.96. Niligundua pia kuwapo kwa hali ya hati fungani za muda mfupi kutakiwa na wawekezaji kuliko kiwango kilichotolewa, kwani wawekezaji walitoa kiasi cha Shilingi bilioni 3,853.05 kitu ambacho kilisababisha kuzidi kwa kiasi cha Shilingi bilioni 2,459.65.

Suala la kulegalega kwa uwezo wa taasisi za kifedha kukopesha na kuongezeka kwa mikopo isiyolipika limepelekea taasisi za fedha kuvutiwa zaidi kuwekeza katika dhamana za Serikali za muda mfupi ambazo hazina vihatarishi. Mtazamo huu unaendana na mashaka yaliyojiteza kwenye Mkakati wa Madeni wa Muda wa Kati wa Desemba 2017 na Waraka wa Benki Kuu Na. FA.178/461/01/02 wa tarehe 19 Februari, 2018. Masuala haya pamoja na kushuka kwa uingiaji wa fedha za kigeni ni kati ya sababu kubwa zilizochangia soko la dhamana za Serikali lionekane linafanya vizuri. Hata hivyo, ni muhimu Serikali kutazama mwenendo huu wa kiuchumi kwa makini, kwani kwa mtazamo wangu uwezeshwaji wa sekta binafsi kifedha unaathiriwa na taasisi za fedha kupendelea zaidi dhamana za Serikali.

*Kwa mantiki hiyo, ni muhimu Serikali ichukue hatua sahihi za kisera katika kurekebisha hali hii ambayo inahatarisha ukuaji wa sekta binafsi na uchumi kwa ujumla katika muda wa kati na mrefu.*

### **5.1.6 Shughuli za ukopaji**

#### **5.1.6.1 Mikopo iliyosainiwa mikataba lakini haijapokelewa, Shilingi bilioni 2,367**

Katika mapitio yangu ya orodha ya mikopo iliyosainiwa lakini haijapokelewa niligundua kuwapo kwa mikataba 16 iliyosainiwa kati ya mwaka 2001 na 2016 inayofikia kiasi cha Shilingi bilioni 2,367 ambayo haijatambuliwa wala kuripotiwa katika taarifa za deni la taifa hadi kufikia 30 Juni 2017.

Ufuatiliaji zaidi ulibaini kuwa, kati ya mikataba hiyo, ipo miwili ilioingiwa mwaka 2001 kiasi cha Shilingi bilioni 11; ambapo, mkopeshaji anadai kufanya malipo yote lakini Serikali imeshindwa kuthibitisha mapokezi wala matumizi ya ya fedha hizo. Hii inadhihirisha kwamba mfumo wa uwajibikaji katika mapokezi na matumizi ya mikopo hapa nchini hauko thabiti.

*Napendekeza Serikali ifanye yafuatayo: (i) Kuweka utaratibu thabiti wa kufuatilia na kutathmini mapokezi na matumizi ya fedha zitokanazo na deni la taifa. Utaratibu wa ufuatiliaji utahakikisha watekelezaji wa miradi wanatunza kumbukumbu sahihi za matumizi ya fedha hizo; na (ii) Kuanzisha utaratibu ili kuwezesha usuluhishi wa taarifa za madeni na kuboresha maandalizi na mipango ili kuhakikisha masharti ya mikopo yanatekelezwa kabla ya kusaini mikataba na kupokea fedha hizo.*

#### **5.1.6.2 Mapungufu katika utaratibu wa kuingiza kumbukumbu za mapokezi ya mikopo**

Katika mapitio niliyofanya katika sampuli ya miamala 53 ya mikopo iliyopokelewa kiasi cha Shilingi bilioni 56.1 ambazo kumbukumbu zake ziliingizwa katika mfumo wa kutunza kumbukumbu za madeni ‘CS-DRMS’ sambamba na nyaraka zake za uthibitisho, niligundua kwamba mapokezi ya fedha za mikopo

yaliingizwa katika kumbumumbu bila kuwa na uthibitisho kutoka kwa waliopokea fedha hizo. Kumbukumbu hizo ziliingizwa kwa kigezo cha taarifa ambazo Fungu 22 ilipokea kutoka kwa wakopeshaji.

Kwa mtazamo wangu, Idara ya Fedha za Nje, ambayo ndiyo yenye wajibu wa kufuatilia kutolewa kwa fedha kwa wakopeshaji na wapokeaji inapaswa kuwapatia uthibitisho wa maandishi kwa fungu 22 juu ya mapokezi ya fedha za mikopo ili kutunza kumbukumbu stahili na sahihi.

*Naishauri Serikali kupata kutoka kwa wanufaika uhakika wa mapokezi ya fedha za mikopo kabla ya kuingiza kumbukumbu hizo katika mfumo wa kutunza kumbukumbu za madeni.*

#### 5.1.6.3 Usimamizi usioridhisha wa mikataba ya mikopo iliyohaulishwa ‘on-lending contracts’

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa muundo wa usimamizi wa mikataba ya mikopo iliyohaulishwa na usimamizi wa deni la taifa kwa ujumla umegawanyika. Msajili wa Hazina anasamamia kanzi data, kutoa taarifa na malipo ya mikopo iliyohaulishwa kwa Mashirika ya Umma wakati ile ya Serikali ya Zanzibar iko chini ya Idara ya Sera iliyopo chini ya Fungu 21-Hazina, lakini taarifa ya bakaa yake inatolewa na Fungu 50-Wizara ya Fedha. Mgawanyiko wa namna hii umekuwa ni moja ya changamoto kubwa katika uratibu na kutoa taarifa za deni la taifa.

zaidi ya hapo, kupitia taarifa kutoka Fungu 22 ya mikataba ya mikopo iliyohaulishwa, nilibaini kuwapo kwa mikataba 30; kati ya hiyo saba (7) ikiwa ni kwa Serikali ya Zanzibar na 23 kwa Mashirika ya Umma. Hata hivyo, mpaka kufikia kipindi cha uandishi wa taarifa hii, mwezi Februari 2018, sikuweza kupatiwa mikataba 25 kati ya 30 iliyopo katika taarifa ya Fungu 22.

Kinyume na taarifa nilizopokea kutoka Fungu 22, taarifa za fedha za Msajili wa Hazina za mwaka unaoishia 30 Juni 2017 zinaonesha kuwapo kwa mikataba minne tu ya mikopo iliyohaulishwa kwa Mashirika ya Umma hivyo kuwa na tofauti ya mikataba 19 ambayo Msajili wa Hazina hajaitambua. Tofauti hizi zinazidi

kudhihirisha kutokuwapo kwa mfumo thabiti wa uratibu na changamoto za utoaji taarifa za deni la taifa na usimamizi wake kwa ujumla.

Kwa kuongezea, mikataba minne iliyopo katika taarifa za Msajili wa Hazina ina kiwango tofauti na taarifa za Fungu 22, kitu ambacho kinashuhudia kutokuwepo kwa urari wa taarifa kati ya pande zinazohusika. Kwa kuzingatia mapungufu niliyoeleza, taarifa za mikataba ya mikopo iliyohaulishwa katika idara mabalimbali za Serikali ni za kupotosha.

#### **5.1.6.4 Kutolipwa kwa mikopo iliyohaulishwa**

Katika mapitio ya marejesho ya mikopo iliyohaulishwa nilibaini kwamba mikataba yote 13 iliyopo katika taarifa ya Msajili wa Hazina marejesho yake hayafanyiki kulingana na matakwa ya mikataba husika. Hii imepelekea mikopo minne kuombewa kufutwa na mitatu kuongezewa muda wa kulipa. Mikopo sita hailipwi kwa wakati kutohana na changamoto za fedha katika Mashirika husika. Kwa mikopo iliyohaulishwa ambayo haipo katika taarifa za Msajili wa Hazina sikuweza kupata taarifa za urejeshwaji wake. Kuhusu changamoto zinazojitokeza katika kurejesha mikopo iliyohaulishwa, maoni yangu ni kwamba miradi ipitiwe kwa makini; na uchambuzi wa kina wa kiufundi ufanyike kabla haijaidhinishwa.

*Napendekeza yafuatayo kwa Serikali: (i) Kutekeleza pendekozo langu la muda mrefu la kuanzisha ofisi ya pamoja ya kusimamia shughuli za deni la taifa; (ii) Kuhakikisha mikopo inayotolewa katika utaratibu wa kuhaulisha inarejeshwa na wahusika kadiri ya makubaliano; (iii) Kuhakikisha uhifadhi bora wa mikataba na kupatikana ile ambayo hajaonekana na kuiwasilisha kwa uhakiki; na (iv) Kuhakikisha usuluhishi wa viwango vya mikopo iliyohaulishwa ili kutunza kumbukumbu sahihi baina ya pande zote zinazohusika na utunzaji wake.*

### 5.1.6.5 Kuchelewesha kulipa madeni ya Benki Kuu, Shilingi bilioni 46.73

Uchambuzi wangu wa mwenendo wa gharama za kuhudumia madeni ambayo Serikali inadaiwa na Benki Kuu ulibaini kuwapo kwa jumla ya Shilingi bilioni 46.73 ambazo hazikulipwa kwa wakati. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 42.57 zinatokana na riba ya nakisi ya Serikali, na Shilingi bilioni 4.15 ikiwa ni sehemu ya Serikali ya gharama za kudhibiti ukwasi kwa mwaka 2015/16 ambapo zilikuwa hazijalipwa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Oktoba 2017.

Katika kufanya uchambuzi zaidi, niligundua kuwapo kwa mkataba wa makubaliao (MoU) kati ya Serikali na Benki Kuu ambao unaitaka Serikali kulipa kila robo mwaka sehemu yake ya gaharama ya kudhibiti ukwasi pindi hati ya madai inapotolewa. Suala la ucheleweshaji wa malipo likiendelea litaongeza kuwapo kwa mali za Benki Kuu zisizo na tija; na kwa mtazamo wangu, hii ni dalili ya Serikali kushindwa kutimiza majukumu yake ya kifedha kinyume na Sehemu ya 3.02 ya mkataba wa makubaliao kati yake na Benki Kuu.

*Hivyo, natoa wito kwa Serikali: (i) Kulipa sehemu yake ya gharama ya kudhibiti ukwasi pamoja na riba ya nakisi katika akaunti yake kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 na mkataba wa makubaliao (MoU) baina yao. Kuwezesha bajeti ya Fungu 22 kuweza kumudu gharama hizo ndio njia sahihi hapo mbeleni; na (ii) Kuzingatia kufanya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 ili kuruhusu Benki Kuu kupunguza madeni yake kwa Serikali kutoka katika gawio lake. Juhudi hizi zitapunguza kasi ya ukuaji wa madeni yatokanayo na gaharama ya kudhibiti ukwasi pamoja na riba ya nakisi ya Serikali.*

### 5.1.7 Taarifa ya Fedha ya Kitengo cha Deni la Taifa

#### 5.1.7.1 Kushushwa Kiwango cha Deni la Taifa kwa Kiasi cha Shilingi Bilioni 4,588.39

Mapitio yangu ya mchanganuo wa deni la taifa yalibaini kwamba kiwango cha deni la taifa kilifikia Shilingi bilioni 46,081.43

kufikia tarehe 30 Juni, 2017. Kiwango hiki hakijumuishi madeni ya Shilingi bilioni 4,588.39 ikiwa ni madeni ya mifuko ya pensheni kiasi cha Shilingi bilioni 4,421.75<sup>20</sup> na dhamana zilizokiukwa masharti kiasi cha Shilingi bilioni 166.64 chini ya Idara ya Msajili wa Hazina.

Mapitio ya taarifa maalum ya serikali juu ya uhakiki wa madeni ya serikali kwa Mifuko ya Pensheni uliofanywa Aprili na Desemba 2016 ilibainisha kuwa mifuko iliwasilisha madeni ya jumla ya Shilingi bilioni 5,343 kwa uhakiki. Hata hivyo, Mkaguzi Mkuu wa Ndani alikubali madeni ya Jumla ya Shilingi bilioni 3,183 sawa na asilimia 59 ya madeni yaliyowasilishwa na kuacha madeni ya jumla ya Shilingi bilioni 2,160 yakikataliwa kwa sababu ya usahihi wa takwimu na sababu nyingine.

Mapitio yangu zaidi kuhusu msingi wa kukataliwa yalibaini kwamba, baadhi ya madeni hayo, kimsingi, hayakukataliwa; bali kulikosekana nyaraka za kuthibitisha wakati wa uhakiki; na baadhi yamekataliwa kulingana na makosa ya kiufundi. Kwa mfano, nimeona mfano ambao mkopo ulikataliwa kwa sababu tu mkopeshaji [NSSF] alielekeza fedha kwenye akaunti ya benki aliyoelekezwa na wizara mama, ambayo kimsingi ni akaunti ya mkopaji (serikali) badala ya ile aliyoelekezwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali awali. Kwa mtazamo wangu, hili suala haliwezi kuthibitisha msamaha kwa mkopaji; hii ni kwa sababu mkopo, kwa kweli, ulikuwa umemfikia mkopaji [serikali].

Nilitambua kuwa, adhabu zinazohusiana na madeni hayo pia zimeachwa kwa kuwa Kamati ya Akaunti ya Bunge ilielekeza hivyo; bila kuzingatia masharti ya mikataba ya mikopo kati ya serikali na mifuko ya pensheni na taratibu zingine zilizotakiwa kufuatwa kabla ya kuondolewa. Hata hivyo, taarifa zangu za kikao cha PAC, ambacho suala hili lilijadiliwa, zinaonesha kuwa kuondolewa kwa adhabu kulipaswa kufikiriwa na kupitishwa na Bodi za Wakurugenzi za mifuko ya pensheni husika; pia kulipaswa kuendane na utoaji wa hati fungani maalum. Ninachokitambua ni

<sup>20</sup> Shilingi bilioni 4,422 ni sawa na 4.14% ya pato la taifa ambalo ni shilingi bilioni 106,867

kwamba, kwa hakika, utoaji wa hati fungani maalum bado haujafanywa na serikali, kitu ambacho kinafanya maelekezo ya PAC kutotekelzeza kwa sasa.

Kwa hiyo, nina mtazamo tofauti kuhusiana na kukataliwa kwa malimbikizo ya riba na adhabu za kisheria juu ya madeni ya serikali yaliyokokotolewa kwa kuzingatia sheria za mifuko husika, na ninafikiria kuwa Serikali imefanya uamuzi huo kibinafsi. Kuondolewa kwa riba na adhabu hakuwezi kufanywa na mtu ye yote mwingine isipokuwa Bodi za Wakurugenzi za mifuko ya pensheni husika. Kwa hiyo, kutojumuishwa kwenye orodha ya madeni ya serikali kunashusha kiwango cha deni la taifa; na hii ndiyo sababu iliyofanya uthibitisho toka mifuko ya pensheni Machi 2018 ulikuwa na takwimu za juu kuliko takwimu ambazo serikali inaripoti.

Tatizo jingine ni kwamba, PSPF haikutaja deni la Serikali kabla ya 1999 katika hesabu zake kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2017. Hii pia ilikuwa hivyo kwa mifuko mingine iliyokadiria kiasi kikubwa cha uharibifu (impairment) baada ya kutokuwa na uhakika kuhusiana na utoaji wa hati fungani maalum kwa mifuko ya pensheni na uamuzi binafsi wa serikali wa kutaka kufuta baadhi ya madeni. Kwa hiyo, Mifuko ya pensheni imethibitisha madeni ya Shilingi bilioni 4,421.75 kinyume na takwimu za serikali ambazo zinataja Shilingi bilioni 3,182.83 zilizotajwa kwenye hesabu za fungu 22 mnamo 30 Juni 2017. Hii inafanya upungufu unaofikia Shilingi bilioni 1,238.75 baina ya mifuko ya pensheni na Serikali.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo, ninachukulia kwa uzito wa juu suala la kushushwa kwa kiwango cha deni la serikali kwa mifuko ya pensheni kwa kuwa linahatarisha maendeleo uendelevu ya sekta ya pensheni nchini Tanzania kama Serikali inashindwa kuheshimu ahadi yake katika utoaji wa hati fungani maalum [Hotuba ya bajeti 2015/16; 2016/17; 2017/18] kulingana na mchakato unaoendelea wa kuunganisha mifuko ya pensheni. Kwa namna yoyote ile, hatua ya kutolipa madeni ya serikali kwa mifuko ya pensheni kabla ya kuunganisha kutaongeza hatari ya

uendelevu wa sekta ya pensheni. Ukweli huu unahitaji kuzingatiwa kwa tahadhari kubwa na watunga sera ili kuufikia ustawi wa kifedha wa nchi wa baadaye. Madeni ya mifuko ya pensheni yameoneshwa kwa muhtasari katika jedwali la Na.2 chini;

#### Jedwali Na. 20: Madeni ya serikali kwenye mifuko ya pensheni

Kiasi katika Shilingi bilioni						
S/ No	Mfuko	Kilichoku baliwa na serikali	Kilichothib itiswa na mfuko mnamo 30 Juni 2017	tofauti <sup>21</sup> [kilichosh ushwa]	Kilichope leksa kwa IAG na mifuko	Kilichothib itiswa na mfuko mnamo 31 Des 2017
1	LAPF	178.00	220.00	42.00	199.00	231.00
2	NSSF	409.00	1,104.00	695.00	1,212.00	1,188.00
3	PPF	100.00	278.00	178.00	132.00	283.00
4	GEPF	8.00	8.75	0.75	25.00	9.20
5	NHIF	151.00	189 <sup>22</sup>	38.00	166.00	189.00
6	PSPF	235.00	520.00	285.00	533.00	521.00
7	PSPF pre-1999	2,102.00	2,102 <sup>23</sup>	-	3,077.00	2,102.00
	<b>Grand Total</b>	<b>3,183.00</b>	<b>4,421.75</b>	<b>1,238.75</b>	<b>5,344.00</b>	<b>4,523.20</b>

<sup>21</sup> Tofauti ya taarifa inatokana na: kwanza, na tofauti ya muda katika ripoti; na pili uamuzi wa kufuta madeni fulani kama ilivyooneshwa awali.

<sup>22</sup> \* kiasi kimechukuliwa toka kwenye taarifa za kifedha za Mfuko kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2017

<sup>23</sup> \*\* takwimu imetolewa kutoka katika ripoti maalum ya serikali [Mkaguzi Mkuu wa Ndani] juu ya Madeni ya serikali kwa mifuko ya Pensheni mnamo Juni 30.

**Jedwali Na. 21: Muhtasari wa dhamana zilizokiukwa masharti  
mnamo 30 Juni 2017**

Na	Mkopeshaji	Mkopaji	Kiasi kisicholipwa
1	Wallis trading Inc.	ATCL	69,213,679,476.21
2	NSSF	General tyre E. A Ltd	19,050,540,000.00
3	Exim Bank of China	Urafiki-Friendship textile	36,583,497,775.58
4	CRDB bank	Tanzania Fertilizer company	26,055,439,680.01
5	ABC bank		15,735,444,827.00
Jumla			166,638,601,758.80

Kutotambuliwa kwa Madeni ya serikali kwenye mifuko ya pensheni na dhamana zilizokiukwa masharti hakuna athari kwenye uhimiliyu wa deni la taifa kwa kuwa taarifa ya uchambuzi wa uhimiliyu wa deni kwa mwaka 2016 ilizingatia kuwapo kwa madeni haya.

Katika uchambuzi wangu wa taarifa za fedha za Fungu 22 za mwaka 2016/17 pamoja na Mpango wa Uuzaji Hati Fungani wa mwaka 2015/16, nilibaini kuwapo kwa taarifa za madeni tarajiwa zisizoendana, na ambazo hazikuwa na vielelezo vyta kutosha (Deni la mafao ya kabla ya Julai 1999 ni Shilingi bilioni 2,044.45 kwa mujibu wa Mpango wa Uuzaji Hati Fungani. Hii ni kinyume na Shilingi bilioni 2,102.32 zilizotajwa kwenye hesabu).

*Kwa kuzingatia hayo, ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali: (i) Kuharakisha utoaji dhamana isiyo ya fedha kwa mifuko ya pensheni ili kuwezesha madeni yake kuingia katika kasma ya deni la taifa; (ii) Kuweka utaratibu madhubuti wa kukusanya madeni kutoka kwa wadaiwa waliokiuka masharti ya dhamana na kuweka masharti madhubuti ya utaratibu wa utoaji dhamana hapo mbeleni; na (iii) Kuhakikisha madeni na madeni tarajiwa yanakuwa na vielelezo vyta kutosha kabla ya kuwasilishwa katika taarifa za fedha.*

### 5.1.7.2 Kutokuwapo kwa uwiano wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS-DRMS)

Katika ukaguzi wangu wa hesabu za Fungu 22 za mwaka 2016/17 na taarifa za mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS-DRMS), nilibaini kuwapo kwa tofauti baina ya taarifa hizo kulikotokana na kutokuwepo kwa uwiano wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS-DRMS) kabla na wakati wa kuandaa taarifa za fedha hesabu za Fungu 22.

Kwa mtazamo wangu, taarifa za fedha hazikuwanishwa na vyanzo vyake hivyo kuhatarisha uadilifu wa taarifa zilizowasilishwa.

*Napendekeza Serikali ifanye yafuatayo: (i) limarishe mifumo ya ndani ili kuhakikisha hesabu zinapitiwa kwa umakini kabla ya kuwasilishwa kwa ukaguzi; na (ii) Iwianishe tofauti kati ya taarifa za mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS-DRMS) na taarifa za fedha za Fungu 22.*

### 5.1.8 Huduma za Jumla

#### 5.1.8.1 Mapungufu katika mfumo wa kielektroniki wa kufuutilia majalada ya malipo ya mafao

Idara ya mafao ina mfumo wa kielektroniki wa kufuutilia majalada ya malipo ya mafao (Treasury Pension Payment System (TPPS)) tokea Juni 2014. Nilipitia matakwa ya mtumiaji wa mfumo huo na kubaini kuwa moduli za kufuutilia majalada na ukokotoaji wa mafao ya hitimisho la kazi, kupokea na kutoa majalada, kufuutilia mwenendo wa jalada na utafutaji wa taarifa za mstaafu hazikuwezesha kufanya kazi. Kwa mtazamo wangu, kutowevezeshwa kwa moduli hizo kunasababisha ucheleweshaji wa malipo, na hivyo, kusababisha kuwapo kwa malalamiko toka kwa wastaafu.

*Napendekeza Serikali iongeze bidii ili kuhakikisha moduli zote za mfumo wa kielektroniki wa kufuutilia majalada ya malipo ya mafao zinawezeshwa kama ilivyo kwenye matakwa ya mtumiaji.*

### **5.1.8.2 Malipo ya nyongeza ya mafao bila kuwepo kwa kanzidata**

Mapitio yangu ya vocha za malipo na barua yenye Kumb. PSPF/PA.24/1049/01/03 ya tarehe 15 Agosti, 2017 yalinibainishia kuwa Fungu 22 walilipa Shilingi bilioni 127.94 kwa PSPF ikiwa ni malipo ya nyongeza ya mafao kwa ajili ya wastaifu 7,486.

Hata hivyo, haikuweza kuelezwani kwa nini malipo hayo ya nyongeza yalifanyika licha ya idadi ya wastaifu kutobadilika kwa kipindi cha miaka minane tokea 2009/10. Kwa mtazamo wangu, kutobadilika kwa idadi ya wastaifu kwa muda mrefu wakati matukio ya vifo na kustaifu yapo dhahiri, kunamaanisha kuwa hakuna kanzidata sahihi na kamilifu. Hivyo ni dhahiri kuwa usahihi wa malipo haukuweza kuthibitika kwa kutumia taarifa zilizopo. Udhafu huu unaweza kutoa mwanya wa malipo ya mafao kutumika kwa namna isiyokusudiwa.

*Napendekeza yafuatayo kwa serikali: (i) Iweke utaratibu wa kuhuisha kanzidata mara kwa mara ili kuwa na kanzidata sahihi na iliyokamilika muda wote; na (ii) Ichunguze malipo ya nyongeza ya mafao yaliyolipwa ili kufahamu iwapo yaliyolipwa kwa wanufaika sahihi.*

## 5.2 UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA MAFAO YA WASTAAFU

### 5.2.1 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi hufanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005) na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi No.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 5(a) cha sheria hiyo kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuidhinisha malipo yafanyike kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali baada ya kujiridhisha kwamba, Ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Hivyo ni muhimu kufanya ukaguzi wa awali kwenye malipo yote ya Serikali ambayo siyo rahisi kuyatabiri na kutengewa fedha.

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi hufanyika kwa kuzingatia sheria za mafao ya hitimisho la kazi ambazo ni pamoja na Sheria ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999; Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2006; Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 1997; Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 (Iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002); Sheria ya Utumishi wa Usalama wa Taifa ya mwaka 1996; Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008; Sheria ya Mafao ya Kustaafu ya GEPF ya mwaka 2013 na Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999.

### 5.2.2 Lengo la kufanya Ukaguzi wa Awali

Lengo la ukaguzi huu ni kuhakiki usahihi wa mafao ya hitimisho la kazi yaliyokokotolewa na waajiri kwa ajili ya kuwalipa wanufaika ili kuwezesha kutambua makosa mapema huku kukiwa na lengo la kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa kile wanachostahili. Hii pia ni muhimu kwakuwa, kiasi chochote kitakacholipwa kimakosa ni vigumu kurejeshwa kutoka kwa wastaafu.

Kwa upande mwingine, madhumuni ya uhakiki wa mafao ni kuhakikisha kuwa sheria husika, kanuni za mafao ya hitimisho la kazi, sera za kazi zinazohusiana na utumishi wa umma, nyaraka mbalimbali, lkama na muundo wa mishahara vinazingatiwa.

### **5.2.3 Mawanda ya Ukaguzi**

Ukaguzi wa awali wa mafao ya hitimisho la kazi unahusisha Watumishi wa Umma ambao mafao yao hulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na hauhusishi Watumishi wa umma ambao ulipwaji wa mafao yao unashughulikiwa na Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Mashirika ya Umma (PPF), Mfuko wa Hitimisho la Kazi kwa Serikali za Mitaa (LAPF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii. Kazi ya ukaguzi wa awali inayofanywa na ofisi yangu ni kwa ajili ya malipo ya mafao ya hitimisho la kazi yanayolipwa moja kwa moja kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, malipo ambayo yanahusisha:-

- Pensheni na kiinua mgongo kwa watumishi wa umma watoa huduma mchanganyiko, wanajeshi na viongozi wengine, walimu na maafisa wa usalama.
- Malipo ya kimkataba kwa viongozi wa kisiasa, wageni toka nje, wastaifu waliorejeshwa kwenye utumishi, na raia walioajiriwa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45.
- Kiinua mgongo kwa watumishi wasio kwenye masharti ya pensheni na;
- Malipokiinua mgongo kwa askari polisi.

### **5.2.4 Ufafanuzi wa Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo**

Sehemu hii ya ripoti inaeleza mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya uzeeni na mapendekezo kwa mwaka wa fedha 2016/17 kama ifuatavyo;

#### **5.2.4.1 Mukhtasari wa matokeo ya ukaguzi**

Zoezi la ukaguzi wa awali lilianza na majalada 273 yaliyotokana na ukaguzi wa kipindi cha mwaka 2015/16 na jumla ya majalada ya wastaifu 3,671 yalipokelewa na kufanya jumla ya majalada

3,944 yaliyokuwepo kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha mwaka 2016/17. Kati ya hayo majalada 3,694 yalikaguliwa na kuidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa malipo na kubaki majalada 250 ambayo yalijumuisha majalada yaliyorejeshwa kwa Maafisa Masuuli husika kwa ajili ya masahihisho na mengine yalikuwa bado yakiendelea na ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha tarehe 30 Juni, 2017 kama inavyooneshwa katika jedwali Na.1 hapo chini:-

#### **Jedwali Na. 22: Mafaili ya wastaifu yaliyokaguliwa 2015/2016**

Maelezo	Majalada
<b>Majalada yaliyokuwepo tarehe 1 July, 2014</b>	273
<b>Majalada yaliyopokelewa</b>	3,671
<b>Jumla ya majalada yaliyokuwepo kwa ukaguzi</b>	3,944
<b>Majalada yaliyokaguliwa</b>	3,694
<b>Majalada yaliyosalia tarehe 30 June, 2016</b>	250

#### **5.2.4.2 Kuzidisha mafao ya hitimisho la Kazi- TZS. 24,886,232.80**

Ukaguzi niliyofanya katika nyaraka za malipo ya pensheni kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulibaini kuwa baadhi ya nyaraka zilizoletwa kwangu kwa ukaguzi wa awali zilionyesha mafao ya uzeeni yaliyokokotolewa kwa makosa.

Kati ya majalada 3,694 yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 mafao ya uzeeni kwa wastaifu 406 (11%) yalibainika kukokotolewa kimakosa. Kati ya hayo, majalada 230 yamebainika kuwa na ziada ya malipo ya TZS 541,065,048.91 huku majalada 176 yakiwa na pungufu ya malipo ya TZS. 516,178,816.11 Hata hivyo, makosa yaliyoainishwa hapo juu yanatia shaka juu ya kutosheleza kwa utaratibu wa uhakiki wa karatasi za mafao, uwezo wa waandaaji na wahakiki katika ustadi na uzoefu wa masuala ya pensheni na sheria husika, na ufungashaji wa majalada ya mafao ya uzeeni. Mukhtasari unaonyeshwa katika jedwali namba 2 hapo chiniKama ilivyo ainishwa kwenye jedwali Na.2 hapo chini

**Jedwali Na. 23: Makosa katika ukokokotozi wa mafao ya hitimisho la akazi**

S/N	Maelezo	Mafao yaliyozidishwa (a)		Mafao yaliyopunjwa (b)		Jumla Halisi (a-b) (TZS)
		Idadi ya kesi	Kiasi (TZS)	Idadi ya kesi	Kiasi (TZS)	
1	Kipindi cha utumishi kisicho sahihi	104	145,819,468.77	94	171,667,021.06	-25,847,552.29
2	Mishaharaya iliyokosewa	45	154,329,202.53	41	157,300,602.02	-2,971,399.49
3	Makosa katika michango ya NSSF	38	62,051,566.82	25	38,773,558.42	23,278,008.40
4	Mikopo/madeni	7	12,033,885.72	2	857,246.34	11,176,639.38
5	Kuchangia kimakosa PSPF	10	58,298,558.00	0	-	58,298,558.00
6	Makosa mbali mbali katika ukokotoaji	26	108,532,367.07	14	147,580,388.27	-39,048,021.20
	Jumla	230	541,065,048.91	176	516,178,816.11	24,886,232.80

*Chanzo: fomu za malipo ya mafao, 2016/17*

Kutokana na uchambuzi wa hapo juu, serikali ingepata hasara ya TZS 541,065,048.91 kutokana na kuzidishwa kwa mafao lakini pia, wastaifu wangeweza kupunjwa mafao yao kwa kiasi cha TZS. 516,178,816.11. Ukokotoaji wa mafao kwa makosa ungesababisha serikali kupata hasara halisi ya TZS 24,886,232.80.

Kiasi hicho kilichookolewa ni matokeo ya ufanisi wa ukaguzi wa awali wa mafao yanayolipwa moja kwa moja toka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. zaidi ya hayo inaonesha jinsi ambavyo kushindwa kwa mifumo ya ndani ya udhibiti na mapungufu ya maafisa masuuli yangeweza kuigharimu Serikali na wastaifu kama ukaguzi wa awali usingefanyika.

### 5.2.5 Ucheleweshwaji katika uaandaji wa mafao

Kanuni ya 89 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inawataka waajiri na waajiriwa kutunza kumbukumbu za kiutumishi kwa lengo la kufanya marejeo wakati wa ukokotozi wa mafao ya hitimisho la kazi. Kanuni ya 32(2) inaeleza kuwa ni wajibu wa waajiri kuitia taarifa za waajiriwa walioko chini yao ili kuhakikisha kuwa utumishi wa watumishi wa umma unakoma pale wanapofikisha umri wa kustaaifu. Pia Kanuni Na. F.48 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 32(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inamtaka mtumishi wa umma aliyetayari kwa kustaaifu, kutoa taarifa ya maandishi ya kusudio lake hilo

kwa mwajiri wake kupitia taratibu za kawaida, kwa uchache miezi sita kabla ya kustaaafu.

Hata hivyo, ukaguzi wa awali wa majalada ya wastaafu 102 kati ya majalada 3,694 ulibaini kuwepo kwa waajiri waliochelewa kuaandaa na kuwasilisha taarifa za mafao kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya ukaguzi wa awali. Ucheleweshwaji huo ulikuwa kati ya miezi sita (6) hadi miezi 326 na waathirika wakuu katika ucheleweshwaji huu ni wastaafu waliokuwa katika utumishi wa umma wa masharti ya kawaida.

Aidha, ukaguzi niliofanya katika mchakato wa malipo ya mafao ulibaini kuwa majalada 170 kati ya 1,094 ya mafao ya uzeeni ambayo yalipokelewa kutoka kwa waajiri na Idara ya Pensheni katika Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 yalikataliwa na kurudishwa kwa waajiri bila kulipwa. Hii ni inaashiria kukataliwa kwa asilimia 16 ya mafaili yaliyowasilishwa kwa malipo, kutokana na sababu za kutojazwa kikamilifu kwa nyaraka zinazohusiana na malipo ya mafao ya uzeeni na kukosekana kwa nyaraka muhimu zinazopaswa kuambatana na mafao yaliyokokotolewa kwa malipo.

Katika mazingira yote hayo, ukiukwaji wa taratibu unaofanywa na waajiri umepelekea kucheleweshwa kwa ulipaji wa mafao ya hitimisho la kazi. Ni maoni yangu kuwa vitendo hivyo visingeweza kutokea kama waajiri wangekuwa makini katika kuandaa mafao na kupelekea ukiukwaji wa matakwa ya sheria na kanuni, suala linaloathiri wanufaikaji na kusababisha usumbufu usio wa lazima achilia mbali kupungua kwa thamani ya fedha/mafao.

### 5.2.6 Hitimisho

Kutokana na mchanganuo hapo juu, kuna umuhimu mkubwa kwa waajiri kuwa na udhibiti na utaratibu wa uhakiki katika kuandaa karatasi za mafao ya wastaafu. Kukosekana kwa mfumo wa udhibiti wa ndani na udhaifu kwa afisa Masuuli kunatoa mwanya kwa watumishi wasio waaminifu kuharibu utaratibu wa ulipaji wa mafao kwa ukokotozi usio sahihi kitu ambacho kingeigharimu serikali na wastaafu kama tu ukaguzi wa awali

usingewezesha kubaini. Ucheleweshaji wa uandaaji wa mafao ya hitimisho la kazi kwa wastaifu wa utumishi wa umma unachangia pia na kuwepo makosa ambaayo ukaguzi unayabaini. Usumbuu huu usio wa lazima ungeweza kuepukika kama umakini ungezingatiwa katika uaandaaji wa mafao na uwasilishaji wa karatasi za mafao kwa ajili ya ukaguzi wa awali.

Kwa upande mwingine, ucheleweshwaji wa michango na ulipaji wa madai kwa mifuko ya hifadhi ya jamii imepelekeea ucheleweshwaji zaidi wa ulipaji wa kiinua mgongo kwa wastaifu katika kipindi cha mwaka 2016/2017. Kitendo hiki kinasababisha usumbu uusio wa lazima kwa wastaifu na matatizo ya kifedha kwa Mifuko ya Pesheni kama haikukaguliwa.

### **Mapendekezo**

- a) Serikali kupitia kwa afisa Masuuli iimarishe udhibiti na utaratibu wa kufanya mapitio ya uandaaji wa mafao. Hii itahakikisha kuwa waandaaji wa mafao ya kiinua mgongo na pensheni wanafuata kanuni na vigezo vya ukokotoaji na sheria kabla ya kuwasilisha kwa ukaguzi wa awali na malipo na kuepuka kucheleweshwa kwa mafao ya hitimisho la kazi na hasara kwa serikali.
- b) Serikali ihakikishe kuwa mafisa Masuuli wote wanaandaa na kuwasilisha karatasi za mafao ya wastaifu zikiwa na nyaraka muhimu zimeambatishwa kwa ukaguzi wa awali miezi sita kabla ya tarehe halisi ya kustaifu kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya mafao.
- c) Serikali ihakikishe michango ya mafao inapelekwa kwa wakati na madai yote yanalipwa kwa lengo la kuepuka matatizo ya kifedha kwa Mifuko na ucheleweshwaji wa malipo kwa wastaifu.
- d) Serikali ihakikishe maafisa masuuli wote wanawajengea uwezo maafisa wanaohusika kuandaa karatasi za mafao ili kuleta uelewa hususani katika uandaaji wa mafao, taratibu na sheria za mafao. Kuhimiza uendeshwaji wa mara kwa mara wa program za mafunzo ya waandaaji wa pensheni ili kuboresha uelewa wa pamoja juu ya sheria, kanuni na taratibu.
- e) Serikali itoe muongozo au waraka kwa maafisa masuuli jinsi ya kuaandaa karatasi za mafao na kuonyesha aina za nyaraka zinazopaswa kutumika

## 5.3 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

### 5.3.1 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 na ilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 01 Julai 1996, ikiwa na majukumu ya kusimamia na kukusanya mapato ya kodi kwa niaba ya Serikali.

Mamlaka inatayarisha aina mbili za Taarifa za Fedha, Taarifa za Mapato na Taarifa ya Hesabu za Matumizi. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 taarifa zote mbili za Hesabu zimeandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya misingi ya fedha taslimu (IPSAS Accrual basis of accounting). Taarifa za mapato hufafanua masuala yahusuyo makusanyo ya kodi mbalimbali, na ile ya hesabu za matumizi hufafanua kuhusu jinsi fedha zilizotolewa na serikali na vyanzo vingine ziliyyotumika.

### 5.3.2 Mwelekeo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita

Katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ya mwaka wa fedha uliopita (2015/16) mapendekezo hamsini na manane (58) yalitolewa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2016; na mapendekezo mia moja thelathini na manane (138) yalisalia yakisubiri kufanyiwa kazi toka mwaka wa fedha 2001/02 mpaka 2014/15. Nimepitia hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa jumla ya mapendekezo mia moja na tisini na sita (196). Kati ya hayo, mapendekezo 73 (asilimia 37.2) yanahusiana na Kitengo cha Forodha na Ushuru wa bidhaa, mapendekezo 45 (asilimia 23) yanahusiana na kitengo cha walipa kodi wakubwa, na mapendekezo 78 (asilimia 39.8) yanahusiana na kitengo cha mapato ya ndani kama ilivyoainishwa hapo chini.

**Jedwali Na. 24: Idadi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa miaka iliyopita**

Na.	Mwaka	Kitengo cha Forodha na Ushuru wa Bidhaa	Kitengo cha Walipa kodi Wakubwa	Kitengo cha Mapato ya Ndani	Jumla
1.	2001/2002	1	0	0	1
2.	2002/2003	0	0	0	0
3.	2003/2004	0	0	0	0
4.	2004/2005	2	0	0	2
5.	2005/2006	4	0	0	4
6.	2006/2007	3	0	0	3
7.	2007/2008	5	1	1	7
8.	2008/2009	1	2	2	5
9.	2009/2010	2	2	2	6
10.	2010/2011	1	4	1	6
11.	2011/2012	3	5	0	8
12.	2012/2013	2	6	3	11
13.	2013/2014	7	6	4	17
14.	2014/2015	20	13	35	68
	Jumla Ndogo	51	39	48	138
14.	2015/2016	22	6	30	58
	Jumla Kuu	73	45	78	196

Kati ya mapendekezo 196, thelathini na matano (asilimia 18) yalitekelezwa, mia moja arobaini na tano (asilimia 74) yalikuwa kwenye hatua za utekelezaji na kumi na sita (asilimia 8) hayakutekelezwa kabisa. Muhtasari wa mwelekeo wa utekelezwaji wa mapendekezo kwa vitengo vyote vitatu umeoneshwa katika Jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 25: Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita**

Mwelekeo wa Utekelezaji	Kipaumbele cha Juu	Kipaumbele cha Kati	Kipaumbele cha Chini	Jumla	
	(idadi)	(idadi)	(idadi)	Idadi	%
Yaliyotekelzwa	35	-	-	35	18
Yapo kwenye utekelezaji	145	-	-	145	74
Hayajatekelezwa	16	-	-	16	8
Jumla	196	-	-	196	100

Jumla ya mapendekezo yaliyo kwenye hatua za utekelezaji na

yale ambayo hayajatekelezwa ni mia moja sitini na moja (asilimia 82). Baada ya kupitia zaidi utekelezaji wa mapendekezo niligundua kuwa, kati ya jumla ya mapendekezo yaliyotolewa, kumi na matano (15) sawa na asilimia 9 yanahitaji maamuzi ya Taasisi nyingine nje ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kama vile Bodi za Rufani za Kodi, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania na Bunge kwa madeni ya kodi yaliyopendekezwa na Mamlaka ya Mapato kupitia Hazina kwa ajili ya kufutwa. Maamuzi ya kesi hizo na kufutwa kwa madeni yamesubiriwa kwa muda mrefu toka mwaka wa fedha 2001/2002. Mapendekezo mia moja arobaini na sita (146) yaliyobaki, sawa na asilimia 91, yanashughulikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kulingana na uhalisia wa mapendekezo husika, mwelekeo wa utekelezaji unaridhisha, lakini Uongozi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania unatakiwa kuongeza jitihada katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyoko chini ya utekelezaji ili kukomboa mapato yaliyozuiwa kutokana na mapungufu yaliyoainishwa. Hatua hii itaongeza ukusanyaji wa mapato zaidi.

### **5.3.3 Mwelekeo wa Mapato nchini Tanzania**

Kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 14,249.2 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya Shilingi bilioni 15,261.5. Hii inaonesha makusanyo yalikuwa pungufu kwa Shilingi bilioni 1,012.1 ambazo ni sawa na asilimia 6.63 ya malengo. Jumla ya makusanyo haihusishi Shilingi bilioni 22.13 za makusanyo ya hazina katika vipengele vya misamaha ya kodi pamoja na fedha zilizorejeshwa. Mapato halisi ya mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi bilioni 14,271.38. Jedwali la hapo chini linaonesha jumla ya makisio na makusanyo ya mapato toka Tanzania bara na visiwani:


**Jedwali Na. 26: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2016/17  
kiidara (Shilingi kwa mamilioni)**

Idara	Lengo - Tanzania bara na visiwani	Makusanyo halisi kwa Tanzania bara na visiwani	Makusanyo pungufu	Makusanyo pungufu kwa asilimia
Mapato ya ndani	3,166,464.90	2,659,011.83	-507,453.07	-16.03%
Walipa kodi wakubwa	6,539,234.20	5,981,295.28	-557,938.92	(8.53%)
Forodha na ushuru wa bidhaa	6,322,291.16	5,685,192.55	-637,098.61	-10.08%
Marejesho ya kodi	-766,504.50	-76,250.08	-690,254.42	-90.05%
Jumla	<b>15,261,485.76</b>	<b>14,249,249.58</b>	<b>-1,012,236.18</b>	<b>-6.63%</b>
Vocha za misamaha ya kodi	32,413.59	22,132.55	-10,281.04	-31.79%
Jumla Kuu	<b>15,293,899.35</b>	<b>14,271,382.13</b>	<b>-1,022,517.22</b>	<b>-6.69%</b>

*Chanzo: Taarifa za mapato zilizokaguliwa za mwaka 2016/17*

Kwa ujumla, idara zote tatu zilishindwa kufikia malengo kwa mwaka huu wa fedha 2016/17. Kielelezo cha hapo chini kinaonesha kwamba Idara ya walipa kodi wakubwa ilikusanya asilimia 42 ya makusanyo yote ambayo ndiyo sehemu kubwa kuliko idara zote; ikifuatiwa na Idara ya Forodha yenye asilimia 40 na idara ya kodi za ndani yenye asilimia 18 ambayo ndiyo ya mwisho kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ukitoa vocha za misahama ya kodi.

**Uwiano wa Makusanyo halisi Kwa Idara kwa mwaka 2016/17**



Kutokana na mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa mchango wa makusanyo kutokana na mapato ya ndani umekuwa nyuma ikilinganishwa na idara nyingine. Hivyo basi, nashauri ufanisi na makusanyo katika idara hii uongezwe kwa kutumia mbinu

mbalimbali ikiwemo kuongeza wigo wa vyanzo vya kodi, ufatiliaji wa karibu kwenye kukusanya madeni ya kodi na kutumia taratibu za kisheria ili kuhakikisha kodi inalipwa.

#### 5.3.4 Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kwa wastani, ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ambapo makusanyo halisi yalikuwa juu ya makadirio kwa asilimia 0.13. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha, Mamlaka imefanikiwa kuongeza kidogo ufanisi wa mapato (uwiano wa kodi dhidi ya pato la jumla la ndani la taifa (GDP)) mpaka kufikia asilimia 13.2 ikilinganishwa na asilimia 12.9 kwa mwaka 2015/16. Ijapokuwa naipongeza Serikali kwa juhudhi ilizochukua za kuweka mikakati madhubuti dhidi ya wakwepa kodi na makusanyo ya mapato, uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani la taifa bado uko chini kwa asilimia 6.7 ya lengo ambalo ni asilimia 19.9 lililowekwa na Mamlaka ya Mapato hadi kufikia mwaka 2017/2018. Jedwali la hapo chini linaonesha mwelekeo wa makusanyo na uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani la taifa kwa kipindi cha miaka mitano kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

**Jedwali Na. 27: Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa Tanzania na nchi za Afrika Mashariki, 2013 - 2017 (Shilingi kwa milioni)**

Maelezo	Mwaka wa fedha				
	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17
<b>Lengo</b>	7,978,158	10,957,001	12,078,015	13,220,252	15,293,800
<b>Makusanyo halisi</b>	7,912,304	10,026,659	10,743,765	13,238,045	14,271,300
<b>Tofauti ya lengo na makusanyo</b>	-65,854	-930,342	-1,334,250	17,793	-1,022,500
<b>Tofauti ya lengo na makusanyo kwa asilimia</b>	-1%	-8%	-11%	0.13%	-6.69%
<b>Uwiano wa kodi dhidi ya pato la jumla la ndani (Kodi/pato la jumla la ndani)</b>					
<b>Tanzania</b>	<b>11.70%</b>	<b>12.50%</b>	<b>11.60%</b>	<b>12.90%</b>	<b>13.20%</b>
<b>Uganda</b>	<b>11.10%</b>	<b>11.30%</b>	<b>12.30%</b>	<b>12.80%</b>	<b>14.00%</b>
<b>Kenya</b>	<b>17.80%</b>	<b>19.10%</b>	<b>18.70%</b>	<b>18.80%</b>	<b>19.30%</b>
<b>Rwanda</b>	<b>14.50%</b>	<b>14.90%</b>	<b>15.1%</b>	<b>16.10%</b>	<b>15.20%</b>
<b>Burundi</b>	<b>15.10%</b>	<b>13.60%</b>	<b>13.70%</b>	<b>13.00%</b>	<b>13.40%</b>

*Chanzo: Takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2013 -2017*

Mchanganuo linganifu wa ufanisi wa kodi kwa nchi za Afrika Mashariki unaonesha kwamba, Tanzania iko nafasi ya mwisho kwa mwaka huu wa fedha. Kwa kuzingatia mwelekeo linganifu wa nchi za Afrika Mashariki, ni vema Serikali iongeze ufanisi<sup>24</sup> katika ukusanyaji wa kodi ili kufikia malengo yake, kwani bado kuna fursa za kuboresha zaidi ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza wigo wa vyanzo nya kodi, kudhibiti mianya ya upotevu wa kodi na kuongeza ulipaji kodi kwa hiari. Kwa ujumla, hatua zote hizi zitasaidia kupunguza kiwango cha utegemezi wa bajeti.

### **5.3.5 Changamoto katika ukusanyaji wa mapato na mapendekezo**

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Mamlaka ya mapato Tanzania haikuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa kodi, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 na mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato umekuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa kwa wastani wa asilimia 5 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kuna changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na Serikali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ambazo ni pamoja hizi zifuatazo:

- a) Kuwapo kwa kesi za kodi za muda mrefu katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB), Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) na Mahakama ya Rufaa Tanzania. Pamoja na maboresho kidogo katika kushughulikia kesi za kodi kwa mwaka wa fedha 2016/17, swala hili limekuwa kikwazo kikubwa katika juhudi za ukusanyaji wa mapato. Mahojiano yangu na Uongozi wa Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi juu ya ufanisi mdogo kwenye kusikiliza na kukamilisha kesi za kodi, yalinijuza kwamba Taasisi hizi zina tatizo la idadi ndogo na uwiano usio sawa wa Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Taasisi unaosababisha kushindwa kufanyika kwa kikao zaidi ya

---

<sup>24</sup> Kuongeza uwezo wa walipa kodi wa kujikadiria wenyewe, kutoa Elimu ya kodi, kuendelea kurahisisha sheria za kodi na usimamizi wa kodi, usimamizi bora wa viashiria hatarishi, kusaidia kuboresha biashara, kuongeza umakini katika uchambuzi na ukaguzi wa kodi, kupunguza gharama za utekelezaji wa sharia za kodi, kuendelea kuboresha mifumo ya kodi ili kurahisisha utekelezaji wa sheria na ufanisi katika ukusanyaji wa kodi.

kimoja kwa wakati mmoja kwani akidi inayotakiwa inashindwa kutumia, hasa kutokana na upungufu wa Makamu Wenyeviti. Kadhalika, Taasisi hizi zimekuwa na tatizo la ufinyu wa bajeti, hivyo kuathiri kufanya kwa vikao vya kutosha vya kusikiliza kesi kama inavyotakiwa na sheria. Mapungufu haya yamesababisha wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia mwanya huu kuchelewesha malipo ya kodi kisheria kwa kupeleka kesi zao kwenye taasisi hizi wakijua zitachukua muda mrefu kusikilizwa. Jambo hili linazuia ukusanyaji wa mapato makubwa ya Serikali, kwani kesi hizi zinakuwa na kodi nyingi sana. Ni vema Serikali ikahakikisha Taasisi hizi zinakuwa na idadi kamili wa Makamu Wenyeviti na wajumbe, pia zipewe bajeti ya kutosha ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

*Naishauri Serikali iziboreshe na kuziongezea uwezo Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi kwa kuteua makamu wenyeviti na wajumbe wa kutosha ili kuziwezesha Taasisi hizi kufanya vikao vya kusikiliza kesi za kodi zaidi ya kimoja kwa wakati mmoja. Hatua hii itasaidia kupunguza mlundikano wa kesi za kodi zilizokaa muda mrefu bila kuhitimishwa. Kadhalika, naishauri Serikali iongeze bajeti na kutoa pesa za kutosha kwa ajili ya kuziwezesha Taasisi hizi kufanya shughuli zao kwa wakati na kwa ufanisi.*

- b) Uwezo hafifu wa Mamlaka wa kushughulikia maswala ya mapingamizi ya kodi umepelekea kuchelewa kuyashughulikia maswala hayo na kushindwa kukamilishwa kwa wakati. Ufuatiliaji wangu pamoja na mahojiano na uongozi wa Mamlaka juu ya sababu za kuchelewa kumaliza mapingamizi haya, vilinibainishia kuwa kuna upungufu wa wafanyakazi wenyewe uzoefu na weledi wa kutosha katika kitengo cha ukaguzi wa kodi na kitengo cha ufundu wanaoweza kushughulikia na kuendana na idadi kubwa ya mapingamizi ya kodi kutoka kwa walipa kodi. Kadhalika, Utaratibu wa kupokea mapingamizi ya kodi kutoka kwa walipa kodi bila kukusanya amana au kuwa na kibali cha kutokukusanya amana kwa mujibu wa matakwa ya sheria, umechangia na kuhamasisha wafanyabiashara wengi kuleta mapingamizi ya kodi katika Mamlaka ya mapato.

*Nashauri Uongozi wa Mamlaka uhakikishe kuwa unaongeza kasi katika kushughulikia mapingamizi ya kodi ili kuyamaliza mapingamizi yote yaliyokaa kwa muda mrefu bila kupata ufumbuzi. Jambo hili linaweza kufanyika kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi wenyewe uwezo, uzoefu na weledi wa kutosha katika kushughulikia mapingamizi ya kodi. Kadhalika, Mamlaka ihakikishe mapingamizi yote ya kodi yanapokelewa baada ya walipa kodi kulipa amana (sehemu ya moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichokadiriwa au kiasi cha kodi ambacho hakijapingwa) au Mamlaka itoe kibali cha kutokukusanya amana kwa mujibu wa matakwa ya sheria za kodi.*

*Uongozi wa Mamlaka ushirikiano na Serikali ili kuongeza wafanyakazi watakaowezesha kutatua mashauri ya mapingamizi ya kodi. Hii itasaidia kuinua makusanyo ya mapato ya ndani.*

- c) Usimamizi usioridhisha wa udhibiti wa mifumo ya uagizaji wa bidhaa, mafuta yanayonunuliwa kutoka nchi za nje na mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi za nje pia umesababisha upotevu wa mapato kwa Serikali.

*Naishauri Serikali iendelee kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa bidhaa za mafuta zinazoingia kwa matumizi ya hapa nchini na zinazokwenda nchi nyingine na kuhakikisha kuwa hazitumiki nchini bila kulipa kodi stahiki; na endapo zimeuzwa katika soko la ndani, Mamlaka ikusanye kodi stahiki kwa mujibu wa sheria. Pia naishauri Serikali itumie mita za mafuta kwenye maghala ya forodha ya mafuta “off-bond meters” na kuweka au kujenga Tanki la Akiba la Mafuta (National Reserve Tank) katika kila bandari inayoingiza mafuta ili kuhakikisha kuwa taarifa za mafuta yanayoingizwa nchini zinaandikwa sawasawa na usimamizi wa utoaji mafuta unaimarishwa sambamba na ulipaji wa kodi zinazotakiwa. Matumizi ya mita za mafuta “flow meters” na tenki la akiba la mafuta (National Reserve tank) yatasaidia Mamlaka kuwa na taarifa sahihi za mafuta yaliyoingia na yanayotoka; na hatimaye, kuimarisha makusanyo ya kodi kwenye mafuta.*

- d) Mapungufu katika usimamizi wa makusanyo ya kodi, tozo na riba zinazotokana na uchunguzi wa kodi, na kodi ambazo hazijalipwa na walipa kodi kwa kipindi kirefu kama inavyotakiwa na Sheria za kodi. Mapungufu haya ambayo ni kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni za kodi yanaathiri ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

*Naishauri Serikali iboreshe mikakati katika usimamizi, ufuatiliaji na ukusanyaji wa madeni na kuhakikisha kuwa kodi zote, tozo na riba zinakusanya kwa wakati. Maboresho haya yataepusha malimbikizo ya kodi zilizokaa muda mrefu bila kukusanya wakati tayari zimekadiriwa na walipa kodi wenyewe, au Idara ya Uchunguzi wa Kodi au kitengo cha ukagazi wa kodi.*

- e) Kutotilia mkazo matumizi ya mashine za kielektroniki za kodi (EFD) kwa wafanyabiashara wanaotakiwa kutumia mashine hizo, na kuwapo kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara zisizo rasmi kumechangia katika kupunguza kasi ya ukusanyaji wa mapato.

Naishauri Serikali iendelee kusisitiza matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) kwa kuhakikisha kuwa kila mlipa kodi mwenye vigezo vyta kutumia mashine hizi anapata hizo mashine na *kuzitumia* kwa usahihi ili kuendana na matakwa ya kifungu namba 36 cha sheria ya Usimamizi wa kodi (Tax Administration Act, 2015) na kanuni za sheria ya mashine za kielektroniki (EFD Regulations). Utaratibu huu utasaidia sana kurasisimisha baiashara na kuhakikisha kwamba kodi stahiki inalipwa na kuongeza mapato kwa serikali.

### 5.3.6 Masuala maalum yaliyoonekana katika ukagazi wa mwaka 2016/17

Sehemu hii inatoa taarifa juu ya maeneo makuu manne ambayo yanahitaji usimamizi na uangalifu wa karibu wa Mamlaka ya Mapato ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Maeneo hayo muhimu ni: Usimamizi wa mapingamizi ya Kodi, Usimamizi wa Misamaha ya Kodi, Usimamizi wa Makusanyo ya Kodi na makusanyo ya tozo na ada zinazokusanya na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine.

### 5.3.6.1 Usimamizi wa Mapingamizi za Kodi: Kesi za muda mrefu katika mamlaka za rufaa za kodi Shilingi trilioni 4.44

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2017, nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina masuala yaliyo katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya rufaa kwa muda mrefu yenye jumla ya Shilingi trilioni 4.44, ambapo, kiasi cha Shilingi trilioni 3.57 (asilimia 80.2) kimekwama katika Bodi ya rufaa za kodi, Shilingi bilioni 144.55 (asilimia 3.3) kimekwama katika Baraza la Rufaa za Kodi, na kiasi kilichobaki cha Shilingi bilioni 733.83 (asilimia 16.5) kinasubiri maamuzi katika Mahakama ya Rufaa Tanzania. Katika mahojiano yangu na Uongozi wa Taasisi hizi nilibaini kwamba hali hii huchangiwa na upungufu wa watendaji unaosababisha kushindwa kufanyika kwa vikao vya kutosha kwa ajili kusikiliza kesi za kodi. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2016/17 Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) lilifanya asilimia 48 tu ya vikao vilivyohtajika ili kusikiliza mashauri ya kesi za rufaa. Sababu kubwa ikiwa ni upungufu wa makamu wenyeviti watatu na wajumbe wawili ambao bado hawajateuliwa. Hali hii imepelekea kutotimia kwa akidi inayowezesha kufanyika kwa vikao vya kutosha na kuendesha mashauri ya kesi za rufaa, kwani kila kikao ni sharti kiendeshwe na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti. Jedwali la hapa chini linaonesha muhtasari wa kesi za kodi katika Mamlaka za Rufaa za kodi. Jedwali Na.5: Muhtasari wa kesi zilizo katika Mamlaka za Rufaa za Kodi

### Jedwali Na. 28: Kesi za Rufaa ya Kodi ambazo Bado Kuamuliwa

Idara	Idadi ya kesi	Kesi za Bodi ya Rufaa za Kodi		Kesi za Baraza la Rufaa za Kodi		Kesi za Mahakama ya Rufaa		Jumla SH. (Milioni)
		DK	SH.	DK	SH.	DK	SH.	
		(million i)	(Milioni)	(million i)	(Milioni)	(milioni)	(Milioni)	
Walipa Kodi Wakubwa	315	91.87	1,308,664.25	-	34,297.94	273.09	77,512.72	2,226,470.82
Kodi za Ndani	338	21.135	1,949,380.57	17.99	60,696.99	-	34,469.79	2,128,755.55
Ushuru wa Forodha	56	-	60,042.07	-	9,827.88	-	18,725.35	88,595.30
Jumla kwa 2016/17	<b>709</b>	<b>112</b>	<b>3,318,086.89</b>	<b>17.99</b>	<b>104,822.80</b>	<b>273.09</b>	<b>130,707.86</b>	<b>4,443,821.67</b>
Jumla kwa 2015/16	<b>451</b>	<b>56.19</b>	<b>6,691,855.00</b>	<b>30.68</b>	<b>139,191.00</b>	<b>41.25</b>	<b>124,582.00</b>	<b>7,233,644.00</b>
Jumla ya mapato yaliyokwama kwenye rufaa kama asilimia ya Bajeti <sup>25</sup> ya mwaka 2016/17								15%
Jumla ya mapato yaliyokwama kwenye rufaa kama asilimia ya Pato <sup>26</sup> la Ndani la Taifa kwa mwaka 2016/17								4.2%

Ikililinganishwa na taarifa yangu ya mwaka wa fedha uliopita (2015/16), mapato yaliyokwama katika rufaa za kodi yamepungua kwa Shilingi trilioni 2.9 sawa na asilimia 39.9 (kutoka Shilingi trilioni 7.23 kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia Shilingi trilioni 4.44 kwa mwaka 2016/17). Uchanganuzi wangu unaonyesha kuwa mapato yaliyokwama katika rufaa ni asilimia kumi na tano (15%) ya bajeti ya mwaka 2016/2017; na ni asilimia nne nukta mbili (4.2%) ya pato la ndani la Taifa (GDP) kwa mwaka 2016/2017, uwiano ambaeo ni wa juu. Hivyo, thamani ya kodi inayobishaniwa katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa za kodi ni kubwa mno, na serikali inaingia gharama kubwa kuendesha kesi hizi bila ufanisi kwa vile zinachukua muda mrefu. Pia, Serikali huingia hasara kwenye mapato pale mrufani anapofilisika kabla ya kesi kuamuliwa.

<sup>25</sup> Bajeti ya mwaka 2016/17 ilikuwa Shilingi trilioni 29.54 [2015/16: Shilingi trilioni 22.50].

<sup>26</sup> Pato la ndani la Taifa kwa 2016/17 lilikuwa Shilingi Trilioni 106.867 [2015/16: Shilingi Trilioni 96.80 ]

Ninaishauri Serikali iimarishe utendaji wa mfumo mzima wa Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi katika kuendesha kesi za rufaa za kodi kwa kuhakikisha kuwa wakati wote nafasi za makamu wenye viti na wajumbe wa Taasisi hizi zinajazwa kulingana na sheria husika; jambo hili litaharakisha usikilizwaji wa kesi za rufaa za kodi ambazo zinazuia kiasi kikubwa cha mapato ya Serikali. Pia, ni muhimu sana kuziongezea uwezo wa kifedha taasisi hizi kwani bajeti zao ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji na majukumu yao.

#### **5.3.6.2 Mapungufu na mifumo isiyoridhisha kushughulikia mapingamizi ya kodi**

Katika ukaguzi wangu wa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/17, nilibaini kuwa jumla ya mapingamizi mia mbili themanini na tisa (289) ya kodi kutoka kwa walipa kodi yenye thamani ya Shilingi 2,566,348,814,547.35 yaliwasilishwa katika Mamlaka ya Mapato yakipinga kiasi cha kodi kilichokokotolewa na kufanyiwa tathmini na Kamishna wa kodi. Kati ya mapingamizi hayo, mamlaka ya mapato imefanikiwa kushughulikia na kumaliza mapingamizi hamsini na tano (55) yenye thamani ya Shilingi 1,558,116,225,302.76 ambayo ni sawa na asilimia 61 ya mapingamizi yaliyowasilishwa. Uongozi wa Mamlaka umeonesha maboresho katika kushughulikia mapingamizi ya kodi katika kipindi cha mwaka huu wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita wa 2015/16 ambapo mapingamizi yalizoshughulikiwa na kukamilishwa yalikuwa na thamani ya Shilingi 1,378,200,249 kati ya mapingamizi yenye thamani ya Shilingi 858,236,909,894 yaliyowasilishwa na walipa kodi, ambayo ni sawa na asilimia 0.16 tu. Hata hivyo, ushahidi wa nyaraka kuthibitisha kuwa kodi ya Shilingi 1,558,116,225,302.76 ilikusanywa kutokana na mapingamizi yaliyoshughulikwa na kumalizwa haukutolewa kwa ajili ya uhakiki.

Kadhalika, katika ukaguzi wa mapingamizi 234 yaliyobaki yenye thamani ya Shilingi 1,008,232,589,244.59 nilibaini kuwa mapingamizi 13 yenye thamani ya Shilingi 269,612,850,131.28 yaliyatiliwa na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kwani walipa

kodi walishindwa kuwasilisha mapingamizi hayo ndani ya siku 30 baada ya kutoa maamuzi ya kodi, hii ni kwa mujibu wa Kifungu Na. 51 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015. Hivyo, idadi ya mapingamizi 221 yenye thamani ya Shilingi 738,619,739,113 bado hayajashughulikiwa na Mamlaka. Hata hivyo, mamlaka ya mapato haikukusanya kodi ya kiasi cha Shilingi 269,612,850,131.28 kutoka kwenye mapingamizi yaliyokataliwa na Kamishna. Kushindwa kukusanya kodi za mapingamizi yaliyotolewa maamuzi kunaashiria kuwapo kwa mifumo isiyoridhisha ya usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa kodi za pingamizi zilizotolewa maamuzi na kutakiwa kukusanya.

Vile vile, katika ukaguzi wangu wa mapingamizi ya kodi kwa mwaka huu wa fedha nilibaini kuwa, Mamlaka ya Mapato ilipokea na kushughulikia mapingamizi ya kodi bila kukusanya Shilingi 296,099,930,972.27 ambazo ni fedha za amana zinazotakiwa kulipwa na walipa kodi ikiwa ni kiasi kikubwa kati ya moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichofanyiwa tathmini na kutakiwa kulipwa, au kiasi cha kodi ambacho hakijapingwa na walipa kodi, wala kupewa msamaha wa kutolipa hiyo amana (waiver) kutoka kwa Kamishna Mkuu. Swala hili ni kinyume na Kifungu Na. 51 (5) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015.

Kutokukusanya kwa fedha za amana kunachangia kwa kiasi kikubwa walipa kodi kutumia mwanya huu kuwasilisha mapingamizi mengi ili wakwepe kodi. Hii inatokana na kutokuwapo kwa ufanisi katika kushughulikia mifumo ya mapingamizi ya kodi, hivyo kusababisha mapato ya Serikali kutokukusanya kwa wakati na Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya makusanyo ya mapato, hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Kuwapo kwa mapingamizi mengi ya kodi ambayo hayashughulikiwi kwa wakati na kutolewa maamuzi kunachangiwa na uwezo na ufanisi hafifu wa kitengo cha ukaguzi wa kodi na kitengo cha ufundi katika Mamlaka ya Mapato. Kutokana na mahojiano yangu na uongozi wa mamlaka nilibaini kuwa swala hili limesababishwa pia na upungufu wa wafanyakazi

wenye weledi na uzoefu wa kutosha kwa ajili ya kushughulikia mapingamizi ya kodi ikilinganishwa na idadi kubwa ya mapingamizi yanayoletwa na walipa kodi.

### **Ninaishauri Serikali:**

- (a) Kuongeza ufanisi katika kushughulikia kesi za mapingamizi ya kodi yaliyoletwa na walipa kodi kwa wakati ili kutoa maamuzi juu ya kodi stahiki inayopaswa kulipwa kwa wakati. Hili linawezekana kwa kuongeza idadi ya watumishi wenye uzoefu na ujuzi pamoja na kuwaongezea mafunzo watumishi wote walio katika kitengo cha Huduma za Kiufundi na Kitengo cha Ukaguzi wa Kodi ili kuboresha utoaji wa tathmini ya kodi inayopaswa kulipwa kwa wakati; hivyo, kupunguza idadi kubwa ya kesi za pingamizi za kodi ambazo zinachelewa kushughulikiwa.
- (b) Kukusanya amana ya kodi ambayo ni thamani kubwa kati moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichofanyiwa tathmini na kutakiwa kulipwa na walipa kodi au kiasi cha kodi ambacho hakijapingwa, amana hii inatakiwa kulipwa na walipa kodi kabla Mamlaka haijapokea mapingamizi ya walipa kodi kwa ajili ya kusikilizwa.
- (c) Kuhakikisha ukusanyaji wa kodi zote ambazo mapingamizi yake yalikataliwa na ambazo maamuzi ya mapingamizi yametolewa na kuhitimishwa.

#### **5.3.6.3 Ufuatiliaji na usimamizi usioridhisha wa Misamaha ya Kodi**

Serikali, kwa kupitia Mamlaka ya Mapato, ilitoa misamaha ya kodi kwa ajili ya shughuli maalum zilizoainishwa katika sheria za kodi mbalimbali kama vile uwekezaji katika bidhaa za mtaji kwa kipindi maalum ili kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi. Vilevile na kukuza sera maalum za kiuchumi kama vile kuhamasisha uwekezaji katika sekta maalum, kuendeleza uhusiano na mataifa mengine kwa kutoa misamaha kwa shughuli za kidiplomasia na kwa sababu za kibinadamu.

Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2016/17 zinaonesha misamaha ya kodi yenye jumla ya Shilingi bilioni 1,037.6 ikiwa ni pungufu ya Shilingi bilioni 62.7 (asilimia 5.7) ikilinganishwa na misamaha ya kodi iliyotolewa mwaka 2015/16 ambayo ilikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 1,100. Ingawa kiasi cha misamaha ya kodi iliyotolewa katika mwaka huu wa fedha kimepungua kidogo ikilinganishwa na mwaka jana,

lakini bado kiasi kilichotolewa ni kikubwa, kwani ni asilimia moja (1) ya pato la ndani la taifa (GDP) kwa mwaka 2016/17 ikilinganishwa na malengo ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi kuwa chini ya asilimia moja (1) ya pato la ndani la taifa (GDP). Jitihada za kupunguza misamaha ya kodi zitasaidia Mamlaka ya Mapato kuongeza uwezo wake wa kukusanya kodi, hivyo kufikia malengo yaliyowekwa. Mwenendo wa misamaha ya kodi iliyotolewa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ni kama inavyoonekana katika jedwali la hapo chini:

**Jedwali Na. 29: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2012-2017 (Shilingi kwa mamilioni)**

Mwaka	Pato la Taifa kwa mwaka	Jumla ya misamaha ya kodi	Asilimia ya misamaha ikilinganishwa na Pato la Ndani la Taifa
2012/13	48,385,100	1,515,607	3
2013/14	55,619,077	1,834,097	3
2014/15	84,279,922	1,627,012	2
2015/16	97,304,216.4	1,100,337	1
2016/17	106,866,941.4	1,037,643	1

*Chanzo: Taarifa za Mapato za Mamlaka ya Mapato, takwimu na uchambuzi wa wakaguzi, 2012-2017*

Kutokana na mchanganuo wa hapo juu, kiasi cha misamaha ya kodi kwa asilimia ya Pato la Ndani la Taifa (GDP) kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa wastani kilikuwa asilimia 2.10 ya Pato la Ndani la Taifa, kiwango hicho bado kiko juu ikilinganishwa na lengo la chini ya asilimia moja (1) ya pato la Ndani la Taifa au asilimia tano ya makusanyo yote (Rejea bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2013/14).

*Ninashauri; Kuendelea na mikakati na juhudzi za makusudi zinazowezesha kupunguza misahama ya kodi hadi kufikia chini ya asilimia moja ya pato la ndani la taifa kwa kuboresha mifumo ya udhibiti ya ndani na ya ufatiliaji. Kwa mfano, matumizi ya Sheria mpya ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 na Sheria ya*

*Kodi ya Ongezeko la thamani ya mwaka 2014 yamesaidia sana kupunguza misamaha ya kodi isiyo halali. Kuendelea kupertia sera za kiuchumi na kodi kwa lengo la kuondoa misamaha yote ya kodi isiyo na tija. Swala hili linawezekana kwa kuboresha kaguzi na udhibiti wa motisha za kodi, na kuimarisha usimamizi na uchunguzi dhidi ya matumizi ya motisha za kodi.*

#### **5.3.6.4 Tathmini ya mifumo ya udhibiti wa misamaha ya kodi za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji wa madini**

Ulingenishi wa nyaraka za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za matumizi ya uchimbaji wa madini zinazohusiana na kampuni za uchimbaji wa madini za Buzwagi, Bulyanhulu, North Mara na Geita pamoja na mapitio ya mifumo inayotunza taarifa za bidhaa za mafuta zilizotolewa na kitengo cha forodha makao makuu ulibaini kuwa jumla ya magari 94 yenye lita 3,147,289 za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi yalisafirishwa kwenda kwenye migodi hii minne. Hata hivyo, sikuweza kujiridhisha kama mafuta hayo yalipokelewa na makampuni ya uchimbaji madini kwa sababu hapakuwa na nyaraka za zinazothibitisha mapokezi ya mafuta hayo huko migodini. Magari husika yaliondoka Dar es Salaam katika kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Juni, 2017. Nina mashaka kuwa lita 3,147,289 za mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi ya Jumla ya Shilingi 2,083,246,836.00 yanaweza kuwa yametumika kwa ajili ya matumizi mengine tofauti na shughuli zilizokusudiwa za uchimbaji wa madini; hivyo kuisababishia Serikali hasara ya ukosefu wa mapato.

Kadhalika, katika uchambuzi wangu wa nyaraka za matumizi ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi katika kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ya Buzwagi, Bulyanhulu, North Mara na Geita niligundua mafuta yenye jumla ya lita 21,095,595 katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi Juni, 2017 yalikuwa yametolewa kwenda kwa wakandarasi na watu wengine ambao sio wanufaika wa misamaha ya kodi. Jumla ya thamani ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi kwa

wakandarasi na watu ambao sio wanufaika ilikuwa ni Shilingi 11,052,806,957.20. Utilewaji wa mafuta kwenda kwa wakandarasi na watu ambao hawastahili kunufaika na misamaha ya kodi ni kinyume na matakwa ya Agizo Na. 480 la Serikali lilitolewa tarehe 25 Oktoba 2002 ambalo linazuia kutolewa kwa misamaha ya kodi za mafuta kwa makampuni na watu ambao hawastahili kunufaika na misamaha hiyo.

**Ninaishauri Serikali:**

- Kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na mafuta yaliyosamehewa kodi lakini hayakufika kwenye makampuni ya uchimbaji wa madini, na kukusanya ushuru wa forodha kwenye mafuta hayo wenye jumla Shilingi 2,083,246,836.00.
- Ihakikishe inakusanya kodi yenyenye jumla ya Shilingi 11,052,806,957.20 kwenye mafuta ya msamaha wa kodi ambayo yalitolewa kwenda kwa makampuni na watu wengine ambao sio wanufaika wa msamaha wa kodi.

Kufanya Ukagazi na uchunguzi wa kila mara wa wanufaika wanaopewa misamaha ya kodi ili kuhakikisha kuwa makampuni yanatii sheria na kanuni za misahama ya kodi; hivyo kuepuka hasara inayoweza kutokea kwa kutumia vibaya misahama hii ya kodi.

#### **5.3.6.5 Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizokaa katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na bidhaa zilizoruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum**

Ukagazi wa uhakiki uliofanyika katika maghala ya forodha ya Makao makuu ya Mamlaka, maghala ya forodha katika ofisi za mikoa na ofisi za mipakani ulibaini kuwa, bidhaa 115 za aina tofauti katika maghala hayo zenye kodi ya zaidi ya Shilingi 6,899,846,547.25 zilikaa kwenye maghala kwa zaidi ya miaka minne (4) zikisubiri taratibu na hatua za utoaji mizigo inayotakiwa kulipiwa ushuru wa forodha na bidhaa hizi hazikuwa katika hali nzuri. Pia, nilibaini bidhaa zenye kodi ya Shilingi 5,602,098,766.50 katika maghala binafsi 35 ambazo zilikaa kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita (6). Kipindi cha miaka minne ni zaidi ya kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa kifungu Na. 42(1)

cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambacho kinataka bidhaa zote ambazo zimekaa katika maghala yaliyo chini ya uangalizi wa Idara ya Forodha (customs warehouses and customs bonded warehouses) kwa zaidi ya siku 60 ziuzwe kwa njia ya mnada wa wazi au kwa njia yoyote ambayo Kamishna ataona inafaa. Kwa upande mwingine bidhaa zilizokaa katika maghala ya watu binafsi kwa zaidi ya miezi sita zinatakiwa pia ziuzwe kwa njia ya mnada wazi au kwa njia yoyote ambayo Kamishna ataona inafaa, hii ni kwa mujibu wa kifungu Na. 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Kuchelewa kuzinadi bidhaa hizi kunaweza kussababisha hasara ya kukosa mapato ya Serikali kutokana na uchakavu au kuharibika, kwani bidhaa zinakuwa zimekaa kwenye maghala kwa muda mrefu.

Kadhalika, baada ya kupitia nyaraka za maghala ya forodha nilibaini bidhaa 689 zenye thamani ya Shilingi 9,516,695,998 na kodi ya jumla ya Shilingi 3,876,583,713 ambazo zilipewa kibali cha kuhamishwa kutoka Kiwanja cha Ndege Dar es Salaam na Bandari ya Dar es Salaam kwenda kwenye maghala binafsi ya forodha. Hata hivyo, wakati wa uhakiki kwenye maghala husika, bidhaa hizi hazikuwemo kwenye hayo maghala na hakukuwa na ushahidi wa nyaraka kuthibitisha kuwa kodi husika ililipwa. Orodha ya bidhaa hizo imeoneshwa kwenye jedwali hapa chini.

#### **Jedwali Na. 30: Bidhaa ambazo hazikupatikana kwenye maghala binafsi ya forodha**

Na.	Kituo	Bidhaa	Thamani (TZS)	Kodi (TZS)
1.	Uwanja wa Ndege (JNIA)	275	1,599,218,443.87	320,301,655.00
2.	Bandari (Wharf)	414	7,917,477,554.14	3,556,283,058.00
	Jumla	<b>689</b>	<b>9,516,695,998.01</b>	<b>3,876,584,713.00</b>

*Chanzo: Taarifa za mfumo wa kodi za forodha (TANCIS) na uhakiki uliofanyika kwenye maghala*

Mapitio yangu zaidi ya taarifa kutoka mfumo wa kodi za forodha wa Mamlaka (TANCIS) na rejista zinazohifadhi taarifa za bidhaa na magari kutoka nje ya nchi na kuruhusiwa kuingia nchini kwa muda maalum katika mipaka ya Holili, Tarakea na Rusumo

yalibaini magari 459 yaliyoingizwa katika kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Juni 2017 lakini hayakutoka nje ya Tanzania kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12; na hakukuwa na vibali vilivyotolewa kisheria kuruhusu kuongezwa kwa muda wa magari hayo kuendelea kukaa hapa nchini. Mapungufu haya ni kinyume na Kifungu Na. 117(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 kinachotaka magari yaliyoingia kwa muda maalum hapa nchini yawe yametoka nje ya Tanzania ndani ya miezi 12 au pawepo na idhini ya kuruhusu kuongezewa muda wa kukaa hapa nchini.

**Jedwali Na. 31: Magari yaliyoingia nchini kwa muda maalum lakini hayakutoka nje ya Tanzania**

Na	Mahali	Idadi ya magari
1	Holili	42
2	Tarakea	173
3	Rusumo	244
	Total	459

*Chanzo: Taarifa kutoka mfumo wa TANCIS*

Kwa mtazamo wangu, kuwapo kwa bidhaa zilizokaa zaidi katika maghala ya kuhifadhia bidhaa zikisubiri kulipiwa ushuru wa forodha na magari yaliyokaa nchini zaidi ya muda ulioruhusiwa kunaonesha usimamizi usioridhisha wa bidhaa katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na magari yaliyoruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum kinyume na Kifungu Na. 117(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Mapungufu haya yanatoa mianya kwa wafanyabiasha wasio waaminifu kutumia vibaya utaratibu wa kuweka bidhaa kwenye maghala ya kulipia ushuru na kuingiza magari kwa kipindi maalum, hivyo Serikali kushindwa kukukusanya kodi stahiki.

**Ninaishauri Serikali:**

- a) Kupitia upya uhalisi wa bei za uuzaaji wa bidhaa zilizokaa kwa muda mrefu katika maghala bila kupata wanunuzi katika minada iliyofanyika.

- b) Kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na utambuaji wa bidhaa zilizokaa zaidi katika maghala ya kulipia ushuru wa forodha na kuzinadi ili kuепuka hasara inayotokana na uchakavu wa bidhaa hizo, ambapo hupelekeea Serikali kukosa mapato.
- c) Kufanya minada mara kwa mara kwa bidhaa zote zilizokaa kwa muda mrefu ili kuепuka hasara itakayotokana na uchakavu au kuharibika kwa bidhaa hizo, hivyo, kuikosesha Serikali mapato.
- d) Kuimarisha mifumo ya utoaji wa taarifa za bidhaa na magari yalioingia nchini na kupewa muda maalum ili kujua mahali yalipo na kuiunganisha mifumo hii katika mipaka yote ambayo magari haya yatatokea ili kuyafuatilia kwa ukaribu.
- e) Kuyatafuta magari yote yalioingia nchini kwa muda maalumu lakini hayakurudi na ikusanye kodi zote pamoja na tozo za adhabu kwa kuingiza magari nchini bila kulipia kodi, kwani ni kinyume na sheria.

#### **5.3.6.6 Mifumo isiyoridhisha ya udhibiti wa mizigo inayosafirishwa kwenda nchi nyingine.**

**Mizigo iliyoingia na baadae kuuzwa nje ya nchi (re-export):**

Ukaguzi wangu wa bidhaa zinazotoka kwenye maghala ya forodha na kwenda nchi nyingine kuitia bandari ya Mwanza kwa kipindi cha kuanzia Januari 2014 hadi Juni 2017 ulibaini makontena 1,846 kati ya makontena 2,267 (sawa na asilimia 81.13) ambayo hayakuwa na amana za kusafirishia, isipokuwa kwa makontena 421 tu (sawa asilimia 18.57) ambayo yalikuwa na amana zenye thamani ya Shilingi 26,720,135.176. Mapungufu haya ni kinyume na kifungu na.104 (3) cha kanuni za sheria ya forodha ya Afrika Mashariki za mwaka 2011. Ni vigumu kwa Mamlaka kukadiria kiasi cha kodi stahiki endapo makontena hayana dhamana za kusafirishia mizigo.

Ingawa makontena yote yalionesha kupokelewa kwenye vitabu na mfumo wa taarifa wa TANCIS na kuthibitishwa na afisa wa forodha kuwa yalitoka kuitia bandari ya Mwanza, lakini sikupata ushahidi wa nyaraka kuthibitisha kuwa makontena hayo yalitoka kwenda nchi nyingine kwa mujibu wa matakwa ya sheria.

Hata hivyo, katika mahojiano yangu na maafisa wa ofisi ya idara forodha katika mkoa wa Mwanza walinifahamisha kuwa hawajapokea bidhaa za kwenda nchi nyingine kwa muda mrefu, na hawakuwa na taarifa yejote kuhusu makontena haya. Jambo hili linaleta mashaka kwa sababu bidhaa hizi zilioneshwa kwenye mfumo wa taarifa wa TANCIS kuwa zimetoka kupitia bandari ya Mwanza ijapokuwa maafisa wa forodha wa mkoa hawakuwa na taarifa. Hivyo basi, nina wasiwasi kwamba bidhaa hizi zilitumika nchini bila kulipiwa kodi, na hivyo, kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.

***Bidhaa na mafuta zinazopita nchini kwenda nchi nyingine (Transit goods and fuel)***

Katika ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine kwa kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Juni 2017, nilibaini mizigo 68 yenye kodi ya thamani ya Shilingi bilioni 1.71 ambayo haikutoka kwenda nchi husika. Wakati wa uhakiki wangu sikupata ushahidi wowote wa vitabu (registers) au mfumo wa taarifa wa TANCIS kuthibitisha kuwa bidhaa hizi zilitoka kwenda nchi zilizokusudiwa kupitia mipaka ya Rusumo (Shilingi bilioni 0.33), Mutukula (Shilingi bilioni 0.4), na Kabanga (Shilingi bilioni 0.98)

Kadhalika, ukaguzi wa mafuta yanayoingia nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine hadi mwezi Septemba 2017 ulibaini lita 21,228,114.55 za mafuta ambazo zilikuwa zisafirishwe kwenda nje ya nchi kupitia mipaka mbalimbali ambazo hazikuthibitishwa kwenye mfumo wa taarifa wa TANCIS wala hakukuwa na ushahidi wa nyaraka kuthibitisha kuwa mafuta hayo yalitoka kwenda nchi zilizokusudiwa. Mafuta hayo yaliingia kupitia bandari ya Dar es Salaam kati ya mwezi January 2016 hadi Juni 2017 na yalikuwa na kodi yenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 13.05.

Kutokana na mazingira haya, nina mashaka kuwa bidhaa hizi ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine, ziliuzwa na kutumika nchini bila kulipia kodi, jambo linaloonesha kuwa kuna mapungufu makubwa katika udhibiti wa

bidhaa zinazipita nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nydingine.

### **Ninaishauri Serikali:**

- a) Ilimarishe mifumo ya bidhaa zinazopita nchini kuelekea nje ya nchi na zile zinazotoka kwenye maghala ya forodha kwenda nje ya nchi ili kuhakikisha kwamba sheria na taratibu zilizowekwa zinafuatwa ili kuepuka uuzwaji holela wa bidhaa zisizolipiwa ushuru, hivyo kuisababishia serikali upotevu wa mapato.
- b) Kufanya uchunguzi wa makontena ambayo hayakusafirishwa kwenda nje ya nchi na ikusanye kodi kwenye makontena 2,267 ambayo hayakulipiwa kodi kwa kipindi cha kuanzia 2014 hadi 2017 kupitia bandari ya Mwanza.
- c) Serikali ikusanye kodi ya kiasi cha Shilingi bilioni 13.05 kwenye lita 21,228,114.55 za mafuta ambazo hazikusafirishwa kwenye nchi nydingine.

#### **5.3.6.7 Mafuta yaliyoingizwa nchini ambayo hayakuoneshwa kulipiwa kodi wala kusafirishwa kwenda nchi nydingine, na mafuta ambayo hayakuingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kukadiriwa na kulipiwa kodi ya Shilingi 28,400,160,309.58**

Nilifanya ulinganisho wa Jumla ya mafuta yaliyoingizwa nchini na meli 92 na kiwango cha mafuta kilichooneshwa kulipiwa kodi kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi, kiasi kilichosamehewa kodi na kiasi kilichosafirishwa kwenda nje ya nchi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, nilibaini tofauti ya lita 26,136,813 katika meli 9. Mafuta hayo yalikuwa na kodi yenye thamani ya Shilingi 13,650,756,155.32 ambazo hazikukusanywa na Mamlaka. Kadhalika, baada ya kupitia taarifa za mafuta yaliyoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani na kulinganisha na taarifa za mafuta zilizoingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kukadiriwa na kulipiwa kodi, nilibaini kuwa kiasi cha lita 31,254,211 za mafuta zeny kodi yenye thamani ya Shilingi 14,749,404,154.26 ambayo yaliingizwa kupitia nyaraka 73 za kuagizia bidhaa nje ya nchi (bills of ladding) za makampuni ya mafuta 22 hakikingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya

kukadiriwa na kulipiwa kodi. Kitendo hiki kinyume na matakwa ya taratibu za Mamlaka. Mafuta kutokuingizwa kwenye mfumo wa kodi (TANCIS) humaanisha kuwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia nyaraka hizi hayakulipiwa kodi, na hivyo, kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Mambo ya msingi yanayotia mashaka yapo katika maeneo mawili, (a) ni namna gani mafuta katika nyaraka 73 za kuingizia mizigo yalitolewa kwenda kwa wahusika bila kulipia kodi iwapo udhibiti katika mfumo wa TANCIS unafanya kazi na usuluhihi baada ya vipimo unafanyika mara kwa mara; na (b) ni namna gani mafuta lita 26,136,813 katika meli 9 hayakuweza kubainika kwa kutumia taratibu zilizowekwa. Kwa namna yeote ile, mapungufu haya yanaonesha kuwa kuna udhaifu katika udhibiti wa mafuta yanayoingizwa nchini, ambayo kwa maoni yangu unatoa mianya kwa wafanyakazi kuitumia vibaya mifumo ya kodi na kupelekeea walipa kodi kukwepa kulipa kodi na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

### ***Ninashauri Serikali***

- Ifanye uchunguzi wa maswala yote mawili ili kujuu ni kwa namna gani taarifa za mafuta lita 26,136,813 katika meli tisa hazikubainika kupitia taratibu zilizowekwa, na makampuni 22 ya mafuta yalikiuka taratibu za kukadiriwa kodi; na Serikali ihakikishe kuwa kodi zote ambazo hazikulipwa zinakusanywa.
- Imarishe udhibiti wa taarifa na ukusanyaji wa kodi kwenye mafuta yanayoingizwa nchini kwa kufanya usuluhihi wa mara kwa mara kati ya nyaraka zote za kuagizia mafuta (bills of ladding) na zile zilizoingizwa kwenye mfumo wa kodi (TANCIS) ili kuzuia mapungufu kama haya kujirudia.

#### **5.3.6.8 Usimamizi usioridhisha wa makusanyo ya madeni ya kodi Shilingi 262,293,791,682:**

#### ***Makadirio ya kodi ambayo hayajakusanywa***

Mapitio ya rejista inayohifadhi taarifa za uchunguzi wa kodi, rejista inayohifadhi taarifa za kodi ambazo hazijalipwa pamoja na nyaraka mbalimbali yameonesha kuwa kiasi cha kodi cha

Shilingi 262,293,791,682 hakikukusanya kutoka kwa walipa kodi. Katika kiasi hicho, jumla ya Shilingi 144,204,393,621 kinatokana na Idara ya Walipa kodi Wakubwa na Kiasi cha Shilingi 118,089,398,061 kinahusiana na Idara ya Uchunguzi wa Kodi kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini:

**Jedwali Na. 32: Kodi iliyokokotolewa na kutokukusanya (Kiasi katika Mamilioni)**

Idara	Deni la Kodi iliyokokotolewa (SH.TZ)	Kodi iliyokusanya (SH.TZ)	Kodi isiyokusanya (SH.TZ)
<b>Idara ya Walipa kodi Wakubwa</b>	<b>162,694.66</b>	<b>18,490.27</b>	<b>144,204.39</b>
<b>Idara ya Uchunguzi Kodi</b>	<b>136,661.68</b>	<b>18,572.28</b>	<b>118,089.40</b>
<b>Jumla</b>	<b>299,356.34</b>	<b>37,062.55</b>	<b>262,293.79</b>

Kuwapo kwa madeni ya kodi ambayo hayajakusanya kwa muda mrefu ni dalili kwamba Mamlaka imeshindwa kukusanya kodi hizo. Kwa mtazamo wangu, mifumo na mikakati isiyoridhisha ya ukusanyaji wa madeni ya kodi, hasa katika ofisi za mikoa vimechangia Mamlaka kushindwa kukusanya madeni haya kwa wakati. Hii inamaanisha kuwa kunahitajika uboreshaji wa mifumo ya ukusanyaji wa madeni yanayotokana na kodi.

**Makadirio pungufu ya kodi Shilingi 9,363,346,393.23**

Mapitio yangu katika baadhi ya majalada ya walipa kodi na nyaraka nyingine zinazowahu walipa kodi kama vile marejesho ya kodi za mapato, taarifa za wanufaika wa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani, marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani na nyaraka mbalimbali kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka yalibaini kuwa kiasi cha kodi chenye thamani ya Shilingi 9,363,346,393.23 kilifanyiwa makadirio pungufu. Katika kiasi hicho cha kodi, Shilingi 1,970,294,443.08 kilitokana na uchunguzi wa taarifa za walipa kodi wa Idara ya Walipa kodi Wakubwa, Shilingi 124,216,200 kilitokana na Idara ya Uchunguzi wa Kodi na

Shilingi 7,268,835,750.15 kilitokana na uchunguzi wa taarifa za walipa kodi katika mikoa ya kodi 13 katika Idara ya Mapato ya Ndani.

Makadirio pungufu ya kodi yalisababishwa na uchambuzi hafifu wa taarifa za walipa kodi katika marejesho yao ya kodi za mapato ya kila mwaka, marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani pamoja na makadirio binafsi ya walipa kodi.

Kwa mtazamo wangu, kutokuwapo kwa ufanisi wa mifumo thabiti kunaweza kutoa mianya kwa watumishi wa Mamlaka wasio waaminifu kushirikiana na walipa kodi wasio waaminifu kutoa makadirio yasiyo stahiki hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki.

***Ninaishauri Serikali:***

- a) Kuimarisha uhakiki na udhibiti wa ukaguzi, uchunguzi na ukusanyaji wa kodi zote zinazostahiki kukusanywa ili kupunguza mlundikano wa madeni ya kodi zinazotokana na makadirio binafsi ya walipa kodi, uchunguzi wa kodi, kitengo cha ufundi na kitengo cha ukaguzi.
- b) Kuboresha ukaguzi na uchunguzi ili kupunguza madai yasiyo stahiki ya walipa kodi yanayotokana na ukusanyaji wa kodi za ongezeko la thamani na ukadiriaji usio sawa wa kodi ya mapato.
- c) Kufanya uchunguzi katika maeneo yote yaliyogundulika kuwa na makadirio pungufu ya kodi na kuhakikisha kodi hizo zinakusanywa pamoja na riba kama inavyotakiwa na Sheria za kodi.

**5.3.6.9 Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine ambayo hayakuwasilishwa kwenye Taasisi husika**

Ukaguzi wangu wa ada, tozo na mapato mengine yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato kwa niaba ya Taasisi nyingine kama vile Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya bandari na tozo za maendeleo ya reli kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2017 ulibaini kuwa kiasi cha Shilingi 410,448,166,098.44 kilichokusanywa na Mamlaka ya Mapato lakini hakikuhamishwa

kwenda kwenye Taasisi husika, kitu ambacho ni kinyume na matakwa ya sheria.

Katika mahojiano yangu na Uongozi wa Mamlaka, nilifahamishwa kwamba kwa mapato yaliyoingizwa kwenye akaunti ya makusanyo, Mamlaka haina ruhusa ya kuyatoa na kuyahamisha kwenda kwenye taasisi husika. Makusanyo hayo yanahu tozo za usambazi wa maji, tozo ya maendeleo ya reli, na ada ya bandari ambazo kwa ujumla ni asilimia 98.82 ya makusanyo ambayo hayakuhamishwa kwenda kwenye Taasisi husika. Wizara ya Fedha na Mipango, kupitia Hazina yenyewe, ndio ina wajibu wa kuhamisha fedha hizi kwenda kwenye Taasisi husika baada ya kukusanya na Mamlaka ya Mapato.

Ucheleweshwaji wa fedha kwenda kwenye Taasisi lengwa unaathiri utoaji wa huduma na utekelezwaji wa mipango ya Taasisi hizo. Ni maoni yangu kwamba, mapungufu haya yakiachwa yaendelee yataharibu nia nzuri ya uanzishwaji wa utaratibu huu wa makusanyo. Aidha, sio tu yatazuia utekelezwaji wa mipango ya Taasisi, bali pia yataathiri kwa ujumla upatikanaji wa huduma zilizotarajiwa kwa jamii. Muhtasari wa makusanyo hayo umeoneshwa katika jedwali hapa chini:

#### **Jedwali Na. 33: Muhtasari wa mapato yaliyokusanya na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine**

Na	Aina ya mapato	Makusanyo ya Mamlaka [TZS ]	Makusanyo yaliyohamishwa [TZS ]	Makusanyo ambayo hayakuhamishwa [TZS ]	Taasisi husika
1	Tozo za mafuta	744,100,054,886.23	741,429,506,006.01	2,670,548,880.22	Mamlaka ya Mapato
2	Tozo ya Petroli	316,518,926,711.18	314,957,113,082.28	1,561,813,628.90	Mamlaka ya Mapato
3	Tozo za nishati	17,240,550,741.87	16,645,165,064.09	595,385,677.78	Mamlaka ya Mapato
4	Usambazaji na usalama wa maji	134,463,913,485.95	134,453,825,069.65	10,088,416.30	Wizara ya fedha
5	Tozo ya maendeleo ya reli	194,687,198,522.06	46,164,191,789.25	148,523,006,732.81	Wizara ya fedha
6	Ada ya bandari	264,086,275,189.00	6,998,952,426.57	257,087,322,762.43	Wizara ya fedha
	Jumla	1,671,096,919,536.30	1,260,648,753,437.90	410,448,166,098.44	

#### **Mapendekezo**

- Ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa mapato yote yaliyokusanya na Mamlaka ya Mapato kupitia akaunti ya amana ya mafuta kwa niaba ya Taasisi nyingine yanahamishwa

kwa wakati kwenda kwenye Taasisi hizo ili kuziwezesha kutekeleza malengo na mipango yao iliyokusudiwa.

- b) Serikali ihakikishe kuwa tozo za bandari na za maendeleo ya reli zilizokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya Bandari na Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji katika akaunti za makusanyo kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) zinahamishwa bila kuchelewa.
- c) Uongozi wa Mamlaka ya Mapato uhamishe kiasi cha Shilingi 4,827,748,186.90 kinachohusiana na tozo za mafuta, nishati na usambazaji wa maji kwenda kwa wanufaika husika, na Hazina ihamishe tozo za maendeleo ya reli na tozo za bandari zenye Jumla ya Shilingi 405,620,417,911.54 kwenda Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji na Mamlaka ya Bandari kwa mujibu wa sheria.

## 5.4 UKAGUZI WA HESABU ZA TAIFA-HESABU JUMUIFU

### 5.4.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilirasimisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Hivyo Serikali iliandaa hesabu jumuifu kwa mara ya kwanza mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2013 kwa kuzingatia matakwa ya IPSAS 6. Pamoja na nia ya dhati ya serikali katika kuboresha uwazi na uwajibikaji, ujumuishwaji wa taasisi za umma kwenye Taarifa za Hesabu za Majumuisho umeendelea kukumbwa na changamoto kadha wa kadha katika utekelezaji. Changamoto hizo ni pamoja na:

### 5.4.2 Hali juu ya Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa katika sekta ya Umma visivyo na Msingi wa Taslimu (IPSAS Accrual) mnamo mwisho wa kipindi cha mpito

Serikali ilihamia kutoka Viwango vya Kimataifa katika sekta ya Umma vya Msingi wa Taslimu kwenda Viwango vya Kimataifa katika sekta ya Umma visivyo na Msingi wa Taslimu mwaka wa fedha 2012/2013 ambapo kwa mujibu wa mpango wa utekelezaji (IPSAS roadmap), kipindi cha mpito cha miaka mitano kiliishia tarehe 30 Juni 2017. Natambua juhudi zilizofanywa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN) na Kurugenzi ya uhakiki Mali za Serikali (DGAM) kuelekea upatikanaji hesabu ambazo zimefuata kikamilifu Viwango vya Kimataifa katika sekta ya Umma visivyo na Msingi wa Taslimu.

Mapitio yangu ya mpango wa utekelezaji wa IPSAS pamoja na hali ya uthamini wa mali uliofanywa na kurugenzi ya mhakiki Mali za Serikali, nilibainisha mapungufu yafuatayo:

#### **Uthamini wa mali za serikali**

Uthamini wa samani, Vifaa, Magari na mitambo haujafanyika katika taasisi 12 (16%) kati ya taasisi 73 kwa upande wa ardhi na majengo ambao ndio uthamini mgumu zaidi kufanyika, tassisi 54 (74%) hazijafanya uthamini.

Ili kuendana na mpango wa utekelezaji, kwa mwaka uliopo wizara, wakala na idara zinazojitegemea (MDAs) nyingi zilichagua kutumia gharama za kihistoria na kutumiwa kushuka kwa thamani kwa jumla (accumulated depreciation) kwenye gharama za mali hizo kuanzia mwaka 2012/13. Hii kwa mtazamo wangu itapelekea mali nyingi kuwa zimeshuka thamani kikamilifu (Fully depreciated) kwa kipindi kifupi kijacho jambo litakalopelekea serikali kugharimia uthamini.

### **Uanzishwaji na uhuishaji wa rejesta ya mali za kudumu**

Mhasibu Mkuu ameanzisha Daftari ya Mali za kudumu kwa wizara, wakala na idara zinazojitegemea (MDAs) 87. Nilibainisha rejista kwa baadhi ya taasisi hizo na Ofisi nyingine za Serikali ikiwa ni pamoja na Mashirika na Serikali za Mitaa bado hazijaanzishwa kwa kiwango cha kuweza kujumuishwa. Pia, Moduli ya mali za kudumu (Asset Management) haijaunganishwa na moduli zingine kwenye mfumo wa mahesabu (IFMS) kama vile moduli ya akaunti za malipo. Jambo hili linasababisha uhuishaji wa taarifa kwenye Rejista ya Mali za kudumu kutumia mfumo unaojiendesha wenyewe.

zaidi ya hayo, nilibaini, taratibu za Serikali, miongozo na sera bado viro katika msingi wa taslimu (Cash basis) na hivyo husababisha changamoto za kiutendaji kwa msingi usiokuwa wa taslimu (Accrual basis). Kuhuishwa kwa moduli ya Madeni yasiyolipwa kwenye mfumo wa Epicor 9.05 ili kuzalisha taarifa za matumizi na madeni yasiyolipwa bado ni changamoto kama ilivojionesha kwenye upatikanaji wa miamala ya kihasibu na uandaaji wa hesabu jumuifu zenye kufuata Viwango vya Kimataifa katika sekta ya Umma visivyo na Msingi wa Taslimu.

#### **5.4.3 Hesabu zilizojumuishwa zikiwa na tarehe tofauti na hesabu Jumuifu Bila Kufanya Marekebisho**

Ukaguzi wa Hesabu jumuifu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazoishia tarehe 30 Juni 2017 ulibaini kuwapo kwa taasisi moja; Twiga bancorp ambayo haikujumuishwa kwa sababu hesabu zake hazikuwasilishwa. Pia nilibaini, hesabu za taasisi

nne zilizojumuishwa wakati ziliwa na terehe tofauti ukilinganisha na hesabu jumuifu; taasisi hizo ni Benki ya uwekezaji ya Tanzania (TIB), Benki ya wanawake (TWB) na Benki ya maendeleo ya kilimo Tanzania (TADB) ambazo hesabu zake zilifungwa tarehe 31 desemba 2016 na Shirika la reli Tanzania (TRL) ambalo hesabu zake zilifungwa tarehe 31 desemba 2013. Hii ni kinyume na aya ya 46 ya IPSAS Na. 35, Waraka wa Hazina Na.12 uliotolewa tarehe 9 Januari 2015 na Waraka wa Uhasibu Na 3 wa 2015/16; ambazo zinahitaji taarifa za fedha za Taasisi inayodhibiti na Taasisi zinazodhibitiwa kuwa na tarehe sawa ya ufungaji wa hesabu. Pia, nilibaini kuwa hakuna marekebisho yaliyofanyika katika hesabu ili kuoanisha tarehe. Hali hii inatia shaka kwenye uhalisia wa hesabu jumuifu. Tazama **Jedwali Na 34** hapa chini:

**Jedwali Na. 34: Uondoshaji usiokamiliwa wa miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa shilingi bilioni 359**

Mfuko	Michango ya serikali kwa mujibu wa fungu 22	Mapato kwa mujibu hesabu za mifuko (TZS)	Tofauti (TZS)
LAPF	218,053,120,921	209,168,330,096	(8,884,790,825)
NHIF	200,511,342,363	175,324,961,000	(25,186,381,363)
PSPF	549,028,566,434	523,141,220,000	(25,887,346,434)
<b>Total</b>	<b>967,593,029,717</b>	<b>907,634,511,096</b>	<b>(59,958,518,622)</b>

*Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa Taasisi zake zinaandaa taarifa za ziada na marekebisho ya kifedha yanafanyika kwa usahihi ili kuendana na mahitaji ya IPSAS 35, Waraka wa Hazina No 12 wa tarehe 9 Januari 2015 na Waraka wa Uhasibu Na 3 wa 2015/16.*

#### **5.4.4 Hesabu zilizojumuishwa kwenye hesabu jumuifu bila kusainiwa/kutolewa na mamlaka husika**

Kanuni 11(3) (a) ya kanuni za fedha umma, 2001 (iliyorejewa 2004) inahitaji afisa masuuli kusaini hesabu kabla ya kutolewa. Kwa kufanya hivyo hukubali binafsi wajibu kwa ajili ya usahihi na kufuata masharti ya sheria na kanuni hizi za fedha za umma au na Mhasibu Mkuu.

Mapitio yangu ya sampuli ya hesabu za taasisi zinazodhibitiwa yalibainisha uwepo wa taasisi 64 ambazo hesabu zake hazikusainiwa na mamlaka husika ili kukubali wajibu kwa usahihi, ukamilifu na muonekano stahiki (**Rejea Kiambatisho Na. 5.2**)

Nina wasiwasi na usahihi wa taarifa zilizojumuishwa kutokana na kukosa umiliki wa maafisa masuuli husika.

*Ninapendekeza serikali ihakikishe hesabu zinasainiwa/kupata umiliki wa afisa masuuli na mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi kabla ya kuijumuisha kwenye hesabu jumuifu.*

#### **5.4.5 Uondoshaji usiokamiliwa wa miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa Shilingi bilioni 359**

Aya 40 (c) ya IPSAS 35 inahitaji taasisi inayojumuisha (a consolidating entity) kuondoa kikamilifu mali, madeni, mali halisi, Mtaji, mapato, matumizi na mtiririko wa fedha ambazo zinazohusiana na miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa. Lengo la utaratibu ni kuondoa kuhesabu mara mbili na kuongeza uhalisia wa matukio yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha.

Mapitio yangu ya hesabu jumuifu yalibainisha uondoshwaji (Elimination) wa matumizi kiasi cha Shilingi 63,781,917,503,000 dhidi ya mapato ya Shilingi 63,482,869,159,000 baina ya taasisi zinazojumuishwa hivyo kusababisha kushusha/kupandisha matumizi na mapato kwa kiasi cha Shilingi 299,048,344,000.

zaidi ya hayo, mapitio yangu ya jumla ya uondoshwaji wa mapato na amtumizi ya mifuko ya hifadhi ya jamii yalibainisha kuondoshwa kwa Shilingi 1,216,046,479,000 katika pande zote

mbili za Taarifa ya ufanisi wa fedha hivyo kupelekea madhara halisi kuwa sifuri. Hata hivyo kwa upande wa michango, niligundua serikali ilichangia Shilingi 967,593,029,717 kwa mifuko ya LAPF, NHIF na PSPF lakini mifuko hiyo ilikiri kupokea Shilingi 907,634,511,096. Tazama **Jedwali Na. 35** hapa chini:

**Jedwali Na. 35: Uondoshaji usiokamilika wa miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa shilingi bilioni 359**

Mfuko	Michango ya serikali kwa mujibu wa fungu 22	Mapato kwa mujibu hesabu za mifuko (TZS)	Tofauti (TZS)
LAPF	218,053,120,921	209,168,330,096	(8,884,790,825)
NHIF	200,511,342,363	175,324,961,000	(25,186,381,363)
PSPF	549,028,566,434	523,141,220,000	(25,887,346,434)
<b>Total</b>	<b>967,593,029,717</b>	<b>907,634,511,096</b>	<b>(59,958,518,622)</b>

Kwa mantiki hiyo, serikali iliondosha miamala hiyo kwa kuzingatia matumizi ya upande wa serikali, kitendo ambacho kilipelekea uondoshwaji wa kuzidi kwa Shilingi 59,958,518,622 kutoka mapato ya mifuko husika.

*Ninapendekeza Serikali kurekebisha uondoaji uliofanywa ili kusahihisha takwimu zake.*

#### 5.4.6 Uwekezaji wa mtaji wa biashara uliothaminishwa kwa gharama ya awali Shilingi bilioni 549

Mapitio yangu ya sampuli 13 za hesabu za taasisi zilizojumuishwa na zenye uwekezaji wa mitaji kibiaresha wenyewe thamani ya Shilingi 549,199,224,690; ulibainisha kuwa, uwekezaji hauna maelezo ya kina juu ya idadi ya hisa inayomilikiwa, bei ya soko la hisa, na mbinu zilizotumika kuthaminisha bei za hisa zilizotajwa. Kwa taasisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Ujiji, Shirika la Maendeleo la Petroli la Tanzania (TPDC) yaliripoti uwekezaji ambao ulibakia sawa na kipindi kilichopita. **Tazama Jedwali hapa chini:**

**Jedwali Na. 36: Uwekezaji wa mtaji wa biashara  
uliothaminishwa kwa gharama ya awali shilingi bilioni 549**

S/N	Entity	Amount TZS 000'
1	NBAA	93,800
2	PSPF	45,737,484
3	PPF	305,437,509
4	LAPF	68,220,549
5	GEPF	38,001,565
6	TIB DEV	19,163,024
7	TPDC	43,573,927
8	KYELA DC	550.00
9	TANESCO	1,055,000
10	UTT PROJECT	1,390,000.00
11	UTT-AMIS	13,810,149
12	KIGOMA UJIJI DC	1,605
13	NIC	12,714,063
	<b>TOTAL</b>	<b>549,199,224.69</b>

Chanzo: Hesabu za Fedha za Mwaka wa Fedha 2016/17

Hii ni kinyume na aya ya 48 ya IPSAS 29 ambayo inahitaji mali za kibashara (financial assets) baada ya kutambua thamani ya uwekezaji kwa mara ya kwanza; kuthaminishwa kwa bei ya soko la wakati husika bila kuondoa gharama za miamala inayoweza kuhusika wakati wa kuuza mali hiyo. Katika hali hiyo, msingi wa thamani ya Shilingi 607,361,958,000.amabazo zimeoneshwa katika hesabu jumuifu kama uwekezaji mitaji haikuweza kuthibitishwa.

*Ninapendekeza Serikali kupima uwekezaji wa mitaji ya biashara kwa thamani halisi (fair value) na kuonesha/taja habari muhimu (husika) juu ya hisa zilizopo.*

#### 5.4.7 Kutoainisha na kutotambua dhima tarajiwa baada ya kuamuliwa

Mapitio yangu ya dhima tarajiwa zilizotajwa kwenye hesabu jumuifu Shilingi bilioni 864 yalibainisha kutokuainishwa kwa dhima hizo kwa misingi ya uwezekano wa kulipwa na kitambo cha dhima tarajiwa kama inavyotakiwa na Aya 100 (a) - (c) ya IPSAS 19.

Nilibaini kuwepo kwa dhima za Shilingi 430,500,000 kutokana na kesi tano (5) ambazo hukumu ya mwisho ilifanyika dhidi ya serikali lakini hazikutambuliwa pia. **Tazama Jedwali hapa chini:**

**Jedwali Na. 37: kutotambua dhima tarajiwa baada ya kuamuliwa shilingi 430,500,000**

S/n	Fungu	Jina la taasisi	kesi	Hali ya kesi	tarhehe ya hukumu	Kiasi kilichoamuliwa na mahakama serikali ilipe (Shilingi)
1	43	Wizara ya kilimo, mifugo na uvuvi	kesi No.4/2004 Jacob Swalehe Vs P/S. MoAFSC	Imefungwa	Haijatajwa kwenye hesabu jumuifu	10,000,000.00
2	43	Wizara ya kilimo, mifugo na uvuvi	Kesi No.15/2003 TPM Company Vs P/S MoAFSC	Imefungwa	Haijatajwa kwenye hesabu jumuifu	500,000.00
3	43	Wizara ya kilimo, mifugo na uvuvi	Kesi No.15/2003 TPM Company Vs P/S MoAFSC	Imefungwa	Haijatajwa kwenye hesabu jumuifu	400,000,000.00
4	52	Wizara ya Afya na maendeleo ya jamii	Kesi No. 7/2008 Jared N. Mariwa Vs Wizara ya Afya	Imefungwa	23 Juni 2014	15,000,000.00
5	52	Wizara ya Afya na maendeleo ya jamii	Kesi No. 37/2004 Raphael Alberto na wenzake 35 Vs Wizara ya Afya	Imefungwa	23 Juni 2014	5,000,000.00
					Jumla	430,500,000.00

*Napendekeza Serikali kufanya uainishaji sahihi na kutambua dhima zilizokwisha kuamuliwa ili kuongeza uelewa wa taarifa zilizoripotiwa katika hesabu jumuifu na watumiaji wake.*

#### 5.4.8 Uwekezaji hasi katika Mshikamano (Associate) na Ubia (Joint venture) Shilingi 405,349,237,000

Aya ya 41 ya IPSAS 36 inahitaji mwekezaji kuacha kutambua sehemu yake ya upungufu/hasi alikowekeza mara tu uwekezaji huo unapokuwwa umepungua hadi kufikia sifuri. Baada ya hapo, kunahitajika kutaja/kuonesha (Disclose) upungufu wa thamani (impairment) wa mali husika. Aya ya 42 ya IPSAS 36 inahitaji pia mwekezaji kuendelea na kutambua sehemu yake ya ziada baada ya sehemu yake ya faida kuwa sawa na sehemu ya hasara / upungufu ambao haukutambuliwa awali.

Hata hivyo, mapitio ya hesabu jumuifu; maelezo ya ziada (Note) 77 yanayohusiana na uwekezaji katika Mashirika (associate) na Mipango ya pamoja (joint ventures) imebainishwa taasisi visa tisa

(9) zilizoripoti uwekezaji hasi katika Mashirika na Mipango ya pamoja wa Shilingi 405,349,237,000 kwa mwaka 2016/2017 na Shilingi 362,241,134,000 kwa mwaka 2015/2016. Hii ni kinyume na IPSAS iliyotajwa hapo juu. Matokeo yake, uwekezaji katika mashirika na mipango ya pamoja umeonyeshwa pungufu kwenye mizania jumuifu ya taarifa za fedha kwa Shilingi 405,349,237,000. Tazama **Jedwali Na.**

**Jedwali Na. 38: uwekezaji hasi**

Taasisi/Shirika		TZS '000	TZS '000	TZS '000
Airtel (T) Limited	40%	-273,336,400	-49,972,800	-323,309,200
Datel Tanzania Limited	35%	-235,502	-	-235,502
Friendship Textile Co. Limited	49%	-7,431,094	-1,579,779	-9,010,873
Tanscan Timber Co. Limited	49%	-104,321	-19,979	-124,300
Tanzania Development Finance Limited	32%	-7,677,578	-2,809,920	-10,487,498
TAZAMA Pipelines Limited	33%	438,152	-950,357	-512,205
Williamson Diamond Limited	25%	-73,059,356	11,786,880	-61,272,476
Darbrew Investment Limited	40%	-396,883	-	-396,883
Tancoal Energy	0%			-300
Total			-43,545,955	-405,349,237

*Napendekeza Serikali kutaja/kuonesha jumla ya upungufu/nakisi itokanayo na uwekezaji katika Mashirika na Mipango ya pamoja kulingana na mahitaji ya IPSAS 36. Pia, irekebishe salio la kipindi kilichopita na la sasa kwenye mizania jumuifu ya taarifa ya fedha na Taarifa jumuifu ya ufanisi wa fedha kama ipasavyo.*

#### 5.4.8 Kuhesabu mara mbili mapato yaliyokusanya na TRA kwa niaba ya taasisi nyingine TZS 325,308,753,499.97

Mapitio ya hesabu jumuifu yalibainisha kuwa Shilingi 15,094,949,741,000 zilionyeshwa kwenye hesabu jumuifu kama mapato ya kodi iliyokusanya na TRA. Kiasi hiki kinajumuisha kodi iliyokusanya na TRA kwa niaba ya taasisi nyingine Shilingi 2,165,273,630,236 kama vile mapato ya meli kutia nanga kwa TPA, kodi ya mauzo kwa bodi ya korosho, tozo ya maendeleo ya ujuzi (SDL) kwa VETA na mikopo ya elimu ya juu (HESLB).

Kati ya kiasi cha Shilingi 2,165,273,630,236, jumla ya Shilingi 1,478,502,889,386 ingawa kwa kiwango kidogo kulinganisha na kiasi kilichokusanywa kutokana na ukomo wa bajeti na fedha zingine kutotolewa na Hazina, kiliripoti na taasisi husika. Hata hivyo, ni kiasi cha shilling 1,153,194,135,886 kilichoripotiwa na taasisi husika kama ruzuku ya serikali na ada ya mafuta, kiliondoshwa (elimination) katika hesabu jumuifu ipasavyo. Kiasi kilichobaki cha shilling 325,308,753,499.97 kilichoripotiwa na taasisi husika kama mapato na ada mbalimbali hakikuondoshwa na hivyo kusabaibisha kiasi hicho kuhesabiwa mara mbili katika hesabu jumuifu. (**Kiambatanisho Na. 5.3**)

Katika hali hiyo, mapato yaliyoripotiwa katika hesabu jumuifu yanapotosha watumiaji wa taarifa hiyo.

Napendekeza serikali kurejea hesabu Jumuifu na kufanya marekebisho stahiki.

## SURA YA SITA

### 6.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI NA UTAWALA BORA

Sura hii inaelezea matokeo ya tathmini ya mifumo udhibiti wa ndani inayoendeshwa ndani ya Taasisi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Inaelezea mapungufu yaliyojitekeza katika tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, pamoja na masuala ya utawala bora ,mfumo wa teknolojia na habari, Kamati za Ukaguzi, Kazi za Ukaguzi wa Ndani, Tathmini za udanganyifu pamoja na usimamizi wa mali zilizonyang'anywa.

Ripoti hii inaelezea matokeo ya tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na mapendekezo. Pia inaangalia njia ambazo zinaweza kudhibiti na uendeshaji ambao unaweza kuboreshwa ili kuondokana na udhaifu unaoonekana katika kudhibiti na kuongeza ufanisi, ili kudhibiti vihatarishi vinavyojitekeza.

Uchunguzi wetu wa udhibiti wa ndani ulikuwa na madhumuni machache, haungeweza kutambua mapungufu yote katika udhibiti wa ndani..Mambo yaliyojitekeza katika taarifa hii ni yale tu yanatokana na ukaguzi, na ambayo tunaamini kuwa yanatakiwa kuletwa mbele ya umma. Hatuwezi kuwajibika na kuripoti vitu vyote vya vihatarishi vinavyohusiana na udhaifu wa udhibiti wa ndani.

Bodi zinahusika na sera, utawala na kazi za uangalizi. Wakati viongozi wanawajiibika kwa masuala ya uendeshaji ikiwa ni pamoja na wafanyakazi na mifumo ya udhibiti wa ndani.

Mambo yaliyomakinikiwa zaidi ni, Utendaji wa Kamati za Ukaguzi, na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Udhibiti Mkuu wa TEHAMA, taratibu za tathmini ya vihatarishi, uendeshaji wa ulaghai na udhibiti pamoja na masuala ya utawala. Mapungufu yafuatayo yalibainika Ufafanuzi wa ufuatayo wafuatayo ulibainishwa.

## 6.1 Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani katika Taasisi

Kulingana na Kanuni ya 28(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, kila Afisa Masuuli anatakiwa kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kutoa uhakika iwapo mifumo ya ndani ya Taasisi inafanya kazi ipasavyo. Hata hivyo, tathmini yangu kuhusu ukaguzi wa ndani kwenye sampuli ya Wizara, Idara na Taasisi pamoja na Sekretarieti za Mikoa ilibani kuwa Taasisi 33 zikijumuisha Wizara na Idara 14, Sekretarieti za Mikoa 17 na Taasisi nyingine 2 zilionekana na mapungufu yakiwemo: kutokuanzishwa kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani, vitendea kazi hafifu na mipango ya ukaguzi wa ndani kutoidhinishwa na Kamati ya Ukaguzi.

Orodha ya Taasisi zenyе mapungufu kwenye kitengo cha Ukaguzi wa Ndani zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 6.1**

**Jedwali Na. 39:Mlinganisho wa Tathmini ya Udhibiti wa Ndani**

Mwaka wa Fedha Taasisi	30 June, 2016	30 June, 2017	Tofauti	Tofauti ya Asilimia
Wizara	14	3	11	35.5
Sekretarieti	17	15	2	6.5
Jumla	31	18	13	42

Jedwali la hapo juu linaonesha kupungua kwa idadi ya mapungufu katika kitengo cha ukaguzi wa ndani. Jumla ya mapungufu yaliyojitokeza kwa mwaka huu ni taasisi 18 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilikuwa taasisi 31 na kuleta tofauti ya taasisi 13 ambazo ni sawa na 42%

Kutokuwapo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani ambacho ni madhubuti ni hatari kwa sababu kunaongeza uwezekano wa kuwapo udanganyifu, na kutofuatwa kwa sheria, taratibu, maelekezo na sera . Mbali na hayo, Taasisi zinakosa nafasi ya kupata mapendekezo kwa ajili ya kuimarisha sera na taratibu za utendaji.

Upitiaji huru wa shughuli za taasisi ni jambo muhimu, na napenda kushauri Maafisa Masuuli kuwa na vitengo vya Ukaguzi wa Ndani vyenye rasilimali za kutosha; na kutimiza wajibu wao ambapo ni pamoja na kuainisha mapungufu ya udhibiti wa ndani na kutoa mapendekezo ya marekebisho na ushauri utakaoleta tija.

## 6.2 Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi

Kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inataka kila Taasisi kuwa na kamati ya Ukaguzi. Wajumbe wa Kamati na majukumu yake vimeainishwa kwenye Kanuni ya 31 na 32 ya Sheria ya Fedha. Majukumu yake ni pamoja na ; kuwa na vikao vya kila robo mwaka, uidhinisha mpango wa ukaguzi wa ndani kila mwaka, kupitia taarifa za ukaguzi wa ndani na nje, kutoa ushauri kwa Afisa Masuuli juu ya hatua za kuchukuliwa juu ya mambo yaliyojitekeza kwenye ripoti ya ukaguzi wa ndani au kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa ripoti ya kila mwaka juu ya kazi zake.

Hata hivyo, tathmini ya ukaguzi katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi katika Wizara, Idara, Sekretari za Mikoa ilibaini Taasisi 24 zikijumuisha Wizara na Idara 6, Sekretarieti za Mikoa 18 zilipatikana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Taasisi kutokuwa na Kamati ya Ukaguzi, kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka wa ukaguzi wa ndani na kutokupitia taarifa za hesabu za Taasisi.

Orodha ya Taasisi zenyе mapungufu kwenye Kamati za Ukaguzi zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 6.2**

**Jedwali Na. 40: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi**

Mwaka wa Fedha	30 June, 2016	30 June, 2017	Tofauti	Tofauti ya Asilimia
Taasisi				
Wizara	14	6	8	26
Sekretarieti	12	18	-6	-19
Taasisi zingine	5	0	5	16

Jedwali la hapo juu linaonesha kupungua kwa idadi ya mapungufu katika kamati ya ukaguzi. Jumla ya mapungufu yaliyojitekeza kwa mwaka huu ni tasasi 27 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilikuwa taasisi 31 na kuleta tofauti ya taasisi 4 ambazo ni sawa na 13%

Menejimenti ina wajibu wa kuanzisha na kudumisha utawala bora, hasa katika kamati ya ukaguzi, ili kuleta mawasiliana ya vihatarishi na kuhabarisha maeneo husika katika wizara.

Napendekeza kwamba, Maafisa Masuuli wahakikishe Kamati za Ukaguzi zinafanya kazi kulingana na sheria kama zilivyoainishwa kwenye sheria ya Fedha za Umma ili kuhakikisha malengo ya Taasisi husika yanafikiwa na kuhakikisha uwajibikaji, kuwepo kwa taarifa za fedha za kuaminika pamoja na kufuata sheria, taratibu na sera.

### **6.3 Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi**

Usimamizi wa vihatarishi ni utaratibu wa kufanya na kutekeleza maamuvi ambayo hupunguza madhara makubwa katika utendaji wa Taasisi. Utaratibu wa usimamizi wa vihatarishi inahusisha: kutambua na kuchambua vihatarishi vinavyoweza kuleta hasara, kuchunguza mbinu mbadala za kudhibiti vihatarishi, kuchagua mbinu sahihi zaidi ya usimamizi wa vihatarishi, kutekeleza mbinu iliyochaguliwa pamoja na ufuatiliaji wa matokeo.

Pia, nilitathimini Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi katika utaratibu uliopo wa usimamizi wa vihatarishi kwa lengo la kupima maandalizi yao kwa matukio yasiyotarajiwa ambayo kama yatatokea yataathiri uendelevu wa utoaji wa huduma kwa umma. Nilibaini kuwa Taasisi 15, ikiwa ni pamoja na Wizara 11, Sekretarieti za Mikoa 1 na Balozi ambazo, zina mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokuwa na Rejista ya vihatarishi, kutokuwa na sera ya kudhibiti vihatarishi, kuwa na Rejista isiyoenda na wakati, pamoja na kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na majanga.

Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 6.3**

**Jedwali Na. 41: Tathmini katika usimamizi wa vihatarishi**

Mwaka wa Fedha Taasisi	30 June, 2016	30 June, 2017	Tofauti	Tofauti ya Asilimia
Wizara	9	3	6	23
Sekretarieti	12	11	1	4
Taasisi zingine	5	0	5	19
Balozi	0	1	-1	-4
<b>Jumla</b>	<b>26</b>	<b>15</b>	<b>11</b>	<b>42</b>

Jedwali la hapo juu linaonesha kupungua kwa idadi ya mapungufu kwenye Tathmini katika usimamizi wa vihatarishi. Jumla ya mapungufu yaliyojitekeza kwa mwaka huu ni tasisi 15 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilikuwa taasisi 26 na kuleta tofauti ya taasisi 11 ambazo ni sawa na 42%

Ili kuhakikisha huduma bora kwa umma na kuwa na athari ndogo ya matukio yenyeye athari yasiyotarajiwa, Maafisa Masuuli wanashauriwa kuimarisha taratibu za usimamizi wa vihatarishi kwa: kuwa na kumbukumbu za usimamizi wa vihatarishi kwa kuvitambua, kuvichunguza, kuwa na mbinu mbadala ya usimamizi wa vihatarishi, kuchagua mbinu sahihi zaidi ya usimamizi wa vihatarishi, kutekeleza mbinu iliyochaguliwa pamoja na kufuatilia matokeo.

#### 6.4 Kupitia Mifumo ya TEHAMA

Ikiwa ni sehemu ya ukaguzi, tathmini ilifanyika kwenye mifumo ya TEHAMA ili kujiridhisha kama Taasisi za Serikali zimeweka mfumo wa ndani wa TEHAMA unaodhiihirisha usiri, wenyewe uwezo wa kutoa taarifa sahihi za kihasibu na nyinginezo ambazo zinatunzwa humo.

Matokeo ya ukaguzi yalionesha kuwa Taasisi 31 zimekiuka taratibu za TEHAMA; ambazo ni Wizara 5, Sekretarieti 13 na Balozi 13. Ukiukwaji huo ni pamoja na;

Kutokuwa na Mpango wa kukabiliana na majanga ya TEHAMA, sera, kutokujaribu ufanisi wa mpango uliopo wa kukabiliana na majanga. Hii inapelekea kuwa vigumu katika kurejesha mfumo

kwa wakati kama mfumo utapata hitilafu yoyote, hivyo kupata hasara ya taarifa ambazo zinaweza kusababisha mwendelezo wa shughuli za taasisi kusitishwa.

Hakuna Kamati ya Uendeshaji ya TEHAMA ambayo ina wajibu wa kuboresha ubora wa taarifa, mfumo na teknolojia ya habari na mawasiliano. Kamati inatakiwa kubuni mikakati ya TEHAMA katika Taasisi na mipango ya kuhakikisha gharama zinakuwa nafuu katika usimamizi wa mfumo na rasilimali kuitia taasisi za serikali

Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 6.4**

Teknolojia ya Habari imekuwa muhimu katika shughuli za Serikali. Hata hivyo, pia ina madhara yake ambapo kuna haja ya Taasisi za Serikali kuhakikisha usiri, usalama, usahihi wa taarifa za uhasibu na taarifa nyingine.

Ili kufafanua na kuweka mfumo wa TEHAMA ambao utawezesha ufanisi wa maamuzi ya kimkakati ya TEHAMA, uwekezaji na mipango ya kuhakikisha kwamba udhibiti wa TEHAMA unawekwa vizuri.

Mfumo huo unapaswa kuhamasisha uundaji wa Kamati ya Uendeshaji wa TEHAMA, Mpango wa Mkakati wa Teknolojia na muundo wa utumishi ambayo itawezesha kufikia malengo ya taasisi

Inaonyesha kuwa idadi ya Taasisi zenye mapungufu katika TEHAMA imeongezeka kutoka 19 hadi 31 ikilinganishwa na mwaka jana ikiwa ni ongezeko la taasisi 12 ambayo ni sawa na asilimia 39

Serikali inapaswa kuwa na muundo mzuri wa mipango ya kukabiliana na majanga na mikakati ya kuhakikisha kuwa vifaa vyta kompyuta na programu vinatunzwa ili kuweza kukabiliana na majanga pale yanapotokea.

## 6.5 Tathmini ya kutambua na kuzuia udanganyifu

Kama sehemu ya ukaguzi, tathmini ilifanyika ili kuthibitisha udhibiti sehemu za Wizara ili kujihakikishia kwamba vipengele vya ulaghai vinatambuliwa na kuzuiwa kutokea na sio kutafuta udanganyifu. Kwa ujumla, udanganyifu ni tendo la kukusudia, pengine kwa mene jimenti, wale wanaohusika na utawala, wafanyakazi au watu wengine ambao wanajihuisha na matumizi ya udanganyifu, ili kupata faida isiyofaa au kinyume cha sheria. Ndani ya udanganyifu kwa Serikali inaweza kuwa na taarifa za ulaghai za fedha au matumizi mabaya ya mali za serikali.

Wajibu wa msingi wa kutambua na kuzuia udanganyifu na makosa mengine na uwekaji mzuri wa mfumo wa ufanisi wa kutosha na udhibiti wa ndani ni wa na menejimenti.

Katika ukaguzi wa mwaka huu nilibaini tukio moja la udanganyifu katika ubalozi wa Maputo. Mhasibu wa balozi huo alifanya miamala mitatu kwa ajili ya kujinufaisha na kusababisha hasara ya USD 150,000 ambayo ni sawa na Shilingi 332,856,000 za kitanzania .Uhamishaji wa fedha ulifanyika kati ya tarehe 26 oktoba, 2016 na 13 Aprili, 2017 kutoka ‘Millennium bin Julius Nyerere Prestige’ kwenye akaunti namba 79667362 kwenda akaunti namba 182283177 ambayo inamilikiwa na huyo mhasibu

Balozi hakufanya ufatiliaji katika maombi ya fedha na utoaji wa fedha katika benki.

Ninahimiza Serikali iendelee na ufuatiliaji na kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kuja na mfumo thabiti ambao unasaidia ufanisi katika kupunguza matukio ya udanganyifu.

Mamlaka ya uchunguzi inapaswa kufanya uchunguzi wa kina juu ya shughuli hizi za udanganyifu ambazo zitahakikisha kwamba, hatua za nidhamu na kisheria zimefanyika dhidi ya mfanyakazi baada ya kupata ushahidi wa kutosha ambao unaweza kuthibitisha kesi bila shaka.

## 6.6 Masuala ya Kiutawala

Utawala ni mchanganyiko wa utaratibu na miundo ya taasisi iliyotekelizwa na Bodi ya Wakurugenzi ili kuwajulisha, kuelekeza, kusimamia, na kufuatilia rasilimali za taasisi, mikakati na sera kuelekea kufikia malengo ya taasisi.

Kazi za bodi hiyo ni kutoa ushauri kwa Wizara na Katibu Mkuu juu ya maendeleo na matengenezo ya mfumo wa kimkakati na malengo ya taasisi hiyo, bodi inapitia mipango na bajeti zilizohusishwa, na utendaji wa taasisi kila mwaka.

Kwa mtazamo wa taratibu za ukaguzi wangu, nilitathmini kuwapo kwa utendaji wa Bodi za Uongozi katika vyombo vy ya Serikali zilizopangwa. Kuna mapungufu yaliyoyoitokeza katika utekelezaji wa muundo wa taasisi na kwenye Bodi ya Ushauri kama ifuatavyo:

**kutokuwapo kwa Bodi ya Ushauri ya Usimamizi kwa wanachama**

Nimepitia muundo wa Bodi ya Kamati ya Ushauri wa Idara ya Ofisi ya Rais na Idara ya Usimamizi wa Kumbukumbu na nilibaini kwamba kwa sasa, Bodi ina mjumbe mmoja tu anayefannya kazi kama mwenyekiti aliyechaguliwa Januari 2017, wanachama wengine walikuwa bado hawajachaguliwa. Hii ni kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Kumbukumbu, sehemu ya 7 (2) ya 2002.

## 6.7 Ukosekanaji wa Bodi ya Ushauri

Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya 1997 kifungu 6 (1) inasema kuwa kila wakala inatakiwa kuwa na bodi ya ushauri itakayoundwa na waziri husika. Bodi hiyo itaundwa na Katibu Mkuu kama mwenyekiti wa bodi na wajumbe wasiopungua wanane kutoka katika utumishi wa umma au kwingineko wenye vigezo na uzoefu wa shughuli za wakala husika.

Wakati wa ukaguzi wa wakala nimebaini kuwa kuna wakala nne (4) ambazo hazina Bodi za Ushauri. Tazama Jedwali Na. 42 hapo chini

**Jedwali Na. 42: Wakala zisizokuwa na Bodi Ya ushauri**

Muda wa Mwisho wa Bodi	Kipindi bila Bodi Ya shauri	Jina la wakala
Aprili 2016	Miezi 20	Chuo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki
Juni 2016	Miezi 18	Wakala wa Mbegu za Kilimo
Mei 2015	Miezi 32	Wakala wa Elimu ya Uvubi na Mafunzo
2013/2014	Miezi 48	Wakala wa Ndege za Serikali

Kipindi tajwa ni mpaka wakati wa ukaguzi Desemba 2017

Ukosekanaji wa bodi ya ushauri katika wakala hizi unasababisha shughuli za wakala kuendeshwa bila usimamizi, uangalizi na ushauri wa bodi. Kwa kipindi kirefu sasa wakala hizi zimekosa ushauri wa bodi hii katika masuala ya kupitia na kupitisha mpango kazi wa wakala, kuidhinisha malengo ya wakala ya kila mwaka, tathimini ya utendaji wa wakala na kuidhinisha taarifa za fedha za wakala.

Nazishauri menejimenti za wakala husika, kwa kushirikiana na Makatibu Wakuu wa Wizara husika, kuwasiliana na Mawaziri wa wizara hizo ili waweze kuteua bodi ya ushauri ili kufanikisha shughuli za ushauri kufanyika katika wakala hizi. Mapitio ya muundo wa taasisi

### **6.8 Ukaguzi wa Miundo ya Kiutawala**

Nimepitia muundo wa Ofisi ya Idara ya Rais na Idara ya Usimamizi wa Kumbukumbu na kubaini kwamba unapingana na kanuni moja ya utawala bora ambayo ni uhuru. Kwa mujibu wa muundo wa taasisi ya Idara ya usimamizi wa nyaraka, nafasi ya Bodi ya Ushauri iko chini ya Mkurugenzi Mkuu ambayo inaonyesha kwamba Bodi inaripoti kwa Mkurugenzi.

Mapitio zaidi yalibainisha kuwa hakuna tofauti kati ya Mkurugenzi wa Taasisi ya Idara ya usimamizi wa nyaraka (mkuu wa taasisi) na Mwelekeo wa wakurugenzi wasaidizi ambao wote wanaonekana kama ni Wakurugenzi. Pia tumeona kuwa hakuna tofauti za kazi

zinazoonyesha utofauti kati ya wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi ndani taasisi.

Taasisi ya Idara ya usimamizi wa nyaraka inashauriwa kupitia muundo wa taasisi yake ili kushughulikia suala la Utawala

### **6.9 Changamoto katika utekelezaji wa sheria za kutaifisha na kuokoa mali**

Utaifishaji ni upotevu wa moja kwa moja wa umiliki wa haki kwa mali binafsi au mali isiyohamsshika kwa kutofuata sheria , au kama mahakama iliamuru fidia kwa kupoteza au uharibifu kwa mdai.

Nimepitia kazi za Ofisi ya DPP. Hata hivyo, nimeona changamoto zifuatazo: katika ofisi hiyo kuhusiana na mchakato wa kuokoa mali kama zifuatazo

### **6.10 Kuwapo kwa miongozo Mingi inayoongoza Masuala ya kuokoa mali na utaifishaji**

Huokoaji wa mali unasimamiwa na miongozo mbali mbali ya sheria .Na kila mwongozo unautaratibu wake katika usimamizi katika kutaifisha mali kama ilivyoonyeshwa katika *kiambatisho 6.5.*

### **6.11 Udfaifu wa Udhibiti wa Mali Zilizotaifishwa**

#### **a) Kukosekana kwa Taarifa ya Mali Zilizotaifishwa**

Ukosefu wa sera na taratibu za kushiriki katika taasisi za serikali zinazohusiana na taarifa za uhasibu na fedha za mali zilizotaifishwa. Serikali haiandai ripoti moja ya kifedha ya kutaifisha mali, na matokeo yake, nilishindwa kuthibitisha mapato yanayotokana na mali za nchi zilizotaifishwa.

#### **a) Ukosefu wa Mwongozo juu ya Uendeshaji wa Akaunti ya AFR "9921161271"**

Hakuna mwongozo wa jinsi gani fedha zilizowekwa katika akaunti kwa ajili ya uondoaji wa mali zilizotaifishwa ambazo zinapaswa kutumiwa na vyanzo vingine vya amana, zinaweza kutumika kuongeza mfuko. Matokeo yake, sehemu ya mapato

yaliyowekwa katika akaunti hiyo haiwezi kutumiwa kufidia gharama za uchunguzi na mashtaka, udhibiti wa mali na gharama za uhamisho wa fedha; na fedha hizo haviwezi kutoka katika vyanzo vingine ili kuhakikisha upatikanaji wa mfuko wa kuendeleza programu ya uokoaji wa mali.

**b) Mapitio ya Mifumo ya Kisheria ya utaifishaji katika Sheria ya Mapato ya Uhalifu, [Cap 256 R.E.2002].**

Sheria ya Uhalifu haielezi masharti ya kutosha ambayo yatasaidia usimamizi bora na uondoaji wa mali zilizoshikiliwa na kutaifishwa. Udfaifu ulibainishwa katika maeneo yafuatayo:

Sheria ya Uhalifu haionyeshi masharti yoyote ya kufuta na kufungwa kwa mali ambayo inaharibika. hivyo huleta shida ya kuzisimamia. Hii hukwaza utekelezaji wa utaifishaji wa mali zinazoharibika.

Sheria ya uhalifu pia ipo kimya juu ya utoaji wa mali ambazo zimetaifishwa na utolewaji na fidia kwa walioathirika. Pia hii huleta ugumu katika kuzirejesha mali ambazo zimetaifishwa.

Sheria ya uhalifu haitoi masharti ya wazi juu ya usimamizi na uondoaji wa mali zilizotaifishwa. Inatoa mbadala wa usimamizi wa mali ambazo ziko chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina.

**c) Kutokutathiminiwa kwa Mali zilizotaifishwa**

Niligundua kuwa magari 15, boti moja na pikipiki mbili katika mikoa ya Lindi, Tanga, Morogoro na Mbeya zilikuwa ni mali ambazo zimetaifishwa na hazikufanyiwa tathimini.Hii ni kinyume na sehemu ya 14 (2) ya Sheria ya Uhalifu inayosema kwamba, mahakama inapoamuru kuwa mali isiyohamishika nje ya pesa itaifishwe kwa Jamhuri ya Muungano, itaelezea kiasi ambacho kinadhani kuwa ndiyo thamani ya mali hiyo wakati wa amri hiyo inapotolewa.Wakati wa kuhakiki mali zilizotaifishwa, tulibaini kwamba ,mahakama iliagiza kutaifisha mali bila ya kuzifanya tathmini.

Kutokuwapo kwa tathmini kunasababisha vigumu wakurekodi mali katika kitabu cha akaunti

Naishauri Serikali kuzitambua taasisi husika ili kujua thamani ya mali za kuuzwa na zile ninazotakiwa ziorodheshwe kama mali za Serikali.

**d) Kutokuwapo na rejista ya mali zilizotaifishwa**

Katika zoezi la uhakiki wa mali zilizotaifishwa kwenye kituo cha polisi huko Dar es salaam, Lindi, Mbeya na Morogoro nilibaini kuwa rejista ya mali isiyohamishika kwa ajili ya mali zilizotaifishwa haikuwepo. Mali zilizotaifishwa zinaweza kupotea bila menejimenti kutambua.

**e) Utunzajii wa Mali zilizozuiliwa kwa Muda mrefu bila matengenezo**

Uhakiki wa mali zilizozuiliwa katika mikoa ya Morogoro, Lindi, Tanga na Dar es Salaam unaonyesha kuwa magari 10, pikipiki moja, nyumba 7 na mashine moja ya boti zilizuiliwa zikisubiri hukumu ya mahakamani kwa muda kati ya mwaka mmoja mpaka miaka 7; na bado zingine ziko chini ya taasisi mbalimbali za uchunguzi kama vile Polisi, PCCB zikisubiri mchakato wa uchunguzi. Mali zimehifadhiwa kwa muda mrefu bila ukarabati na kusababisha kuchakaa. Kwa sababu ya hali iliyoelezwa hapo juu, serikali inaweza kuingia hasara na kushindwa kutambua malengo ya kurejesha mali katika thamani yake katika kutaifisha na uwenda ikapotea kabisa.

**f) Mali zilizotaifishwa hazikuchukuliwa kutokana na ukosefu wa maagizo ya kutaifishwa au Hukumu**

Kifungu namba 14 (1) cha Sheria ya Uhalifu kinasema kuwa “wakati Mwanasheria Mkuu anatumwa na mahakama kwa kutaifisha, chini ya kifungu cha 9 dhidi ya mtu anayehukumiwa na kosa na Mahakama ikaridhika kuwa, mali yake ni mali iliyotokana na kosa, mahakama inaweza iwapo itaona kuwa inafaa, kuagiza kuwa mali hiyo kama ilivyo kwenye agizo kutaifishwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano”

Wakati wa uhakiki wangu wa mali zilizotaifishwa katika Mkoa wa Tanga na Mbeya nimegundua kuwa, baadhi ya mali zilitaifishwa lakini Mwanasheria Mkuu wa Mkoa wa Tanga na Mbeya

*Ukaguzi wa Mifumo ya Udhibiti wa Ndani Na Utawala Bora*

wameshindwa kuzitaifisha kwa sababu hukumu au agizo la kutaifisha halijapatikana kutoka Mahakamani. Bila ya hukumu au agizo la kutaifisha, mali haiwezi kusajiliwa kwa jina la Msajili wa Hazina kama mali ya Serikali na mchakato wa kutaifisha hauwezi kufanyika.

Namshauri Mkurugenzi wa Mashtaka kufanya kazi na Taasisi zote zinazohusika kutengeneza, kutekeleza na kurasimisha sera na taratibu za udhibiti ili kuhakikisha utaratibu wa kutaifisha ni sahihi Vile vile zionyeshwe katika taarifa za fedha kwa wakati, na ionyeshe sera mahususi na taratibu sahihi za kihasibu kwa kanuni za mali zilizotaifishwa au kuwekewa pingamizi la kutaifishwa.

Ninashauri Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu, kuendelea kuimarisha utaratibu wa vyombo vyaya uchunguzi ili kuhakikisha kumbukumbu za mali zinazotaifishwa zinatunzwa vema kulingana na mabadiliko ya thamani ya mali hizo yatakavyotokea.

## SURA YA SABA

### 7.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

#### 7.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo muhimu yaliyotokana na ukaguzi wa rasilimali watu na mishahara katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/17 kama ifuatavyo:

#### 7.2 Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi Kutofanyika

Katika ukaguzi wangu wa rasilimali watu kwa mwaka huu wa fedha nilibaini yafuatayo:

Mikutano ya baraza la watumishi haikufanyika. Hii ni kinyume na Kanuni namba Q12 (a), (b), na (c) ya Kanuni za Kudumu Za Utumishi wa Umma 2009 ambayo inathibitisha lengo la mikutano ya baraza la watumishi ili kutoa mazingira mazuri ambayo yanaleta ushauri na mazungumzo kati ya Serikali na watumishi wa umma juu ya masuala yanayoathiri ufanisi na ustawi wa huduma za umma.

Kufanya mikutano ya baraza la watumishi mara kwa mara katika sehemu ya kazi huongeza sana jitihada za mawasiliano ambazo hupelekea watumishi kuwa na msingi wa kufanya kazi kwa pamoja. Mikutano ya watumishi inaruhusu watumishi kuwa sehemu ya mchakato wa kufanya maamuzi ya Taasisi kwa sababu watumishi wanaweza kuwasilisha maoni yao, mawazo yao, nk kwa njia inayokubalika kwa pamoja. Hii inaonesha utaratibu unaofaa na utawala bora.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Taasisi tatu (3) hazikufanya mikutano ya Baraza la Watumishi kwa mwaka uliopita kinyume na utaratibu ulioelezwa hapo juu wa utendaji mzuri na utawala bora..

**Jedwali Na. 43: Taasisi ambazo hazikufanya mikutano ya baraza  
la Watumishi**

S/N	Fungu	Taasisi
1	35	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka
2	55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
3	59	Tume ya Marekebisho ya Sheria

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016 / 17*

Ninapendekeza kwa Menejimenti kufuata kifungu namba Q12 (a), (b), na (c) cha Kanuni ya Kudumu ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 ili kuwapa watumishi fursa ya kutoa maoni yao kama njia ya utawala bora.

### 7.3 Mapungufu yaliyobainishwa kwenye usimamizi wa kumbukumbu za Mishahara

Kanuni ya 110 ya Kanuni ya Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004) inawataka Maafisa Masuuli kuhifadhi kumbukumbu sahihi za watumishi ndani ya mamlaka zao, na kuhakikisha usahihi na mabadiliko yanafanyika mara kwa mara katika taarifa zao. Tumbaini Taasisi nyingi bado hazijaboresha kumbukumbu za watumishi wake.

Pia, Kanuni ya 45 (1) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 toleo la tatu (III) inasema kuwa "mtumishi wa umma atastahili kuthibitishwa katika ofisi yake mara kipindi chake cha majaribio kitakapokoma kutokana na kuridhishwa na utendaji na ufanisi wake"

Katika ukaguzi wangu kwenye utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kwenye mfumo wa utunzaji wa taarifa za watumishi (HCMIS naLawson) niliofanya kwenye sampuli Taasisi saba (7), nilibaini kuwa kumbukumbu zinazohusiana na watumishi hazirekodiwi vizuri. Kwa mfano tarehe za kuzaliwa zisizo sahihi, watumishi waliohamishwa lakini taarifa zao bado hazijarekebishwa kwenye mfumo, uthibitisho wa baadhi ya watumishi hauonekani kwenye mfumo pamoja na kuwapo kwa watumishi wengine ambao wamestaafu lakini majina yao bado

yanaonekana kwenye malipo ya mishahara, kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 7.1:**

Taarifa zisizo sahihi za watumishi zinaweza kusababisha kulipa watumishi wasiokuwepo bila faida yoyote ya kiuchumi kwa Taasisi hiyo.

Ikilinganishwa na ripoti yangu iliyopita, kuna ongezeko la Taasisi kutoka sita hadi saba zilizo na mapungufu katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za watumishi licha ya kwamba Serikali tayari imeshafanya zoezi la kusafisha na kuboresha taarifa za watumishi katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za watumishi.

*Ninashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanaboresha mara kwa mara wa taarifa za watumishi katika mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za watumishi na kumbukumbu za watumishi zinatunzwa vizuri.*

#### **7.4 Kuchelewa Kutuma Makato ya Kisheria ya Mishahara Shilingi 8,156,136**

Vifungu 40 na 41 vya Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Umma, 1999 vinaelekeza kwamba kila mwajiri wa mwanachama wa mifuko ya hifadhi achangie mfuko kwa kwa kukata wanachama makato kutoka kwenye mshahara ghafi wa mwajiriwa kiasi cha asilimia tano na mwajiri kuchangia asilimia kumi na tano ya mshahara kwa kila mwezi.

Mifuko ya Hifadhi ya jamii na Bima ya Afya inawataka waajiri wote wakate na kuwasilisha makato kutoka kwa waajiriwa na kuwasilisha michango yao kila mwezi. Ucheleweshaji wa makato ya Kisheria husababisha faini kutoka kwa Taasisi husika.

Licha ya mapendekezo yangu katika ripoti za ukaguzi zilizopita nilizowashauri Maafisa Masuuli kuacha kuchelewesha kutuma makato ya kisheria, nimebaini tena, jumla ya kiasi cha Shilingi 8,156,136 zimechelewa kulipwa na Serikali kwa mifuko ya hifadhi ya jamii ambapo zilichelewa kwa muda wa siku 60 hadi 730

baada ya malipo ya mshahara wa kila mwezi kinyume na sheria ya Mfuko wa hifadhi ya jamii na bima ya afya.

**Jedwali Na. 44: Taasisi zilizochelewa kutuma makato ya kisheria.**

Na	Fungu	Taasisi	Mfuko	Kiasi(Sh.TZ)	Miezi iliyacheleleweshwa
1	37	Ofisi ya Waziri mkuu	PSPF	1,096,136	24
2	59	Tume ya Marekebisho ya Sheria	PSPF	7,060,000	02
<b>Jumla</b>				<b>8,156,136</b>	

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Matokeo yake Serikali ilitozwa adhabu ya kulipa jumla ya Shilingi 9,154,429.6 kama adhabu kwa kuchelewesha makato ya kisheria kwa mfuko wa kijamii wa PSPF.

Nilibaini kuwa, taasisi mbili hizo zilitozwa adhabu ya Shilingi 9,154,429.6 kwa kuchelewesha makato hayo kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini. Malipo kama haya ni hasara kwa walipa kodi.

**Jedwali Na. 45: Taasisi zilizopata adhabu kwa kuchelewa kupeleka makato**

Na	Fungu	Taasisi	Kiasi (Sh.TZ)
1	37	Ofisi ya Waziri mkuu	6,365,729.60
2	59	Tume ya Marekebisho ya Sheria	2,788,700.00
		<b>Jumla</b>	<b>9,154,429.6</b>

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Ninashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba ulipaji wa makato ya kisheria unafanywa kwa wakati. Hatua za kutosha zinapaswa kuzingatiwa ili kuepuwa hasara ya fedha za umma kutokana na adhabu zinazotolewa kwa kuchelewa kuwasilisha makato ya kisheria kwa vyombo husika.

**7.5 Malipo ya Mishahara kwa Watumishi ambao Hawapo kwenye Utumishi wa Umma Shilingi 31,296,376**

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa taasisi 4 zililipa kiasi cha Shilingi 31,296,376 kama mishahara kwa watumishi 10 walioacha

kazi, waliokufa, waliostaafu na waliofukuzwa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 7.4** hapo chini. Mishahara hii ililipwa kwa kipindi kati ya mwezi mmoja hadi miezi kumi na nne. Hii ni kinyume na Kanuni ya 113 ya kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) inayosema Maafisa Masuuli watunze nyaraka za watumishi ili watumishi wanaolipwa wawe ni wale waliokuwepo na kufanya kazi.

Kulipa mishahara kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa umma ni kupoteza fedha za umma au Serikali ishughulikie hali hiyo.


#### **Jedwali Na. 46: Malipo ya Watumishi ambao hawapo kazini.**

Na	Fungu	Taasisi	Idadi ya Watumishi	Kiasi (Sh. TZ)	Kiasi kilichorejeshwa (Sh. TZ)
1	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	2	5,222,017	1,851,000
2	83	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	1	1,296,000	0
3	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto.	6	11,478,359.38	0
4		Bonde la maji la Mto Kiabakari	1	13,300,000	0
		Jumla	10	31,296,376.38	1,851,000

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Mwenendo wa miaka mitatu (3) ya Mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao hawakuwa tena katika Utumishi wa Umma kama inavyooneshwani katika kielelezo hapa chini:

**Kielelezo Na. 20: Chati ya Mwenendo wa Malipo ya Mishahara  
Hewa**



*Chanzo: Taarifa za CAG za miaka mitatu.*

Mwenendo hapo juu unaonyesha kuwa kiwango cha mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao hawapo katika utumishi wa Umma imepungua mwaka huu kutoka Shilingi bilioni 1.4 mwaka jana hadi Shilingi milioni 31.3 mwaka huu wakati idadi ya Taasisi zinazohusika pia zimepungua kutoka 19 mwaka jana hadi 10 mwaka huu. Mwenendo huu unaonyesha kwamba, Serikali imeonyesha nia madhubuti ya kuondokana na malipo kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha watumishi ambao hawapo katika utumishi wa umma kama watumishi waliostaafu na walioacha kazi wanaondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kwa wakati.

Nawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba kiasi kilicholipwa kwa watumishi waliokuwa wamemaliza muda wao kinarejeshwa na watumishi husika kwa Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa kuongezea, nawashauri Maafisa Masuuli kuendelea kufuatilia na kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kuboresha taarifa za kumbukumbu za watumishi kupitia mfumo wa LAWSON na uboreshaji wa taarifa za watumishi kuwa zoezi endelevu kwa Wizara na Sekretarieti za Mikoa yote.

Kwa kuongezea, nawashauri Maafisa Masuuli kuwaondoa kwa wakati watumishi wote walioacha kazi katika taarifa za malipo ya mishahara ili kuepuka upotetu wa fedha za Serikali na kurejesha fedha zilizolipwa kwa watumishi ambao hawapo katika utumishi wa umma.

### **7.6 Kutokufanya Tathimini na Kupima Utendaji wa Watumishi**

Kanuni ya D.62 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa, Taasisi zote ziwe na mfumo wa wazi wa kutathimini utendaji wa mtumishi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni ya 22 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003.

Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 inasema kuwa, kila Taasisi katika utumishi wa umma iwe na mfumo wa wazi wa kutathmini utendaji wa watumishi wake wote. Lengo la kutathmini utendaji ni kubainisha, kupima na kuweka kumbukumbu za uwezo na mapungufu ya kila mtumishi ili kuweza kuchukua hatua za kuboresha ufanisi katika utumishi wa umma kama lengo endelevu.

Ukaguzi wangu kuhusiana na ufuutiliaji wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa taasisi tano za mfano nilibaini kuwa watumishi 74 hawakufanyiwa tathmini na kupima utendaji wao kwa kutumia mfumo wa wazi kama inavyotakiwa na Kanuni tajwa hapo juu. Muhtasari wake ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na 7.5 hapo chini.

**Jedwali Na. 47: Taasisi ambazo hazikufanya tathmini na kupima watumishi**

Na	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi
1	54	Sekretarieti ya mkoa -Njombe	03
2	89	Sekretarieti ya mkoa - Rukwa	32
3	71	Sekretarieti ya mkoa - Pwani	19
4	70	Sekretarieti ya mkoa - Arusha	07
5	84	Sekretarieti ya mkoa - Singida	13
<b>Jumla</b>			<b>74</b>

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Kushindwa kutathmini na kupima utendaji wa watumishi husababisha uongozi kushindwa kutambua mapungufu ya kiutendaji ya watumishi wake ili kutengeneza mikakati na namna bora ya kuyashungulikia. Mbali na hayo, ni vema kuwa na mfumo wa wazi wa kupima na kutathmini utendaji ambao utazingatia utendaji wa mtumishi katika kupanda vyeo, mafunzo na uhamisho.

Ikilinganishwa na ripoti yangu iliyopita, ushindwa kutathimini na kupima utendaji wa watumishi kumepungua kutoka watumishi 764 hadi watumishi 74; hii inaonyesha nia dhabiti ya Serikali katika kushughulikia suala hili.

*Nawashauri Maafisa Masuuli wapime na kutathimini utendaji wa watumishi kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 ili uimara na udhaifu uonekane na kutatuliwa.*

## **7.7 Watumishi Wanaokaimu kwa zaidi ya Miezi Sita**

Kanuni ya D.24(3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa, pale inapowezekana, watumishi wa umma wasikaimu kwenye nafasi kwa kipindi kinachozidi miezi sita. Mamlaka ya uteuzi ifanye mchakato wa uteuzi kwa nafasi iliyio wazi ndani ya kipindi cha miezi sita.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa watumishi 50 katika Taasisi 15 wanakaimu nafasi mbalimbali zaidi ya miezi sita bila kuthibitishwa au nafasi hizo kujazwa kinyume na kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma. Watumishi hao wamekaimu kwa kipindi cha kuanzia miezi 9 hadi 89 kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini:

**Jedwali Na. 48: Taasisi zenyе watumishi wanaokaimu zaidi ya miezi sita**

Na	Fungu	Taasisi	Idadi ya watumishi	Muda(miezi)
1	4	Idara ya usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu	1	30
2	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	3	24 hadi 84
3	58	Wizara ya Nishati na Madini	9	12 hadi 19
4	65	Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenyе ulemavu	3	29 hadi 31
5	96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	4	12 hadi 48
6	51	Wizara ya Mambo ya Ndani	3	32 hadi 89
7	63	Sekretarieti ya mkoa - Geita	3	19 hadi 51
8	87	Sekretarieti ya mkoa - Kagera	4	14 hadi 60
9	36	Sekretarieti ya mkoa - Katavi	2	12 hadi 16
10	82	Sekretarieti ya mkoa - Ruvuma	4	10 hadi 26
11	90	Sekretarieti ya mkoa - Songwe	2	18
12	76	Sekretarieti ya mkoa - Lindi	2	15 hadi 48
13	70	Sekretarieti ya mkoa - Arusha	3	10 hadi 54
14	84	Sekretarieti ya mkoa - Singida	3	09 hadi 29
15	79	Sekretarieti ya mkoa - Morogoro	4	21 hadi 64
		Jumla	50	

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Ikilinganishwa na ripoti yangu iliyopita, kuna ongezeko la watumishi wanaokaimu zaidi ya miezi sita kutoka watumishi 49 hadi 50 mwaka huu ambao wanaokaimu nafasi kwa zaidi ya miezi sita.

Kushindwa kuwathibitisha watumishi katika nafasi wanazokaimu kwa zaidi ya miezi sita kunaweza kuathiri uwezo wao juu ya ufanyaji maamuzi na kuwaondolea morali ya kazi hivyo kuathiri utendaji wao kazi.

Nawashauri Maafisa Masuuli wanaohusika kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, kuwathibitisha watumishi wanaokaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita.

Watumishi wanafanya kazi bila mikataba ya ajira

Nimebaini kuwa Tume ya Mipango ina watumishi wanne (4) kwenye nafasi za juu ambao walikuwa na mikataba ya ajira kwa muda wa miaka mitatu ambapo mikataba yao tayari imeisha muda wake kwa kipindi kati ya miezi nane na mwaka mmoja.

Licha ya mikataba yao kuisha muda wake, watumishi hao wameendelea kuituimikia Serikali bila mikataba yoyote halali kinyume na kanuni namba D.33 na D.34 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009. Menejimenti pia iliendelea kuwalipa mishahara kwa kutumia masharti ya mikataba uliyopita. Kwa kukosekana kwa mkataba halali unaoonesha vigezo na masharti inakuwa vigumu kwa mtumishi kuwajibishwa endapo atashindwa kutekeleza wajibu wake.

#### **Watumishi ambao hawajapandishwa madaraja**

Katika ukaguzi wangu wa juu ya kupandishwa madaraja watumishi katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu (Fungu 16), nilibaini kuwa watumishi 26 hawakuwa wamepandishwa madaraja kutoka kwenye cheo kimoja kwenda kingine kutokana na maelekezo ya Serikali, ingawa kulikuwa na pendekazo la kuwapandisha vyeo tangu mwaka wa fedha 2014/15. Hii ni kinyume na kanuni za Kudumu D51 (a-c) ya mwaka 2009. Hali hii inaleta athari kwa utendaji wa watumishi na inaweza kushusha morali ya watumishi.

Kutokana na matokeo ya ukaguzi wangu, kuendeleza na kubakiza watumishi kazini kunaweza kuwa na changamoto. Hivyo nahimiza Mafisa Masuuli kuja na mfumo madhubuti ambao utatoa motisha kwa watumishi na kuwapandisha watumishi madaraja kwa wakati.

Ninashauri Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhakikisha kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma zinafuatwa.

## 7.8 Stahili za Watumishi Ambazo Hazijalipwa kwa Muda Mrefu Shilingi 4,604,984,055

Ukaguzi wangu wa rasilimali watu katika taasisi mbili ulibaini kuwa stahili mbalimbali za watumishi kiasi cha Shilingi 4,604,984,055 hazikulipwa kwa kipindi cha kati ya mwaka mmoja hadi miaka mitatu kama inavyooneshwaa katika jedwali Na 7.7. Kuchelewesha kulipa stahili za watumishi kunaweza kusababisha kukosa motisha, hivyo kusababisha ufanisi mdogo katika kutoa huduma bora kwa Umma.

**Jedwali Na. 49: Taasisi ambazo stahili za watumishi hazijalipwa**

Na	Fungu	Taasisi	Kiasi(Sh TZ)	Muda(miaka)
1	39	Jeshi la kujenga Taifa(JKT)	3,827,120,499.17	zaidi ya mwaka 1
2	5	Tume ya Umwagiliaji maji	777,863,555.47	3.
<b>Jumla</b>			<b>4,604,984,054.64</b>	

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Kuchelewa kulipa madai ya watumishi kwa muda mrefu kunaweza kushusha motisha ya watumishi, hivyo kupelekea utendaji mdogo katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Ninashauri Maafisa Masuuli, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, wahakikishe kuwa stahiki za watumishi zinalipwa kwa wakati.

## 7.9 Upungufu wa Watumishi

Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi zina ikama iliyopitishwa ya idadi ya watumishi katika kila Taasisi. Nimebaini wakati wa ukaguzi kwamba, kutoka kwenye ikama nafasi nyingi katika Taasisi zina upungufu wa watumishi. Upungufu wa watumishi husababisha kuelemewa na kazi kwa watumishi wachache waliopo hivyo kuathiri kiwango cha huduma inayotolewa kwa jamii.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, kwa mara nyingine tena nilipitia muundo wa watumishi wa vyombo vyya Serikali na mahitaji ya watumishi, nilibaini tatizo kubwa la upungufu wa watumishi. Uchache wa watumishi unaweza kukwamisha kufikiwa kwa

malengo, kutokana na kukosekana kwa ujuzi, uwezo na utaalamu haitawezekana. Vile vile, mgawanyiko wa majukumu na mzunguko wa kazi kwa watumishi ambao ni lazima katika uthibiti mzuri wa ndani hautaweza kufanyika kwa ufanisi.

Katika ukaguzi wa sampuli ya Taasisi 48, nilibaini kuwa kuna upungufu wa watumishi 34,081 ukilinganishwa na mahitaji ya watumishi 54,937 kama inavyoonyeshwa katika Kiambatisho 7,2. Upungufu huu ni sawa na asilimia 62 ya mahitaji ya watumishi.

Upungufu wa watumishi unazuia ufanisi wa utoaji wa huduma wa Taasisi kwa umma. Serikali inahitaji kuongeza juhudzi zaidi ili kuboresha idadi ya watumishi kulingana na mahitaji ya sasa.

Ikilinganishwa na ripoti yangu ya mwaka uliopita, upungufu wa watumishi umeongezeka kutoka 11,892 katika Taasisi 38 hadi 34,081 katika Taasisi 52; hii inaonyesha kwamba bado kuna upungufu mkubwa katika Taasisi nyingi za Serekali.

Ninashauri Maafisa Masuuli, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuhakikisha Taasisi zenye mapungufu ya watumishi zinapatiwa watumishi.

### **7.10 Watumishi wa Umma Kupokea Mishahara Chini ya Kiwango Kinachokubalika Kisheria**

Katika kupitia malipo ya mishahara ya watumishi, nimegundua baadhi ya Taasisi zina watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika, kinyume na kifungu namba 3 cha Sheria ya kurejesha Madeni ya mwaka 1970 na Waraka wa Serikali wenye kumbukumbu namba C/CE.45/271/01/1/87 wa tarehe 19 mwezi wa tatu 2009 uliotolewa na Katibu mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora ukiwaelekeza Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa, makato yote ya mishahara ya watumishi kwaajili ya marejesho ya madeni katika mwezi yasizidi moja ya tatu ya mshahara wa mtumishi kwa mwezi.

Katika ukaguzi wa Taasisi kumi na mbili nimegundua kuwa, watumishi 278 wanapokea mishahara chini ya kiwango

kinachokubalika kisheria. Hali hiyo ya watumishi kupokea mishahara midogo kuliko wanavyotegemea inasababisha watumishi kukosa ari ya kufanya kazi, hivyo kushusha ufanisi. Hii huwafanya watumishi kutokuwa na uhakika na kipato chao kazini.

Taasisi zenyne watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango kilichokubalika kisheria ni kama zinavooneshwa kwenye Jedwali la hapo chini.

**Jedwali Na. 50: Taasisi zenyne watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango**

Na	Fungu	Taasisi	Idadi ya Watumishi
1	27	Msajili wa Vyama vya Siasa	2
2	33	Ofisi ya Rais- Sekretarieti ya Tume ya Maadili	12
3	47	Sekretarieti ya mkoa - Simiyu	21
4	53	Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.	21
5	54	Sekretarieti ya mkoa - Njombe	23
6	81	Sekretarieti ya mkoa - Mwanza	28
7	87	Sekretarieti ya mkoa - Kagera	24
8	96	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.	32
9	76	Sekretarieti ya mkoa - Lindi	28
10	86	Sekretarieti ya mkoa - Tanga	28
11	70	Sekretarieti ya Mkoa - Arusha	34
12	50	Wizara ya Fedha na Mipango	25
		<b>Jumla</b>	<b>278</b>

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti ya 2016/17*

Kama ilivyobainishwa kwenye ripoti yangu iliyopita, Taasisi nyingi bado hazifuati muongozo na taratibu. Idadi ya watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria imeongezeka kutoka watumishi 49 hadi kufikia 278, na idadi ya Taasisi pia imeongezeka kutoka Taasisi sita mpaka kufikia kumi na mbili mwaka huu.

Kwa hiyo, narudia mapendekezo yangu kwamba Maafisa Masuuli wanahitaji kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kuthibitisha mikopo yote ya watumishi kabla ya kutoa mkopo mwagine na

kuwasiliana na watoaji wa mikopo ili makato yasizidi moja ya tatu ya mshahara wa mtumishi kwa mwezi.

*Ninashauri Taasisi zote kufuata Kanuni na miongozo ya Serikali kwa kuchunguza na kuhakikisha mishahara na makato ya watumishi kabla ya kutoa mkopo kwa watumishi.*

## SURA YA NANE

### **8.0 UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE**

#### **Utangulizi**

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali 35, Mifuko Maalumu ya Fedha 17, Taasisi Nyingine za Serikali 38, na Mabonde ya maji 13. Sura hii inaonyesha masuala mahususi na musuala mtambuka yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Bunge, Bodi ya Ushauri ya Wizara na menejimenti za taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo.

#### **8.1 UKAGUZI WA WAKALA WA SERIKALI**

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Wakala za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

##### **8.1.1 Utegemezi wa Ruzuku ya Serikali**

Kifungu. Na. 12 (2) (a) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na 30 ya 1997, kinataka Wakala zote kufanya kazi zao kwa mujibu wa kanuni za biashara na kuhakikisha kuwa, mapato yao yanatosha kulipia matumizi ya Wakala husika. Kifungu Na. 12 (3) kinataka sehemu ya mapato ya Wakala kutumika ndani ya Wakala hizo na sehemu nyingine ipelekwe Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali.

Ifuatayo ni taarifa ya ukaguzi juu ya utegemezi wa Wakala kwa Serikali katika Ufadhilli wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida na bajeti ya Maendeleo:-

##### **8.1.2 Uwezo Mdogo wa Wakala kutekeleza Bajeti zao za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kutumia mapato yao ya ndani**

Uwezo wa Wakala za Serikali kutekeleza bajeti zao za matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kutumia vyanzo vyao vya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umepungua kwa kiasi cha asilimia 27 kulinganisha na mwaka uliopita 2015/2016.

Kwa mwaka 2015/2016 mapato ya ndani yalikuwa na uwezi wa kutekeleza bajeti ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa asilimia 45. Kwa mwaka 2016/2017 mapato ya ndani yana uwezo wa kutekeleza bajeti kwa asilimia 18 tu. Tazama Jedwali 8.0 hapo chini

**Jedwali Na. 51: Ulinganifu wa Bajeti kuu na makusanyo ya fedha kutumia vyanzo vya ndani**

Mwaka	Jumla Kuu ya Bajeti (Shilingi)	Mapato ya ndani (Shilingi)	Asilimia ya mapato ya ndani katika bajeti kuu
2016/2017	2,369,119,704,458 <sup>27</sup>	426,061,768,231	18
2015/2016	1,050,130,006,901	472,090,811,427	45

*Chanzo: Taarifa ya fedha za Wakala za mwaka 2016/2017*

Jedwali hapo juu linaonyesha kuwa kwa ujumla wake Wakala za Serikali haziwezi kujiendesha kwa kutumia mapato yao ya ndani kwa asilimia 82.

Mchanganuo wa kina wa ukusanyaji wa mapato ya Wakala za serikali, unaonyesha kuwa, ni Wakala 15 (45%) tu ambazo zina uwezo wa kutekeleza bajeti zao kwa asilimia 100 na zaidi kwa kutumia mapato ya ndani. Wakala nyingine 18 (55%) hazina uwezo wa kutekeleza bajeti zao kwa asilimia 100 kwa kutumia mapato ya ndani, hivyo kutegemea ufadhili wa Serikali kujiendesha.

Mchanganuo wa makusanyo ya mapato ya Wakala wa serikali na ulinganifu wa uwezo wa kufadhili bajeti zao za matumizi umeonyeshwa katika **kiambatisho 8.1**

Nazishauri menejimenti za Wakala 18 (55%) ambazo hazina uwezo wa kukusanya mapato ya ndani kujiendesha, kubuni vyanzo vinya mapato, kuendesha shughuli zao kwa kutumia

<sup>27</sup> Jumla ya Bajeti ya matumizi ya kawaida Shilingi 863,713,444,873

Jumla ya bajeti ya maendeleo Shilingi 1,505,406,259,577

Jumla Kuu ya bajeti Shilingi 2,369,119,704,450

mbinu za kisasa za kibiashara, pamoja na kupitia upya viwango vya tozo wanazotumia.

*Pia, nazishauri menejimenti kuhakikisha kuwa kiwango cha ziada cha mapato yao, kinawakilishwa katika mfuko mkuu wa fedha za serikali kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya 1997*

### 8.1.3 Ulinganifu wa fedha iliyoidhinishwa na fedha iliyotolewa na Serikali

#### 8.1.3.1 Fedha iliyoidhinishwa na serikali kwa matumizi ya kawaida haikutolewa Shilingi 266,580,795,590

Kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 nimebaini kuwa Serikali haikutoa kiasi cha Shilingi 266,580,795,590 (18%) ulinganisha na makisio ya Shilingi 863,713,444,873. Kwa mwaka huu, fedha ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa na Wakala wa serikali ni Shilingi 597,132,649,284 ulikinganisha na kiasi cha Shilingi 588,776,834,907 kilichopokelewa mwaka jana.

Upungufu wa fedha za matumizi ya kawaida zinazotolea na serikali kwenda kwa Wakala umeongezeka kwa asilimia 13 ukilinganisha na mwaka jana. Tazama jedwali 8.1 hapo chini

**Jedwali Na. 52: Ulinganifu wa Fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha iliyotolewa**

Mwaka wa Fedha	Jumla Kuu ya Makisio (shilingi)	Fedha iliyotolewa (Shilingi)	Fedha ambayo haijatolewa (Shilingi)	Asilimia ya fedha ambayo haijatolewa
2016/2017	863,713,444,873	597,132,649,284	(-266,580,795,590)	-18
2015/2016	617,624,835,456	588,776,834,907	(28,848,000,549)	-5

*Chanzo: Taarifa ya fedha za Wakala za mwaka 2016/2017*

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa shughuli za Wakala wa Serikali hazikufanikiwa kwa kiwango kinachokusudiwa kutokana na upungufu wa fedha shilingi 266,580,795,590 sawa na asilimia 18.

Mchanganuo wa fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha halisi zilizopokelewa na Wakala umeoneshwa kwenye **Kiambatisho 8.2**

Kwa kuzingatia Sheria ya Wakala wa Serikali, inazitaka Wakala zote za serikali kujiendesha kwa kutumia mapato yao ya ndani. Kulingana na upungufu huo wa Fedha zilitolewa na Serikali, nazishauri Wakala wote wa serikali kuboresha ukusanyaji wa mapato yao ya ndani ili waweze kujiendesha kulingana na sheria ya uanzishwaji wa Wakala.

#### **8.1.3.2 Fedha ya Maendeleo iliyoidhinishwa haikutolewa Shilingi 854,055,913,769**

Katika fedha za maendeleo, kiasi cha Shilingi 854,055,913,769 sawa na asilimia 57 ya bajeti ya maendeleo ya Wakala 33 zilizokaguliwa mwaka huu 2016/2017 hakikutolewa na Serikali. Kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha Shilingi 651,350,345,808 kilitolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo kulinganisha na bajeti ya maendeleo ya Shilingi 1,505,406,259,577 iliyoidhinishwa.

Hii inaashiria kwamba, Wakala wa serikali zimeshindwa kutekeleza shughuli zao za maendeleo kutokana na ukosekanaji wa fedha za maendeleo.

Mwaka wa fedha uliopita Serikali ilipeleka fedha za maendeleo Zaidi ya bajeti kwa kiasi cha Shilingi 389,985,894,370 (90%). Tazama jedwali la hapo chini

**Jedwali Na. 53: Ulinganifu wa Fedha za maendeleo ziliyoidhinishwa na fedha iliyotolewa**

Mwaka wa Fedha	Jumla Kuu ya Makisio (Shilingi)	Fedha iliyotolewa (Shilingi)	Fedha ambayo haijatolewa (Shilingi)	Asilimia ya fedha ambayo haijatolewa
2016/2017	1,505,406,259,577	651,350,345,808	-854,055,913,769	-57
2015/2016	432,505,171,445	822,491,065,815	389,985,894,370	90

*Chanzo: Taarifa ya fedha za Wakala za mwaka 2016/2017*

Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na fedha halisi zilizotolewa umeonyeshwa kwenye **Kiambatisho 8.2**

Nazishauri menejimenti za Wakala, kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani, ili waweze kutumia fedha hizo katika kufanya shughuli zao za maendeleo, kuliko kutegemea mgao toka serikali kuu.

#### **8.1.4 Ukusanyaji wa Mapato kutoka vyanzo vyatuhusu ndani umepungua kwa asilimia 10**

Katika ukaguzi wa ukusanyaji wa Maduhuli ya Wakala za serikali, nimebaini kuwa makusanyo ya mwaka 2016/2017 yamepungua kwa asilimia 10 ukilinganisha na makusanyo ya mwaka 2015/2016.

Kwa mwaka 2016/2017 kiasi cha shilling 426,061,768,231 kimekusanya na Wakala 33, ukilinganishwa na kiasi cha Shilingi 472,090,811,427 kilichokusanya mwaka 2015/2016, hivyo kuna anguko la Shilingi 46,029,043,197 katika ukusanyaji wa Maduhuli sawa na asilimia 10.

Mchanganuo unaoonesha makisio na ukusanyaji halisi wa maduhuli umeonyeshwa katika Jedwali 8.3 hapo chini

**Jedwali Na. 54: Ukusanyaji wa Maduhuli kutumia vyanzo vyatuhusu ndani**

Mwaka wa fedha	Makisio ya Maduhuli (Shilingi)	Makusanyo ya Maduhuli (Shilingi)	Kiasi (pungufu)/Zaidi kulinganisha na makisio	Asilimia ya makusanyo na ultiunganisho wa makaditio
2016/2017	465,832,080,527	426,061,768,231	-39,770,312,297	-9
2015/2016	456,839,140,654	472,090,811,427	15,251,670,773	3

*Chanzo: taarifa za fedha za Wakala kwa mwaka 2016/2017*

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kulikuwa na ukusanyaji uliozidi makisio kwa shilling 15,251,670,773 sawa na asilimia 3 kilinganishwa na makisio ya Shilingi 456,839,140,654.

Ukaguzi wa ukusanyaji wa Wakala mmoja mmoja umebainisha kuwa, Wakala 20 (59%) wamekusanya chini ya makisio yao kwa kiwango cha asilimia 2 mpaka 67. Wakala nyingine 13 (41%) zimefanikiwa kukusanya zaidi ya makisio yao kwa kiwango cha asilimia 0.14 mpaka 500. Tazama **Kiambatisho 8.3**

### 8.1.5 MAPUGUFU YALIYOONEKANA KWENYE UKAGUZI WA WAKALA

- i. Malipo zaidi yaliyotolewa kwa wakandarasi kutokana na marekebisho ya bei katika mikataba ya ujenzi wa barabara Shilingi 1,177,740,226

Mapitio ya masharti ya jumla ya mikataba ya ujenzi wa barabara nchini inayofanyika chini ya Wakala wa Barabara Tanzania, yilibaini kuwa Kifungu Na. 49.1 kinahitaji kiasi kinacholipwa kwa mkandarasi kurekebishesha kulinga na kuongezeko au kushuka kwa gharama za wafanyakazi, vifaa vya ujenzi, mitambo, malighafi na hali ya kiuchumi kwa kuzingatia kanuni iliyoelezwa katika kifungu hiki cha mkataba. Pia, Kifungu cha 49.4 kinaelekeza kutumia kanuni zilizoambatishwa katika Kiambatisho cha nyaraka za mkataba.

Katika ukaguzi wa mikataba ya ujenzi wa barabara nimebaini kuwa kiasi cha Shilingi 1,177,740,226 kimelipwa kimakosa kwa wakandarasi kutokanana mapugufu katika kutumia kanuni za ukokotozi wa kiasi cha malipo kinachotokana na mabadiriko ya bei kulingana na kifungu cha 49.1. Rejea jedwali 8.4 la hapo chini

**Jedwali Na. 55: Malipo ya ziada kutokana na madabiliko ya bei katika mikataba**

Na	Jina La Mkandarasi	Taarifa za Mkataba	Kiasi-Shilingi
1	Nyanza Roads Works Ltd	Mkataba TRD/HQ/1022/2013/14 wa marekebisho ya barabara ya Nyamuswa - Bunda - Kisorya - Nansio mpaka Bitumen (121.9 km) pamoja na marekebisho ya barabara ya Bulamba - Kisorya (51km)	225,924,562
2	Mbutu Bridge JV	Marekebisho ya barabara ya Makutano - Nata (50km)	951,815,664
<b>Jumla Kuu-shilingi</b>			<b>1,177,740,226</b>

*Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya Wakala wa Barabara Tanzania*

Mabadiliko ya bei ya vitu mbalimbali na matumizi ya kanuni katika kukokotoa malipo ya wakandarasi imesababisha malipo zaidi kwenda kwa wakandarasi. Kutokana na ushauri wangu kwa menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania katika miaka iliyopita, nimebaini kuwa kwa mwaka huu wa fedha, menejimenti hii imefanikiwa kuokoa na kurejesha kiasi cha shilingi Milioni 100 kutoka kwa Wakandarasi waliolipwa zaidi katika malipo yaliyopita kutoka na makosa ya kikanuni na mabadiliko ya bei.

Mikataba yote ya ujenzi wa barabara inahusisha Mshauri wa ujenzi. Moja ya kazi za Mshauri ni kuisaidia Wakala katika usimamizi wa ujenzi wa barabara pamoja na malipo ya madai ya Mkandarasi kulingana na kazi iliyofanyika. Pamoja na kuwapo kwa mshauri huyu katika mikataba yote ya Ujenzi, bado kuna malipo yasiyo sahihi ambayo yanalipwa kwenda kwa Mkandarasi.

Ninashauri Menejimenti ya Wakala wa barabara Tanzania, kuboresha mifumo yake ya ndani katika kukokotoa kiasi anachotakiwa kulipwa Mkandarasi. Pia, ninashauri utazamwe upya uwajibikaji wa Mshauri wa ujenzi, ili kumfanya awajibike kikamilifu katika kuhakikisha malipo anayolipwa Makandarasi ni sahihi kabla ya malipo kufanyika.

**ii. Malipo ya Posho ya Kukaimu yamefanyika kabla ya kuidhinishwa na Mamlaka Husika Shilingi 164,639,854**

Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, kifungu Na. D.19 (1) cha kanuni hii, kieleza kwa menejimenti kutafuta na kupata kibali cha awali kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi wa Umma (Uanzishwaji) kabla ya kuteua mtu katika nafasi ya iliyowazi. Pia, kanuni hii inabainisha kwamba mapendekezo ya uteuzi wa nafasi ya kukaimu ni lazima iwe imewasilishwa kwa Katibu Mkuu (Uanzishwaji) mara moja pale nafasi inapokuwa wazi.

Pia Kifungu Na. L.16 cha kanuni hizi za kudumu za Utumishi wa Umma, kinaelekeza kuwa Katibu Mkuu anao uwezo wa kuidhinishwa malipo ya kukaimu kwa mtumishi wa umma anayekaimu katika nafasi ambayo ina mshahara mkubwa.

Katika ukaguzi wa hesabu za Wakala wa serikali, nimebaini kuwa Wakala waliooneshwa katika Jedwali 8.5 hapo chini wamelipa kiasi cha shilingi 164,639,854 kwenda kwa watumishi waliokaimishwa nafasi mbalimbali bila kupata idhini ya Katibu Mkuu Kiongozi kama ilivyoelekezwa katika Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009.

#### **Jedwali Na. 56: Malipo ya fedha za kukaimu bila idhini**

Na	Jina La Wakala	Kiasi Shilingi.
1	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	25,409,854
2	Wakala wa Hifadhi ya chakula	139,230,000
	<b>Jumla Shilingi.</b>	<b>164,639,854</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Nashauri Wakala wa serikali kuhakikisha wanaendana na matakwa ya kanuni za kudumu za utumishi wa umma kwa kuomba kibali kutoka kwa Katibu Mkuu pindi nafasi za kazi zinapokuwa wazi ili kupata idhini ya kujizaja nafasi hizo.

#### **iii. Matumizi yasiyo na tija yaliyofanywa na Wakala wa Serikali kupitia adhabu ya kucheleva kulipa madeni kwa muda kiasi cha Shilingi 587,226,567**

Katika mwaka 2016/2017, nimebaini kuwa Wakala Serikali zimelipa fedha kwa matumizi ambayo Serikali haijanufaika na kitu. Malipo haya ni adhabu iliyotozwa kwa Wakala hizi kutokana na kuchelewesha malipo kwa Wakandarasai, pamoja na kucheleva kulipa marejesho ya mkopo. Taasisi hizo ni Wakala wa barabara nchini ambayo imelipa kiasi cha Shilingi 204,359,067, na Wakala wa Majengo ya Serikali kiasi cha shilingi 382,867,500 kama inavyoonyeshwa katika jedwali 8.6 hapo chini.

#### **Jedwali Na. 57: Malipo yasiyo na tija kwa Serikali Shilingi 587,226,56;**

Na	Maelezo ya Muamala	Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	Adhabu kwa kucheleva kumlipa Mkandarasi Milka Singh Jawala Sing	Wakala wa barabara nchini	14,045,595

Na	Maelezo ya Muamala	Taasisi	Kiasi (Shilingi)
2	Adhabu kwa kuchelewa kumlipa Mkandarasi Elerai Construction Co.	Wakala wa barabara nchini	39,226,425
3	Adhabu kwa kuchelewa kumlipa Mkandarasi Rocktronic Ltd	Wakala wa barabara nchini	55,972,462
4	Adhabu kwa kuchelewa kumlipa Mkandarasi Arusha Aggregates LTD	Wakala wa barabara nchini	10,342,981
5	Adhabu kwa kuchelewa kumlipa Mkandarasi Controlled Blasting and Construction Co. Ltd	Wakala wa barabara nchini	7,685,648
6	Interest paid to M/S Builders & Limeworks Ltd due to delay in settling approved IPC	Wakala wa barabara nchini	19,187,812
7	Adhabu kwa kuchelewa kumlipa Mkandarasi Luneco Investment Ltd	Wakala wa barabara nchini	57,898,144
8	Tozo kwa kuchelewa kulipa mkopo wa shirika la mafao la PSPF	Wakala wa Nyumba	382,867,500
<b>Jumla Shilingi</b>			<b>587,226,567</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Katika Ukaguzi wa utekelezaji wa Mikataba ya Ujenzi wa barabara, nimebaini kuwa kifungu Na. 46.1 cha masharti ya jumla, kinabainisha kuwa, Mwajiri anatakiwa kumlipa Mkandarasi kiasi kilichohakikiwa ndani ya siku 28. Endapo Mwajiri atachelewa kufanya malipo hayo kwa wakati, atalazimika kulipa tozo (adhabu) ambayo itakokotolewa kwa kuzingatia kiwango cha riba za mikopo ya kibiashara iliyopo sokoni kwa kipindi hicho.

Katika Ukaguzi wa Wakala wa Nyumba, nilibaini malipo yasiyo na tija kwa serikali ya Shilingi 382,867,500 yaliyotokana na Mkopo kutoka Mfuko wa Mafao ya Kustaafo wa shilingi 3,500,000,000 wenye riba ya asilimia 15. Mpaka ninafanya ukaguzi, Wakala wa Nyumba alikuwa amebakiza shilingi 2,552,450,000; hivyo kwa kuchelewa kufanya malipo ya mkopo huu, imelazimika kulipa tozo ya Shilingi 382,867,500.

Kwa maoni yangu, tozo hizi zisingekuwepo kama Serikali ingekuwa inafanya malipo yake kwa wakati. Na kiasi hiki cha shilingi 587,226,567 kilicholipwa kingeweza kutumika kutekeleza shughuli nyingine za maendeleo.

Nashauri menejimenti za Wakala za Serikali kufanya malipo yao kwa Wazabuni na Wakandarasi kwa muda sahihi ili kuепusha adhabu kama hizi.

**iv. Kutokukata Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi 81,894,582 na ucheleweshaji wa kuwasilisha makato ya kisheria ya shilingi 97,749,131**

Sheria ya Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma Na. 2 ya 1999, inawataka Watumishi wa Umma na Waajiri wao kuchangia katika Mfuko wa Pensheni kila mwisho wa mwezi. Makato haya yanatakiwa kuwasilishwa kwenye Mfuko ndani ya siku 30 baada ya kulipa mshahara wa mwezi. Mwajiri anawajibika kuwasilisha makato haya kwenye mfuko kwa wakati mwafaka kama inavyoelekezwa katika sheria hii.

Kifungu Na. 20 (1) na (2) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Na. 9 ya 2004 kiawataka waajiriwa wote kushirikiana na waajiri wao kukata makato ya mikopo yao ya elimu ya juu na kuwasilisha katika Bodi ya Mikopo. Mwajiri atakata makato hayo ya mikopo kutoka katika mishahara ya Waajiriwa na kuyawasilisha ndani ya siku 15 baada ya mwisho wa mwezi.

Katika ukaguzi wa mwaka 2016/2017, nimebaini kuwa Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo hakukata marejesho yenyе jumla ya shilingi 81,894,582 ya mikopo ya bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, na hivyo kushindwa kuwasilisha katika bodi hii ya mikopo. Pia, nimebaini kuwa Wakala wa Maabara za Serikali amechelewesha kuwasilisha makato ya kisheria katika mifuko mbalimbali ya pensheni yenyе jumla ya shilingi 97,749,131. Tazama jedwali 8.7 hapo chini

**Jedwali Na. 58: Mapungufu katika kukata makato ya kisheria na uwasilishwaji wake**

Na.	Jina la Taasisi	Maelezo	Kiasi (Shilingi)
1	Wakala wa Maabara za Serikali	Ucheleweshwaji wa kuwasilisha makato ya kisheria	97,749,131

Na.	Jina la Taasisi	Maelezo	Kiasi (Shilingi)
2	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo	Kutokukatwa kwa marejesho ya mikopo ya wanafunzi	81,894,582
<b>Jumla</b>			<b>179,643,713</b>

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Mikopo ya wanafuzi wa elimu ya juu ni mfuko unaojiendesha kwa kutegemea marejesho ya mikopo. Hivyo ili wanafunzi wengi waendelee kupata mikopo wale waliohitimu wanatikiwa kurejesha mikopo waliochukua.

Ninashauri menejimenti za Wakala kuwatambua watumishi wote waliosoma elimu ya juu kwa kutumia mikopo ya bodi hii na kuwakata katika mishahara yao kama inavyoilekezwa katika sheria ya mikopo ya elimu ya juu.

Kuhusu ucheleweshwaji wa kuwasilisha makato ya kisheria katika mifuko ya pensheni, naishauri menejimenti kutekeleza sheria ya mifuko ya mafao kwa watumishi wa umma kwa kuwasilisha makato yote ndani ya siku 30 baada ya mwisho wa mwezi ili kuepuka adhabu itokanayo na ucheleweshwaji.

## 8.2 UKAGUZI WA TAASISI NYINGINE ZA SERIKALI

### 8.2.1 Ukaguzi wa miradi, uzalishaji mali na uwekezaji unaofanywa na kampuni za Majeshi ya Ulinzi

#### Utangulizi

Katika ukaguzi wa mwaka 2016/2017, nimekagua shughuli za uzalishaji mali na uwekezaji zinazofanywa na SUMA-mradi wa matrekta, SUMA-kampuni ya Ulinzi na SUMA-kampuni ya Ujenzi. Pia nimekagua kampuni ya uzalishajimali ya jeshi la Magereza, na Shirika la Nyumbu.

Yafuatayo ni matokeo ya Ukaguzi wa mashirika haya yanayoendeshwa na majeshi;

### 8.2.2 Makoteo ya Ukaguzi wa shughuli za SUMA JKT.

SUMA JKT ni taasisi ya kujitegemea iliyoanzishwa kisheria chini ya Sheria ya Uwezeshaji (Sura ya 23) ya 1974 (Sura ya 119 Iliyorejewa 2009) kwa amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1982. Kampuni hii inajihuisha na uwekezaji na uendeshaji wa miradi katika maeneo ya uhandisi na ujenzi, kilimo na ufugaji, huduma za usalama, utengenezaji wa samani na uuzaji wa matrekta na vifaa vya kilimo.

- i. **Mikataba ya ubia isiyo na tija baina ya SUMA JKT na Wabia wengine**

Sheria ya uanzishwaji wa SUMA unalitaka shirika hili kujihusisha na shughuli za uzalishaji mali, ujenzi, kilimo, viwanda na nyinginezo. Kutokana na ghamama na teknolojia kuwa kubwa, SUMA imejikuta ikilazimika kuingia ubia na mashirika mengine ili kuwezesha kufanikisha shughuli zake. Nimekagua kuangalia ufanisi wa mikataba ya ubia na kugundua mapungufu yafuatayo, tazama jedwali 8.8 hapo chini;

#### Jedwali Na. 59: Mapungufu katika Makubaliano ya Ubia

Makubaliano ya	Aina ya biashara	Umiliki	Hali ya sasa ya
----------------	------------------	---------	-----------------

Ubia		SUMA	Mbia	utekelezaji wa Ubia
<b>SUMA JKT na Cami Textile Tanzania Ltd kutoka China Jina la kampuni ni Cami-SUMA Garments IlianZHISHWA 5 Julai, 2006</b>	Utengenezaji wa Nguo wa ajili ya soko la ndani ya Nchi, Afrika na dunia kwa ujumla	39%	61%	Kiwanda kilijengwa Mgulani, kwa sasa kimefungwa. Baada ya kujunjika wa ubia kiwanda kinamilikiwa na SUMA JKT kwa asilimia 100. Kwa sasa hakuna uzalishaji unaoendelea katika kiwanda hiki.
<b>SUMA JKT na CHENGGONG (CG) (T) Ltd IlianZHISHWA 26 Agosti, 2015</b>	Kukodisha na kuuza mitambo ya ujenzi.	80%	20%	Mkataba haukufanyika kwa sababu ya matatizo ya kupata Barua ya Mikopo kwa ajili ya kuagizaji Mitambo
<b>SUMA JKT na Equator Automech Company Ltd</b>	Kutengeneza magari makubwa, malori, Mabasi, Mashine za kilimo, magari ya kuzima moto, na vipuri vya mitambo	30%	70%	Mkataba haujakelezeka na kwa sasa wabia wameridhiana kwa pamoja kuvunja ubia.

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Katika ukaguzi huu, nimebaini kuwa katika makubaliano yote ya ubia hapo juu, hakuna taarifa yoyote ya faida, mapato au gawio iliyopatikana kwa SUMA JKT kutokana na ubia hizo.

Hii inaashiria kuwa SUMA JKT imewekeza mali zake katika ubia ambao hauna faida kwa maendeleo ya SUMA.

Kwa kuwa kwa sasa Tanzania inatekeleza sera za viwanda, naishauri menejimenti ya SUMA kuunga mkono sera hii kwa kuvifungua viwanda vyote vilivyofungwa na kuanza uzalishaji, na

kujihusisha katika mikataba ya ubia yenyе kuleta tija na uzalishaji.

**ii. Mashine mpya za kusaga nafaka zilizogharimu Shilingi 147,135,000 zimetelekezwa na SUMA**

SUMA JKT Ruvu ilichukua mkopo wa Shilingi 147,135,000 kutoka SUMA Makao Makuu kwa ajili ya kununua mashine za kusagia nafaka. Mashine hizi zimetengezwa na shirika jingine ya kijeshi liitwalo Mzinga mnamo mwaka 2014. Katika kutembelea mradi huu, nimebaini kuwa tangu mashine hizi zichukuliwe mwaka 2014, hazijafanya kazi iliyokusudiwa kwa kipindi cha miaka minne.

Lengo la mashine hii ilikuwa ni kusaga na kukboa nafaka kwa ajili ya matumizi ya jeshi na kwa ajili ya malengo ya kibashara. Nilifahamishwa na menejimenti kuwa mashine hizi hazifanyi kazi kutokana na ukosekanaji wa malighafi ya kusaga na kukboa ya kutosha kuendesha mashine hizo.

Naishauri menejimenti ya SUMA, kuboresha kilimo cha mahindi na nafaka kwa ujumla katika mashamba yake, kwa kutumia kilimo cha kisasa na cha umwagiliaji, ili kuweza kupata malighafi ya kutosha kuweza kuendesha mashine hizo.

**iii. Utunzaji mbovu wa Matreka na vifaa vya kilimo vilivyo igharimu SUMA shilingi 772.454,445**

SUMA Chita ilichukua mkopo wa matreka 14 kutoka SUMA Matrekta kwa ghamama ya shilingi 772,454,445 mnamo mwaka 2011. Wakati wa ukaguzi nilitembea SUMA Chita na kubaini kuwa ni matreka matatu tu yanayofanya kazi, mengine kumi na moja (11) yametelekezwa na kuachwa yakiharibika kwa uchakavu wa kukosa matengenezo.

Katika mkopo huo, SUMA Chita wameshalipa kiasi cha shilingi 10,000,000 kwa SUMA matreka; na bakaa ya mkopo kwa sasa ni shilingi 762,454,445 ambayo haijarudishwa kwa kipindi cha miaka sita.

Licha ya kuwa na matreka matatu yanafanya kazi, nilibaini kuwa SUMA Chita imempa mkataba wa shilingi 114,410,000 Bw.

Michael David Lukindo kwa ajili ya kukodisha matreka kwa ajili ya kulima mashamba ya mpunga ya SUMA. Katika hili, SUMA ilitakiwa kutumia matreka yake kulima mashamba hayo na sio kukodisha Matreka kwa Mtu binafsi wakati Matreka ya Kampuni hayatumiki.

Naishauri menejimenti ya SUMA CHITA;(i) Kukarabati matrekta 11 kwa ajili ya shughuli zake za kilimo (ii) Kutumia rasiliamali (watu na mitambo) zake kuendesha shughuli za kilimo; na (iii) Kuacha kukodisha watu katika shughuli ambazo zipo ndani ya uwezo wa shirika.

**iv. Vifaa vya umwagiliaji vilivyoharibika na visivyouzika vyenye thamani ya Shilingi 2,912,368,000**

Mnamo tarehe 27.08.2009 SUMA JKT iliingia makubaliano na Kampuni ya Escort Limited ya India wa ajili ya kununua matrekta, pampu za umwagiliaji na vifaa vingine vya kilimo kwa gharama ya Dola za Kimarekani 40,000,000.

Katika mkataba huu pampu za umwagiliaji 1,100 pamoja na vifaa vyake viliingizwa nchini. Mpaka kipindi cha ukaguzi Novemba 2017, ni mashine 147 sawa na asilimia 13 zilikuwa zimeshauzwa na kubaki mashine 953 sawa na silimia 87 ambazo hazijauzwa.

Nilitaarifiwa na menejimenti ya SUMA kuwa pampu hizi zilikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuvuta maji. Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa, sababu ya kutokuuza mashine hizi za umwagiliaji ni na kuagiza vifaa vya kilimo bila ya kufanya upembuzi yakinifu kuanzia sokoni, pamoja na kutojua mahitaji halisi soko.

Naishauri menejimenti ya SUMA matrekta kufanya upembuzi yakinifu kuhusu uhitaji sahihi ya vifaa kabla ya kuagiza kabla ya kuingiza vifaa vya kilimo na umwagiliaji,. Pia, naishauri menejiment hii kuangalia uwezekano wa kuboresha pumpu hizo kwa matumizi mengine ya kilimo.

**v. Kutorejeshwa kwa Mikopo ya matrekta kwenda kwa wakulima yenye thamani ya shilingi 40,047,937,000.**

Katika ukaguzi wangu nimebaini kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 mpaka 2016, SUMA matrekta imetoa mikopo ya matrekta na vifaa mbalimbali vya kilimo kwa njia ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 40 kwenda kwa wakulima tofauti kama inavyooneshwaa katika jedwali 8.9 hapo chini.

**Jedwali Na. 60: Mauzo ya Matrekta na vifaa vyake vya kilimo kwa mkopo**

Maelezo	Idadi ya trekta	Mwaka wa mauzi	Kiasi-Shilingi
<b>Mauzi ya trekta na vifaa vingine vya kilimo kwa njia ya mkopo</b>	1,846	2011	36,293,029,000
	268	2013	1,690,084,000
	108	2015	1,663,664,000
	80	2016	401,160,000
	<b>2,302</b>		<b>40,047,937,000</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti.*

Jumla ya madai ya SUMA matrekta ni shilingi bilioni 41; kati ya kiasi hiki, kiasi kinachotokana na madai ya kukopesha matrekta ni shilingi bilioni 40 sawa na asilimia 97 ya madai yote yasiyokusanya. Kiasi hiki kikubwa cha fedha za SUMA kimekuwa nje kwa kipindi cha saba bila kukusanya.

Naishauri menejimenti ya SUMA kutumia dhamana zilizowekwa na wakopaji wakati wa kukopa ili kuhakikisha inakusanya madai yake yote ya shilingi bilioni 40 yaliyotokana na mikopo ya Matrekta.

### 8.2.3 Ukaguzi wa Miradi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi wa Magereza

Shirika la uzalishaji mali la Magereza ni taasisi ya kujitegemea ilioanzishwa kisheria chini ya Sheria ya Uvezeshaji (Sura 23) ya 1974 (Sura ya 119 Iliyorejewa 2009) kwa amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1982. Katika ukaguzi wa shirika hili la Magereza, nilibaini mapungufu yafuatayo.

#### i. Mradi wa Mashine za kushonea nguo umetelekezwa

Katika ukaguzi wa shughuli za uzalishaji mali za shirika la Magereza, nilibaini kuwa shirika hili linamiliki mashine za kisasa 70 za kushonea nguo lakini mashine hizi za kushana nguo

hazifanyi uzalishaji. Mashine hizi zilipokelewa mjini Arusha mwaka 2015. Mpaka sasa, hakuna uzalishaji uliofanyika katika kiwanda hiki.

Kiwanda hiki kina uwezo wa kushona sare za Wafungwa, Polisi wa Magereza, Jeshi na mahitaji mengine. Nilitaarifiwa na menejimenti ya mradi huu wa kushona nguo kuwa sababu kubwa ya kutokuanza kazi kwa kiwanda hiki ni ukosefu wa fedha za kuajiri na kununua malighafi za kushonea.

Naishauri menejimenti ya Shirika la uzalishaji la Magereza kutafuta fedha kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda hiki.

#### **8.2.4 Masuala mengine yaliojitokeza katika ukaguzi wa Wakala wa Serikali**

##### **i. Ukaguzi wa Wakala wa Umeme Vijijini**

Katika ukaguzi wa Wakala wa umeme vijijini, nilikagua Mikataba na miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya umeme inayotekelvezwa na Wakala. Katika ukaguzi huu nilitembelea utekelezaji wa Mradi wa uenezaji wa umeme, ujenzi wa umeme mkubwa pamoja na Mpango wa Umeme Vijijini. Ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini kama inavyoonekana katika jedwali 8.10 hapo chini;

**Jedwali Na. 61: Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi ya umeme vijijini**

Na.	Taarifa ya Mkataba	Bei Ya Mkataba	Hali ya Utekelezaji wa Mradi
1	Utekelezaji wa Mradi wa Mkataba Na.AE/008/2014-15/HQ/G/8 wa Ujenzi wa njia ya umeme ya 33KV, ujenzi wa kituo kidogo cha uzalishaji umeme mdogo wa 33, na ujenzi wa njia za umeme mdogo kwa ajili ya kuunganisha wateja katika mkoa wa Iringa	Dola za Marekani 3,432,199 Na Shilingi 2,066,092,059	Mpaka kipindi cha ukaguzi mwezi wa Oktoba 2017 utekelezaji ulikuwa ni wa asilimia 31. kulingana na mpango kazi, mradi huu ulikuwa umecheleweshwa kwa Mwezi Moja.
2	Ukaguzi wa utekelezaji wa	Dola za Marekani	Mradi haujetekelzeza

Na.	Taarifa ya Mkataba	Bei Ya Mkataba	Hali ya Utekelezaji wa Mradi
	Mkataba Na.AE/008/2015-16/HQ/G/39 wa Ugavi na Ujenzi wa Mtandao wa Usambazaji wa umeme mdogo na Uunganishaji wa Watumiaji umeme- Fung la 2-Mkoa wa Iringa (Mradi wa Densification)	1,098,869.81 Na Shilingi 1,222,702,562.74	kwa asilimia 97.3 na hakuna hatua iliyochu kuliwa na menejimenti ya Wakala kuhakikisha mkataba unatekelezwa kwa wakati
3	Ukaguzi wa utekelezaji wa Mkataba Na.AE/008/2015-16/HQ/G/39 wa Ugavi na Ujenzi wa Mitandao ya Usambazaji wa miundombinu ya umeme mdogo na uunganishaji wa watumiaji- Fungu la 1 mikoa ya Mbeya na Songwe (Mradi wa Densification)	Dola za Marekani 9,138,022.59 na Shilingi 580,827,471.10	Maendeleo ya jumla ya mradi huu wakati wa ziara ilikuwa ni asilimia 39. Kazi kubwa iliyofanywa ni kusimamisha nguzo tayari kwa ajili ya kuvuta waya za umeme.
4	Ukaguzi wa mradi wa Mkataba Na.AE/008/2015-16/HQ/G/39 Fungu Na 6 Mkoa wa Mara	Dola za Kimarekani 3,347,620.78 Na Shilingi 1,498,345,852	Muda uliobaki kumaliza utekelezaji wa mradi ni miezi 5. Nimebaini kuwa sehemu kubwa ya mkataba hajatekelezwa kabisa katika wilaya za Tarime, Bunda, Seregenti, Ranya pamoja na Msoma. Mkataba hajatekelezwa kwa asilimia 90.

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Kutokana na ukaguzi wa miradi hiyo, nimebaini kwa kuna ucheleweshwaji wa utekelezaji wa Mradi. Ninaishauri menejimenti ya Wakala wa Umeme vijijini kuimalisha usimamizi wa Miradi ili kuwezesha miradi hiyo kukamilika kwa muda muafaka ili ipatikane thamani ya fedha ya serikali.

- ii. Malipo yaliyofanywa na taasisi za serikali bila ya kuwepo kwa Mikataba ya Makubaliano ya kazi TZS 698,654,826

Katika ukaguzi wa mwaka 2016/2017, nilibaini kuwa kuna taasisi za serikali zilitozo toa mikopo pamoja na kufanya manunuzi bila ya kuwa na mikataba ya makubaliano. Ni muhimu kuwa na mikataba ya kisheria kabla ya kufanya miamala yoyote ya kifedha baina ya Serikali watu wengine hii itasaidia kupata haki ya kisheria kipindi ambapo mgogoro utatokea.

Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa kiasi cha shilingi 698,654,826 kililipwa bila ya kusainiwa kwa mikataba ya makubaliano. Tazama jedwali 8.11 hapo chini.

**Jedwali Na. 62: Malipo yaliyofanywa bila ya kuwepo kwa mikataba**

Na	Jina la taasisi	Kiasi -Shilingi
1	Mamlaka ya vitamblisho vya taifa	23,952,375
2	SUMA-JKT Agri-Machinery	145,484,800
3	Mzinga Corporation	529,217,651
	<b>Jumla Shilingi</b>	<b>698,654,826</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

*Ninazishauri menjimenti za taasisi za serikali kuwa na mikataba ya makubaliano kabla ya kufanya manunuzi au kutoa mikopo ya aina yoyote ile. Pia, nawashauri wanasheria wa taasisi hizi kuzishauri menejiment zao namna ya kuboresha mikataba.*

### 8.3 UKAGUZI WA MABONDE YA MAJI

Bodi za Mabonde ya Maji zilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Maji Na. 42 ya 1974 na marekebisho yake ya baadaye sheria hii imechukuliwa na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Na. 11 ya 2009.

Katika ukaguzi huu, nimekagua Bodi a Mabonde ya maji 13, na matokeo ya Ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:

- i. **Fedha pungufu zilizotolewa katika kutekeleza mpango wa maendeleo sekta ya maji TZS 42,889,557,718**

Bodi za Mabonde ya Maji zinapokea fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo kuitia mradi wa Maendeleo sekta ya Maji. Nimepitia utoaji wa fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kubaini upungufu wa kiasi cha shilingi 42,889,557,718 (87%) kutoka katika bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi 49,472,627,301.

Kwa ujumla, Mabonde haya yalipokea jumla ya shilingi 6,583,069,583 sawa na asilimia 13 ya bajeti nzima ya Maendeleo. Utoaji pungufu wa fedha umeathiri utendaji wa bodi za Mabonde. Tazama Jedwali 8.12 hapo chini

**Jedwali Na. 63: Utolewaji pungufu wa fedha**

Jina la Taasisi	Masikio (Shilingi)	Fedha zilizopokelewa (Shilingi)	Fedha ambazo hazijatolewa (TZS)	%
Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Handeni	2,000,000,000	0	2,000,000,000	100
Bondi ya Bonde la Maji Ziwa Rukwa	3,820,453,671	770,616,700	3,049,836,971	80
Bodi ya Bonde la maji ziwa Victoria	3,118,500,000	118,661,480	2,999,838,520	96
Bodi ya Bonde la maji ziwa Nyasa	2,200,000,000	448,875,157	1,751,124,843	80
Mamlaka ya maji safi bonde la Makonde	951,225,662	101,000,000	850,225,662	89
Mamlaka ya maji safi Mugango-kiabakari	331,475,290	172,154,608	159,320,683	48
Bodi ya Bonde la maji Pangani	5,065,000,000	1,053,999,277	4,011,000,723	79
Bodi ya Bonde la maji Rufiji	6,173,001,800	432,285,399	5,740,716,401	93
Bodi ya Bonde la maji Ruvu	2,065,140,000	275,080,000	1,790,060,000	87
Mamlaka ya Maji Wanging'ombe	2,000,000,000	874,649,000	1,125,351,000	56
Bodi ya Bonde la Maji Pwani ya kusini Ruvuma	4,707,238,866	1,381,963,942	3,325,274,924	71
Bodi ya Maji ya Bonde la Ndani	17,040,592,012	953,784,020	16,086,807,992	94
Jumal	49,472,627,301	6,583,069,583	42,889,557,718	87

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka 2016/2017*

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa Bodi hizi za Mabonde ya Maji zinahitaji fedha kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa jamii. Naishauri Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kutoa fedha za uendeshaji wa Bodi hizi za Maji kama ilivyoidhinishwa katika bajeti zao.

**ii. Fedha za Mradi wa Maendeleo ya Maji (WSDP) zilizokopeshwa Wizara ya Maji Hazijarudishwa TZS 110,702,495**

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha za Bodi za Mabonde ya Maji, nimebaini kuwa kati ya Bodi hizi 13, kuna Bodi 5 (38%) zimeikopesha Wizara ya Maji na Umwagiliaji kiasi cha Shilingi 110,702,495, na mpaka mwisho wa mwaka 2016/2017 fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa na Wizara hiyo. Katika makubaliano baina ya Wizara na Bodi hizo ni kuwa Wizara ingerejesha fedha hizo kipindi Wizara itakapopata fedha za kujiendesha kutoka Hazina. Tazama jedwali 8.13 hapo chini

**Jedwali Na. 64: Mkopo kwenda Wizara ya Maji**

Na.	Jina la bonde la Maji	Kiasi -shilingi
1	Bodi ya Bonde la Maji Rukwa	16,328,495
2	Bodi ya Bondi la Maji Ziwa Nyasa	2,159,000
3	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji	45,150,000
4	Bodi ya Bondi la Maji Ziwa Tanganyika	21,000,000
5	Bodi ya Maji ya Bonde la Ndani	26,065,000
	<b>Jumla (Shilingi)</b>	<b>110,702,495</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Jedwali la hapo juu, linamaanisha kuwa kuna baadhi ya shughuli za Bodi za Mabonde ya Maji hazikuweza kutekelezeka kwa sababu ya kuhamisha fedha kuzipeleka Wizara ya Maji.

Naishauri Wizara ya Maji na Umwagiliaji kurejesha fedha zote ilizokopeshwa na Bodi za Bonde la Maji ili zitumike katika maendeleo ya Bodi hizi.

**iii. Kiasi cha Shilingi 251,437,021 kutoka Mradi wa Maendeleo Sekta ya Maji (WSDP) kama kodi ya ongezeko ya thamani (VAT) haijarejeshwa na Mamlaka ya Mapato**

Kulingana na Mkataba wa Maelewano (MOU) baina ya Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) kwa kutumia Mipango ya Utekelezaji wa Kawaida, Serikali ya Tanzania imekubali kutoa kodi zote katika matumizi yote sahihi yatokanayo na ununuzi wa bidhaa, kazi na huduma zilizofadhiliwa chini ya mradi wa Maendeleo sekta Maji ya (WSDP).

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Bodi ya Bonde la Maji 3 zililipa jumla ya Shilingi 251,437,021 kama kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wakati wa manunuzi yao ya bidhaa.

Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa menejimenti hizi za Bodi ya Bonde la Maji hazijachukua hatua za kudai kurejeshewa fedha hizi na Mamlaka ya Mapato (TRA). Tazama jedwali 8.14 hapo chini

**Jedwali Na. 65: fedha zilizolipwa kama VAT hazijarudishwa**

Na	Jina la Bodi ya Bonde la Maji	Kiasi(Shilingi)
1	Mamlaka ya Maji Wanging'ombe	95,370,036
2	Mamlaka ya maji safi bonde la Makonde	2,409,622
3	Bodi ya Bonde la Maji Pwani ya kusini Ruvuma	153,657,363
	<b>Jumla Shilingi</b>	<b>251,437,021</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Ninazishauri menejimenti za Mabonde ya Maji kuzingatia Mkataba wa Makubaliano (MoU) kati ya Serikali na Mafadhili wa Mradi wa WSDP kwa kufuata taratibu za kurudishiwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) iliyolipwa kwa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Pia, ninaishauri Mamlaka ya Mapato TRA kufuata Makubaliano (MOU) hayo hayo kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo na kurejesha kodi zote zilizolipwa na taasisi za serikali wakati zimepewa msamaha wa kodi.

**iv. Uchepushaji wa fedha zilizotegwa kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa ya maji TZS.333,790,806**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilipanga kutumia kiasi chs Shilingi 500,000,000 kwa ajili ya kukarabati mabwawa manne ya Hodo- shinyanga, Nkiniziwa-Nzega, Enguikment II-Monduli na Lemino-Monduli. Wakati wa ukaguzi wa fedha hizi nilibaini kuwa Shilingi 333,790,806 zilichepushwa na kupelekwa katika shughuli ambayo iko njeya ukarabati wa mabwawa yaliotajwa hapo juu. Fedha hizi zilipelekwa kufanya tathimini ya ardhi kwa ajili ya kulipa fidia kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Farkwa katika Wilaya ya Chemba. Nilitaarifiwa kuwa maamuzi ya kuhamisha fedha hizi ulitoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji

Pia, nilibaini kuwa ujenzi wa bwawa hili la Farkwa bado haujaanza. Sehemu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu ulianza Mnamo Septemba 2012 kwa kufanya upembuzi yakinifu na tathimini ya athari kwa Mazingira na kwa kijamii.

Sehemu nyingine ya utekelezaji wa mradi huu ni kujua makadirio ya fidia itakayopaswa kulipwa kwa ajili ya kuwahamisha wananchi katika maeneo yao. Kwa mujibu wa utafiti wa awali, jumla ya Shilingi bilioni 10.9 zimekadiriwa kama fidia, ambayo mpaka kipindi cha ukaguzi fedha hizo zilikuwa bado hazijatolewa na Serikali. Bwawa hili la Furkwa litajengwa kwa ajili ya kutoa huduma maji ya kuaminika ya kwa Dodoma Manispaa na wilaya za Bahi, Chemba na Chamwino.

Ninashauri Menejimenti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kurudisha fedha zilizochepushwa kutekeleza ukarabati wa mabwawa manne. Nashauri pia menejimenti kuzingatia umuhimu wa bwawa la Farkwa; na hivyo, kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo na ulipaji wa

## 8.4 UKAGUZI WA MIFUKO MAALUMU YA SERIKALI

### 8.4.1 Udhibiti wa Mikopo inayotolewa na Mifuko MaaluKielelezo Na. 21:mu

- i. **Mfuko wa Udhampini wa pembejeo za kilimo (AGITF)- Mikopo iliyotolewa na Mfuko haijarejeshwa shilingi 1,141,590,806**

Mfuko wa Udhampini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ni mfuko unaojiendesha ulio chini ya usimamizi wa Bodi ya Wadhamini. Mfuko huo ulianzishwa na Sheria ya Bunge namba 9 ya 1994 kwa lengo la kuunga mkono ununuza na usambazaji wa pembejeo za kilimo kupitia utoaji wa mikopo kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo.

Wakati wa ukaguzi wa Mfuko huo wa pembejeo, nilibaini kuwa kiasi cha mikopo pamoja na riba wenyewe thamani ya shilingi 2,647,694,736 kilitolewa kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo katika mikoa ya Mtwara, Dodoma, Morogoro na Pwani. Mikopo hii imerejeshwa kwa kiasi cha shilingi 1,506,103,930 (asilimia 57), hivyo kiasi ambacho hakijarejeshwa mpaka kipindi cha ukaguzi ni shilingi 1,141,590,806 (asilimia 43).

Kwa kuwa Mfuko huu wa Pembejeo za Kilimo unaojiendesha kwa marejesho yatokanayo na mikopo, hivyo kushindwa kurejeshwa kwa mikopo hii kwa wakati huathiri wakulima wengine ambaa wanahitaji msaada wa pembejeo za kilimo.

Ninashauri menejimenti ya mfuko huu wa Pembejeo za Kilimo kuweka jitihada zaidi za kupata marejesho ya mikopo yote ya shilingi bilioni 1.14 na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote walioshindwa kurejesha mikopo yao kulingana na mikataba ya mkopo na kwa kuzingatia dhamana za mkopo zilizowekwa.

- ii. **Mfuko wa udhamini wa Rais - Mikopo ya Shilingi 510,572,419 hazijarejeshwa**

Mfuko wa Udhampini wa Rais (PTF) ni Taasisi ya Fedha, ilioanzishwa na Serikali ya Tanzania, mwaka 1984 chini ya Sheria ya Usimamizi wa Wadhamini, Sura ya 375. Lengo la Mfuko

huu ni kuhamasisha hali ya kujitegemea, ufanyaji kazi na kuhamasisha kujajili kwa Watanzania wa hali ya chini, pamoja na kuwawezesha Vijana na Wanawake nchini kwa kuwapa huduma za kifedha, ushauri na fursa mbalimbali katika kuhakikisha Watanzania wanainuliwa kiuchumi.

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa Mfuko huu ulitoa mkopo wa shilingi 538,545,669 kwa vituo vitano ambavyo ni Kituo cha Vijana cha Shabani Robert, Kituo cha Vijana cha Mkwawa, Kituo cha Vijana cha Benjamini Mkapa, Kituo cha Vijana cha Mtwango na Kituo cha Vijana cha Mdete vyote vya mjini Makambako.

Mpaka mwisho wa mwaka 2016/2017 kiasi kilichorejeshwa na vikundi hivyo ni shilingi 13,248,575 sawa na asilimia 2.5 na kuacha kiasi cha shilingi 510,572,419 (97.5%) kama mkopo ambao haujarejeshwa na vikundi hivyo.

Ni muhimu sana kwa vikundi vya Vijana vilivyopewa mkopo kurudisha fedha za mfuko ili zitumike kusaidia vikundi vingine vya vijana na wanawake, na kufanya mfuko uendelee kukuwa zaidi.

Ninashauri Usimamizi wa Mfuko wa Udhagini wa Rais kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa vituo vyote vya vijana na wanawake vilivyokopeshwa na kuhakikisha vinarejesha mikopo waliopewa kwa wakati ulipangwa.

**iii. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake - fedha za mfuko zilizokopeshwa kwa Fungu 53 shilingi 326,282,817 na kiasi cha shilingi 759,148,107 kwenda halmashauri hazijarejeshwa.**

Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ni mfuko ambao unalenga kusaidia na kuwawezesha Wanawake Tanzania kwa kuwapa mikopo ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kufanya Ujasiriamali.

Katika ukaguzi wa Mfuko huu wa wanawake, nilibaini kuwa kuna uhamisho wa shilingi 326,282,817 kwenda Fungu 53 ili kuwesha utekelezaji wa shughuli za Fungu hilo kutokana na upungufu wa fedha za matumizi ya kawaida kutoka Hazina. Katika uhamisho

huu wa fedha nilibaini kuwa fedha hizi zilizohamishwa hazikuwa na makubaliano yoyote ya namna gani fedha, hizi zitarejeshwa kwenye Mfuko kwa ajili ya utekelezaj wa malengo ya Mfuko wa Maendeleo kwa Wanawake.

Uhamisho wa fedha kwenda fungu 53 ni kinyume na Kifungu Na. 2.1 cha Masharti ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2016 ambayo inawataja wafaidika wa fedha kuwa: (i) Wanawake wenyе umri wa miaka 18 na zaidi au chini ambaо wanawatoto na wanasifa zinazohitajika, (ii) Kikundi cha wanawake/ mtu binafsi kutoka kwa kundi la mahitaji maalum; (iii) Mwanamke Mjasiriamali aliyejiunga na vikundi vya kijamii VICOBA SACCOS nk, ambaо wanahusika katika shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, mifugo, biashara ndogo na za kati (SME), usafiri, madini na biashara nyingine.

Pia nilibaini kuwa kuna mikopo ya Shilingi 759,148,107 iliyotolewa kwa Halmashauri mbalimbali za Wilaya. Ukwasi wa Mfuko huu upo mashakani kwa sababu za kushindwa kurejeshwa mikopo na kuhamisha fedha kwenda Wizarani bila ya makubaliano ya kurejeshwa kutasababisha Mfuko huu kushindwa kutopa mikopo zaidi kwa wahitaji wengine, hivyo kushindwa kuwainua kiuchumi Wanawake.

Ninashauri menejimenti ya Fungu 53 na wale wa Halmashauri za Wilaya kurejeshwa mikopo yote iliyotolewa na Mfuko wa maendeleo ya Wanawake ili fedha hizo zitumike kwa makundi mengine ya wanawake. Ninashauri pia usimamizi wa Mfuko kuandaa mikakati ya kuhakikisha kuwa mikopo yote inarejeshwa pale muda wa kurejeshwa unapofika. Masuala mengine ya kiukaguzi yaliyobainika katika ukaguzi wa Mifuko ya Serikali

### 8.4.1.1 Ukaguzi wa Akaunti ya Uwezeshaji wa Maendeleo ya Madini (MDEF)

#### 8.4.1.1.1 Mchango wa Maendeleo ya sekta ya Madini Haujalipwa na Kampuni ya Mgodi wa Dhahabu ya Buzwagi (ACACIA Ltd) TZS 732,631,200

Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya madini (MDEF) ulianzishwa kutokana na kifungu Na 4.1.3 cha Mkataba wa Maendeleo ya madini baina ya Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini na kampuni ya Pangea Madini (Kampuni tanzu ya Barick Gold). Mkataba huo ulisainiwa tarehe 17 Februari 2007 wakati wa kuanzishwa kwa Mgodi wa Dhahabu ya Buzwagi huko Kahama. Kifungu Na. 4.1.3 cha makubaliano hayo kinautaka Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi kuilipa Serikali jumla ya dola la Kimarekani 125,000 kila ifikapo tarehe 31 Desemba ya kila mwaka wa uzalishaji kama mchango kwa Mfuko wa Maendeleo Sekta ya Madini.

Hata hivyo, mapitio ya utekelezaji wa mkataba huu, nilibaini kuwa jumla ya Shilingi 732,631,200 zilikuwa hazijalipwa kwa kipindi cha miaka minane iliyopita. Uchambuzi wa kina wa kiasi ambacho hakijalipwa ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali 8.15 hapo chini

**Jedwali Na. 66: Mchango wa maendeleo ya madini haujalipwa na Acacia Ltd TZS 732,631,200**

Mwaka	Kiasi cha madai (Dola za kimarekani)	Viwango vya kubadilishia fedha TZS/USD	Kiasi cha Madai kwa Shilingi	Kiasi kilicho lipwa na Mgodi (Shilingi)	Kiasi ambacho hakijalipwa (shilingi)
31.12.2009	125,000	1,594.68	199,335,400	-	199,335,400
31.12.2010	125,000	1,594.68	199,335,400	-	398,670,800
31.12.2011	125,000	1,594.68	199,335,400	-	598,006,200
31.12.2012	125,000	1,594.68	199,335,400	-	797,341,600
31.12.2013	125,000	1,779.17	222,396,038	777,500,000	242,237,638
31.12.2014	125,000	1,779.17	222,396,038	-	464,633,675
31.12.2015	125,000	1,779.17	222,396,038	224,625,000	462,404,713
31.12.2016	125,000	2,161.81	270,226,488	-	732,631,200
Total	1,000,000		1,734,756,200	1,002,125,000	732,631,200

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimentiya mfuko wa maendeleo ya madini*

Ninashauri menejimenti ya Wizara ya Madini kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mkataba huu na kuitaka ACACIA kulipa mchango wa kiasi cha shilingi 732,631,200 na kuanza kuzingatia kikamilifu matakwa ya Mkataba kati yao na Serikali kwa kulipa dola za kimarekani 125,000 kila ifikapo tarehe 31 Desemba ya kila mwaka wa uzalishaji.

#### **8.4.1.2 Ukaguzi wa mfuko wa Misitu (TaFF)**

##### **8.4.1.2.1 Mapungufu yaliyojitekeza katika ukaguzi wa Mradi wa Shilingi 104,072,000 wa ufugaji wa nyuki**

Mfuko wa Misitu Tanzania ni Mfuko wa Uhifadhi wa Hifadhi za Misitu ulioanzishwa chini ya Sura ya 323 ya sheria ya Misitu chini ya kifungu Na. 79 - 83[liliyorejewa 2002], kwa malengo ya kutoa msaada wa kifedha kwa malengo ya kutunza na kuendeleza hifadhi za Msitu na Usimamizi wa Kudumu wa Msitu yote nchini.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa kiasi cha shilingi 104,072,000 kilitolewa kwa wafugaji saba wa nyuki kwa zaidi ya miaka miwili iliyopita, lakini wakati wa ziara yangu kwenye maeneo ya mradi nilibainisha kuwa mizinga mingi ya nyuki haina nyuki, hivyo lengo la mradi halijafanikiwa kama ilivyotegemewa. Tazama jedwali 8.16 hapo chini.

### Jedwali Na. 67: Mapungufu katika mradi wa ufugaji Nyuki

Na	Jina la mradi	Eneo	Mapungufu yaliojiokeza.	Kiasi (Shilingi)
1	Mradi wa Utunzaji wa Nyuki na ufugaji wa kuku-Zuzu	Manispaa ya Dodoma	Mizinga ya nyuki 150 iliwekwa, ukaguzi ulibaini kuwa ni mizinga 7 tu yenye nyuki kwa kipindi chote cha miaka miwili iliyopita.  Mizinga 143 haina nyuki.	15,360,000
2	Umoja wa akina mama Mwankoko	Manispaa ya Singida	Katika Mizinga 32 iliyowekwa katika kipindi cha miaka miwili ni mizinga 4 tu yenye nyuki, hivyo Mizinga mingine 28 imekaa kipindi kirefu bila nyuki.	5,000,000
3	Mradi wa kufuga nyuki - Uyuwi Magharibi	Halmashauri ya wilaya Uyuwi	Katika Mizinga ya nyuki 76 iliyowekwa katika kipindi cha miaka miwili ni mizinga 18 tu yenye nyuki, hivyo mizinga 58 haina nyuki	18,000,000
4	Mradi wa ufugaji Nyuki Mipa	Halmashauri ya wilaya Kisapu	Mizinga ya nyuki 150 imewekwa kwenye eneo kavu ilisilokwa na vivutio na mazingira sahihi kwa mazalia ya nyuki.  Kwa zaidi ya miaka miwili hakuna nyuki katika mizinga hii	40,712,000
5	Ufugaji wa Nyuki Mwasonge	Halmashauri ya Wilaya Misungwi	Katika Mizinga ya nyuki 150 iliyowekwa, ukaguzi ulibaini kuwa ni mizinga 14 tu yenye nyuki katika kipindi cha miaka miwili. Na hivyo Mizinga 136 haikuwa na nyuki.	20,000,000
6	Mradi wa ufugaji wa nyuki wa Andrew B. Marejesi	Halmashauri ya wilaya ya Bunda	Mizinga ya nyuki 30 imewekwa kwa muda wa miaka miwili, hakuna nyuki katika mizinga hiyo	5,000,000
Jumla				104,072,000

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Mapitio yangu ya utekelezaji wa mradi na majadiliano baina yangu na Menejimenti ya Mfuko huu, juu ya changamoto zilizotokana na utekelezaji wa mradi huu, yilibaini kuwa udhaifu mkubwa katika miradi hii ya ufugaji wa Nyuki ni ukosefu wa upembuzi yakinifu wa mazingiza kabla ya utekelezaji wa Mradi. Mizinga yote imewekwa katka mazingira yasiyoruhusu nyuki kuzaliana na kuzalisha asali.

Naishauri menejimenti ya mfuko huu, kabla haijatoa msaada wa kifedha kwa wafugaji wa nyuki, wafanye upembuzi yakinifu kuona kama eneo la kuweka Mizinga hiyo ya nyuki litawezesha nyuki kuzaliana na Kuzalisha asali.

### **8.4.1.3 Ukaguzi wa Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji**

#### **8.4.1.3.1 Fedha za Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Sekta ya Maji zilizokopeshwa kwenda Wizara ya Maji hazijarudishwa TZS 171,843,000**

Katika ukaguzi wa shughuli za Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Sekta ya Maji, nilibaini kuwa, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko huu wa uwekezaji umehamisha shilingi 171,843,000 kwenda Wizara ya Maji na Umwagiliaji kama mkopo. Katika kutafuta sababu za uhamisho wa fedha, niliambiwa na uongozi wa Mfuko huu kwamba Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilihitaji fedha hizi kwa sababu ya upungufu wa fedha za matumizi ya kawaida kutoka Hazina.

Katika ukaguzi wa fedha hizo zilizohamishwa, nilibaini kuwa hakuna mkataba wa makubaliano kati ya Mfuko huu na Wizara ya Maji, hivyo nilishindwa kubaini ni lini fedha hizi zitarudishwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya Uwekezaji katika sekta ya Maji.

Ninashauri menejimenti ya Wizara kurejesha kiasi hicho cha fedha za mkopo kutoka Mfuko wa Uwekezaji Sekta ya Maji ili kuruhusu utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishwa.

### **8.4.1.4 Ukaguzi wa Mfuko wa Maafa**

#### **Fedha za Mfuko wa Maafa Hazijarudishwa Shilingi 206,318,360**

Katika Mapitio yangu ya nyaraka za utendeji wa kamati ya Maafa katika Mkutano uliofanyika tarehe 4 Novemba 2016 nilibaini kuwa, Kamati ya Maafa ilimuagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam kurejesha kiasi cha Shilingi 139,757,860 kilichobaki katika shughuli za maafa. Pia, katika kikao hicho iliamuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa kurejesha kiasi cha shilingi 66,560,500 ambacho kililipwa mara mbili kimakosa.

Hata hivyo, nilibaini wakati wa ukaguzi wa Hesabu za Mfuko wa Maafa kuwa kiasi hicho hakikurejeshwa na Katibu Tawala-Dar es Salaam kama ilivyo kubalika katika kikao cha Novemba 2016. Kwa maelezo zaidi rejea Jedwali 8.17 hapo chini:

**Jedwali Na. 68: Fedha ambazo hazijarejeshwa na Katibu tawala-Dar Es Salaam**

<b>Na</b>	<b>Taarifa</b>	<b>Kiasi (Shilingi)</b>
<b>1</b>	Pesa iliyolipwa mara mbili kwa watu wengine wakati wa kulipa fidia kwa waathirika wa mabomu ya Gongolamboto	66,560,500
<b>2</b>	Fedha iliyobaki baada ya kuwanunulia viwanja waathirika wa mabomu ya Gongolamboto's	139,757,860
<b>Jumla</b>		<b>206,318,360</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Maelekezo aliyopewa katibu Tawala wa Dar Es Salaam na kamati ya Maafa, hayajafanyiwa Kazi. Hivyo fedha za Maafa hazijatumika kwa malengo yaliokusudiwa.

Ninamshauri Katibu Tawala Dar es Salaam kurejesha kiasi cha shilingi 206,318,360 kwenye Mfuko wa Taifa wa Maafa ili fedha hizo zitumike kwa ajili ya kuwasaidia wengine wakati wa Maafa.

#### **8.4.1.5 Ukaguzi wa Mfuko wa Barabara**

##### **8.4.1.5.1 Fedha za Ujenzi wa Barabara zilizohamishwa kimakosa kwenda Halmashauri ya Njombe Hazijarudishwa Shilingi 152,877,500**

Katika ukaguzi wa akaunti ya Mfuko wa Barabara, nilibaini kuwa tarehe 31 Machi 2017, Katibu Mkuu TAMISEMI iliiagiza benki ya CRDB kuhamisha fedha za maendeleo Shilingi 152,877,500 kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Makete. Nambari ya akaunti iliyotolewa kwa wa ajili ya uhamishwaji wa fedha kutoka benki ya CRDB ilikuwa ya Akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe yenye Na. 60610001200 badala ya akaunti Na. 60410000340 ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

Benki ya CRDB ilihamisha shilingi 152,877,500 kwenda Halmashauri ya Njombe badala ya Halmashauri ya Makete. Ukaguzi zaidi wa kiasi kilichohamishwa, ulibaini kuwa Halmashauri ya Njombe haijakiri kupokea fedha hizo. Nilitaarifiwa na menejimenti ya Mfuko kuwa wamefanya juhud

za kuhakikisha fedha hizi zinarejeshwa na Halmashauri ya Njombe.

Ninaishari menejimenti ya Mfuko wa Barabara kuwa makini wakati wa kuhamisha fedha ili kuepuka kuhamishia katika akaunti zisizo sahihi na pengine upotevu wa fedha. Pia nashauri Mkurugenzi wa Halmashauri ya Njombe kurejesha fedha hiso kwenda Akaunti ya Mfuko wa barabara ili iweze kuhamishiwa kwenda Halmashauri ya Makete kutekeleza shughuli zilizopangwa.

## 8.5 OMambo Mtambuka Yaliobainika Katika Ukaguzi Wa Wakala, Mifuko Maalumu ya Fedha, Bodi za Mabonde ya Maji na Taasisi Nyingine Za Serikali

### 8.5.1 Madeni ya Muda Mrefu Shilingi 1,312,983,248,513

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Nilibaini kuwa jumla kuu ya madeni katika Wakala 32 wa serikali, taasisi 29 za serikali, na Bodi 13 za Mabonde ya Maji ni shilingi 1,312,983,248,513.

Katika mwaka 2015/2016 jumla ya madeni katika taasisi hizi ilikuwa ni shilingi 2,075,795,283,641, hivyo kwa mwaka 2016/2017 kuna upungufu wa madeni kwa shilingi 762,812,035,128 sawa na asilimia 37 ya madeni ya mwaka jana.

Katika madeni yote ya serikali, nimebaini kuwa kiasi cha shilingi 1,201,546,490,218 sawa na asilimia 92 ni madeni yaliyozidi miezi 12 na kiasi cha shilingi 111,436,758,295 sawa na asilimia 8 ni madeni yaliojitokeza ndani ya miezi 12. Tazama jedwali 8.18 hapo chini

**Jedwali Na. 69: Madeni yasiolipika**

Kipindi	Mwaka wa fedha unaishia tarehe 30 Juni 2017	
	Kiasi (Shilingi)	Asilimia
Ndani ya miezi 12	111,436,758,295	8
Zaidi ya miezi 12	1,201,546,490,218	92
Jedwali	<b>1,312,983,248,513</b>	<b>100</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Mchanganuo wa kina wa madeni haya umeonyeshwa katika **Kiambatisho 8.4**

Sababu kuu ya kutokulipwa kwa madeni haya ya muda mrefu ni upungufu wa fedha zinazotolewa na Serikali wakati wa utekelezaji wa shughuli za serikali. Kushindwa kulipa madeni kwa muda muafaka kuna athiri sifa za taasisi za Serikali kwa watoa huduma na Makandarasi.

Nilibaini kuwa katika mikataba ya ujenzi wa barabara kuchelewa kwa malipo baada ya siku 28 husababisha kutozwa adhabu. Hii

imeonekana katika madeni TANROADS ya kiasi cha Shilingi 998,669,929,000, sawa na asilimia 77. Kuchelewa kulipa madai ya wakandarasi ndani ya muda wa siku 28 kumesababisha Wakala huyu kulipa adhabu.

Ninaishauri Serikali kutoa fedha za utekelezaji wa bajeti yake kwa muda mwafaka ili kuziwezesha taasisi hizi kulipa madai yao kwa muda na kuepuka uwezekano wa kulipa adhabu kutokana na madeni hayo.

#### **8.5.2 Madai ya serikali yasikusanywa Shilingi 657,992,846,515**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 nilibaini kuwa jumla kuu ya madai ya serikali kutoka kwa Wakala wa serikali 32, taasisi za serikali 29, na Bodii za Mabonde ya Maji 13 ni shilingi 657,992,846,515.

Kwa mwaka uliopita wa 2015/2016 jumla kuu ya madai ilikuwa shilingi 991,228,165,607, hivyo kwa mwaka 2016/2017 serikali imeweza kukusanya kiasi cha shilingi 333,235,319,092 sawa na asilimia 34 kutoka wa wadaiwa wake.

Katika jumla kuu ya madai ya Serikali nimebaini kuwa kiasi cha shilingi 360,450,449,442 (55%) ni madai yaliyokaa zaidi ya miezi 12 na kiasi cha shilingi 297,542,397,073 (45%) ni madai mapya yalio chini ya miezi 12

Kutokusanya madeni kwa muda muafaka kunapunguza rasilimali za taasisi hizi katika kujiendesha, hivyo kushindwa kutimiza malengo yao. Tazama Jedwali hapo chini

#### **Jedwali Na. 70: Madai yasiokusanywa**

<b>Kipindi</b>	<b>Mwaka wa fedha unaishia tarehe 30 Juni 2017</b>	
	<b>Kiasi (Shilingi)</b>	<b>Asilimia</b>
<b>Ndani ya miezi 12</b>	297,542,397,073	45
<b>Zaidi ya miezi 12</b>	360,450,449,442	55
<b>Jedwali</b>	<b>657,992,846,515</b>	<b>100</b>

*Chanzo: Barua ya Ulaguzi kwa Menejimenti*

Mchanganuo wa Madai haya ya serikali yamechananuliwa katika Kiambatisho 8.5

Naishauri Serikali kufuutilia kwa ukaribu madai yake yote kwa wadaiwa wake na kuweza kukusanya madeni hayo pale muda wa kukusanya unapofika.

### **8.5.3 Mapungufu yaliyojitekeza katika Ukaguzi wa Fedha za Matumizi ya Matumizi ya kawaida**

Wakati wa ukaguzi wa Wakala wa Serikali, Bodi za Bonde la Maji, Mifuko ya Fedha Maalum za Serikali na Taasisi nyingine za Serikali, nilibaini mapungufu kwenye usimamizi wa matumizi ambayo yanahitaji kushughulikiwa na menejimenti.

Mapungufu yote niliyoyabaini mwaka huu nilishayatolea taarifa katika taarifa zangu za miaka iliyopita, hii ina maana kuwa utekelezaji wa mapendekezo yangu kwa taasisi za serikali ni mdogo.

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2016/2017 nilibaini kuwa kuna: (i) Matumizi yasiyokuwa na nyaraka za kutosha ya Shilingi 3,742,714,498, (ii) Masurufu yasiyorejeshwa ya shilingi 706,469,653; na (iii) Malipo ya TZS 31,673,330 yaliyofanywa bila kukata kodi za zuio.

Kwa kuwa mapungufu haya yote ya matumizi ya fedha za serikali nilishayatolea taarifa kipindi cha nyuma, hivyo narudia kusositiza kwa menejimenti zote; (i) Kutengeneza mifumo imara ya uthibiti wa ndani ili kusaidia kutunza nyaraka zote za matumizi, (ii) Kurejesha masurufu yote ya kazi ambazo zimekamilika na (iii) Kuhakikisha taasisi hizi zinaisaidia Serikali kukusanya Mapato kwa kukata Kodi ya zuio pale ambapo taasis hizi zipokuwa zinafanya malipo ya huduma.

Katika ukaguzi wa ugavi na menejimenti ya mikataba, nimebaini kuwa kuna ukiukwaji wa sheria ya manunuvi. Nilibaini kuwa; (i) Kuna malipo ya shilingi 140,524,858 yaliyofanyika bila ya kukagua mali zilizonunuliwa; (ii) Ununuvi wa magari ya shilingi 65,830,014 bila ya ushindanishi wa bei; na (iii) Manunuvi ya shilingi

932,422,979 yaliyofanyika bila kupata idhini ya bodi ya manunuzi.

Katika suala la utekelezaji wa sheria ya Ununuzi ya Umma, ninazishauri menejimenti; (i) Kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinavyonunuliwa vinakaguliwa na kamati maalumu ya ukaguzi kabla ya malipo kufanyika; (ii) Kuhakikisha kuwa ushindani unafanyika katika manunuzi ili kusaidia Serikali kupata thamani ya fedha katika manunuzi na (iii) Zabuni zote zipitishwe kwenye bodi ya manunuzi kuweza kupata idhini ya bodi.

Pia, nilibaini kuwa kuna malipo yaliyofanyika bila kufuata utaratibu wa kibajeti. Katika suala hili nilibaini kuwa; (i) Kuna malipo ya shilingi 211,135,982 yaliyofanyika nje ya bajeti iliyopitishwa; (ii) Malipo ya shilingi 117,122,668,997 yalifanyika nje ya mfumo wa bajeti; (iii) Malipo ya shilingi 56,957,309 yaliyofanyika nje ya makubaliano ya mkataba (MOU) baina ya Serikali na wafadhili, (iv) Malipo ya shilingi 89,473,398 yaliyofanyika bila kuzingatia vifungu stahiki.

Kuhusu suala la matumizi yaliyofanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa, ninashauri menejimenti kufuata Kanuni ya 46 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (Marekebisho ya 2004) na kuboresha udhibiti wa ndani katika kuhakikisha matumizi yanaendana na bajeti.

Kuhusu suala la matumizi yaliyofanyika nje ya makubaliano ya serikali na mkataba wa wafadhili nashauri menejimenti kufuata masharti yaliyokubalika kati ya Serikali na washirika wa maendeleo, na kuacha kufanya matumizi ambayo hayaendani na makubaliano baina ya washirika wa maendeleo na Serikali.

Jumla kuu ya mapungufu yaliyo orodheshwa hapo juu yanatokana na ukiukwaji wa sheria ya Fedha ya Umma ya 2001 (iliyoboreshw 2004), Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2013, na sheria ya kodi ya 2008 ni shilingi 123,099,871,0117. Mchanganuo wa taasisi zilizopatikana na mapaungufu hayo katika matumizi ya fedha zinaonekana katika Kiambatisho 8.6

#### 8.5.4 Ukosekanaji wa Hati Miliki za Ardhi zinazomilikiwa na Taasisi za Serikali

Katika mapendekezo yangu ya ukaguzi wa mwaka 2015/2016 nilipendekeza taasisi zote za Serikali kuwa na hati zinazoonesha umiliki wa ardhi zao. Katika ukaguzi wa mwaka huu wa 2016/2017 nilibaini kuwa taasisi kumi na moja hazina Hati ya Umiliki wa ardhi. Tazama jedwali 8.20 hapo chini

**Jedwali Na. 71: Taasisi za Serikali zisizokuwa na hati Miliki ya Ardhi**

S/N	Jina ya Wakala
1	Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania
2	Tanzania Shirika la Maabara ya Mifugo
3	Wakala wa Utafiti wa miamba Tanzania
4	Wakala wa Hifadhi ya Chakula
5	Wakala wa Huduma ya Misitu
6	Taasisi ya Uhasibu
7	Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi
8	Bodi ya Bonde la Maji Ruvu
9	Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Handeni
10	Bodi ya Bonde la Maji Pwani ya kusini Ruvuma
11	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Ukosekanaji wa hatimiliki ya ardhi katika taasisi za serikali ni kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi kuitia barua yake yenye Na. AB 225/305/01 ya tarehe 7 Septemba 2016. Barua hii iliwataka Wakuu wote wa taasisi kuzitambua ardhi zao, kuzithaminisha na kuomba kupatiwa hati za umiliki za ardhi hizo.

Ninazishauri Menejimenti za Wakala ambazo hazina hati miliki za viwanja vyao, kufuata maagizo yaliyotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi , kuthaminisha ardhi zao, na kuomba kupatiwa hati hizi na wizara ya ardhi.

### 8.5.5 Malipo yaliyofanyika bila kudai risiti za kielektroniki (EFD) - Shilingi 42,407,098,471

Sheria ya Usimamizi wa kodi ya Mwaka 2017 kifungu Na. 36 inamtaka kila mtu anayetoea huduma yoyote ile kutoa stakabadhi kwa kutumia kifaa cha kielektroniki.

Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017, taasisi za serikali 19 zilifanya malipo ya kiasi cha Shilingi 42,407,098,471 bila Taasisi hizo kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD) kinyume na Kanuni Na. 28(1) ya Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Mashine za Stakabadhi za Kielektroniki) ya mwaka 2012.

Mwaka 2015/2016 niliripoti kiasi cha malipo ya shilingi 5,388,147,654 kutoka katika Wakala 11, Bodi 6 za Mabonde ya Maji, na taasisi nyingine 12 za serikali kilichofanyika bila kudai risiti za kielektroniki (EFD).

Kwa mwaka huu wa 2016/2017 tatizo hili la kutokudai risiti limeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka kwa taasisi za umma kwa ongezeko la kiasi cha Shilingi 37,018,950,817, sawa na asilimia 87. Tazama Jedwali 8.21 hapo chini

**Jedwali Na. 72: Malipo yasiyokuwa na risiti za kielektroniki-EFD**


Na.	Jina la Wakala	Kiasi (shilingi)
1	Baraza la Wakunga na Wauguzi Tanzania	3,370,000
2	Baraza la Madaktari Tanganyika	4,330,816
3	Mfuko wa Barabara	5,220,771
4	Baraza la Wafamasia	11,223,400
5	Bodi ya Maabara Binafsi	11,738,700
6	Bodi ya Bonde la maji Ziwa Tanganyika	12,065,000
7	Bonde la Ndani la Mto	13,531,000
8	Wakala wa Mbegu za Kilimo	14,370,623
9	Bodi ya Bonde la maji Ziwa Rukwa	19,375,000
10	Chuo cha Madini	23,762,929
11	Mfuko wa Maendeleo ya Umeme Vijijini	24,292,000
12	Wakala wa vitambulisho vya Taifa	33,021,464
13	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	35,486,096

Na.	Jina la Wakala	Kiasi (shilingi)
14	Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mtaa	63,633,965
15	Mfuko wa Maendeleo ya maji	84,980,000
16	Wakala wa Majengo Tanzania	205,745,090
17	Taasisi ya uzalishajimali Magereza	265,847,292
18	Taasisi ya Uhasibu Tanzania	303,843,588
19	Wakala wa Barabara Tanzania	41,271,260,737
	<b>Jumla Kuu</b>	<b>42,407,098,471</b>

*Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Mwenendo wa kutokuchukua EFD kwa Wakala wa Serikali kwa miaka miwili unaonyeshwa katika chati hapa chini.

#### Kielelezo Na. 22: Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za Kielektronik



Kwa mujibu wa Jedwali la hapo juu, taasisi zisizochukua stakabadhi za kieletronmalipo zimepungua kwa asilimia 57 wakati kiasi cha malipo kisichokuwa na stakabadhi za

kielektroniki kimeongezeka kwa asilimia 87 kulinganisha na kiasi cha mwaka jana.

Nashauri Serikali iendelee kutoa elimu juu ya utekelezaji wa hiari wa Kanuni na Sheria ya Kodi ya Mapato za mwaka, 2012 kuhusu matumizi ya hiari ya mashine za EFD zitakazochangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya Serikali kama kila Manunuzi ya Serikali yataambatana na Stakabadhi za kielektroniki.

## SURA YA TISA

### 9.0 MANUNUZI NA USIMAMIZI WA MIKATABA

#### 9.1 Utangulizi

Viwango vya uzingatifu vinaendelea kuwa chini katika vyombo vya umma kwa vinaendelea kutofuata taratibu za manunuzi. Hali isiposhughulikiwa, inaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya serikali katika utoaji wa hudma kwa umma. Ununuzi wa bidhaa na huduma ni muhimu kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekretarieti; mara nyingi huhusisha inahusisha matumizi makubwa ya fedha za Serikali. Kesi zilizopita za rushwa zinaonesha kuwa hili ni eneo la hatari zaidi la kufanya udanganyifu na ubadhiribifu. Rushwa yoyote katika manunuzi haitaleta tu hasara za kifedha kwa kampuni au Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekeretarieti, bali pia huathiri sifa/ taswira ya Taasisi kama mshirika wa kuaminika katika utoaji huduma kwa jamii.

Manunuzi ya Umma ni nguzo muhimu ya kimkakati katika utoaji wa huduma Serikalini. Kutokana na Manunuzi ya Umma kutumia kiasi kikubwa cha fedha za Serikali, usimamizi wake ni muhimu katika kukuza ufanisi wa sekta ya Umma.

Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya 2011 pamoja na Kanuni zake za msingi za mwaka 2013, na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2016 iliyotolewa hivi karibuni hutoa mfumo wa kisheria unaosimamia taasisi na mchakato wa manunuzi katika sekta ya umma. Licha ya kuwapo kwa sheria, vyombo vingine vya serikali bado havizingatii kikamilifu na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2011 na Kanuni zake za 2013.

Mamlaka ya CAG kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma (2011) ni kuhakikisha kuwa michakato ya manunuzi katika sekta ya umma ni wazi, ya haki, na ya uwazi na kwamba kwa ujumla wamekubaliana na mahitaji ya Sheria ya manunuzi ya umma Na.7 ya 2011 na Kanuni zake za msingi za 2013.

Sura hii inaoneesha matokeo ya ukaguzi kuhusu ununuvi na usimamizi wa mikataba kutokana na kaguzi za Kanuni ya 55 ya Kanuni za Ununuvi wa Umma wa 2013 kwa mwaka huu wa fedha husika. Katika ripoti yangu nimejumuisha ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuvi ya Umma na Taarifa ya Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa mali za Serikali.

#### **9.1.1 Manunuvi Yaliyofanyika bila Idhini ya Bodi ya Zabuni Shilingi 2,997,009,109**

Ukaguzi niliofanya kwa kuzingatia Kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Manunuvi ya Umma ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni 55 ya Kanuni za Manunuvi ya Umma za 2013 inayotaka Manunuvi kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni nilibaini kuwa jumla ya Taasisi za Serikali Kuu saba (7) zilifanya Manunuvi yenyeye thamani ya Shilingi 2,997,009,109 bila idhini ya Bodi ya Zabuni kama zilivyoorodheshwa kwenye Jedwali Na.9.1

##### **Jedwali Na. 73:Manunuvi Yaliyofanyika bila Idhini ya Bodi ya Zabuni**

<b>Na</b>	<b>Fungu na Mapungufu yaliyobainika</b>	<b>Kiasi (Sh)</b>
1	Fungu 54 Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe Matengenezo ya Gari DFP 8998 na ununuvi wa matairi ,na mafuta ya dizeli lita 8,908 yalifanywa bila kibali cha Bodi ya Zabuni.	28,530,178
2	Fungu 36 Sekretarieti ya Mkoa wa Katawi Ilibainika kuwa manunuvi ya madawa na vifaa vya hospitali, matairi 7 na tyubu za ukubwa wa 250/65R17, vyakula na viburudisho yalifanywa bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.	157,294,700
3	Fungu 43 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi MUunuvi wa matairi ya magari ya serikali yenyeye namba za usajili STK 8142 na STL 2675, matengenezo ya gari lenye namba ya usajili STK 4770, machapisho ya sherehe za maonesho ya Nanenane ya 2016/2017 na ukodishaji wa matrubai na mapambo hayakuwasilishwa wala kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni ya Wizara.	47,801,487

Na	Fungu na Mapungufu yaliyobainika	Kiasi (Sh)
4	Fungu 93 Idara ya Uhamiaji -Zanzibar Kuna manunuzi ambayo yalifanyika kwa njia ya “circular resolution” ikiwa imepitishwa na pungufu ya wajumbe wanne (4) wa Bodi ya Zabuni ambapo idadi ya wajumbe wote katika Bodi ya Zabuni wako saba (7) katika ofisi ya uhamiaji ya Zanzibar	76,658,561
5	Fungu la 78 Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya Manunuzi ya vifaa mbalimbali vyaa hospitali yalifanyika bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.	10,440,001
6	Fungu la 77 Sekretarieti ya Mkoa wa Mara Zabuni ya mkataba wa ukarabati na ujenzi wa miradi minne yenye mkataba wa thamani ya Shillingi 2,636,526,838 haikuridhiwa na kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.	2,636,526,838
7	Fungu la 63 Sekretariet ya Geita Ukaguzi umebaini manunuzi ya vyakula na viburudisho pamoja na matengenezo ya magari na manunuzi ya matairi ya magari hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni ya Mkoa wa Geita.	39,757,344
	<b>Jumla</b>	<b>2,997,009,109</b>

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2016/2017

Wizara, Idara za Serekali na Sekretarieti za Mikoa zimeendelea kufanya vibaya katika uzingatiaji wa Kanuni ya 55 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2013. Hii ni kutokana na ukaguzi uliofanyika kwa Taasisi za Serikali Kuu saba (7) ambapo jumla ya manunuzi yenye thamani ya Shillingi 2,997,009,109 hayaku fuata Kanuni. Hii inaonesha kuwa Taasisi tatu (3) zimepungua ukilinganisha na mwaka jana ambapo kulikuwa na Taasisi kumi (10) zenye manunuzi yenye thamani ya Shillini 2,485,411,529.

Kufanya manunuzi manunuzi bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kunaweza kusababisha kazi kutolewa kwa wazabuni/wakandarasi wasiokuwa na vigezo au uwezo, hivyo kusababisha uwazi, ufanisi, na tija kukosekana katika manunuzi. bila ya kuiidhinishwa na Bodi ya Zabuni kunaweza kusababisha kazi kutolewa kwa wazabuni/wakandarasi wasiokuwa na vigezo au uwezo hivyo kusababisha uwazi, ufanisi na tija kukosekana katika.

Kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 35 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, nashauri menejimenti za

taasisi husika zizingatie kikamilifu ushiriki wa Bodi ya Zabuni katika kuidhinisha manunuzi ili kuepuka manunuzi yasiyo kuwa na tija au mikataba batili ili iweze kuondolewa.

#### **9.1.2 Manunuzi Yaliyofanyika bila Ushindanishi Shilingi 6,536,468,043 na Dola (\$120,000**

Katika mwaka huu wa ukaguzi nimebaini kuwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekeretarieti kumi na moja (11) zilifanya manunuzi ya huduma na bidhaa zenyet thamani ya Shilingi 6,536,468,043 na Dola 120,000 bila kuzingatia Kanuni ya 163 & 164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

Vilevile, nilibaini matumizi ya njia za manunuzi isivyostahili kama vile kutoka chanzo kimoja au kushindanisha wazabuni wachache kinyume na kanuni ya 159 ya kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2013 ili kupata thamani ya fedha. Hali hii inaweza kupelekea kutokuwa na ushindani, na usambazaji wa bidhaa za chini kwa bei za juu.

Orodha ya Taasisi ambazo zinahusika ni kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na.9.1(a) na (b).

Kiasi cha manunuzi yaliyofanyika bila ya ushindani kimepungua kutoka Shilingi bilioni 24.22 hadi Shilingi bilioni 6.54 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, jumla ya taasisi kumi na tano (15) zilibainika ikilinganishwa na taasisi kumi na moja (11) zilizokaguliwa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017.

Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekeretarieti kutokana na kutofufa taratibu za ushindanishi, kuna uwezekano wa kutopata bei nzuri ya ushindani kwa bidhaa na huduma walizopata. Ninapendekeza kwa menejimenti kuhakikisha wanakuwa makini katika usimamizi ili kuhakikisha kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inatumika ili kukuza ushindani na kupata thamani ya fedha kwa bidhaa na huduma

Ninapendekeza tena kuwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekeretarieti zinapaswa kuepuka matumizi ya mbinu zisizofaa za manunuzi kama vile Mzabuni mmoja au zabuni zisizo za wazi kwa kuwa haziendani na matakwa ya Kanuni ya 159 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma 2013 ili kufikia haki na uwazi wakati wa manunuzi kwa umma.

#### **9.1.3 Manunuzi ya Bidhaa, Huduma na Ujenzi bila ya Mikataba Shilingi 1,453,204,154.68**

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilibaini jumla ya taasisi za Serikali Kuu kumi na moja (11) zilizokaguliwa zilifanya manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa na huduma yenye thamani ya Shilingi 1,453,204,154.68 bila mkataba wowote wa makubaliano kati ya mnunuzi na wauzaji na wakandarasi. Mkataba wa halali ni msingi ambao kila mmojawao atawajibika iwapo atakwenda kinyume na mkataba.

Hii ni kinyume na Kanuni ya 10 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 ambayo inatamka bayana kwamba, taasisi za Umma zitahakikisha kwamba malipo ya mzabuni yanafanywa kwa haraka kulingana na masharti ya mkataba wa manunuzi kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba wa ununuizi iliyoingia.

Kwa kutokuwapo kwa mkataba halali sikuweza kuthibitisha uhalali wa taratibu zilizofuatiwa wakati wa kuingia na kukubali zabuni kama kanuni 60 (8) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma 2013 inavyotaka. "Inasema" mkataba rasmi utakuwa katika namna hiyo na ina vifungu, masharti na Kanuni kama yalivyo katika hati ya zabuni "Taasisi zinazohusika zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho 9.2**

Nimebaini kuwa kuna ongezeko kidogo la mapungufu kwenye Taasisi za serikali kuu, ambapo katika ukaguzi wa mwaka jana, Taasisi kumi (10) zilifanya manunuzi bila mikataba wakati wa mwaka huu kuna Taasisi kumi na moja (11). Hivyo kunaongezeko la taasisi moja (1), sawa na asilimia 10. Hali hiiinaaonesha kwamba, hakuna uboreshaji kwa mwaka huu wa ukaguzi.

Ninapendekeza uongozi wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekeretarieti kuzingatia taratibu za zabuni kwa kuhakikisha kuwa shughuli zote za manunuzi zinaendana na mikataba halali ili atakayeshindwa kutimiza majukumu yake awajibishwe mbele ya sheria.

#### **9.1.4 Manunuzi ya Vifaa na huduma      kutokakwaWazabuni wasiodhinishwa Shilingi 402,496,986**

Kanuni Na.131 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka, 2013 inaeleza bayana taratibu za kununua bidhaa na huduma kutoka kwa Wazabuni waliodhinishwa na Wakala wa Manunuzi ya Serikali (GPSA).

Pia Kanuni 137 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2013 imeweka bayana na kuelezea namna ya kufanya manunuzi ya Huduma za Umeme, Mitambo na vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya matengenezo ya Magari ya Serikali kuititia TEMESA. Vile vile Kanuni za 139-141 za manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 zinatoa mwongozo kwa taasisi za Serikali kununua madawa kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD).

Hata hivyo, nilibaini kuwa jumla ya taasisi za Serikali kuu nane (8) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi 402,496,986 kutoka kwa Wazabuni wasiodhinishwa na TEMESA, GPSA na MSD.Kwa maelezo zaidi angalia jedwali Na.9.4 hapo chini :

#### **Jedwali Na. 74: Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasiodhinishwa**

<b>Na</b>	<b>Fungu na Mapungufu yaliyobainika</b>	<b>Kiasi (Sh)</b>
1	Fungu 78 Sekretarieti ya Mkoa Mbeya: Hospitali ilinunuliwa vifaa na madawa kutoka kwa wazabuni ambao hawakuidhinishwa	10,440,001
2	Fungu 83 Sekretarieti ya Mkoa shinyanga: Manunuzi ya Madawa yalifanyika kutoka kwa Wazabuni ambao hawakuidhinishwa kuititia makubaliano ya mkataba (RAS/SHY/RPV/2016-17/01)	80,020,920
3	Fungu 74 Sekretarieti ya Mkoa Kigoma: Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasiodhinishwa na GPSA.	89,955,393

Na	Fungu na Mapungufu yaliyobainika	Kiasi (Sh)
4	Fungu 36 Sekretarieti ya Mkoa Katavi: Manunuzi ya Madawa, vifaa vya hospitali kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	44,165,000
5	Fungu 81 Sekretarieti ya Mkoa Mwanza: Manunuzi ya Madawa, vifaa vya hospitali kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	23,699,928
6	Fungu 95 Sekretarieti ya Mkoa Manyara: Manunuzi vifaa vya hospitali kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	4,635,400
7	Fungu 86 Sekretarieti ya Mkoa Tanga: Manunuzi ya Madawa, vifaa vya hospitali kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	124,328,344
8	Fungu 70 Sekretarieti ya Mkoa Arusha: Manunuzi vifaa vya hospitali kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD)	25,252,000
	Jumla	402,496,986

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2016/2017

Nimebaini kuwa kuna maboresho ya asilimia 43 ya kufuata Kanuni 131 ambapo mwaka 2015/2016 katika taasisi za Serikali Kuu kumi na nne (14) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi 7,395,231,560 na mwaka huu ni taasisi nane (8) zimefanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi 402,496,986 kutoka kwa Wazabuni wasiodhinishwa.

Ninapendekeza kwamba Afisa Masuuli kuendelea kuzingatia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi na thamani ya fedha inakuwepo katika shughuli za ununuzi.

#### **9.1.5 Mapungufu Yaliyobainika katika Usimamizi wa Mikataba na Miradi Shilingi 15,072,960,426.76 na Dola (\$) 239,244,515.56**

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi ya Umma kusimamia manunuzi yote ya bidhaa, huduma au Ujenzi pamoja na:

Kufuatilia gharama na upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa muda na ubora ulioainishwa kwenye mkataba;

Kufuatilia maendeleo na kukamilika kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba;

Kuchukua hatua za kusahihisha mapungufu yaliyojitokeza katika kutekeleza masharti ya mkataba

Kuhakikisha majukumu yaliyobainishwa kwenye mikataba yanatekelezwa yote.

Kinyume na kanuni hii, nilibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa Mikataba/Miradi, ambapo mikataba/miradi yenyen thamani ya Shilingi bilioni 15.073 na Dola za Kimarekani milioni 239.245 katika taasisi kumi na nane (18) za Serikali Kuu zilizokaguliwa haikusimamiwa vizuri. Kiambatisho 9.3 (a) na (b) kinaonesha taasisi zilizoshindwa kusimamia mikataba/miradi vizuri.

Ikilinganishwa na mwaka wa ukaguzi 2015/2016, idadi ya Taasisi za Serikali kuu zilizokuwa na mapungufu katika usimamizi wa mikataba imeongezeka taasisi kumi (10) ikiwa ni kwa asilimia 125% kutoka taasisi nane (8) mwaka 2015/2016 hadi taasisi kumi na nane (18) katika mwaka huu wa fedha; Hata hivyo, kiasi cha fedha kilibadiliwa kutoka Shilingi milioni 63.254 mpaka shilingi bilioni 15.073 wakati kuna punguzo kutoka na Dola za Kimarekani Milioni 1,000 hadi kufikia na Dola za Kimarekani Milioni \$239.245. Hali ya ongezeko la taasisi kwa asilimia 125% inaonesha uzingatiwaji hafifu wa Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma.

KKwa ujumla, menejimenti ya Wizara, Idara na taasisi za Serikali kuu hazina budi kubadili mtazamo katika usimamizi wa mikataba mbalimbali inayoingia na wakandarasi/wazabuni na kuzingatia masharti ya mikataba.

Pia, nashauri menejimenti ya Taasisi za Umma itambue kuwa pamoja na TBA kupewa jukumu la kujenga nyumba za Serikali inatakiwa ifuate masharti ya mikataba pamoja na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 na Kanuni zake za 2013.

### 9.1.6 Mapungufu Yaliyobainika katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka

Kifungu cha 49(2&3) cha Sheria ya Manunuzi Na.7 ya mwaka 2011 kinaelekeza mamlaka ya bajeti kuidhinisha mpango wa manunuzi wa mwaka wa taasisi ya kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa. Kifungu hiki kinafafanua kuwa, taasisi ya manunuzi inapaswa kufanya manunuzi kwa mujibu wa mpango wa mwaka wa manunuzi na manunuzi yoyote ambayo hayakupangwa yanapaswa kupata barua ya idhini ya Afisa Masuuli wa taasisi ya Umma.

Katika kupitia mchakato wa manunuzi ya Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Balozi nilibaini manunuzi yenye thamani ya Shilingi 501,495,718 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi kinyume na kifungu tajwa hapo juu. Jedwali namba 9.3.

**Jedwali Na. 75: Manunuzi yenye Mapungufu katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka**

Na	Fungu mapungufu yalyobainika	Kiasi Sh.
1	Fungu 96 Wizara ya Habari, Utamaduni, sanaa na Michezo: Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ulikuwa Shilingi 20,000,000 lakini manunuzi yaliyo fanyika ya vitu mbalimbali ni ya thamani ya Shilingi 89,828,224. Tofauti ya manunuzi hayakuwepo kwenye mpango wa manunuzi	69,828,224
2	Kifungu kidogo 2024 Ubalozi wa Tanzania Riyadh Saudi Arabia; Manunuzi ya vifaa vya kudumu (Non currents assets) kwa matumizi ya Ofisi na kwenye makazi ya wafanyakazi, gharama za kumbi, n.k ambavyo havikuwemo katika mpango wa manunuzi wa mwaka.	57,560,294

Na	Fungu mapungufu yalyobainika	Kiasi Sh.
3	Fungu 23 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali: Katika Zabuni Na. IE/031/2016-2017/HQ/C/05 kwa ajili ya huduma ya ushauri kwa Wahasibu 250 wa Serikali kuu, serikali za mitaa na idara zinazo jitegemea. Menejimenti iliweka kwenye mpango wa Manunuzi wa mwaka kwa mchakato wa ushindanishi wa kimataifa ukabadilishwa na kuwa wa kutoshindanishwa bila idhini ya bodi ya Zabuni kinyume na Kanuni 149 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 (kama ilivyorekebishwa 2016),	374,107,200
	Jumla	501,495,718

*Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2016/2017*

Nimebaini kuendelea kuimarika kwa uzingatiaji wa sheria hii katika taasisi za Serikali Kuu. Manunuzi yaliyofanyika kinyume na Mpango wa Manunuzi yamepungua hadi kufikia asilimia 49%, kutoka Shilingi 980,345,532 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Shilingi 501,495,718.

Nazishauri Taasisi husika zizingatie kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ili kuweza kuboresha zaidi mchakato mzima wa manunuzi katika taasisi za Umma.

#### **9.1.7 Mapokezi ya Vifaa Visivyofanyiwa Ukaguzi vyenye thamani ya Shilingi 1,688,784,207.90**

Katika mwaka huu wa ukaguzi, jumla ya Taasisi kumi na nne (14) zilifanya manunuzi ya vifaa vyenye thamani ya Shilingi 1,688,784,207.90 bila ya kukaguliwa na kupokelewa kinyume na Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 ambayo inaelekeza kuwa manunuzi yote yanayofanywa na taasisi za umma yanapaswa kukaguliwa ili kuweza kubaini kama yamefikia vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba.

Kwa nyongeza, Kanuni ya 245 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inamtaka Afisa Masuuli kuteua Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya vifaa ambayo itawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea pindi zinaponunuliwa

kutoka kwa Wazabuni. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye kiambatisho 9.4

Nimeona kwa wastani fulani kuna mabadiliko katika uzingatiaji wa sheria hii ambapo katika ripoti za ukaguzi zilizopita mwaka 2014/2015 kulikuwa na Taasisi kumi na sita (16) zilifanya manunuvi ya bidhaa na huduma yeye thamani ya Shilingi 15,361,328,135; taasisi tisa (9) manunuvi ya Sh 2,315,756,038 kwa mwaka 2015/2016 wakati mwaka wa 2016/2017 kuna manunuvi kumi na nne (14) ya taasisi yeye thamani ya Shilingi 1,688,784,207,90 iliyofanywa bila ya ukaguzi kufanyika wakati wa kupokea bidhaa. ea vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya Vifaa na Huduma kunaweza kukatoa fursa kwa taasisi za umma kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango vya ubora au zisizofuata mahitaji muhimu ya Manunuvi.

Ili kuweza kukabiliana na matukio ya ukiukwaji wa Sheria za Manunuvi katika Taasisi za Serikali Kuu, nazishauri Wizara, Idara Wakala na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kunakuwa na Kamati ya Uhakiki na Kukubali wakati huo huo kufuata Kanuni. 244 (1) ya Kanuni ya Manunuvi ya Umma 2013 na Kanuni. 245 ya Kanuni ya Manunuvi ya Umma 2013

#### **9.1.8 Huduma Zilizolipiwa Lakini Hazikupokelewa Shilingi 52,678,585,370**

Katika Taasisi za Serikali Kuu nane (8) nilizokagua, nilibaini manunuvi ya vifaa na huduma yeye thamani ya Shilingi 161,657,467,370 viliyoagizwa na kulipiwa lakini havikupokelewa; hivyo, thamani ya fedha haikupatikana. Bila ya kupata thamani ya fedha, manunuvi yatahesabika kama yamepotea. Hii ni kinyume na Makubaliano ya Mikataba kati ya Wazabuni na Taasisi za Manunuvi ambayo inataka malipo kufanyika baada cheti cha kazi kutolewa, bidhaa kuletwaa au huduma kutolewa. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye kiambatisho 9.5

Kutokana na mapungufu katika manunuzi, sikuweza kuthibitisha malipo yaliyofanywa. Hii ni Kwa kuwa sikiweza kujiridhisha kama huduma na bidhaa vilitolewa kwa kiasi cha kuridhisha.

Ikilinganishwa na mwaka wa Ukaguzi 2015/2016, Taasisi za Serikali Kuu zilizobainika na mapungufu haya ni nane (8) ambapo kwa mwaka huu pia ni Taasisi nane (8). Ila kiasi cha fedha kimeongezeka toka Shilingi 3,452,112,838 kwa mwaka 2015/16 hadi Shilingi 52,678,585,370 kwa mwaka 2016/2017, ikiwa ni ongezeko la shilingi 49,226,472,532. Ongezeko hilo kubwa limetokana na Shilingi 51,838,352,600 ambazo Serikali imelipa gharama ya manunuzi ya ndege aina ya Q400. Bila ya kupokea bidhaa na huduma zilizolipiwa, manunuzi yatahesabika kama yamepotea. Hii ni kinyume na makubaliano ya mikataba kati ya Wazabuni na Taasisi za Manunuzi ambayo inataka malipo kufanyika baada ya cheti cha kazi kutolewa, bidhaa kuleta au huduma kutolewa.

Napendekeza kwamba menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu zijitahidi kufuatilia uletwaji wa vifaa vyote. Na inaposhindikana zihakikishe fedha zilizolipwa zinarejeshwa kutoka kwa Wazabuni na Wakandarasi, na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale walioshindwa kuleta vifaa na huduma.

#### **9.1.9 Kucheleta Kukamilika kwa Miradi ya Ujenzi yenye thamani ya Shilingi 21,877,102,830.86**

Jumla ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kumi na tatu (13) ziliingia katika makubaliano ya Mikataba na Wakandarasi katika ujenzi wa miradi mbalimbali. Nilibaini kucheleta kukamilika kwa miradi hii yenye thamani ya Shilingi 21,877,102,830.86 kinyume na muda ulioainishwa kwenye mikataba.

Kiambatisho 9.6 kinaonesha taasisi, miradi husika na muda uliocheleweshwa

Kucheleta kukamilika kwa miradi kunaweza kusababisha Serikali kuingia gharama zisizo za lazima zinazotokana na mfumuko wa bei pamoja na kuongezeka kwa gharama za vifaa. Menejimenti za taasisi husika zinashauriwa kuzingatia matakwa ya Kanuni 114

ya Manunuzi ya Umma ya 2013 na katika usimamizi wa mikataba ya manunuzi.

Menejimenti inashauriwa kusimamia kikamilifu mikataba inayoendelea ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati bila kuchelewa. Nazishauri Taasisi ziendelee kufanya juhudzi za ufuatiliaji rasilimali fedha kutoka Hazina ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa katika bajeti. Nashauri pia miradi yenye fedha kidogo itekelezwe kwa hatua ili kurahisisha usimamizi wa miradi na ulipaji wake. Zaidi ninapendekeza ujenzi ufanyike kwa awamu ili kuwezesha kulipa madeni ili kuweza kuepuka kulipa gharama kwa riba.

#### **9.1.10 Manunuzi kwa kutumia Masurufu Shilingi 1,224,684,689**

Ili kuhakikisha mchakato wa manunuzi unafuata kanuni za msingi wa uwazi, ushindani, uchumi, ufanisi, usawa na uwajibikaji; Kanuni ya 166 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inaeleza bayana manunuzi madogo madogo yanaweza kufanyika moja kwa moja kutoka maduka makubwa yanayotambulika, maduka au stoo za dawa, kama thamani ya manunuzi haizidi kikomo kilichowekwa katika jedwali la saba la Kanuni hizi. Taasisi inayofanya manunuzi inaweza kutumia masurufu au kadi ya manunuzi kufanya manunuzi madogo madogo. Kikomo cha manunuzi madogo kilichoruhusiwa ni chini ya Shilingi 5,000,000.

Ukaguzi ulibaini taasisi sita (6) za serikali kuu kufanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi 1,224,684,689 kwa njia ya masurufu au maofisa wa taasisi kulipwa fedha taslimu kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma kama ilivyoneshwa kwenye kiambatiosho 9.7 kinyume na Kanuni 166 ya kanuni za manunuzi ya umma za mwaka 2013

Nashauri taasisi za umma kuzingatia kikamilifu sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 pamoja na kanuni ya 166 ya kanuni za manunuzi za 2013 ili kuweza kuhakikisha kunakuwapo kwa uwazi na thamani ya fedha katika manunuzi ya serikali.

**9.1.11 Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa katika vitabu vyenye thamani ya Shilingi 501,853,534.20**

Kanuni ya 198 na 203 ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2001 zinahitaji kupokea bidhaa, kutoa bidhaa na kiasi cha bidhaa kilichobaki stoo kwa kila aina ya bidhaa taarifa zake zioneshwe kwenye kurasa tofauti katika leja za stoo. Wakati wa ukaguzi wangu, nilishindwa kuthibitisha matumizi ya bidhaa zenye thamani ya Shilingi 501,853,534.20 zilizonunuliwa na taasisi 8 zilizokaguliwa kutokana na kutokuwapo kwa kumbukumbu sahihi katika leja za stoo na daftari la kudhibiti mwenendo wa matumizi ya gari na matumizi ya mafuta baada ya kupokelewa. Orodha ya taasisi zenye bidhaa ambazo hazikuingizwa katika vitabu zimeoneshwa katika **Kiambatisho 9.8**

Ulingenisho wa utendaji wa Taasisi za Serikali Kuu kwa miaka miwili unaonesha kwamba mwaka wa fedha wa 2015/2016 ni Taasisi nane (8) ambazo zilifanya vibaya ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 ni Taasisi kumi na nne (14). Kwa hiyo, Taasisi sita (6) zimeongezeka ikilinganishwa na mwaka jana, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 75%.

Kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za stoo jinsi bidhaa na mafuta yalivyotumika sikuweza kujua namna manunuzi na matumizi ya bidhaa/mali zilizolipiwa.

Kutokana na kuwapo kwa kiasi kikubwa cha fedha za umma zilizotumika kununua vifaa na mafuta ambavyo havikuingizwa popote, napendekeza kwamba uingizaji wa mali/bidhaa ufanyike kwa wakati katika leja kuimarishwe ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali katika kutoa huduma kwa wakati kwa watumiaji wa vifaa vya stoo na kuingiza mafuta katika daftari la kuratibu mwenendo wa Gari na matumizi ya mafuta.

**9.1.12 Taarifa ya PPRA - Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2011 na Kanuni zake za, 2013**

Kutokana na mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 9(1)(i)cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 ,Mamlaka ya

Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ilifanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara na Idara za Serikali zipatazo 17. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kubainisha kama taratibu, mfumo na kumbukumbu za kuingia mikataba ilifanyika kufuatana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 na Kanuni zake za 2013 na fomu ya mkataba iliyoidhinishwa na PPRA na kama manunuzi yalifanywa kuzingatia uchumi, ufanisi na tija yaani kuweza kupata thamani ya fedha.

Yafuatayo ni matokeo ya ripoti ya ukaguzi uliofanywa na PPRA:

#### **9.1.12.1 Matokeo ya Ukaguzi ya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi**

Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi (PPRA) ilifanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi kwa kutumia vigezo saba kama ifuatavyo: Kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi na utendaji kazi wake, kuandaa na kutekeleza Mpango wa Manunuzi wa mwaka, usahihi katika mchakato wa Zabuni, usimamizi wa Mikataba, Utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi, kutumia mifumo ilioanzishwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma; ufuatiliaji wa Malalamiko.

#### **9.1.12.2 Kiasi cha Manunuzi Yaliyokaguliwa**

Jumla ya mikataba ya manunuzi iliyofanywa ukaguzi na PPRA ni 9,280 yenye thamani ya fedha Shilingi bilioni 1,863.72. Kati ya mikataba hiyo, 644 ilikuwa ya kazi zenye thamani ya Shilingi bilioni 1,329.88 au asilimia 71.40 ya jumla ya mikataba yote; mikataba 1,732 ilikuwa ya vifaa na bidhaa mbalimbali yenye thamani ya Shilingi 219.72 bilioni ikiwa ni asilimia 11.80 ya jumla ya thamani ya mikataba yote na mikataba 131 ni ya huduma ya ushauri ya thamani ya fedha ya Shilingi bilioni 103.52 sawa na asilimia 5.60 ya jumla ya mikataba mikataba yote. Pia Mamlaka ya usimamizi wa Manunuzi ilifanya ukaguzi wa mikataba mengine ikiwa ni pamoja na mikataba 831 ambayo ni ya huduma ambazo siyo ya kiuchauri ya Shilingi bilioni 154.76 au 8.30%, na mikataba midogo midogo 5,942 ya thamani ndogondogo ya Shilingi bilioni 54.76 sawa na 2.90%

### 9.1.12.3 Viwango vya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi

Uchambuzi unaonesha, kuwa wastani uliofikiwa wa uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ulikuwa wa kiwango cha asilimia 80%, kwa Serikali yote na Taasisi zake, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9% ikilinganishwa na mwaka jana ambapo ilikuwa asilimia 71%.

Wastani wa asilimia 80% uko sawa na kigezo kilichowekwa cha uzingatiaji kwa mwaka 2016/2017. Uzingatiaji huo mzuri umejikita katika eneo la vigezo viwili ambavyo ni kuwapo kwa mfumo wa manunuzi katika taasisi pamoja na utendaji na ufanisi wa mchakato wa zabuni. Hata hivyo, uzingatiaji ulikuwa chini ya kiwango katika eneo la maandalizi na utekelezaji wa mipango ya manunuzi; usimamizi wa mikataba na utekelezaji; usimamizi wa kumbukumbu za manunuzi pamoja na utekelezaji wa mifumo ya PPRA.

Wastani wa uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Serikali kuu pekee pamoja na Taasisi zake ulikuwa asilimia 81% zaidi ya kigezo cha asilimia 80% kilichowekwa, ikiwa umeongezeka kutoka mwaka jana toka asilimia 75% hadi asilimia 81% sawa na ongezeko la asilimia 6%. Uchambuzi pia unaonesha kuwa Serikali kuu na Taasisi zake zilifanya vizuri katika eneo la kuweka mfumo wa manunuzi katika Taasisi na utendaji wa uzingatiaji wa sheria ulikuwa asilimia 81%. Katika eneo la Ufanisi wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka, maandalizi na utekelezaji, Taasisi za Serikali kuu zilipata asilimia 80% sawa na kigezo kilichowekwa kwa mwaka huu, ambacho kilikuwa ni kiwango cha kuridhisha. Kwa upande wa Mchakato wa kuendesha zabuni nao ulikuwa wa kuridhisha, ambapo zilipata asilimia 87%.

Uchambuzi vile vile umeonesha kuwa Taasisi za Umma za serikali Kuu zilifanya vibaya katika kutekeleza mfumo wa PPRA, ambapo zilipata asilimia 52% ambayo ni chini ya kigezo kilichowekwa cha asilimia 80%.

### 9.1.12.4 Uchunguzi wa Tuhuma, Malalamiko pamoja na Taarifa Zinazowasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti na

### **Manunuvi ya Umma kutokana na Manunuvi yenye Mapungufu**

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Manunuvi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinatoa Mamlaka kwa PPRA kufanya uchunguzi inapotokea tuhuma za Manunuvi yenye mapungufu. Uchunguzi unaweza kufanywa na PPRA kwa kutumia juhudi binafsi au kupitia tuhuma zilizowasilishwa kwa Mamlaka.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mamlaka ilifanya uchunguzi katika Taasisi nane (8) zenyetikana kumi (10) ya thamani ya Shilingi 280 bilioni. Uchunguzi huo ulifanyika kutokana na maelekezo kutoka ngazi za juu na zingine Taasisi zenyewe ziliomba uchunguzi huo ufanyike kwenye Taasisi zao.

Hata hivyo, Taasisi za Serikali kuu zilizofanyiwa uchunguzi ni tatu kati ya nane zilizofanywa na PPRA. Kwa hiyo, Mamlaka ya Manunuvi na Udhibiti wa Umma ilifanya chunguzi katika Taasisi za Serikali kuu kama ilivyooredheshwa hapa chini:

#### **Jedwali Na. 76: Taasisi zilizotakiwa kufanyiwa uchunguzi na PPRA**

Na	Taasisi	Idadi ya chunguzi	Idadi ya Tenda
1	Mamlaka ya vitambulisho (NIDA)	1	1
2	Mamlaka ya Mapato (TRA)	1	1
3	Wizara ya fedha na Mipango (MoFP)	1	1
	Jumla	3	3

*Chanzo: Ripoti ya PPRA ya mwaka 2016/2017*

**Muhtasari wa Matokeo ya Uchunguzi Ulifanyiwa na PPRA katika Taasisi ya Umma NIDA na TRA kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni kama ifuatavyo;**

#### **1) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

Kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 kwenye Mpango wa Manunuvi wa NIDA kulikuwa na Zabuni Na.AE/061/2016-2017/HQ/G/01 zenyetikana loti 3, Loti 1 likuwa ni kununua vifaa vifuatavyo; komputa ya mezani, komputa mpakato, mashine ya

kurudufu, printa na skana kwa njia ya makubaliano ya mfumo wa manunuzi); Loti ya pili ilikuwa ni manunuzi kwa njia ya makubaliano ya mfumo wa manunuzi. Loti ya tatu ilikuwa ni kununua na kusimika printa kubwa yenye uwezo wa kufanya kazi ngumu kwa njia ya manunuzi ya ushindanishi wa kimataifa (ICB).

- i. Wakati wa utekelezaji wa manunuzi hayo yenye loti 3 katika Mpango wa Mwaka wa Manunuzi, NIDA walibadilisha ikawa katika Loti moja na kuitwa zabuni ya kununua, kusimika na matengenezo ya mashine.
- ii. Hapakuwa na ushahidi ulioonesha kama mabadiliko hayo yalipata kibali cha Afisa Masuuli inavyotakiwa na Kanuni za Manunuzi. Pia, hapakuwa na ushahidi kwamba Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ulirekebishwa ili kuingiza mabadiliko yaliyofanywa.
- iii. Hakuna tathimini ya mahitaji iliyofanyika, kwa hiyo NIDA haikubainisha kiasi halisi cha vifaa vilivyokuwa vinatakiwa na wapi kwa kuviweka. Ratiba ya mahitaji haikuwa na maelezo ya kiasi kama inavyotakiwa kwenye hati ya zabuni. Kwa hiyo, kupelekea bei isiyo ya kweli kwa wazabuni.
- iv. NIDA haikuweka vifaa vinavyohitajika kwa hiyo ikawa vigumu kujua vifaa halisi vilivyokuwa vihitajika ambayo wazabuni wanetakiwa kunukuu.
- v. Baadhi ya vifungu vya hati ya Zabuni havikuwekwa vizuri kulingana na zabuni yenyewe.
- vi. Hapakuwa na ushahidi wa Bodi ya Zabuni kuidhinisha mabalidiko ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni.
- vii. NIDA haikuweza kuwasiliana na wazabuni juu ya mabadiliko ya bei.
- viii. Mzabuni aliyependekezwa hakukidhi baadhi ya vigezo vilivyokuwa vinahitajika kwenye zabuni.
- ix. Idara ya manunuzi haikurudishia timu ya tathmini ripoti ya tathmini kwa ajili ya marekebisho baada ya kuona

mapungufu, badala yake walipeleka moja kwa moja kwenye Bodi ya Zabuni.

Maamuzi yaliyofanywa na PPRA baada Uchunguzi Kufanyika: NIDA inatakiwa kuanza upya mchakato wa manunuvi

## **2) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**

Uchunguzi ulifanyika katika Usimamizi wa Mfumo wa Mapato ya ndani. Uchunguzi huo ulifanyika kutokana na ombi la TRA juu ya zabuni iliyofanyika mara nne baada ya kulalamikiwa na watu kwamba uligubikwa na taratibu ambazo hazikuzingatia taratibu za manunuvi. Yafuatatayo ni mapungufu yaliyoibuliwa na PPRA katika uchunguzi wa zabuni ya TRA ambapo ilibainika kwamba;

- i. Hapakuwa na tathimini ya kina ya mahitaji iliyofanywa na TRA kabla ya kuanza huo mradi;
- ii. TRA haikuomba ushauri wa kitaalam kutoka Wakala wa Kielektroniki wa Serikali ili kupata mwongozo wa matumizi ya ufanisi na Matumizi ya teknolojia ya mtandao kwa Taasisi ya Umma;
- iii. Hati ya zabuni haikuandaliwa vizuri, maana haikuainisha bayana muda maalum wa kufanya majoribio;
- iv. Uteuzi wa mjambe mmoja wa timu ya tathmini haukuzingatia matakwa ya Sheria ya Manunuvi ya Mwaka 2011;
- v. Tathmini ya zabuni haikufanyika vizuri; na
- vi. Majoribio ya moja kwa moja hayakuweza kufanyika na kusimamiwa ipasavyo.
- vii. Maamuzi yaliyofanywa na PPRA baada Uchunguzi Kufanyika:
- viii. TRA iliagizwa kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wote waliohusishwa na tuhuma kwa kukiuka sheria ya Manunuvi ya Umma ya Mwaka 2011.

- ix. TRA iliagizwa ifidie gharama za kurudia mchakato wa zabuni kutoka kwa Maofisa waliosababisha hiyo hasara ya kurudia; na
- x. Kuanza upya mchakato wa zabuni hiyo.

### **3) Wizara ya fedha na Mipango (MoFP)**

Katika uchunguzi uliofanyika kwenye Taasisi za Serikali Kuu juu ya mchakato wa manunuzi ulivyofanyika katika Wizara ya fedha na Mipango (MoFP), PPRA ilichunguza na ilibainika kuwa mchakato wa manunuzi uliofanyika haukuwa na dosari. Hivyo, iliamriwa kuwa mradi huo uendelee kutekelezwa kama kawaida kwa kuwa hapakuwa na doasari zozote zilizobainika katika uchunguzi huo.

#### **9.1.12.5 Ushauri wa Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi (PPRA)**

Kama nilivyoshauri katika kagazi za nyuma nashauri tena kuwa hatua stahiki ziweze kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa umma ambao wamebainika kuwa na tabia ya kujihusisha na kufanya udanganyifu na ulaghai katika manunuzi.

Ili kuhakikisha kwamba Taasisi za Umma zinafanya vizuri katika kufanya na kusimamia mchakato wa manunuzi na usimamizi wa miradi na mikataba nashauri wafanyakazi wa umma katika ngazi mbalimbali wawezeshwe kwa kupewa mafunzo ili kuboresha utendaji wa kazi.

Pia, nashauri kwamba Taasisi zote ambazo utendaji wake uko chini ya asilimia themanini (80) ya lengo lililowekwa ziandae mafunzo kwa wafanya kazi wao ya namna ya kutumia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011, Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2013, na Miongozo na maelekezo mbalimbali yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi (PPRA).

#### **9.1.12.6 Taarifa ya Kurugenzi ya Uhakiki Mali za Serikali, Mapungufu katika Manunuzi na Utunzaji wa Bohari/Stoo**

Ikiwa sehemu ya wajibu wangu, nimepokea taarifa kutoka Kurugenzi ya Uhakiki Mali za Serikali yenye Mapungufu katika manunuzi na utunzaji wa bohari/stoo kama ilivyo kwa mujibu wa Kanuni 239-249 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001, Mhakiki Mali wa Serikali anatakiwa kufanya uhakiki wa mali katika bohari/stoo za taasisi za umma na kutoa taarifa kutohana na uhakiki huo.

Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Mhakiki Mali wa Serikali alifanya uhakiki wa mali na matokeo ya uhakiki huo uliofanyika ni kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho 9.9 (a) na (b) pamoja na Kiambatisho Na.9.10 Kinachoonesha Taasisi zilizopata hoja mbalimbali za Mhakiki Mali wa Serikali..

Hoja zilizoripotiwa na Mhakiki Mali ni za msingi sana ili kuwa na usimamizi unaostahili wa mali za Serikali katika Taasis za Umma, ambapo mali ya umma isiposimamiwa ipasavyo inaweza kusababisha upotevu wa raslimali.

Maafisa Masuuli wanashauriwa wawe na usimamizi madhubuti kwa kutimiza wajibu wao na kuhakikisha wanaondoa mapungufu yote yaliyobainishwa na Mhakiki Mali wa Serikali.

Ili kuweza kupunguza au kuepusha hasara ya mali kwa njia ya wizi, ufujaji au utumiaji mbaya wa matumizi, ninashauri uongozi wa Taasis za Umma uimarishe mfumo wa ndani kwa kuhakikisha bidhaa, vifaa na mafuta vinaponunuliwa viingizwe kwenye leja la mapokezi na kutolewa kwenye leja ya kutolea na pia kwa upande wa mafuta licha kuingizwa kwenye leja ya mafuta, yaingizwe kwenye leja ya kudhibiti mwenendo wa safari za gari na viweze kupatikana wakati wowote vinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi.

## SURA YA KUMI

### **10.0 USIMAMIZI WA MATUMIZI**

#### **10.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu matokeo niliyobaini katika ukaguzi wa matumizi ya fedha yaliyofanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Balozi na Sekretarieti za Mikoa (RSs) katika mwaka wa fedha 2016/2017. Muhtasari wa matokeo muhimu ya Ukaguzi na Mapendekezo niliyoyatao ni kama ifuatavyo:

#### **10.2 Ubadhirifu wa Fedha-Ubalizi wa Tanzania-Maputo-USD 150,000 (Tzs 332,856,000)**

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu wa Ubalizi wa Tanzania-Maputo kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, mapitio ya Taarifa ya Fedha katika kipindi hicho yamebaini ubadhirifu wa fedha wa kiasi cha Dola za Kimarekani 150,000 (Sh.TZ.332,856,000)<sup>28</sup> ambacho kilihamishwa kutoka katika akaunti ya Ubalizi. nambari 79667362 yenye jina Millennium bin Julius Nyerere Prestige kwenda akaunti binafsi No.182283177 iliyoko katika benki hiyo na ikimilikiwa na mhasibu wa Ubalizi. (Jedwali la hapa chini linaonesha miamala hiyo). Mapungufu yaliyobainika ni :

- i. Kutokuwapo kwa hati ya malipo wala viambatisho vyake vilivyowasilishwa kwa ukaguzi, hivyo imenipelekea kutoweza kubaini uhalali, uhalsia, aina na madhumuni ya matumizi hayo.
- ii. Taarifa ya benki iliyokuwa imeambatishwa kwenye Taarifa ya uwianish wa Kibenki haikuwa imesainiwa na afisa wa Benki husika; vilevile, taarifa inayoshukiwa haikuwemo katika Taarifa hiyo ya Benki.
- iii. Taarifa ya uwianishi wa Benki ya Mwezi Februari 2017 na Aprili 2017 haikuwasilishwa kwa Wakaguzi kwa Uhakiki

---

<sup>28</sup> BOT kiwango cha kubadilisha fedha 30/06/2017= Tzs/USD 2,219.04

**Jedwali Na. 77: Miamala ya uhamisho wa Fedha kutoka Akaunti ya Amama kwa ubadhirifu**

Na.	Tarehe	Maelezo	Kiasi (USD)
1	26/10/2016	Joyce Moshi INSTR 1610055161-61026152517019	10,000
2	14/02/2017	Joyce Moshi INSTR170202145-170214112406795	100,000
3	13/04/2017	Joyce Moshi INSTR170401991-170413135739559	40,000
<b>Jumla</b>			<b>150,000</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Katika suala hili, Menejimenti ya Ubalozi ilikubali kuwa, Miamala iliyoripotiwa na Timu ya Ukaguzi yenye thamani ya dola za Kimarekani 150,000 ilikuwa na udanganyifu na imesharipoti suala hili kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa hatua zaidi. Wakati huo huo, tuhumiwa anashikiliwa ili kujibu tuhuma. Mwezi Januari 2018 suala hilo lilifikishwa mahakamani.

Ninaamini kwamba, Udhibiti wa Mfumo wa Ndani usiotosheleza kama uwianishii huru wa benki na utenganisho wa majukumu ya Watumishi upande wa Ubalozi umesababisha udanganyifu huu kutokea.

Ninapendekeza Menejimenti ya Ubalozi kwa kushirikiana na taasisi/mamlaka husika za kiuchunguzi kukamilisha jambo hilo kwa lengo la kurejesha kiasi kilichopotea.

**10.3 Matumizi Yasiyokuwa na Manufaa - Shilingi 61,793,117**

Ukaguzi wa hati za malipo na viambatisho vyake ulibaini kuwa Taasisi tatu (3) zilifanya malipo kiasi cha Shilingi milioni 61.793 ambayo yalifujwa na hayakuwa na manufaa yoyote kwa Serikali; ambapo, hasara hiyo ingeepukwa laiti kama hatua stahiki zingefuatwa kwa umakini kabla matumizi hayo kufanyika kama inavyoainishwa katika Kanuni 21 ya Kanuni za Fedha, 2001. Taasisi zilizolipa malipo yasiyokuwa na manufaa zinaonekana kwenye **Jedwali** hapo chini:


### Jedwali Na. 78: Matumizi Yasiyokuwa na Manufaa - Shilingi 61,793,117

Na	Fungu na.	Taaasisi	Kiasi	Maelezo
1	55	Kamisheni ya Haki za Biinadamunaaaa Utawala Bora	1,399,214	Adhabu ya kuchelewa kulipa pango
2	99	Wizara ya Kilimo Mifugo na uvuvi	9,000,000	50% Adhabu ya Menejimenti kuchelewa kulipa ,michango ya kila mwezi ya PSPF
3	72	Sekretariati ya Mkoa wa Dodoma	51,393,903	Riba ya kuchelewesha Malipo ya Cheti cha Mkataba namba RAS/002/W/2013/2014/13 wa ujenzi na ukarabati wa makazi ya Mkuu wa Wilaya za Kongwa na Kondoa pamoja na ukarabati wa makazi ya Katibu Tawala wa Mkoa
		Jumla	61,793,117	

Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017

Ulinganisho na mwenendo wa Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na manufaa kwa miaka minne iliyopita:

### Kielelezo Na. 23: Mwenendo wa miaka 5 wa malipo yasiyokuwa na manufaa



Ulinganisho wa hapo juu unaonesha kupungua kwa malipo yasiyokuwa na manufaa kutoka Shilingi milioni 1,460.57 kwa mwaka 2015/2016 hadi Shilingi milioni 61.793 kwa mwaka huu 2016/2017. Pia, idadi ya Taasisi zilizohusika zimepungua kutoka

6 hadi 3 mwaka huu. Pia, mwenendo kwa ujumla kwa miaka minne iliyopita unaonesha kupungu kwa tatizo hili hivyo kuashiria kuimarika kwa udhibiti wa ndani na umakini kabla ya malipo kufanyika. Ninapendekeza kuwa Manejimenti za Wizara husika & Sekretarieti za Mikoa waimarishe mifumo yao ya udhibiti wa ndani kukabili changamoto hii.

#### **10.4 Hasara ya Shilingi 343,616,421 iliyotokana na NHIF kutozilipa hospitali zenyenye madai ya bima ya afya yenye dosari**

Katika kupitia madai ya Hospitali za Serikali wanayoidai NHIF yatokanayo na huduma za matibabu walizowapatia wanachama wa Mfuko, nilibaini kuwa, Mfuko huo ama ulipunguza au ulikataa kuyalipa madai ya kiasi cha Shilingi milioni 343.616. Hali hiyo ilitokea na madai hayo Kanuni ya 27(2) ya Sheria ya NHIF ya Mwaka 1999 kutokana na hospitali husika za Serikali kukiuka bila sababu za msingi taratibu, Kanuni, sheria na mikataba walioingia, hivyo kwa kutolipwa fedha hizo kutasababisha hospitali hizo kupata hiyo hasara.

Kwa sehemu kubwa, mapungufu yametokana na ujazwaji fomu za NHIF zikiwa na mapungufu kama vile kukosekana kwa sahihi za daktari ama mgonjwa, kukosekana kwa taarifa ya uchunguzi wa kitabibu matibabu yaliyotolewa, utoaji tiba na dawa zilizo nje ya wigo ulioruhusiwa na NHIF, utoaji wa huduma kwa wagonjwa ambao uanachama wao umekoma, madai zaidi ya mara mbili, idadi isiyo sahihi ya siku za kulazwa, kukosekana kwa maelezo sahihi ya tiba zilizotolewa n.k.

Taasisi zilizokutwa na mapungufu hayo ni kama jedwali linavyoonesha hapa chini:

**Jedwali Na. 79: Taasisi zenyenye madai yaliyokataliwa na NHIF**

na	Jina la Taasisi	Kiasi Sh.TZ
1	Fungu 47-Sekretarieti ya Mkoa- Simiyu	12,136,255
2	Fungu 72-Sekretarieti ya Mkoa- Dodoma	117,725,645
3	Fungu 73-Sekretarieti ya Mkoa-Iringa	42,690,080
4	Fungu 82-Sekretarieti ya Mkoa- Ruvuma	40,713,770
5	Fungu 84-Sekretarieti ya Mkoa- Singida	19,241,998

na	Jina la Taasisi	Kiasi Sh.TZ
6	Fungu 86-Sekretarieti ya Mkoa-Tanga	71,006,895
7	Fungu 87-Sekretarieti ya Mkoa- Kagera	18,292,572
8	Fungu 89-Sekretarieti ya Mkoa- Rukwa	12,286,570
9	Fungu 95-Sekretarieti ya Mkoa- Manyara	9,522,636
	<b>Jumla</b>	<b>343,616,421</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Ikilinganishwa na Mwaka 2015/16, kiwango cha hasara itokanayo NHIF kutolipa madai ya marejesho ya gharama za matibabu kwa sababu mbalimbali kimepungua kutoka Sh.TZ 569,995 milioni hadi 343,616 milioni kwa mwaka huu wa Fedha 2016/17 ikihusisha pia kupungua kwa idadi ya Taasisi zilizohusika kutoka 10 hadi 9.

Ninashauri hatua zaidi ziendelee kuchukuliwa kurekebisha kasoro hii; vinginevyo, hospitali hizi zitaelemewa na mzigo mkubwa wa hasara ya gharama za kutibu wanachama wa Mfuko wa NHIF bila mfuko huo kuzirejesha fedha hizo.

Narejea tena ushauri wangu kuwa Wizara zinazohusika, kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa NHIF, kuweka katika hospitali zote kubwa za Serikali angalau mtumishi mmoja wa NHIF ambaye pamoja na majukumu mengine, atakuwa akisimamia utekelezaji wa udhibiti wa ndani na pamoja na kuzikagua na kuhakiki uanachama na kuhakikisha kuwa fomu zimekidhi viwango kabla ya matibabu kutolewa.

#### **10.5 Malipo Yaliyolipwa zaidi Kiwango Stahiki-Shilingi 306,376,812**

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu 2015/16, nilibaini malipo ya kiasi cha Shilingi Shilingi 306,376,812 yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki yakihusisha Taasisi sita (6) za Serikali kuu. Fedha zilizolipwa zaidi ya kiasi kinachostahili au kwa kazi ambazo hazijafanyika zinasababisha kutofanikisha kwa shughuli nyingine zenye manufaa kwa Umma. Malipo zaidi ya kiasi kilichostahili ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapa chini:


**Jedwali Na. 80: Taasisi zilizolipa zaidi ya malipo ya stahiki**

s/n	Jina la Taasisi	Kiasi	Mapungufu Yaliyobanika
1	Fungu 71- Sekretarieti ya Mkoa- Pwani	9,898,130	Kiasi cha 10,043,000 kilicholipwa kwa PPF kwa mwezi wa Januari 2017 kama makato Hata hivyo kiwango stahiki kilipaswa kuwa Sh.Tz 144,900 hivyo kupelekeea kilicholipwa kuzidi kiwango stahiki kwa 9,898,130
2	Fungu 87- Sekretarieti ya Mkoa- Kagera	8,760,000	Menejimenti ya Sekretarieti ililipa gharama za chakula kwa watu 250 X Siku 10 badala ya siku 8 kama ilivyoonesha kwenye daftari ya Mahudhurio kusababisha ziada ya Shilingi 8,760,000
3	Fungu 2005- Ubalozi wa Tanzania-Abuja	3,000,000	Kiasi hiki kililipwa zaidi ya kiwango stahiki kwenye mkataba wa zabuni ya manunuzi ya kamera za CCTV
4	Fungu 2014- Ubalozi wa Tanzania-Beijing	114,770,538	Kiasi hiki kililipwa kwa maafisa Ubalozi wawili kama gharama za uhamisho zaidi ya kiwango stahiki kwa Shilingi 23,370,156 (EURO 10,450.04) na Shilingi 8,134,751 (Euro 3,637.48) mtawalia pia Ziada ya RMB 238,440 (83,265,631) kililipia ada ya shule ya watoto wa Wafanyakazi wa Ubalozi
5	Fungu 48-Wizara ya Ardh, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	149,411,850	Kiasi kilicholipwa zaidi ya bei stahiki ya mkataba kwa ajili ya huduma ya ushauri kwa ajili ya maandalizi ya Ramani ya Mpango Mji wa Arusha na Mwanza
6	Fungu 42-Ofisi ya Bunge (Fungu 42)	20,536,294	Menejimenti ya Bunge ililipia gharama za usafiri, malazi na bima kwa wajumbe wawili waliohudhuria semina nchini Finland licha ya semina kufadhili kikamilifu na Serikali ya Finland, hivyo kupelekeea malipo kufanyika mara mbili zaidi.
		306,376,812	

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Chati inayoonesha Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki kwa miaka sita (6) iliyopita ni kama inavyoonekana kwenye Kielelezo hapa chini:

### Kielelezo Na. 24: Mwenendo wa miaka saba (7) wa malipo zaidi ya Stahiki



*Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Ikilinanishwa na mwaka uliopita, kiasi kilicholipwa mwaka huu kimeongezeka mpaka Shilingi milioni 306.377 ikilinanishwa na Shilingi milioni 77.481(sawa na ongezeko la 295%) inayojumuisha taasisi 6 na 4 mtawalia. zaidi ya hayo,mstari wenyewe mwendelezo wa nukta unatoa taarifa ya mwenendo wa jumla wa malipo yaliyolipwa zaidi katika kipindi cha miaka mitano unaonesha kupungua kwa kiasi.Hivyo,,hivyo Maafisa Masuuli husika wanashauriwa kuendelea kuimarisha udhibiti wao wa ndani ili kupunguza vihatarishi vinavyosababisha malipo zaidi ya kiwango stahiki. Ninawasihi Maafisa Masuuli kuweka mipango ya kurejesha malipo yaliyozidishwa

#### 10.6 Kukosekana kwa Hati za Malipo Shilingi 243,846,688

Kinyume ma kanuni ya 43 ya kanuni za Ulaguzi wa Umma Mwaka 2009 inayoeleza kuwa “CAG atakuwa na nguvu isiyo na ukomo kupitia na kuhifadhi taarifa kutoka kwa mtu yoyote, mamlaka au chomo chochote ambayo kwa maoni yake taarifa hizo ni muhimu katika kutimiza kazi zake”

Taasisi tano (5) zilishindwa kutoa hati za malipo na vielelezo vyake kudhibitisha matumizi ya Shilingi 243,846,688. Kulingana na kifungu cha 47(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, Mtumishi wa Umma atakuwa ametenda kosa la jinai kama atashindwa kumpa CAG, au mtu yoyote aliyeidhinishwa na yeze taarifa na maelezo kama yanayohitajika.

Jedwali lifuatato linaonesha taasisi zilizoshindwa kuwasilisha hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi:

**Jedwali Na. 81: Taasisi zenyé malipo yasiyo na hati za malipo**


s/n	Jina la Taasisi	Kiasi Sh.TZ
1	Fungu 70-Sekretarieti ya Mkoa- Arusha	24,060,000
2	Fungu 2017-Ubalozi wa Tanzania-Tokyo	5,330,320
3	Fungu 2024-Ubalozi wa Tanzania -Riyadh Saudi Arabia	13,904,557
4	Fungu 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	121,926,029.88
5	Fungu 63-Sekretarieti Mkoa-Geita	78,625,782
	Jumla	243,846,688

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Kutowasilishwa kwa hati za malipo na viambatisho vyake kulisababisha kutoweza kubaini uhalali, uhalisi, aina na madhumuni ya matumizi hayo ya kiasi cha Shilingi milioni 243,846,86. Kwa maoni yangu, kitendo hiki kinaashiria kuzuia mawanda ya ukaguzi na kinaweza kusababisha kufanyika udanganyifu. Aidha fedha hizo zaweza kutumika kinyume cha sheria au kufujwa.

Mwenendo wa malipo yasiyokuwa na viambatisho vya kutosha kwa kipindi cha miaka sita (6) yameainishwa hapa chini kwa ulinganisho:

**Kielelezo Na. 25: Mwenendo wa malipo ambayo Hati zake za Malipo zilikosekana na Taasisi zake:**



Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita

Kutokana na kielelezo cha hapo juu, mwenendo unaonesha kuwa tatizo la hati za malipo kukosekana limepungua kwa kiasi kikubwa kwa Shiliingi milioni 91,104.11 sawa na asilimia 99.73. Kutoka mwaka jana hadi mwaka huu. Pia, idadi ya Taasisi zenyenye mapungufu hayo zimepungua kutoka 8 hadi 5 mtawalia. Aidha, mwenendo kwa ujumla kwa miaka 7 iliyopita ambao unaoneshwa kwa mstari wenyenye nuktanukta unabainisha kuwa udhibiti wa tatizo hili ulidhibitiwa kati ya mwaka 2010/11 hadi 2013/14, ilipofika Mwaka wa fedha 2014/2015 hali imekuwa ya kutoridhisha.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 18(1)(f) & (2) ya PFR 2001, kukosekana kwa hati za malipo ni sawa na hasara ya upotevu wa fedha. Hivyo, itampasa Mhasibu Mkuu wa Serikali kuorodhesha malipo hayo kwenye Taarifa ya Hasara ya mwaka ili yachunguzwe kwa kina na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Nilitoa wito kwa Menejimenti za Taasisi husika kuziwasilisha hati za malipo zilizokosekana kwa ajili ya ukaguzi; ambapo kushindwa


kufanya hivyo, hatua stahiki lazima zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake kutokana na kutangaza kupatikana kwa hasara inayofikia Shilingi 243,846,688. Aidha, hatua za kufidia hasara hiyo lazima zichukuliwe kwa mujibu wa Kanuni 24 ya Kanuni za Fedha, 2001 kutoka kwa maafisa waliohusika kusababisha

#### **10.7 Fedha Kutumika kwa Shughuli Zisizokusudiwa Shilingi 6,810,775,133**

Ukaguzi wangu umebaini kuwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali mbalimali walichepusha fedha licha ya mapendekezo ya mara kwa mara kiatika ripoti zangu zilizopita. Kwa mwaka huu nimebaini taasisi 17 zilizokaguliwa bado zinatumia fedha kinyume na malengo yaliyowekwa na matokeo yake jumla ya Shilingi milioni 6,810.775 zilitumika katika shughuli zisizohusiana na ba bajeti iliyoidhinishwa. Matokeo yake malengo ya hiyo fedha hayawezi kutekelezwa kinyume na kanunil ya 115 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kinachotaka fedha zitumike tu kwa malengo yaliyokusudiwa. Taasisi zilizohusika na mapungufu yake zimejumuishwakatika **Kiambatisho 10.1.**

Mchanganuo na mwenendo wa malipo yaliyofanika kwa shughuli sизizokusudiwa kwa miaka 6 ya nyuma kama umeoneshwa kwenye kielelezo cha hapo chini:

**Kielelezo Na. 26: Chati ya Ulinganifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka 5 iliyopita :**



*Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kutokana na kielelezo hapo juu, malipo kwa shughuli zisizokusudiwa yameongezeka kwa kiasi kikubwa kwa Shilingi milioni 2,980.74 ikilinganishwa na mwaka uliopita sawa na 78% ya ongezeko

Nashauri menejimenti husika kuacha kulipa kwa shughuli zisizokusudiwa. zaidi , Maafisa Masuuli husika wasiidhinishe matumizi nje ya fedha iliyotengwa kwa shughuli maalum kwa yale malengo yaliyokusudiwa

zaidi ya hapo, Menejimenti za taasisi zilizokaguliwa wanapaswa kuzingatia bajeti zilizoidhinishwa na kuimarisha udhibiti wa kibajeti kuanzia uandaaji wake hadi kwenye utekelezaji, uchepushaji wowote unapaswa kutambuliwa, kumbukumbu zake kutunzwa na kushughulikiwa ipasavyo


#### 10.8 Hati za Malipo Zenye Nyaraka Pungufu Shilingi 4,508,127,243

Taasisi za Serikali zinatakiwa kudhibiti malipo ya fedha na kuhakikisha kuwa, miamala inafanyika vizuri ili kuonyesha kwamba, kiasi hicho ni halali na kinastahili kulipwa; na matumizi mengine ambayo hayafikii vigezo yanakataliwa. Hata hivyo

nilibaini kuwa hati za malipo kiasi cha Sh 4,508.13 milioni kwa muda uliopitiwa zilipatikana bila kuwa na nyaraka za kutosha kinyume na kifungu 86 (1), 95 (4) & 18 (f) cha Kanuni za Fedha za Umma, 2001. Tazama **Kiambatisho 10.2.**

Muhtasari wa miaka 7 wa mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu ni kama unavyoonekana katika Kielelezo hapa chini:

**Kielelezo Na. 27: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu**



Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita

Kwa kulinganisha na ripoti yangu ya ukaguzi wa mwaka jana, chati ya hapo juu inaonesha kwamba kiasi kilichohusika katika malipo yasiyo na viambatisho vya kutosha imeshuka hadi milioni 4,508.13 kutoka Sh 12,505 milioni mwaka jana sawa na kushuka kwa 64%. Idadi ya taasisi zinazohusika pia imepungua kutoka 29 kwa mwaka uliopita hadi 27 mwaka huu. Hata hivyo, mistari inaonyesha kuwa kiasi kinachohusika katika upungufu huu hupungua kwa kasi ndogo. Hii inaashiria kwamba, wale wanaohusika na utawala hawajaweka mfumo wa udhibiti wa ndani ili kupunguza uharibifu huo. Ninapendekeza kuwa menejimenti ya taasisi zinazohusika lazima ziimarishe mfumo wao wa udhibiti wa ndani na nyaraka zote


ambazo hazikuonekana zifuatilie na kuwasilisha kwa ajili ya ukaguzi.

### 10.9 Malipo Yaliyofanyika bila Kudai Risiti za Kielektroniki (EFD) Shilingi 1,551,184,131

Katika mwaka 2016/2017, taasisi 29 zilishindwa kuomba na kutunza risiti za kielektroniki (EFD) kama viambatisho vya malipo kiasi cha Sh 1,551.184 milioni kinyume na kifungu cha 28(1) cha kanuni za kodi ya mapato (Vifaa vya Fedha za Elektroniki) Kanuni za 2012. Tazama **Kiambatisho 10.3**.

Kwa kuongeza, kwa kutokupokea risiti za kielektroniki (EFD) taasisi za serikali husaidia wamiliki wa biashara husika kukweka kodi na hivyo kusababisha serikali kupoteza kiasi kikubwa cha mapato kila mwaka

**Kielelezo Na. 28: Mwenendo wa Kukosekana kwa EFD Stakabadhi kwa miaka 5**



*Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kutokana na takwimu hapo juu inaonyesha kuwa malipo yasiyo na risiti za kielektroniki (EFD) yamepungua kwa Sh 6,239.12

milioni mwaka huu wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita sawa na asilimia 80 ya kupungua.

Ninashauri Serikali kuendelea kutoa programu za elimu na ufahamu juu ya kufuata kwa hiari kwa Kanuni za Kodi za Mapato ya Electronic, 2012 na matumizi ya mashine za EFD itaongeza mapato moja kwa moja ikiwa kila ununuzi utakuwa na risiti za EFD.

Pia, nilipendekeza kwamba malipo yote lazima yawe na risiti ya kodi inayotokana na mashine ya EFD na serikali ikatae kununua bidhaa na huduma kutoka kwa wasambazaji ambao hawana usajili (VAT) na ambao hawatumii mashine za EFD.

#### **10.10 Malipo katika Vifungu vya Bajeti Visivyostahili Shilingi 751,946,488**

Katika mwaka wa ukaguzi, nilibaini kuwa taasisi saba hazikufuatamasharti ya MTEF kinyume na kifungu cha 51 (1-8) cha Kanuni za Fedha za Umma 2001. Taasisi hizi zilifanya matumizi ya jumla ya Shilingi milioni 751,946 ambayo yalifanywa katika vifungu visivyo sahihi bila kibali. Kufanya matumizi kwa vifungu visivyo sahihi huonesha kwamba nidhamu ya kifedha na bajeti haikuwepo kwa menejimenti. Maelezo ya vyombo vyenye kanuni za matumizi mabaya yameonyeshwa katika Jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 82: Orodha ya Taasisi zilizolipa katika vifungu vya bajeti visivyostahili**


Na	Jina la Taasisi	Kiasi Shilingi
1	<b>Vote 61-Tume ya Uchaguzi</b>	<b>21,708,595</b>
2	Vote 41-Wizara ya Katiba na Sheria (Fungu 41)	334,304,480
3	<b>Vote 81-Sekretarieti ya Mkoa-Mwanza</b>	<b>99,604,410</b>
4	Vote 85-Sekretarieti ya Mkoa- Tabora	71,967,997
5	<b>Vote 96-Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo</b>	<b>12,630,000</b>
6	Vote 36-Sekretarieti ya Mkoa- Katavi	66,602,316
7	<b>Vote 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi</b>	<b>145,128,689</b>
	<b>Jumla</b>	<b>751,946,488</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Uchepushaji huu wa fedha kwa matumizi mengineyo huweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Mtiririko wa malipo yaliyotozwa katika vifungu visivyo sahihi kwa miaka mitano (5) yameonyeshwa kwenye kielelezo hapo chini:

#### Kielelezo Na. 29: Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili



*Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kwa mwaka huu wa kifedha kiasi kilicholipwa kwa vifungu visivyo sahihi kimeitungua kutoka Milioni 4,580 (inayohusisha vyombo 16) mpaka milioni 751.946 (inayohusisha vyombo 7) kwa mwaka uliopita wa fedha.

Ninawashauri Maafisa Masuuli kuendelea kuepuka kuchanganya fedha na kuzingatia matumizi ambayo yanaangukia tu katika bajeti ilioidhinishwa na kanuni za Serikali za Takwimu za Fedha (GFS). pale itakapoonekana uchepushaji hauwezi kuepukika na umepitishwa na Manmlaka husika, basi ni lazia kuomba kibali cha

kuhamisha kulingana na kifungu cha Sheria ya bajeti Na. 11 ya 2015

#### **10.11 Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa-Shilingi 3,044,072,276**

Kinyume na kifungu cha 46 (3) cha ya Kanuni za fedha za Umma 2001, uchunguzi wangu umeona kuwa vyombo 8 vilifanya matumizi ya Shilingi 3,044,072,276 kwa ajili ya kufadhili shughuli mbalimbali ambazo hazikupangwa. Jambo hili lisipokoeshwu huweza kusababisha uharibifu wa shughuli zilizopangwa. Jedwali la hapa chini linaonesha Taasisi zilizohusika kufanya malipo nje ya bajeti iliyoodhinishwa:


#### **Jedwali Na. 83: Taasisi zilizofanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa**

s/n	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	Fungu 43-Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika	310,590,000
2	Fungu 77-Sekretarieti ya Mkoa- Mara	10,160,000
3	Fungu 81-Sekretarieti ya Mkoa-Mwanza	37,335,000
4	Fungu 2003-Ubalozi wa Tanzania-Cairo	5,760,896
5	Fungu 2017-Ubalozi wa Tanzania-Tokyo	154,107,100
6	Fungu 2011-Ubalozi wa Tanzania-New York	2,487,084,911
7	Fungu 2034-Ubalozi wa Tanzania-Comoros	26,298,936
8	Fungu 79-Sekretarieti ya Mkoa-Morogoro	12,735,434
	<b>Jumla</b>	<b>3,044,072,276</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Mwenendo wa malipo yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa miaka 6 ni kama inavyoonesha katika Kielelezo hapa chini;

### Kielelezo Na. 30: Mwenendo wa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa



*Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita*

Kielelezo cha hapo juu kinaonyesha kwamba, Idadi ya vyombo vilivytumia kupita bajeti iliyoidhinishwa vilipungua mpaka 8 kutoka 15 kwa mwaka 2015/16 pia kiasi cha makosa kimepungua mpaka Shilingi milioni 3,044.072 kutoka Shilingi milioni 4,997.962 milioni mwaka uliopita wa fedha 2015/16 sawa na asilimia 39.

Nawashauri Maafisa Masuuli kudhibiti matumizi kwa kuhakikisha huduma zinzotolewa hazizidi bajeti iliyoidhinishwa. Mtu akikihuka hili kulingana na fungu 48 la Kanuni za fedha za Umma 2001, anaweza kuwajibika kwa matumizi yoyote ya ziada yaliyotokana bila kibali sahihi.

#### 10.12 Masurufu Yaliyokaa Muda Mrefu bila Kurejeshwa Shilingi 135,767,151

Wakati wa ukaguzi wangu wa hati za malipo, nilibaini kuwa jumla ya Shilingi 135,767,151 zilitolewa kwa maafisa mbalimbali kwa ajili ya kazi kwa niaba ya taasisi za serikali. Pia, nilibaini kuwa, ingawa Maafisa wamewahi kurudi bado masurufu kiasi cha Shilingi 135,767 milioni yaliyotolewa kwa vyombo 7 hayajarejeshwa baada ya kukamilika kwa shughuli zilizotengwa. Hii kinyume na Kanuni ya 103 ya Kanuni za Fedha za Umma2001.

Kutokurejeswa kwa masurufu kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha na kutokukamilika kwa shughuli tarajiwa. Taasisi na Sekretarieti za Mikoa zilizohusika zimeoneshwa kwenye jedwali la hapo chini:


**Jedwali Na. 84: Taasisi zenyе masurufu ya muda mrefu**

Na	Jina la Taasisi	Kiasi (Shilingi)
1	Fungu 23-Idara ya Mhasibu Mkuu	61,670,600
2	Fungu 70-Sekretarieti ya Mkoa-Arusha	22,288,145
3	Fungu 72-Sekretarieti ya Mkoa-Dodoma	6,358,000
4	Fungu 83-Sekretarieti ya Mkoa-Shinyanga	2,712,000
5	Fungu 93-Idara ya Uhamiaji	3,340,000
6	Fungu 95-Sekretarieti ya Mkoa-Manyara	3,778,406
7	Fungu 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	35,620,000
	Jumla	135,767,151

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Mwenendo wa miaka 7 wa masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ni kama unavyoonekana katika kielelezo cha hapa chini:

### Kielelezo Na. 31: Mwenendo wa Masurufu yasiyorejeshwa



Chanzo: Ripoti Kuu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Miaka iliyopita

Data ya hapo ju inaonesha kuwa kiasi cha masurufu yasiyorejeshwa yamepungua kwa Shilingi milioni 261.809 sawa na asilimia 66. Hata hivyo, kulinganishwa na miaka iliyopita ambapo kulikuwa na ongezeko la asilimia 71 la kiasi cha masurufu yasiyorejeshwa. Pia, idadi ya Taasisi zimepungua kutoka 9 kwa mwaka wa fedha 2015/16 hadi 7 kwa mwaka huu. Hali ya mwaka huu ya kupungua kwa asilimia 66 inaonyesha maboresho kidogo.

Hivyo, nazishauri menejimenti za taasisi na Sekretarieti za Mikoa kuendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo itahakikisha masurufu yaliyotolewa yanarejeshwa kwa wakati baada malengo kusudiwa kuisha.

Vinginevyo, kiasi kisichorejeshwa kikatwe mara moja kutoka kwenye mshahara wowote au haki zingine au kwa kiasi kingine chochote kutokana na wamiliki wa imprest kama inavyotakiwa na Kanuni 103 (2) ya PFR, 2001

### 10.13 Malipo Yasiyokuwa na Stakabadhi za Mapokezi Shilingi 2,142,955,603

Ukaguzi wa hati za malipo ulionyesha kuwa hakukuwa na stakabadhi za kukiri mapokezi zilizopokelewa kutoka kwa walipwaji mbalimbali zenyenye thamani ya Shilingi 2,142.956 kwa taasisi za serikali sita (6) kwa mwaka wa ukaguzi. Nilishindwa kuthibitisha kwamba malipo hayo yalifanyika kwa watu stahiki.

Hali hiyo hapo juu inapingana na kifungu 93 (2) cha Kanuni za fedha za umma, 2001 kinachomtaka Mkuu wa kitengo cha Hesabu ili kuhakikisha kuwa stakabadhi za mapokezi zinachukuliwa wakati wowote malipo yanapofanywa. Maelezo ya kuonyesha mashirika na kiasi kinachohusika katika uhaba huu ni kama yameonyeshwa katika jedwali la 7 hapo chini:


***Jedwali 1: Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi***

s/n	Jina la Taasisi	Kiasi (TZS)
1	Fungu 14-Kikosi Cha Zimamoto	73,150,499
2	Fungu 86-Sekretarieti ya Mkoa-Tanga	11,939,000
3	Fungu 2021-Ubalozi wa Tanzania-Kampala	30,136,268
4	Fungu 2011-Ubalozi wa Tanzania-New York	14,701,093
5	Fungu 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	1,404,714,500
6	Fungu 79-Sekretarieti ya Mkoa-Morogoro	608,314,243
	<b>Jumla</b>	<b>2,142,955,603</b>

*Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Chati inayoonesha mwenendo na ulinganisho wa miaka ya nyuma wa malipo yasiyoambatishwa na stakabadhi za kukiri mapokezi imeonyeshwa hapa chini:

### Kielelezo Na. 32: Mwenendo wa Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za Mapokezi



Chanzo: Ripoti za ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2016


Kutokana na takwimu hapo juu, ikilinganishwa na mwaka jana, kuna ongezeko la kiasi cha Shilingi milioni 2,045.24 kwa mwaka huu 2016/17 sawa na ongezeko la 2093%. Idadi ya mashirika yenye malipo ambayo hayana stakabadhi za kukiri mapokezi pamoja na kiasi kilichohusishwa pia imeongezeka hadi sita (6) kutoka mashirika matatu (3). Wakati huo huo, mwenendo wa jumla unaonyeshwa na mstari unaonyesha uimarishaji wa udhibiti tangu mwaka 2014/15.

#### 10.14 Kodi ya zuijio haikutolewa Sh 109,163,824

Ukaguzi wangu umebaini kufunguliwa kwa kesi za kutokuzingatia mahitaji ya kisheria kwa kukata kodi ya zuijio ya 2% kwa utoaji wa bidhaa na 5% kwa utoaji wa huduma TRA kinyume na Sheria 83 (1) (b) ya Sheria ya Kodi ya Mapato, 2004 (Marekebisho ya 2008). Mapitio yangu ya hati za malipo kwa mwaka wa fedha 2016/17 yalibaini taasisi kushindwa kukata kiasi cha Sh.109,163,824 kama

kodi ya zui. Kielelezo hapo chini kinaonyesha maelezo ya vyombo na kiasi kinachohusika. Tazama **Kiambatisho 10.4**

#### Kielelezo Na. 33: Mtiririko wa malipo bila kutoa kodi ya zui kwa miaka mitatu iliyopita



Data ya hapo juu inaonesha kwamba kwa mwaka huu 2016/2017 kuna kupungua kwa thamani ya malipo yaliyofanywa bila kukata kodi ya zui kwa -89% hili ni punguzo la kiasi kikubwa ikilinganishwa na ongezeko la 43% ya kipindi hicho mwaka jana 2015/2016.

Kwa hiyo, nazikumbusha menejimenti za taasisi zilizokaguliwa juu ya jukumu lao la msingi katika kuhakikisha kwamba, taasisi zinatakiwa kutoa na kuwasilisha kodi ya zui kwenye chanzo na kupelekwa kwenye mamlaka husika kulingana na Sheria ya Kodi ya Mapato.

#### 10.15 Madeni ya nyuma yaliyolipwa lakini hayakuoneshwaa katika vitabu vya fedha Shilingi. 23,181,792

Katika kipindi cha ukaguzi, jumla ya Shilingi milioni 23.182 zililipwa kwa wasambazaji mbalimbali kwa ajili ya kutoa bidhaa na huduma ambazo zimepokelewa lakini hazikulipwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2016. Hata hivyo, nilibaini kwamba madeni haya hayakutambuliwa kama madeni katika mwaka wa fedha husika kinyume na Aya 7 ya IPSAS 1 ambayo inahitaji shughuli zote na matukio mengine kutambuliwa yanapotokea na

kutokutambua shughuli hizi kunamaanisha kwamba hazikuwamo katika rejista ya madeni na kiasi kilichoripotiwa katika mwaka wa fedha uliopita kilikuwa pungufu. Yawezekana kuwa tatizo hili linasababishwa na Epicor kushindwa kutambua ankara na LPO wakati pesa au sawa na pesa inapopokelewa au kulipwa. Taarifa zake zimeoneshwa atika jedwali hapo chini

The table below shows audited entities with undisclosed liabilities:

**Jedwali Na. 85: Taasisi zenyе madeni yasiyoonyeshwa**

Na	Fungu	Maelezo	Kiasi (Shilingi)
1	95	Secretarieti ya Mkoa wa Manyara	2,819,253
2	48	Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi	20,362,539
		Jumla	23,181,792

*Chanzo:Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2017*

Ninamshauri Mhasibu Mkuu wa Serikali kuchunguza kazi za Epicor ili kuwezesha Epicor kuzingatia malipo ya IPSAS. Kwa sasa, Epicor hairuhusu kupitishwa kwa ankara na LPO ikiwa hakuna fedha zilizotengwa kwa ufanisi. Pia, ninaomba kuwakumbusha Maafisa Masuuli kuingiza ndani ya makadirio yao ya matumizi ya kila mwaka kiasi kinachotakiwa kutumiwa kwa kulipa madeni ya awali ili yaweze kupelekwa mbele ya Bunge kila mwaka kwa ajili ya ugawaji. zaidi ya hayo, wakati wa kulipa madeni ya nyuma, Maafisa Masuuli wanapaswa kulipa kutoka katika kifungu na viwango husika ambavyo ni tofauti na makadirio ya mwaka wa sasa.

#### **10.16 Madeni ya ndani yasiyorejeshwa Shilingi 2,113,764,574**

Uchunguzi wangu wa hati za malipo pamoja na nyaraka zake katika taasisi za Serikali 17 kwa mwaka 2016/17 ulibainisha malipo ya Shilingi milioni 2,113.765 zilizokopwa kutoka akaunti ya Amana na Maendeleo ili kulipia shughuli mbalimbali za kawaida kwa kutarajia kurejeshwa. Hata hivyo, hadi mwisho wa mwaka, fedha hizo zilikuwa bado hajizarejeshwa. Hii ina maana kwamba, shughuli ambazo fedha hizo zilipangia haziwezi kutekelezwa.

Orodha ya MDAs zinazohusika zinaonyeshwa katika kifungu 10.15. Ikinganishwa na ripoti yangu ya mwaka uliopita, thamani ya uhamisho wa akaunti ya ndani kwa namna ya mkopo isiyorejeshwa imepungua mpaka Shilingi milioni 2,113.765 mwaka huu wa fedha 2016/17 kutoka Sh 5,924,435 mwaka jana (upungufu wa 65%). Wakati huo huo idadi ya vyombo vinavyohusika pia imepungua hadi 10 kutoka 17 kwa mtawalia.

Hii inaonesha kwamba, vipaumbele vilivyowekwa katika bajeti iliyoidhinishwa vinaweza kutekelezwa kama ilivyo kwenye bajeti iliyoidhinishwa. Hali hiyo ilisababishwa na utoaji wa fedha pungufu kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa matumizi ya mara kwa mara.

Menejimenti za taasisi za Serikali zinapaswa kulipa fedha zilizokopwa baada ya kupokea mgao wao wa bajeti. Mbali na hilo, ninazishauri menejimenti kusimamisha matumizi ya fedha za maendeleo ili kulipia shughuli za matumizi ya kawaida kwa sababu inaweza kutishia uendelevu wa miradi ya maendeleo.

#### **Tazama kiambatisho 10.5**

.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### 11.0 USIMAMIZI WA MALI NA MADENI

#### 11.1 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inalenga kutoa muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi yaliyotokana na ukaguzi wa usimamizi wa mali na madeni ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Serikali katika kuandaa taarifa za fedha kwa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma (IPSAS) katika mwaka wa fedha 2016/2017.

#### 11.2 Changamoto katika utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi usio wa taslimu

Serikali Kuu ilianza kutumia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 badala ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi taslim isipokuwa kuripoti Mali za Kudumu ambapo kipindi cha mpito cha miaka mitano kama ilivyoainishwa chini ya Kifungu cha 95 hadi 106 cha IPSAS 17 (2001) ambacho kilimalizika mwaka wa fedha 2016/17.

Tanzania ilipitisha IPSAS mwaka 2012/2013 kwa Serikali Kuu (Wizara, Idara na Wakala). Hii ilileta mafanikio na hatua muhimu katika kuongeza ubora na uwazi wa maelezo ya taarifa za kifedha. Nilibainisha kuwa kulikuwa na maeneo ambayo yameendelea kuwa na changamoto kama ifuatavyo:

- Kuzitambua na kuziripoti mali zisizoshikika.
- Taarifa za fedha zinaandaliwa kwa kufuata misingi isiyo taslimu (IPSAS accrual) wakati bajeti ya kitaifa inaandaliwa kuzingatia msingi wa fedha taslimu, hivyo taarifa za fedha zinazoandaliwa zinajumuisha viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha kwenye taasisi za umma IPSAS taslim na isiyo taslimu.

Vitabu vya matumizi vya Wizara, Idara na Wakala za Serikali pamoja na Sekretarieti za mikoa vya mwaka wa fedha unaofuata havioneshi salio ishia la mwaka wa fedha uliotangulia kama salio anzia kinyume na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi usio taslim (IPSAS Accrual) badala yake mafungu husika huhamisha fedha kwenda kwa mlipaji mkuu wa Serikali.

- Mfumo wa kudhibiti vifaa hautumiwi kama inavyopaswa; hivyo vifaa vinaponunuliwa vinarekodiwa kwenye mfumo kama vimeshatumika. Wakati wa kufunga mwaka vifaa vilivyobaki huondolewa katika matumizi na kuonekana kama vifaa vilivyobaki stoo hivyo husababisha hatari ya uwezekano wa kuripoti vifaa kimakosa.
- Madeni yanarekodiwa katika mfumo wa IFMS mwishoni mwa mwaka wa fedha lakini si kama yanavyotokea wakati wa utekelezaji wa shughuli.
- Makosa katika kuripoti thamani za Mali za Kudumu katika baadhi ya taasisi kutumia njia ya gharama za awali na nyingine kutumia njia ya kutafuta thamani mpya na baadhi ya taasisi ulishindwa kujua thamani ya baadhi ya mali.

Moduli ya usimamizi wa Mali za Kudumu uliopo kwenye Epicor hautumiki. Usimamizi wa Mali za Kudumu unafanyika nje wa mfumo.

Kwa kuzingatia changamoto zilizotajwa, nashauri Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali kufanya jitihada zaidi ili kuhakikisha mfumo wa uhasibu unaotumiwa, taratibu za usimamizi wa mali na mfumo wa uandaaji wa bajeti unakidhi matakwa ya IPSAS isiyo tasilimu.

### **11.3 Ukaguzi wa Usimamizi wa Mali za Kudumu**

Ukaguzi na usimamizi wa mali kwa mwaka wa 2016/17 ulizingatia uhakiki wa kufuata kikamilifu Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma (IPSAS) kwa Mali za Kudumu zilizoripotiwa katika taarifa za fedha za taasisi mbalimbali.

Mapitio yangu kwenye rejista za Mali za Kudumu kwa ajili ya usimamizi na kutoa taarifa za Mali za Kudumu (PPE) nilibainisha mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kutotenganishwa kwa thamani ya ardhi na majengo, mali zilizoonyeshwa kwenye rejista bila kuonyesha zilipo, mali zisizo na nambari za utambulisho, mali zisizosajiliwa kwenye rejista, maelezo katika rejista hayajasahihishwa na mali zilizosajiliwa katika rejista bila kuonyesha thamani.

Mapitio pia yilibainisha mali zisizo na bima, na makosa katika uthaminishaji kama vile kuthamini mali ambazo thamani zake za awali zipo, kutokuwapo kwa thamani ya ardhi na mali nyingine, kutotambuliwa kwa kushuka kwa thamani kwa miaka ya awali na kuripoti mali za kudumu ambazo thamani yake ni ndogo ikilinganishwa na kiwango kilichoidhinishwa. Upungufu huu huongeza hatari ya upotevu wa mali bila ya kugundulika, na kuripoti Mali za Kudumu kimakosa katika taarifa za kifedha.

Kwa ujumla, kuhusu utaratibu wa usimamizi wa Mali za Kudumu kwa Serikali Kuu pamoja na Sekretarieti za Mikoa nilibainisha kuwa, hakuna wafanyakazi ambao wanakuwa na wajibu wa usimamizi wa moja kwa moja wa Mali za Kudumu zinazomilikiwa na taasisi husika. Ni mtazamo wangu kwamba, kutokana na kukosekana kwa meneja wa Mali za Kudumu chini ya Mkurugenzi wa rasilimali watu ambaye atawajibika kwa kusimamia Mali za Kudumu zote katika taasisi husika, hakutakuwa na ufanisi katika usimamizi wa Mali za Kudumu pamoja na kukidhi matakwa ya kuripoti Mali za Kudumu katika taarifa za fedha.

Mapungufu mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa Mali za Kudumu ni kama ifuatavyo:

#### **11.3.1 Rejista ya Mali za Kudumu Isiyo Timilifu**

Katika sampuli ya taasisi 28 nilizokagua nilibaini kuwa rejista za Mali za Kudumu hazikuujazwa vizuri, vipengele hivyo ni kama vile: ardhi na majengo zimerekodiwa kama kitu kimoja, mali zimerekodiwa bila kuonyesha thamani, kuwapo kwa mali ambazo hazikuonyweshwa kwenye rejista, katika taasisi zingine rejista

kutoonyesha taarifa muhimu kama vile eneo mali ilipo, tarehe ya manunuzi pamoja na kujumuisha mali ambayo thamani yake iko chini ya kiwango kilichoidhinishwa. Taasisi hizo zimeorodheshwa kwenye **Kiambatisho Na.11.1**

Nina mtazamo kwamba, bila kuwapo kwa rejista ya Mali za Kudumu sahihi katika taasisi, utaendelea kukwaza uandaaji wa taarifa za kifedha ambazo zinakidhi viwango vya IPSAS isiyo taslimu. Kushindwa kurekodi rejista ya Mali za Kudumu kwa usahihi kunasababisha ugumu katika kusimamia Mali za Kudumu zisiibiwe au kutumika isivyopasa.

Nasisitiza Maafisa Masuuli wa taasisi husika kutekeleza Muongozo wa usimamizi wa Mali za Kudumu uliotolewa tarehe 10 Desemba, 2012 na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Menejimenti inapaswa kuhakikisha rejista ya Mali za Kudumu zinarekodiwa kwa usahihi kuanzia mali inaponunuliwa, matumizi yake na mpaka kuondoa mali kwenye rejista.

#### **11.3.2 Magari yaliyoegeshwa kwa muda mrefu bila matengenezo**

Katika mwaka wa Ukaguzi, nilibaini Menejimenti ya taasisi mbalimbali hawajachukua hatua ya kuchunguza magari yao ili kuona ni kiasi gani yamepata uchakavu ambao utaathiri hali za baadaye kama taasisi itaendelea kuzitunza kulingana na mahitaji ya IPSAS 21 na 26 au kuyaondosha kwa yale yanayohitaji matengenezo makubwa.

Taratibu za Ukaguzi wangu na tafiti nilizofanya katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa, zilibaini kuwapo kwa magari 347 ambayo yameachwa bila kutumika kwa muda mrefu bila kufanyiwa tathmini ya uharibifu wake.

Ingawa kifungu 253 & 254 cha Kanuni za Fedha za Umma kinatoa miongozo na taratibu za kuuza mali za kudumu ambazo hazitengenezeki na bidhaa zilizokaa ghalani muda mrefu pamoja na vifaa vingine, ukaguzi uliofanywa katika yadi za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa umebaini kuwa

magari mbalimbali ambayo miaka yake ya kununuliwa haijulikani yametelekezwa bila alama yoyote ya kuonyesha kuwa yatafanyiwa matengenezo au yatauzwa kama inavyotakiwa na sheria. Mbali na kushuka kwa thamani kwa magari hayo pia hayachangii kufikia malengo ya kila mwaka ya taasisi hizo. *Magari yaliyoegeshwa kwa muda mrefu bila matengenezo Kiambatisho 11.2*

Ninawahimiza Maafisa Masuuli kuzingatia mwongozo wa Mali za Serikali iliyotolewa tarehe 10 Desemba 2012 ambayo inahitaji Afisa Masuuli kuhakikisha kwamba mali zilizo chini ya udhibiti wao zinatunzwa vizuri kwa mujibu wa viwango vilivyopo.

#### **11.3.3 Isiyothaminishwa na Ukosefu wa Hati Miliki**

Kifungu cha 74 cha Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta ya Umma kinahitaji ardhi ionyeshwe tofauti na majengo na wakati wa ukaguzi nilibaini maeneo ambayo taasisi za Umma zilionesha tu thamani ya majengo bila thamani ya ardhi.

Matokeo yake, thamani ya majengo na ardhi ya Serikali Kuu ilioonyeshwa katika baadhi taarifa za fedha imerekodiwa pungufu kwa kuwa inajumuisha uchakavu katika ardhi ambao hakutakiwa kutolewa katika vitabu vya fedha.

Pia nilibaini kuwa taasisi kumi na mbili (12) hazina hati za umiliki wa ardhi wanazomiliki. Bila ya kuwa na hati za umiliki wa ardhi, sikuweza kuthibitisha ikiwa mali hizo zinamilikiwa na taasisi husika. Hii inaonyesha kuwa taasisi husika hazina umiliki halali wa ardhi zao; na ikitokea siku kukawa na mgogoro wa kisheria, Serikali ina asilimia kubwa ya kushindwa kesi. Pia, ukosefu wa hati za umiliki wa viwanja kunaziacha taasisi za serikali katika hatari ya maeneo yao kuvamiwa na wananchi.

## Jedwali Na. 86: Jedwali la hapo chini linaonyesha taasisi hizo:

Na	Jina la Taasisi	Vote	Mapungufu
1	Idara ya Magereza	29	Umiliki
2	Ofisi ya Makamu wa Rais	31	Kutothaminishwa
3	Kurugenzi ya mashitaka ya umma	35	Umiliki
4	Jeshi la Wananchi wa Tanzania	38	Umiliki
5	Wizara ya Fedha na Mipango	50	Umiliki
6	Wizara ya Mambo ya Ndani	51	Umiliki
7	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	53	Umiliki
8	Sekretarieti ya Mkoa wa Geita	63	Umiliki
9	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	73	Umiliki
10	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	89	Umiliki
11	Idara ya Uhamiaji	93	Umiliki
12	Ubalozi wa Tanzania New Delhi	2010	Umiliki
13	Ubalozi wa Tanzania Ottawa, Canada	2012	Kutothaminishwa
14	Ubalozi wa Tanzania Rome	2015	Umiliki
15	Ubalozi wa Tanzania Washington DC	2018	Kutothaminishwa
16	Ubalozi wa Tanzania Kampala, Uganda	2021	Umiliki
17	Ubalozi wa Tanzania Nairobi	2023	Kutothaminishwa
18	Ubalozi wa Tanzania Bujumbura	2028	Kutothaminishwa

Maafisa Masuuli wanashauriwa Kuhakikisha kuwa hati za umiliki wa viwanja zinachukuliwa kwa kufanya ufuatiliaji katika taasisi husika na pia uthamini wa ardhi ufanyike ili kuonyeshwa katika taarifa za fedha kwa kuzingatia viwango.

ili Serikali iwe na ufanisi wa usimamizi wa mali zake na kuzingatia mahitaji ya kutoa taarifa ya mali za kudumu kama ilivyoelezwa na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma (IPSAS 17), napendekeza Maafisa Masuuli na Mhasibu Mkuu wa Serikal wafanye yafuatayo::.

- a) Waweke mipango mizuri ya mafunzo kwa ajili ya wafanyakazi katika kitengo cha usimamizi wa mali za umma. Kuhakikisha kwamba moduli iliyopo na inayolipiwa ya usimamizi wa mali katika mfumo wa EPICOR (IFMS) inafanya kazi na kutumika

katika swala zima la usimamizi wa Mali za Kudumu kuanzia manunuzi, matumizi (depreciation), kuhamisha na kuondosha (disposal).

- b) Taasisi za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ziwe na Meneja wa Mali ambaye atawajibika katika kusimamia utaratibu mzima wa mali chini ya idara ya Afisa Utawala na rasilimali Watu ambaye hatoki katika Kitengo cha Manunuzi (PMU) au Kitengo cha fedha na atakuwa Mshauri kwa Menejimenti na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali katika masuala yanayohusiana na mali kwa kila taasisi husika.

#### **11.3.4 Mapato yaliyokaa muda mrefu bila kukusanywa Shilingi 194,209,741,540.74**

Mpaka tarehe 30 Juni 2017 taasisi za serikali ishirini na tatu (23) zilikuwa na madai yasiyolipwa yanayofikia kiasi cha Shilingi 194,209,741,540.74. Sehemu kubwa ya madai hayo ni kutoka Wizara ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano yenye jumla ya Shilingi 131,947,757,132 sawa na asilimia 71 ya madai yote. Ya pili ni Wizara ya Nishati na Madini yenye jumla ya Shilingi 40,447,224,824 sawa na asilimia 21 ya madai yote.

**Jedwali Na. 87: Taasisi zenyewe madai yasiyokusanywa**

Na	Jina la Taasisi	Fungu	Kiasi (Shilingi za TZ)
1	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	98	131,947,757,132.00
2	Wizara ya Madini na Nishati	58	40,447,224,824.00
3	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	48	9,336,711,691.20
4	Idara ya Polisi	28	6,415,580,038.00
5	Idara ya Magereza	29	2,070,665,714.20
6	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida	84	1,624,999,900.00
7	Kikosi Cha Zimamoto	14	536,406,500.00
8	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	70	364,119,181.00
9	Idara ya Uhamaaji	93	353,399,502.52
10	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	49	319,371,767.82
11	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	87	244,307,849.00
12	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	53	197,482,121.00
13	Ubalozi wa Tanzania Washington DC	2018	61,008,083.00
14	Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo	96	59,614,956.00
15	Ofisi ya Waziri Mkuu	37	53,081,000.00
16	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	71	49,102,929.00
17	Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu	65	35,161,375.00
18	Ubalozi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa-New York	2011	33,618,600.00
19	Mahakama	40	29,202,457.00
20	Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji	44	17,808,000.00
21	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	95	8,800,000.00
22	Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	32	4,317,920.00
Jumla			194,209,741,540.74

Pia, niliona ongezeko kubwa la madai yasiyolipwa katika Wizara ya Nishati na Madini kutoka Shilingi 9,722,377,845 kwa mwaka 2015/16 hadi Shilingi 28,583,050,603 kwa mwaka 2016/17 kutokana na kodi za madini na mirabaha katika kampuni za madini, na Asisa nyingine ni Polisi ambayo madai yaliongezeka kutoka Shilingi 2,386,352,950 kwa mwaka 2015/2016 mpaka kiasi cha Shilingi 5,649,020,188 kwa mwaka 2016/2017 kilichotokana na adhabu za makosa ya barabarani kama inavyoonyeshwa kwenye kiambatisho....;

Na	Fungu	2016/17	2015/16
		<b>Shilingi za TZ</b>	<b>Shilingi za TZ</b>
<b>1</b>	<b>58</b>	<b>28,583,050,603</b>	<b>9,722,377,845</b>
<b>2</b>	<b>28</b>	<b>5,649,020,188</b>	<b>2,386,352,950</b>

Kwa mtazamo wangu, mapungufu haya yametokana na taasisi za serikali kushindwa kufuatilia madeni hayo na menejimenti kushindwa kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji madai hayo pamoja na kutokuwa na sera ya ukusanyaji madeni.

Nazishauri Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zije na mikakati sahihi ya ukusanyaji wa madeni kwa muda muafaka. Kutokukusanya madeni kunaweza kusababisha taasisi hizo kushindwa kutoa huduma kwa ufanisi.

Nazishauri Menejimenti za Taasisi husika kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kukusanya madeni hayo ndani ya muda na kuwachukulia hatua stahiki wale watakaoshindwa kulipa madeni hayo.

#### **11.4 Usimamizi wa Madeni**

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma Na.1 juu ya uwasilishaji wa taarifa za fedha, inasema “Madeni ni wajibu wa sasa wa taasisi yanayotokana na matukio ya zamani, malipo ya madeni hayo yanatarajiwa kulipwa na vyanzo vya taasisi kutoptana na faida za kiuchumi au uwezo wa huduma”. Katika mwaka huu wa kifedha nilibaini udhaifu kuhusu usimamizi wa madeni katika taasisi nilizozikagua:

##### **11.4.1 Madeni Maalum (Kesi ambazo hazijaisha)**

Madeni maalum ni madeni ambayo yanatokea kulingana na matukio maalum. Imeonekana kuwa Wizara, Idara na Sekretarienti za Mikoa zimeshitakiwa katika mahakama

mbalimbali lakini madai ya kesi hizo hayaonyeshwi kenyе taarifa za fedha.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, nilibaini taasisi kumi (10) zina kesi zenye thamani ya Shilingi 135,598,347,446.55 zinazohusu makampuni na watu binafsi ambazo baadhi zipo katika hatua ya kusikilizwa na zingine zipo kwenye usuluuhishi. Kesi hizi nyingi zina athari hasi katika utendaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa.

Mwelekeo huu unaonekana sio mzuri kwa sababu kesi nyingi zinapelekea kuwa na uwezekano wa kuongeza madeni. Taasisi ambazo zina kesi zimeonyeshwa hapa chini.


Taasisi zenye Madeni tarajiwа		Fungu	Kiasi (Shilingi)
1	Wizara ya Nishati na Madini	58	103,063,591,003
2	Wizara ya Maliasili na Utalii	69	23,399,564,809
3	Wizara ya Ujenzi	98	8,446,467,433
4	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundи	46	363,206,398
5	Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi	99	154,062,000
6	Wizara ya Uchukuzi	62	54,458,654
7	Wizara ya Katiba na Sheria	41	37,063,319
8	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	77	30,738,030
9	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	85	29,195,800
10	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	96	20,000,000
Jumla			135,598,347,446

Kuna hatari ya matumizi yasiyo ya kawaida kufanywa na hizi taasisi kutoчana na faini au adhabu zitakazotozwa na mahakama kama taasisi hizi zitashindwa kesi.

Kama nilivyopendekeza katika taarifa zangu zilizopita, naendelea kupendekeza Serikali ihamasishe kila taasisi yake iwe na mikakati thabiti ya usimamizi wa madeni kulingana na mazingira yao kwa ajili ya kuhakikisha hatari zilizopo katika taasisi zao zinajumuishwa na kupunguzwa mpaka kufikia kiwango cha kudhibitiwa.


#### 11.4.2 Mkusanyiko wa Madeni Shilingi 2,775,297,521,594.43.

Kwa mujibu wa taarifa za fedha Mpaka kufikia 30 Juni 2017 taasisi za Serikali zilikuwa na madeni ya kiasi cha Shilingi 2,775,297,521,594.43 ikilinganishwa na bakaa ya mwaka jana ya Shilingi 1,979,323,563,821 kuna ongezeko la zaidi la Shilingi 795,973,957,773.43 ikiwa ni asilimia 40 ya ongezeko la madeni.



Jeshi la Polisi linachangia asilimia 28 sawa na Shilingi 791,590,826,036, ya pili ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yenye asilimia 27 ambayo ni sawa na Shilingi 712,055,242,561, inafuatiwa na Wizara ya Afya maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye asilimia 10 sawa na Shilingi 276,529,971,057 ya Deni lote kama ilivyoonyeshwa hapa chini kwenye jedwali mduara:

## Madeni tarehe 30 Juni, 2017



Orodha ya taasisi za Serikali ambazo zina madeni ni kama inavyoonyeshwa kwenye kiambatisho 11.1

Nazitambua jitihada zinazochukuliwa na Serikali za kutoa fedha kwa mwaka 2016/17 kiasi cha Shilingi 219.47 bilioni sawa na asilimia 11 ya madeni yaliyoripotiwa kiasi cha Shilingi 1.979 trillioni mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2016 kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kulipa madeni ya nyuma.

Pamoja na juhudini kubwa za Serikali kulipa madeni hayo ya muda mrefu, madeni katika taasisi za Serikali kwa mwaka 2016/17 yamezidi kuongezeka kwa kasi kubwa ikilinganishwa na miaka iliyopita. Hivyo naishauri Serikali:

- Kutoa fedha kwa mujibu wa makisio yaliyoidhinishwa kwa taasisi husika hivyo kuzisaidia taasisi kutokuzalisha madeni mapya katika utendaji wake.
- Kuingiza madeni yote ya miaka ya nyuma kwenye makisio ya miaka ijayo ili yaweze kulipwa na kuondoa migogoro na wazabuni na wadau wengine.

### **11.4.3 Madeni yatokanayo na matibabu ya Nje Shilingi 45,731,070,267.31**

Ukaguzi wangu wa taarifa za fedha katika Wizara ya Afya kwa mwaka unaoishia 30 Juni, 2017 unaonyesha kuwa kupunguzwa

rufaa za nje ya nchi ni sehemu ya mafanikio muhimu kwa Wizara. Takwimu zilizokusanya kutoka Wizara ya Afya inaonyesha kuwa wagonjwa 3,906 walipewa rufaa nje ya nchi kwa matibabu na Kamati ya Matibabu ya Wizara kutoka mwaka 2011 mpaka 31 Desemba 2017. Magonjwa yaliyopewa rufaa nje ya nchi hasa ni magonywa ya mifumo ya fahamu, Kansa, Magonjwa ya Moyo, Magonjwa ya figo, Orthopedics, na Ophthalmology.

Nilibaini kuwa madeni ya matibabu yaliyofikia Shilingi 28,609,803,615,40 katika hospitali mbalimbali nchini India yalikuwa bado hayajalipwa licha ya kuwasilishwa kwa ankara ya madai hayo.

Madai hayo yanajumuisha bakaa ya miaka ya nyuma kiasi cha Shilingi 25,244,449,833.86 na ongezeko la mwaka huu kiasi cha Shilingi 10,375,589,053.59 sawa na asilimia 36 ya madai yote ya Shilingi 28,609,803,615.40. Katika kipindi cha kutoa ripoti hii, Wizara iliweza kulipa Shilingi 7,010,235,272.05 ambayo ni asilimia ishirini na nane (28%) tu kwa hospitali za India. Katika uwiano madeni ya matibabu ni asilimia kumi (10%) tu ya madeni ya Wizara.

Pamoja na malipo hayo, tumepewa taarifa na Balozi wa Tanzania nchini India kuwa kuna ongezeko la Shilingi 17,121,266,651.91 sawa na asilimia 60 ya gharama za matibabu nje ya nchi kutoka Shilingi 28,609,803,615.40 mpaka Shilingi 45,731,070,267.31 kati ya tarehe 1 Julai, 2017 na Desemba 2017 kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

Jina la Hospitali	Madai katika Rupia za India	Viwango vya RI kw Sh. Za TZ	Madai katika Sh.TZ
1 Apoloo Chennai	449,284,628.00	34.63	15,558,726,667.64
2 Apoloo Delhi	461,641,214.00	34.63	15,986,635,240.82
3 Apollo Hyderabad	266,677,589.00	34.63	9,235,044,907.07
4 Apollo Ahmedabad	67,833,722.00	34.63	2,349,081,792.86
5 Apollo Bangalore	36,147,148.00	34.63	1,251,775,735.24
6 Madra Medical Mission	38,977,936.00	34.63	1,349,805,923.68
<b>Jumla</b>	<b>1,320,562,237.00</b>		<b>45,731,070,267.31</b>

Kushindwa kulipa madeni kwa wakati kunahatarisha uendelevu wa huduma ya matibabu na kuwanyima wahitaji wengine nafasi ya kupata matibabu hayo.

Nashauri Serikali ifanye yafuatayo: (i) ije na Mpango Mkakati wa kina katika Sekta ya Afya ili kujijengea uwezo wa matibabu kwa Watanzania ndani ya Nchi ili kuhudumia idadi kubwa ya watu na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni; Ishirikiane na wadau wote kuhamasisha ukusanywaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na mahitaji ya wafanyakazi.

## SURA YA KUMI NA MBILI

### **12.0 KAGUZI MAALUM NA UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA**

#### **12.1 KAGUZI MAALUM**

##### **12.1.1 Utangulizi**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya ukaguzi maalum kwa mujibu wa Kifungu na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008. Kwa kuongezea, Kanuni na. 79 (1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma inasema; “Ukaguzi maalum unaweza kufanyika mahali ambapo Afisa masuuli au mtu yejote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa na vyombo vingine vikiomba kwa maandishi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali halazimishwi kukubali ombi hilo.

Mawanda ya ukaguzi huo yataandalisha na mtu au taasisi inayoomba huo ukaguzi maalum, hata hivyo, Kanuni na. 80 (2) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009 inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye marekebisho katika mawanda ya ukaguzi atakapoona inafaa.

Katika mwaka wa ukaguzi, nilifanya kaguzi maalum sita (6), ambao umehusisha taasisi zifuatazo:-

- a) Ukusanyaji wa mapato na manunuzi ya kiwanja cha Idara ya Uhamiaji Fungu 93;
- b) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA);
- c) Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Mfano Uliotekelezwa na Jeshi la Polisi Katika Mikoa Mbalimbali ya Tanzania Chini ya Mradi wa STACA unaofadhiliwa Na DFID;
- d) Uhakiki wa madai ya Kampuni ya WENTWORTH Gas Limited juu ya gharama zilizotumika kujenga miundombinu ya kusafirishia na kusambaza umeme katika Mradi wa Umeme wa Mtwara.
- e) Chama cha Walimu Tanzania; na

f) Shirikisho la Serikali za Mitaa.

Ripoti hizi za ukaguzi maalum zimeshatolewa kwa kila mamlaka husika kwa mujibu wa kanuni ya 81 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Matokeo ya kaguzi hizi maalum yameonyeshwa hapa chini.

#### **12.1.2 UKAGUZI MAALUM JUU YA UKUSANYAJI MADUHULI/MAPATO NA UNUNUZI WA KIWANJA KATIKA IDARA YA UHAMIAJI (FUNGU 93)**

Kwa mujibu wa kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma 2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliagizwa kufanya ukaguzi maalum juu ya kukusanya mapato na ununuzi wa kiwanja katika Idara ya Huduma ya Uhamiaji (Fungu 93). Kazi hiyo ilikuwa na lengo la kupata ukweli juu ya mashaka juu ya Kamishna Mkuu na Kamishna wa Fedha na Utawala kuhusu matumizi mabaya ya makusanyo ya mapato pia matumizi mabaya ya madaraka na ubadhirifu wa fedha kama ilivyoelezwa katika barua yenyewe Kumb. Na. SAB.365 / 439/01/59 ya tarehe 1 Februari, 2016.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia barua yenyewe Kumb. Na. CAB 193/272/04 na mawasiliano mengine tulikubaliana na kukamilisha hadidu za rejea mnamo Mwezi Novemba 2016. Ukaguzi huo ulifanyika kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia Julai 1, 2011 hadi 30 Juni 2016.

**Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi:**

- a) **Matumizi mabaya ya mapato yanayofikia dola za Kimarekani 198,874 (sawa na Shilingi 321,280,947)**

Ukaguzi maalum ulibaini udhibiti dhaifu wa ndani uliofanywa na wahasibu wanne (4) kwenye makusanyo ya mapato katika Idara ya Uhamiaji uliopelekea mapato yenyewe jumla ya dola za kimarekani 198,874 sawa na Shilingi 321,280,947 kutopelekwa benki mpaka kufikia Januari 31, 2013.

Hata hivyo, baada ya kufuatilia ilibainika kuwa ni kiasi cha Shilingi 115,814,500 tu kilikuwa kimerejeshwa na kuacha kiasi kikubwa cha Shilingi 205,466,447 kikiwa hakijarejeshwa na

kupelekwa benki. Uguzi uligundua kuwa kiasi hicho kilifanyiwa ubadhirifu, kwani ilithibitika kuwa kilichukuliwa na afisa aliyeusika na makusanyo.

**b) Thamani ya kiwanja Iliyozidishwa kwa kiasi cha Shilingi 132,365,604**

Idara ya Uhamiaji, kuitia Bodi ya zabuni ya Wizara ya Mambo ya Ndani, ilikubali kununua Shamba Na. 622 lililoko eneo la Kasumulu kwa Shilingi 340,000,000 kuitia barua yenye Kumb. Na. CAB.48 / 468/01 ya tarehe 22 Juni 2015. Makubaliano ya mauziano yalitiwa sahihi mwezi Septemba 2015 na Katibu Mkuu na muuzaji Bw. Pius Nyambacha, aliyekuwa mmiliki wa kiwanja.

Kiwanja kilithaminishwa kulingana na bei ya soko kwa kutumia njia ya kulinganisha. Bw. Noah Costa, Mthamini wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, alibainisha ukubwa wa shamba /kiwanja kuwa ni hekta 2.4108. Bei ya kiwanja ilifikiwa kwa kuzingatia njia ya kulinganisha, ambapo shamba/kiwanja cha jirani kilichopo ‘Block A’ Lubele lilitumika kama msingi wa bei.

Wakati wa uhakiki wa eneo timu ya uguzi iliongozwa na maafisa wa uhamiaji, mtendaji wa kijiji na mwakilishi wa mmiliki wa shamba kulitembelea shamba. Uhakiki ulifanyika kwa kutumia kifaa maalum kwa kazi hiyo (GPS Code tool) kilichobainisha kuwa ukubwa halisi ulikuwa hekta 1.47225 na wala sio hekta 2.4108 iliyoko kwenye taarifa ya uthamini, na hivyo, kuwa na upungufu wa hekta 0.93855 kwa hiyo, kiasi cha fedha kilicholipwa kilikuwa juu kwa Sh.132,365,604 = (0.93855 x 340,000,000/2.4108).

Kwa ujumla, yalibainika mapungufu katika masuala yanayohusiana na ununuzi wa shamba hilo la Kasumulu, Kyela Mkoani Mbeya na matumizi mabaya ya mapato yaliyokusanya na Idara ya Uhamiaji.

*Mapendekezo kulingana na matokeo ya uguzi maalum huu;*

- i. *Uongozi uhakikishe makusanyo ya mapato ya jumla ya Shilingi 205,466,447 na Shilingi 132,365,604 zilizoongezwa*

*kwenye ununuzi wa kiwanja kwa udanganyifu, Kasumulu Kyela, Mbeya zinarejeshwa na kuweka kwenye akaunti ya Serikali; na*

- ii. Hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika kwenye miamala hiyo.*

#### **12.1.3 Kaguzi Maalum katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

Kufuatia mahitaji ya kimahakama, na kwa kuzingatia Kifungu Na.29 cha Sheria ya Kaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008, niliamua kuongeza mawanda ya Kaguzi katika Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa kipindi cha Julai 2012 hadi Juni 2016.

Ukaguzi huu ulilenga kutoa ushahidi kuhusiana na upangishaji wa majengo ya Ofisi za NIDA; Malipo yaliyofanyika kwa kutumia viwango tofauti vya kubadilishia fedha za kigeni; na Malipo yanayohusiana na ushauri elekezi wa kisheria. Ukaguzi huu ulibaini yafuatayo:

- a) Udanganyifu wa Mita za Mraba Katika Upangishaji wa Ofisi katika Jengo la BMTL Uliosababisha Mamlaka Kupata Hasara ya Shilingi 402,210,885.02**

Mamlaka iliingia Mkataba na kampuni ya BMTL mwezi Januari 2012 kwa ajili ya kupanga jengo la BMTL lililopo Victoria, Kijitonyama - Dar es Salaam kwa matumizi ya Ofisi.

Uhakiki wa mkataba na vipimo katika jengo husika (ghorofa ya pili na ya tatu) ulibaini kuwa eneo la mita za mraba ( $m^2$ ) 2,201 zilizoainishwa katika mkataba halikuwa sahihi. Eneo halisi ni mita za mraba ( $m^2$ ) 1,946.9. Hali hiyo imesababisha Mamlaka kutozwa zaidi kwa mita za mraba ( $m^2$ ) 254.1 isivyostahili, hivyo kupata hasara ya jumla ya Shilingi 402,210,885.02.

Ukaguzi maalum ulibaini kuwa menejimenti ya BMTL walikuwa wakifahamu kasoro hizi lakini walileta madai yao na kulipwa na NIDA. Suala hili limesababisha hasara kwa NIDA ya Sh 402,210,885.02

**b) Mamlaka ilipata Hasara ya Shilingi 167,445,671.96 kwa kutumia viwango vya benki za biashara badala ya viwango vya Benki Kuu kinyume na Mkataba**

Ilibainika kuwa Mamlaka ilifanya malipo ya jumla ya Shilingi 12,538,099,500 kwa Kampuni ya Gotham International Limited (GIL) kama Mshauri Elekezi wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa yaliyokuwa yakitozwa kwa Dola za Marekani.

Malipo yalifanyika kwa kutumia Shilingi ya Tanzania kwa viwango vya kubadilishia fedha vya Benki za Biashara vya siku husika badala ya viwango vya kubadilishia fedha vinavyoainishwa na Benki Kuu ya Tanzania kinyume na matakwa ya Mkataba husika, hivyo kupelekea Mamlaka kupata hasara ya jumla ya Shilingi 167,445,671.96.

**c) Mamlaka kufanya malipo ya Ushauri Elekezi mara mbili na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 551,500 sawa na Shilingi 899,935,494**

Ukaguzi ulithibitisha kuwa Mkataba wenyе thamani ya Dola za Kimarekani 9,000,000 wa miaka mitano (5) kati ya NIDA na Gotham International Limited (GIL) ulisainiwa tarehe 14 Januari 2010 kwa ajili ya kazi ya Ushauri Elekezi, ikiwemo Ushauri Elekezi wa Kisheria wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa.

Pia, ilibainika kuwa NIDA iliingia mkataba mwingine na M-S Law Partners mnamo tarehe 7 Novemba 2011 wenyе thamani ya Dola za Kimarekani 551,500 kwa muda wa miezi mitatu na M/s School of Law (ilijulikana kaam Faculty of Law) kwa ajili ya kazi ya Ushauri Elekezi wa Kisheria kazi ambayo kimsingi ilikwishatolewa kwa Gotham International kuititia Mkataba wake na NIDA.

Hatua hiyo ilisababisha Mamlaka kufanya malipo mara mbili kwa kazi moja ambayo ilipaswa kufanywa na Gotham International Limited, suala ambalo liliisababishia Mamlaka hasara ya jumla ya Dola za Marekani 551,500 sawa na Shilingi za Tanzania 899,935,494.

Ukaguzi huu maalum kwa ujumla umebainisha mapungufu katika upangishaji wa jengo la Ofisi ya NIDA, gharama zaidi katika

malipo kutokana na kutumia viwango vya kubadilishia fedha visivyokuwa vya Benki Kuu kinyume na makubaliano. Vilevile mamlaka ililipia huduma za kisheria ambazo hazikutolewa.

#### **Mapendekezo:**

- i. *Mamlaka ihakikishe urejeshwaji wa jumla ya Shilingi 402,210,885.02 kutoka Kampuni ya BMTL (sasa The Copy Cat Tanzania Ltd).*
- ii. *Mamlaka ihakikishe urejeshwaji wa kiasi cha jumla ya Shilingi 167,445,671.91 kutoka kwa Gotham International Limited na hatua stahiki zichukuliwe na Mamlaka ili kuhakikisha uzingatiwaji wa mikataba katika malipo ili kuepusha hasara zisizotarajiwा.*
- iii. *Menejimenti ya Mamlaka ihakikishe kuwa Gotham International Limited inarejesha jumla ya kiasi cha Dola za Kimarekani 551,500 zilizolipwa kwa ajili ya kufanya mapitio ya sheria ambayo hakuifanya.*

#### **12.1.4 Uguzi Maalumu wa Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Mfano Uliotekelzwa na Jeshi la Polisi Katika Mikoa Mbalimbali ya Tanzania Chini ya Mradi wa STACA unaofadhiliwa Na DFID**

Ukaguzi huu maalum ulifanyika kutokana na ombi kutoka ofisi ya Mratibu wa Mradi wa STACA (STACA - PCO) kuititia barua yenye kumb. Na. STACA/ADM/CONF/01 ya tarehe 17 Agosti, 2016 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Kazi ya ukaguzi ililenga kutoa uhalali na usahihi wa matumizi ya Paundi za Uingereza 2,680,000 sawa na Shilingi za Tanzania 6,946,866,248 fedha za mradi wa STACA wakati wa utekelezaji wa mradi wa uanzishwaji wa vituo vya polisi vya mfano (MPS) na Jeshi la Polisi la Tanzania (TPF), mradi uliofadhliliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID). Shabaha ilikuwa kutaka kuona kama utekelezaji huo ulizingatia mpango kazi na bajeti.

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huu ni kama inavyooneka hapa chini. Hata hivyo, ripoti tayari imewasilishwa kwa mamlaka

husika kulingana na Kanuni ya 81 ya Kanuni za Ugazusi wa Umma wa 2009.

**1. Kiasi cha fedha hakikutolewa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa kwenda Jeshi la Polisi la Tanzania Paundi za Uingereza 320,000**

Makubaliano (MoU) kati ya Serikali ya Uingereza na Ireland ya Kaskazini kupitia Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID) na Serikali ya Tanzania yaliyosainiwa tarehe 20 Februari 2012 yanabainisha kuwa Jeshi la Polisi la Tanzania (TPF) litapokea jumla ya Paundi za Uingereza 3,000,000, sawa na Shilingi za Tanzania 7,732,064,000, kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2015/2016.

Wakati wa ukaguzi tulibaini kuwa, jumla ya Paundi za Uingereza £ 320,000 sawa na Shilingi za Tanzania 785,197,752 zilizuiwa kutolewa na DFID kufuatia Jeshi la Polisi kutokufuata mpango kazi wa mwaka ulioidhinishwa tangu mwaka wa fedha 2011/2012.

Kwa kutokutolewa kwa £ 320,000 na wafadhili kuliathiri utekeleza wa shughuli zilizokuwa zimepangwa katika mpango kazi wa STACA.

**2. Matumizi ya fedha zaidi ya bajeti iliyopangwa katika ujenzi wa Vituo vya Polisi vya mfano Shilingi 365,756,625**

Jeshi la Polisi Tanzania (TPF) kupitia mipango kazi yake ya miaka mitatu ya fedha kuanzia 2012/2013 hadi 2014/2015 ilipanga kutengeneza/kujenga Vituo vya Polisi vya Mfano vipatavyo thelathini na vitano (35) kwa miaka mitatu kwa gharama ya jumla ya Shilingi 1,052,020,000.

Wakati wa ukaguzi tulibaini kuwa kati ya vituo thelathini na tano (35) vilivyokuwa vimepangwa, ni vituo kumi na sita (16) tu ndivyo vilijengwa/kukarabatiwa kwa gharama ya Shilingi 1,417,776,625 ambayo ni zaidi ya gharama iliyopangwa kwa Shilingi 365,756,625.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, kati ya vituo vyote vya mfano vilivyoanzishwa ujenzi, wa vituo Sita (6) ambavyo ni Ikungi, Mkarama, Manyoni, Mkuranga, Simiyu (Bariadi) na Lushoto havijakamilika. Hali hii inamaanisha kwamba kutakuwa na fedha za ziada zinazohitajika ili kukamilisha ujenzi huo. Matumizi ya fedha zaidi ya kiasi kilichopangwa kwenye bajeti yalisababisha kutokujengwa/kuanzishwa kwa vituo kumi na tisa (19) sawa na asilimia 54 kati ya vituo vilivyopangwa.

### **3. Ujenzi wa vituo vitatu vya polisi katika Mkoa wa Singida (Manyoni, Ikungi na Mkalama) kinyume na Mpango Kazi na Bajeti**

Jeshi la Polisi Tanzania (TPF) lilienga vituo vya polisi vya mfano vitatu (3) katika Mkoa mmoja wa Singida katika Wilaya za Manyoni, Ikungi na Mkalama kwa gharama ya Shilingi 592,990,000. Ujenzi wa vituo vitatu katika mkoa mmoja ulifanyika kinyume na Mpango Kazi na Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, ambapo Jeshi la Polisi na Wafadhiri (DFID) walikubaliana kujenga/kurekebisha kituo kimoja cha Polisi katika kila Mkoa.

Ukaguzi ulibainisha kuwa kitendo cha Jeshi la Polisi kujenga vituo vitatu vya Polisi katika Mkoa mmoja kilinyima Mikoa mingine fursa ya kufaidika na huduma za vituo vya mfano katika Mikoa yao.

### **4. Kugawanywa kwa zabuni ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Lushoto ili kukwepa mahitaji ya kisheria katika mchakato wa kumpata Mzabuni Shilingi 515,233,760**

Jeshi la Polisi Tanzania liliingia mkataba na kampuni ya Posh Alliance Ltd ikiwa ni zabuni ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa kituo cha Polisi cha Mfano (MPS) katika Wilaya ya Lushoto zabuni iliyokuwa na thamani ya Shilingi za kitanzania Shilingi 515,000,000. Nukuu ya bei ilitumika kama njia ya manunuzi kumpata mzabuni huyo.

Hata hivyo, zabuni ya ujenzi katika kituo cha Polisi cha Lushoto iligawanywa katika vipande(phases) viwili, hata hivyo mkandarasi huyo alipewa kazi zote mbili na katika kazi zote mbili mkandarasi

alipatikana kwa njia ya nukuu ya bei. Uguzi ulibaini kuwa kugawanywa kwa zabuni hiyo katika vipande viwili ulifanyika kwa lengo la kukwepa katazo la Jedwali la Saba la kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2013 ambayo inahitaji zabuni zote zinazozidi kiasi cha Shilingi milioni Mia Mbili (200,000,000) zisitolewe kwa njia ya nukuu ya bei badala yake njia zingine zakiushindani zitumike kuongeza uwazi na ushindani ili kupata thamani halisi ya fedha katika matumizi ya fedha za Umma.

Kwa ujumla, kuna masuala mbalimbali yaliyobainika juu ya matumizi ya fedha za mradi wa STACA yasiyostahili wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya polisi vya mfano vya Jeshi la Polisi la Tanzania (TPF).

***Kulingana na matokeo hayo,menejimenti inashauriwa kama ifuatavyo:***

- i. *Ihakikishe kuwa shughuli zote za miradi inayotekelizwa na Jeshi hilo zifanyike kwa kuzingatia Mikataba, Mipango kazi na Bajeti husika; na*
- ii. *Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo itahakikisha sheria na kanuni zinafuatwa wakati wa mchakato wa manunuzi.*

**12.1.5 Taarifa ya Uguzi Maalumu wa kuhakiki madai ya Kampuni ya WENTWORTH Gas Limited juu ya gharama zilizotumika kujenga miundombinu ya kusafirishia, kusambaza Umeme katika Mradi wa Umeme wa Mtwara**

Uguzi huu maalum ulifanyika kutokana na ombi kutoka Wizara ya Nishati na Madini kuititia barua yenye kumbu Na.CBD.180 / 229/01/30 ya tarehe 26 Julai 2016 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Kazi ya uguzi ililenga kutoa uhalali na usahihi wa gharama za kurejeshwa kwa Wentworth Gas Limited kutoka Wizara ya Nishati na Madini. Malengo maalum yalikuwa:

- a) **Kutafuta maoni ya kitaalam juu ya gharama halisi inayotokana na M/s Umoja Light kwa Mradi wa “Mtwara Energy Project” kwa taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na**

**ripoti halisi ya “factual findings report” ya tarehe 30 Machi 2012.**

Kuthibitisha uhalali wa taarifa zinazotolewa na kupendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa na serikali.

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huu ni kama inavyoonekana hapa chini. Hata hivyo, ripoti tayari imewasilishwa kwa mamlaka husika kulingana na Kanuni ya 81 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma wa 2009.

Malipo ya Gharama za Menejimenti zisizohusiana na MEP na MICRA Dola za Marekani 2,696,848

Kampuni ya Umoja Light katika ripoti ya “factual findings report” ilionesha kuidai Wizara ya Nishati na Madini (MEM) jumla ya Dola za Marekani 3,246,682 ambazo ilizilipa kwa kampuni ya M/s Manitoba Hydro International kama Gharama za huduma za Menejimenti.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba Dola za Marekani 2,696,848 kati ya madai hayo ni gharama ambazo hazihusiani na MEP na MICRA; ambapo Dola za Marekani 796,836 zililipwa kabla ya kusainiwa kwa mkataba wa MEP na MICRA, na Dola za Marekani 948,804.38 zililipwa na M/s Artumas Group Inc. ikiwa ni gharama kwa ajili ya matawi (subsidiary) mengine; na Dola za Marekani 951,208 hazistahili kudaiwa kwa sababu wakati gharama hizo zikilipwa tayari Serikali ilishahamisha fedha kwa ajili ya Tarrif Equalization Fund (TEF). Kwa hiyo, ni Dola za Marekani 549,834 pekee kati Dola za Marekani 3,246,682 zimethibitika kuwa zinastahili kurejeshwa/kulipwa na MEM kwenda WENTWORTH.

**b) Gharama za Mali na Vifaa zisizo halali Dola za Marekani 1,768,631**

Rekodi za matumizi zilizowasilishwa kwa MEM kuhusiana na gharama za Mali na Vifaa zilibainisha kuwa Umoja Light Co Ltd ililipa jumla ya Dola za Marekani 1,911,749.24 ikiwa ni gharama za ushauri, huduma za kisheria, zabuni, uchunguzi, chakula na malazi, tiketi za ndege na uhandisi na ubunifu. Hata hivyo, takwimu hii ya matumizi ilikuwa ni zaidi ya kiasi cha Dola za

Marekani 1,868,631 kilichoonyeshwa katika “factual finding report”

Hata hivyo, ilibainika kuwa, gharama zinazofikia Dola za Marekani 100,000 pekee ndizo inastahili kulipwa. Hii ni kwa kuwa ndizo gharama pekee zilizolipwa baada ya kusainiwa mkataba wa MICRA mwaka 2008; na ina ushahidi unaojitosheleza. Gharama za kiasi cha Dola za Marekani (US\$) 1,768,631 hazistahili kulipwa, kwani gharama ya kiasi cha Dola za Marekani (US\$) 698,870 zilitumika kipindi cha mwaka 2004 hadi 2007 kabla ya kusainiwa kwa makubaliano ya MICRA mnamo Desemba 2008; na Gharama za kiasi cha Dola za Marekani 1,169,761 hazikubaliki kwa kuwa hazina ushahidi wa kujitosheleza.

**c) Gharama za Ununuzi wa Majenereta 3 katika mradi wa Mtwara Gas - Fired Power Plant kwa kutumia fedha za TEF hazikukatwa wakati wa manunuvi ya mradi huo Dola za Marekani 1,669,568**

Mnamo tarehe 7 Februari 2012 TANESCO na Wentworth Power Limited walisaini Mkataba wa Mauzo na Ununuzi wa Mradi wa Mtwara Gas - Fired Power Plant na mali zake zote kwa gharama ya Dola za Marekani 13,500,000.

Gharama zilizokubaliwa ya Dola za Marekani 13,500,000 kulingana na ripoti ya hesabu ya Kituo cha Gas - Fired Power Plant inajumuisha gharama/thamani ya majenereta 3 yalinayofikia Dola za Marekani 1,169,568 ambapo majenereta hayo yalinunuliwa kupitia fedha za mfuko wa TEF. Gharama hizo zinapaswa kuwa zimetolewa au kupunguzwa katika gharama za mauzo/manunuvi. Hii ni kwa sababu Mkataba wa Ununuzi na Uuzaji wa majenereta matatu (3) ulisainiwa tarehe 31 Machi, 2009 kati ya Group Artumas G&P na Mantrac Tanzania lakini gharama zililipwa na Umoja Light Ltd kutoka akaunti ya TEF. Majenereta yalitumiwa na Mtwara Gas - Fired Power Plant kampuni iliyokuwa inamiliwi na Artumas G&P Power (ambayo haikuwa kwenye mpango wa MEP ambao unafadhiliwa na mfuko wa Tariff Equalization Fund (TEF)).

Kutokupunguzwa au kutokukatwa kwa kiasi cha fedha ambacho kilitumika kununua majenerata 3 kutoka katika mfuko wa TEF ambazo hazihusiani na MEP na MICRA kunapelekea Wizara ya Nishati na Madini kulipa fedha zaidi na kuisabibishia Serikali hasara ya Dola za Marekani US\$ 1,169,568.

**d) Bakaa ya fedha katika mfuko wa TEF haikurudishwa Wizara ya Nishati na Madini (MEM) Dola za Marekani 85,318.86**

Ripoti ya matumizi iliyowasilishwa kwa Wizara ya Nishati na Madini na Wentworth Gas Limited kwa barua yenye kumbukumbu Na.WGL/MEM/2016/063 ya tarehe 17 Juni, 2016 ilibainisha kuwa Serikali ya Tanzania ilitoa Dola za Marekani 13,500,000, sawa na Shilingi 18,158,790,634, kwenda kampuni ya Umoja Light Co Ltd ikiwa ni fedha za uimarishaji bei - Tarrif Equalization Fund (TEF). Ripoti hiyo inaonesha kuwa jumla ya Shilingi 18,024,034,608.99 zilitumika, wakati ya Shilingi 134,756,025.01 sawa na Dola za Marekani 85,318.86 hazijatumika wakati wa kutekeleza mradi.

Hata hivyo, hiyo inaonesha kwamba bakaa hiyo haikurudishwa/kurejeshwa Wizarani licha ya kukamilika na kukabidhiwa kwa mradi wa MICRA tarehe 14 Januari, 2012. Kutorejeshwa kwa bakaa hiyo kunadhirisha matumizi mabaya ya fedha ya Umma.

**e) Gherama zilizoongezwa katika ununuvi wa Mtambo wa Mtwara Gas Fired Power Plant na Mali zinazohusiana nazo Dola za Marekani 4,847,542**

TANESCO ilikubaliana na kampuni ya Artumas Power (Wentworth Gas Limited) kununua Mtwara Gas Fired Power Plant na mali zake zote kwa gharama ya kiasi cha Dola za Marekani 13,500,000. TANESCO ilifanya majadiliano na kukubali kulipa kiasi hicho cha fedha bila kuwa na ripoti yoyote ya udhamini kinyume na matakwa ya "Ministrial Circular" Na. 1 ya mwaka 1969 ambayo inataka taasisi zote za Serikali na Mashirika ya Umma kabla ya kununua au kuuza mali yoyote inapaswa kutafuta ushauri kutoka kwa Mdhamini Mkuu wa Serikali.

Wakati wa ukaguzi kwa kushirikiana na ofisi ya Mdhamini Mkuu wa Serikali tulibaini kuwa mradi huo pamoja na mali zake zote una thamani ya Dola za Marekani 8,652,458 tu. Hivyo basi,

Wizara imelipa gharama kubwa zaidi kuliko thamani halisi ya mradi huo na kuisababishia Serikali hasara ya kiasi cha Dola za Marekani 4,847,542.

Kwa ujumla, Ukaguzi huu umebaini kuwa sehemu ya gharama ambazo Kampuni ya Wentworth Gas Limited inadai kulipwa kutoka Wizara ya Nishati na Madini hazistahili kwa kukosa uthibitisho.

***Kulingana na matokeo hayo, yafuatayo yanashauriwa kama ifuatavyo:***

- i. *Gharama ya jumla ya Dola za Marekani 2,696,848 ikiwa ni gharama za Menejimenti haipaswi kulipwa na MEM kwa WENTWORTH;*
- ii. *Tunapendekeza menejimenti ya MEM kutokulipa gharama za Mali na Vifaa zenye thamini ya Dola za Marekani 1,768,631 kama zinavyodaiwa na kampuni Wentworth Gas Ltd kwa kuwa hazina uhusiano na miradi MEP na MICRA;*
- iii. *Wizara ya Nishati na Madini (MEM) inapaswa kukata/kupunguza gharama za ununuzi wa majenereta matatu yenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani 1,669,568 kutoka kwenye madai yaliyotolewa na Wentworth Gas Limited;*
- iv. *Wizara ya Nishati na Madini (MEM) inapaswa kukata/kupunguza kiasi cha dola za Marekani 85,318.86 kutoka kwenye madai ya Wentworth Gas Limited ikiwa ni bakaa ambayo haikurudishwa MEM; na*
- v. *Wizara ya Nishati na Madini (MEM) inapaswa kukata/kupunguza kiasi cha dola za Marekani 4,847,542 kutoka kwa madai yaliyotolewa na Wentworth Gas Limited kwa kuwa kampuni hiyo ilizidisha gharama za mradi wake ulionunuliwa na Serikali.*

#### 12.1.6 Ukaguzi maalum Chama cha Walimu Tanzania (CWT)

Niliombwa kufanya ukaguzi maalum katika Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kufuatia barua ya maombi kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi Ofisi ya Rais Ikulu kuititia barua yenye Kumb.Na. CAB.38/577/01/F/19 ya tarehe 27 Machi 2017 kwa mujibu wa

Sheria Na.29 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 pamoja na Kanuni na.78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Ukaguzi ulijikita katika tuhuma dhidi ya Uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania zinazohusu ubadhirifu wa fedha na mali za Chama. Ukaguzi maalum ulikagua taarifa za mapato na matumizi ya Chama, uliangalia uhusiano uliopo kati ya Chama cha Walimu, Benki ya Waalimu (MCBL), Kampuni ya Waalimu (TDCL) na Jengo la Mwalimu (Mwalimu House). Vipengele vingine ni uhalali wa mitaji iliyonunuliwa na MCBL, pamoja na uimara wa mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kipindi kinachoanza 2011 mpaka 2016.

**a) Mapungufu katika Udhibiti wa ndani**

- (i) Kukosekana kwa mfumo mzuri wa kumbukumbu za wanachama

Ibara ya (6.1 - 6.4) ya katiba ya Chama cha Walimu pamoja na Kanuni zake na.1(a-d) zimeeleza kuwa, kunatakiwa kuwe na wanachama wa aina nne (4) ambao kumbukumbu zao zinatakiwa kutunzwa na Viongozi tofauti tofauti wa Chama, kitu ambacho kinaleta ugumu wa kutambua idadi ya wanachama waliopo makao makuu ya Chama.

Mapitio ya makubaliano yaliyofanyika tarehe 8 Aprili, 2014 chini ya Kanuni na.3 na Kanuni na.5 zinaonyesha kuna ongezeko la waajiriwa (waalimu) ambao sio wanachama wa Chama na ambao makato yao yatalipwa kupitia akaunti tofauti ya utawala inayodhibitiwa na Chama. Hivyo kuwa na ongezeko la wanachama pamoja na makato kwa mwezi ambayo yanatakiwa yaingizwe katika vitabu vya Chama.

Pia, nimegundua kwa taarifa za wanachama zilizopo makao makuu ya Chama hazina taarifa muhimu za wanachama, hasa aina ya mwanachama, tarehe ya kuingia, mshahara kwa mwezi, namba ya uanachama na kiwango anachochangia kwa mwezi zaidi ya taarifa zilizopo Hazina.

Kwa Menejimenti ya Chama kushindwa kuwa na taarifa za wanachama wake kunaweza kusababisha mapato mengine

yasipatikane au wanachama wengine kuchangia na wengine kutochangia; na inapofika kwenye maslahi inaweza kuleta migogoro kwa kukosa kumbukumbu sahihi. Vilevile inaweza kusababisha fedha za Wanachama kufujwa na watu wasio waaminifu kwa kuficha taarifa za Wanachama.

*Hivyo, nashauri viongozi husika wahakikishe wanaandaa mfumo mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu za Wanachama wao kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi.*

(ii) **Mkanganyiko wa Katiba na Kanuni katika umiliki wa Mali za CWT**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Katiba ya CWT na Kanuni zake zinakinzana juu ya majukumu ya Bodi ya Wadhamini katika kusimamia Mali za Chama. Hii ni kwa kuwa, kulingana na Katiba Ibara ya 35(b) Wadhamini ni waangalizi na wadhibiti wa mali za Chama; wakati Kanuni za Chama Na. 37(a) zinasema mali zote za Chama zitaandikishwa kwa jina la Wadhamini wa Chama. Hali hii inaleta mkanganyiko katika kujua majukumu halisi ya Bodi ya Wadhamini kwenye Mali za Chama, kwani kama Mali za Wanachama zitaandikwa kwa jina la wadhamini inatoa mianya kwa Watu wasio wanachama au watu binafsi kumiliki mali za Chama badala ya Chama kumiliki Mali zake chenyewe.

Hofu yangu ni kuwa, mkanganyiko huo unaweza kusababisha mali za Chama kuingia katika hatari ya kupotea au kuingia katika matumizi mabaya ya mali za chama.

Hivyo, nashauri Menejimenti ya Chama kufanya marekebisho ili Katiba ya CWT ioane na Kanuni zake.

(iii) **Malipo yaliyofanyika bila viambatisho vya kutosha Shilingi 11,924,250,620.13**

Kanuni za Fedha Toleo la pili la Mwaka 2011(b) (v) inasema kuwa nakala ya vielelezo vya udhibitisho au idhini za malipo zitaambatishwa pamoja kwenye Hati za Malipo. Kinyume na Kanuni hiyo, nilibaini kuwa malipo ya matumizi mbalimbali ya Ofisi yenye thamani ya Shilingi 10,272,952,014.83 hayakuwa na vielelezo vya uthhibitisho wa matumizi hayo, hali iliyosababisha kushindwa kujua uhalali wa malipo hayo.

Ni mtazamo wangu kuwa kitendo hiki kilinipunguzia mawanda ya ukaguzi na kuwa kitendo hiki kinaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha, kwani fedha hizi zinaweza kuwa hazikutumika kwa kufuata sheria na kwa ufanisi.

Matumizi haya yanajumuisha kiasi cha Shilingi 1,651,298,605.70 kwa ajili ya Waaalimu na Wachangiaji wenye mahitaji yanayotofautiana, lakini CWT walishindwa kutoa maelezo ya matumizi haya kati ya Mwaka 2011 na 2016 kwa sababu malipo hayo hayakuwa na nyaraka za kutosha.

*Ninapendekeza kwamba, Menejiment ya CWT inaweka mifumo ya Udhibiti wa Ndani kulingana na Memoranda ya Muongozo wa Fedha na ihakikishe hatua stahiki za kinidhamu inachukuliwa dhidi ya Watumishi waliohusika.*

**(iv) Malipo yasiyoidhinishwa Shilingi 3,287,708,358**

Uchunguzi umebaini kuwa malipo yenyeye thamani ya Shilingi 3,287,708,358 yalifanyika bila kuidhinishwa na Katibu Mkuu na Mweka Hazina wa Chama cha Walimu kwa kipindi kinachoanzia 2011 mpaka 2016. Nina wasiwasi juu ya uhalali wa malipo hayo yaliyofanyika bila kuidhinishwa kama mahitaji ya kifungu katika nyongeza ya pili (b)(v) ya kanuni za fedha za mwaka 2011 ambayo inahitaji viambatisho vyote vilivyoidhinishwa viambatishwe kwenye hati za malipo husika.

Naishauri Menejimenti kuwa, wahusika wote wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa upotevu huo wa nyaraka.

**(v) Malipo Yaliyofanyika bila kuzingatia makisio Shilingi 11,924,250,620.13**

Kanuni za Fedha za Chama Toleo la pili la Mwaka 2011 kifungu cha 3.4 (b) (iii),(iv) na kanuni 5.1(a-b) inamtaka Mhasibu Mkuu kuhakikisha kuwa Matumizi yanafanyika kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa na makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka yanaandaliwa kwa kushirikiana na idara zote za chama. Tofauti na kanuni zilizoelezwa, kiasi cha Shilingi 26,857,334,119 kilitumika kwa kipindi cha mwaka 2011 mpaka 2016 bila kuzingatia bajeti.

Matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa yanaonesha ukosefu wa nidhamu ya matumizi ya fedha ambao utasababisha kuleta mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Chama.

zaidi, menejimenti inashauriwa iimarishe uthibiti wa bajeti kuanzia wakati wa maandalizi, utekelezaji, na uchepushaji wowote ujulikane, uandikwe na ushughulikiwe kwa utaratibu.

- (vi) Mapungufu katika umiliki wa Vitega Uchumi vyta Chama
- b) Usimamizi usiofaa wa Miradi ya Uwekezaji ya Benki ya Walimu (MCBL) na Mwalimu House

Ibara ya 31.3(f) ya katiba ya Chama inaeleza kuwa Miradi ya Uwekezaji ni mojawapo ya vyanzo vya mapato ya Chama. Vilevile, ibara ya 32.1(b) nayo inaeleza kuwa moja wapo ya matumizi ya Chama ni ujenzi wa Miradi ya Uwekezaji inayopitishwa na Baraza Kuu la Chama.

Pia ibara na.20.1, 20.3 na ibara na.36 za katiba ya Chama zimetaja wahusika katika usimamizi wa mali za Chama.

Tathmini iliyofanyika kuhusu umiliki wa Benki ya Walimu (MCBL) na Mwalimu House imeibua mapungufu yafuatayo:-

- i. Hakuna nyaraka zinazoonesha umiliki wa moja kwa moja wa Chama cha Waalimu juu ya Miradi yake ya Uwekezaji.
- ii. Hakuna nyaraka zinazoonesha mtiririko wa mapato kutokana na miradi ya uwekezaji iliyofanywa na Chama cha Waalimu tangu kianzishwe.
- iii. Chama cha Waalimu kimenunua hisa 8,000,000 sawa na asilimia 12.94 (12.94%) ya umiliki katika kampuni yake ya MCBL, hivyo kutokuwa na maamuzi ndani ya kampuni yake mwenyewe.
- iv. Kampuni ya Mwalimu House imeanzishwa na CWT na kupelekwa kwa kampuni ya TDCL kwa ajili ya usimamizi bila kuwa na mkataba ambao unaonyesha jinsi CWT na wanachama wake watakavyo faidika na kuwapo wa jengo hilo.

Kwa maoni yangu Miradi ya Uwekezaji ya Chama haisimamiwi vizuri, hivyo kusababisha kutokuwa na faida yoyote kwa chama na wanachama kwa ujumla. Bila kuwa na usimamizi mzuri wa

Miradi ya Uwekezaji, Chama hakitaweza kufaidika na miradi hiyo na hivyo kutumiwa vibaya na watu wasio na nia njema na Chama.

*Naishauri menejimenti ya Chama wahakikishe umiliki wa mali zake unalindwa na nyaraka halisi pamoja na zile zilizotolewa kwa usimamizi wa kampuni zingine kuwa na mikataba ya makubaliano ambayo imeandaliwa kisheria kwa manufaa ya Chama. Pamoja na hayo, nakishauri Chama cha Waalimu kiongeze hisa katika umiliki wa MCBL ili kiwe na maamuzi katika kampuni yake.*

c) Mashaka katika kuwapo na umiliki wa Kampuni ya Chama (TDCL)

Ukaguzi wangu wa nyaraka ulibainisha kuwa Menejimenti ya CWT ulihamishia usimamizi wa jengo la Mwalimu House kwa TDCL yenye nambari ya usajili 45719 kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa jengo lililopo llala Boma DSM.

Mapitio zaidi yaliyofanywa BRELA kuhusiana na uhalali wa Kampuni yenye usajili no.45719 yilibainisha kuwa kampuni iliyosajiliwa huko BRELA kwamba hiyo ni Teachers Development (T) Limited kwa hati ya usajili namba 45719 badala ya TDCL, hii imesisitizwa kwa barua na Ref.No.MITM / RC / MISC / 2017/21 ya 07/05/2017 kutoka BRELA. Pia, ilibainika kuwa Teacher's Development (T) Limited haijawahi kufanya kazi tangu kuanzishwa.

Kupitia ushirikiano na kampuni yenye hati za kughushi, uhalali wa makubaliano na utendaji wa masharti haviwezi kutekelezwa na sheria. Pia, faida inayotarajiwa ipo hatarini kwa sababu uendeshaji wa Kampuni ni kinyume cha sheria; kwa hiyo, hakuna kumbukumbu za uhasibu zinazoandaliwa kwa mujibu wa sheria.

Ninaishauri Menejimenti kuhakikisha kwamba TDCL inafanya shughuli zake baada ya kutimiza mahitaji ya BRELA na mapato na mali zilizopatikana zinathibitishwa na zinagawanywa kulingana na makubaliano yaliyofanywa.

**Kulingana na matokeo ya ukaguzi maalum, ninapendekeza kuwa:**

- Menejimenti inashauriwa kuimarisha mifumo ya Udhibiti wa Ndani. Hii ni kwa kuwa udhaifu uliojitokeza unatokana na kuwapo kwa udhibiti wa ndani usiotosheleza.
  - Mbali na kuimarisha udhibiti wa ndani kama hatua ya kukabiliana na udhaifu uliotajwa katika ukaguzi wa kitaaluma, hatua za kinidhamu na za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa wale maafisa kwa kutotimiza majukumu yao kwa ufanisi, na hivyo kusababisha hasara kwa fedha za wanachama.
  - Kamati ya Ukaguzi inapaswa kuanzishwa kwa kusudi la msingi la kutoa uangalizi wa mchakato wa taarifa za kifedha, mchakato wa ukaguzi, mfumo wa udhibiti wa ndani na kufuata sheria na kanuni.
- c) Menejimenti ya CWT inapaswa kuhakikisha kuwa uwekezaji ulioanzishwa wa MCBL na Mwalimu House unaendeshwa vizuri kupitia sera iliyowekwa ya uwekezaji ambayo itaweka malengo na njia za kufikia malengo yaliyopangwa.

#### **12.1.7 UKAGUZI MAALUMU WA JUMUIYA YA SERIKALI ZA MTAAT (ALAT)**

Nimemaliza ukaguzi maalum wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa (ALAT) ambao umefanyika kufuatia barua ya maombi ya Mwenyekiti wa Jumuiya yenye Kumb.Na.ALAT/F.10/1/XIV/24 ya tarehe 19 Julai, 2017.

Ukaguzi huu ulikuwa na lengo la kupata ukweli wa malalamiko dhidi ya Katibu Mkuu kuhusiana na uwekaji wa fedha za Jumuiya kwenye kampuni binafsi ya M/S Vision Invesment pamoja uwepo wa wafanyakazi wasio na mikataba ya kazi kwa kipindi kilichoanza 2010 mpaka 2017.

a) **Matumizi mabaya ya fedha za Uwekezaji Shilingi 284,599,600**  
 Ilibainika kuwa ALAT ilitumia jumla ya Shilingi 284,599,600 kwa matumizi ya yasiyo ya Maendeleo kati ya 16/6/2012 hadi 22/3/2013 bila kibali kutoka Mkutano Mkuu wa Mwaka au Kamati ya Utendaji.

Fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Uwekezaji wa ALAT. Matumizi ya fedha nje ya malengo yaliyokusudiwa yanaonesha

kutokuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha na inaweza kuvutia matumizi mabaya ya fedha za Umma.

b) Kuwasilishwa kwa taarifa za benki zilizoghushiwa

Nilibaini kuwa Mhasibu wa ALAT aliwasilisha taarifa za kibenki na miamala kwa lengo la kuficha uhalisia wa taarifa za kibenki za ALAT.

Mhasibu alishindwa kuwasilisha miamala ya kibenki na salio katika akaunti ya benki ya uwekezaji yenye namba 0150210630300 katika benki ya CRDB.

c) Malipo yasiyo na nyaraka Shilingi 3,769,667,891.27

Ukaguzi maalum umegundua kuwa malipo yenye thamani ya Shilingi 3,769,667,891.27 yanayojumuisha masurufu ambayo hayakurejeshwa, fedha zilizochepushwa pamoja na madeni hayana viambatisho vya kuthibitisha uhalali wake. Orodha imeonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 88: Malipo yasiyo na nyaraka**

Na.	Maelezo	Kiasi Shilingi
1	Kati ya masurufu yaliyotolewa ya kiasi cha Shilingi 210,650,000 kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Tanga, kipekee Shilingi 167,414,000 zimerejeshwa zote na kuacha bakaa ya Shilingi 43,335,950	43,335,950
2	Masurufu yaliyochukuliwa kwa ajili ya Mkutano Mkuu kati ya mwaka 2011 na 2015 hayakurejeshwa	20,000,000
3	Masurufu yaliyotolewa ni Sh 240,000,000, kati ya hizo Sh 163,055,780 zilirejeshwa na kuacha salio lisilorejeshwa la Shilingi 76,944,220	76,944,220
4	Masurufu yaliyochukuliwa kwa ajili ya shughuli za kiofisi Shilingi 863,467,563.27 hayakurejeshwa.	863,467,563
5	Masurufu kwa ajili ya mkutano wa Bukoba hayakurejeshwa	4,838,790
6	Matumizi mabaya ya fedha za maafa Bukoba	7,520,000
7	Madeni mbalimbali yasiyo na viambatisho	2,753,561,369
	<b>Jumla</b>	<b>3,769,667,892</b>

Nahitimisha kuwa mawanda ya ukaguzi yamezuiwa na hivyo matumizi ya Shilingi 3,769,667,891.82 hayakuweza kuthibitishwa. Hii inaonyesha kuwa matumizi hayo yanaweza yasiwe halali na yametumika kwa kazi binafsi.

d) Fedha za Jumuiya zilizowekwa kwenye Akaunti binafsi ya M/S Vision Investment Shilingi 150,000,000

Menejiment ya Jumuiya ya Serikali za Mitaa iliingia makubaliano na Kampuni ya M/S Vision Investment mnamo tarehe 10 Machi 2015 kwa ajili ya kutafuta fedha kiasi cha Shilingi 350,000,000 kwa ajili ya kugharamia Mkutano Mkuu wa Jumuiya. Kifungu namba tano (5) cha Mkataba kinamtaka M/S Vision Investment kutafuta vyanzo vya mapato kwa ajili ya kugharamia Mkutano Mkuu, zaidi kiasi cha Shilingi 150,000,000 kilichoahidiwa na Benki ya NMB hakibusiani na makubaliano haya.

Mapitio zaidi yalibainisha kuwa menejimenti ya ALAT kupitia barua yenye Kumb.Na. ALAT/C.10/2/VII ya tarehe 08/01/2015 iliyosainiwa na Mwenyekiti na barua Kumb.Na. ALAT/C.10/2/VII/16 ya tarehe 17/02/2015 iliyosainiwa na Katibu zote zikiitambulisha Kampuni ya M/S Vision Investment kama Mshiriki Mkuu katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

Benki ya NMB iliidhinisha malipo kiasi cha Shilingi 150,000,000 kwenda kwa Kampuni ya M/S Vision Investment kama mchango wake kwa ajili ya kugharamia Mkutano Mkuu wa Jumuiya kinyume na matakwa ya barua yenye Kumb.Na. ALAT/C.10/42.II/3 ya tarehe 11/03/2014 iliyotoka Jumuiya ya Serikali za Mitaa ambayo ilielekeza kuwa fedha zote za Jumuiya ziwekwe kwenye Akaunti namba 2061100067 iliyopo Benki ya NMB Morogoro.

Tangu Kampuni ya M/S Vision Investment iteuliwe kama Mshiriki wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa ALAT kuhusiana na kutafuta vyanzo vya mapato kwa ajili ya shughuli za Mkutano huo, hakuna nyaraka zilizotolewa ili kuthibitisha makusanyo halisi yaliyopokelewa na Mshirika kwa ajili ya mkutano uliotarajiwa, hivyo matumizi mabaya ya makusanyo ya ALAT yaliyotolewa.

Kwa hiyo, sikuweza kuthibitisha ikiwa fedha zilizopokelewa zilitumiwa kwa ufanisi na kiuchumi kwa manufaa yaliyokusudiwa.

Ninaishauri Menejimenti kuhakikisha kwamba mfumo wa Udhibiti wa Ndani unaimarishwa, maafisa waliohusika kwenye amana hiyo

wanaadhibiwa na fedha ambayo haikutumika kiasi cha Shilingi 90,000,000 kinarejeshwa kwa ajili ya shughuli za ALAT kutoka M/S Vision Investment. Pia, taarifa za makusanyo halisi yaliyokusanywa na M/S Vision Investment zinapaswa kutambuliwa na kuwasilishwa kwa ALAT.

- e) Hati za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi Shilingi 3,567,766,421.72

Menejimenti ya ALAT imeshindwa kuwasilisha hati za malipo pamoja na viambatisho vyake vya matumizi vyenye thamani ya Shilingi 3,567,766,421.72 kinyume na kifungu na.43 cha Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Hivyo, mawanda ya ukaguzi yalizuiwa. Bila ya kuwa na hati za malipo na viambatisho vyake uhalali wa malipo yenyeye thamani ya Shilingi 3,567,766,421.72 haukuweza kuthibitishwa.

Kwa maoni yangu, kitendo hiki kinapunguza upeo juu ya mawanda ya ukaguzi, na kinaweza kusababisha udanganyifu katika fedha za Umma na kutumika bila kufuata sheria na taratibu.

Ninaishauri menejimenti kuhakikisha mfumo wa kumbukumbu wa ndani unaimarishwa na kuhakikisha hatua za nidhamu zinachukuliwa kwa maafisa waliohusika na upotevu wa hati hizo za malipo.

- f) Makusanyo ambayo hayakupelekwa benki Shilingi 14,330,000

Matokeo ya ukaguzi maalum katika makusanyo yanayotokana na ada za wazabuni na marejesho ya masurufu ilionyesha kuwa kiasi cha Shilingi 14,330,000 kilikusanywa lakini hakikupelekwa benki na hakikuonyeshwa katika vitabu vya hesabu za ALAT kinyume na matakwa ya kifungu na.39 (2) cha Sheria za fedha za Serikali za Mitaa za mwaka 1982.

Makusanyo yasiyopelekwa benki yanaonesha kuwa fedha hiyo imetumika vibaya. Hii inaathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa kutumia vyanzo vya ndani.

Fedha ni mali adhimu ambayo ni nyepesi kuharibika kuliko mali zote, ALAT haiwezi kuishi na kufanikiwa ikiwa haina udhibiti wa kutosha juu ya fedha zake.

Ushauri wangu kwa Menejimenti ni kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani. Mbali na hatua hiyo, hatua za kinidhamu zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya maafisa wanaohusika pamoja na kurejesha kiasi cha Shilingi 14,330,000.

**g) Udanganyifu uliofanyika katika malipo Shilingi 76,666,835**

Ukaguzi wangu maalum juu ya malipo yaliyofanywa kwa muda huo ulibainisha kuwa, Menejimenti ya ALAT iliidhinisha malipo ya Shilingi 58,501,489 lakini kiasi halisi kilicholipwa ni Shilingi 134,668,324, hivyo kusababisha kutoa fedha benki zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwa Shilingi 76,666,835.

Hali hii inaonesha udanganyifu unaofanywa na Mhasibu akishirikiana na Menejimenti ya ALAT, hasa kutokana na udhaifu juu ya udhibiti wa mfumo wa ndani uliopo na kutokuwapo kwa *kitengo cha ukaguzi wa ndani ndani ya mfumo*.

*Nashauri kwamba udhibiti wa ndani uimarishwe, kitengo cha Mkaguzi wa Ndani kianzishwe kama kichocheo cha kuboresha utawala wa taasisi, udhibiti wa hatari, na udhibiti wa menejimenti kwa kutoa ufahamu na mapendekezo kulingana na uchambuzi na tathmini ya data na mchakato wa biashara.*

Pia, Afisa Masuuli anashauriwa achukue hatua za kinidhamu kwa Mhasibu na Menejimenti kwa kushindwa kutimiza wajibu wao.

**h) Malipo yasiyo na viambatisho Shilingi 558,708,963.77**

Kifungu AP.20 (4.4) cha Mwongozo wa fedha wa mwaka 2013 kinahitaji malipo yote yanayofanywa yawe na viambatisho vinavyotosheleza na Meneja wa fedha aridhike kabla ya kuidhinisha malipo hayo.

Kinyume cha kifungu tajwa hapo juu, malipo ya kiasi cha Shilingi 558,708,963.77 yamefanyika bila ya kuwa na viambatisho muhimu, hivyo uhalali wa malipo hayo umeshindwa kuthibitishwa na ukaguzi.

Kwa maoni yangu, tendo hili linapunguza upeo juu ya mawanda ya ukaguzi na huweza kusababisha udanganyifu katika fedha za Umma na kutumika bila kufuata sheria na taratibu.

Napendekeza kuwa, mfumo wa udhibiti wa ndani uimarishwe sambamba na uanzishwaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani.

zaidi ya hapo, napendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa maofisa waliohusika katika udanganyifu huo.

***Kutokana na matokeo ya ukaguzi huo maalum, nashauri kwamba:***

*Menejimenti ya ALAT iimarishe mifumo ya Udhibiti wa Ndani. Hii ni kwa kuwa udhaifu mkubwa uliotambuliwa umetokana na kushindwa kwa mfumo wa udhibiti.*

*Uchunguzi wa kina, hatua za kisheria na za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa maafisa hao kwa kutotimiza majukumu yao kwa ufanisi, hivyo kusababisha hasara kwa fedha za ALAT.*

*Udhibiti wa ndani kuhusiana na makusanyo ya mapato uimarishwe, na makusanyo yasiyopelekwa benki yenyeye thamani ya Shilingi 14,330,000 yanapatikana na kuwekwa kwenye akaunti husika.*

*Mkataba ulioingiwa kati ya Menejimenti ya ALAT na M/S Vision Investment hauhuishwi upya baada ya kukamilika. Hii ni kwa kuwa, asili yake ya kuwapo si wazi. zaidi, Menejimenti lazima ihakikishe kuwa makusanyo yasiyowasilishwa kiasi cha Shilingi 90,000,000 na M/S Vision Investment yanarejeshwa.*

## **12.2 UKAGUZI WA VYAMA VYA SIASA**

### **12.2.1 Utangulizi**

Kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu 14(1)(b)(ii) cha Sheria za uanzishwaji wa Vyama vya Siasa, Ninawasilisha mapungufu yaliyojitekeza sana katika mawanda yangu ya ukaguzi wakati wa ukaguzi wa vyama vya siasa.

Nastahili kuwahakikisha washika dau wa vyama husika kuwa hesabu zao zimeonesha uhalisi na utekelezaji wa chama pamoja na matakwa ya sheria zinavyohitaji

Nilifanya taratibu za kupata ushahidi kwamba Vyama vya Kisiasa vimetekeleza na sheria zinazohusika kuhusu masuala ya kifedha, usimamizi wa kifedha na masuala mengine yanayohusiana.

Nimezingatia udhibiti wa ndani katika ukaguzi wa hesabu za mwisho za vyama vya siasa. Maoni yangu kwa mambo ambayo hayakuzingatia sheria zilizopo ni kama ifuatavyo:-

- a. Mapungufu katika hesabu zilizowasilishwa chini ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma (IPSAS)

Nilipitia taarifa za hesabu za vyama vya siasa na kuona mapungufu kwa mwaka husika kama inavyoonyeshwa hapo chini:-

- i. Muundo wa uandaaji wa hesabu haukuweza kujulikana kwa sababu hesabu zilizowasilishwa zinaonesha mapato na matumizi na hazikuwa na maelezo ya ujumla ya vyama.
- ii. Taarifa za fedha zinatofautiana na msingi wa uandaaji hesabu na muundo wake ambao ultakiwa utumike wakati wa uandaaji.
- iii. Mpangilio na muda wa hesabu zinatofautiana, na hazingyeshi maelezo sahihi juu ya asili ya kuandaa hesabu hizo.
- iv. Pia sera za hesabu na maelezo ya ziada ya hesabu zilikosekana katika ukaguzi, hivyo kuzuia mawanda ya ukaguzi. Vyama ambayo vimekutwa na mapungufu hayo ni Chama cha Wakulima (AFP), ADC, Chama cha Kijamii (CCJ), Chama cha Demokrasia (DP), Demokrasia Makini na Chama cha Sauti ya Umma ((SAU)).

Kukosekana kwa uwasilishwaji mzuri wa hesabu, kunakwamisha kufikiwakwa lengo la jumla la kufikisha taarifa za mizania ya

fedha, taarifa ya ufanisi wa fedha na taarifa ya mtiririko wa fedha ya chama ambazo ni taarifa muhimu kwa watumiaji kwa ajili ya kufanya maamuzi.

*Ninarejea ushauri wangu kwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa kuwa na programu ya kuwajengea uwezo vyama vya siasa sawa na mahitaji ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya 2009 (R.E 2015) pamoja na Kanuni zake za msingi na mahitaji ya IPSAS.*

*b. Taarifa za fedha hazikuwasilishwa*

Wajibu wa maandalizi na uwasilishaji wa taarifa za kifedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi upo kwa Katibu Mkuu wa Chama. Kifungu cha 14 cha Shera ya Vyama vya Siasa Na.5 ya mwaka 1992 (Toleo liliorekebishwa 2015) Kinakitaka kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kuandaa taarifa nzuri za fedha na taarifa ya mali za chama. Pia kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya mwaka ya hesabu za chama iliyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na taarifa ya hesabu na tamko la kila mwaka la mali yote inayomilikiwa na Chama.

Kati ya Vyama kumi na tisa (19) vilivyosajiliwa usajili wa kudumu, vyama tisa (9) havikuwasilisha taarifa za fedha za kila mwaka wakati wa tarehe ya kisheria ya tarehe 30 Septemba, kama inavyotakiwa na kifungu cha 14 (1) (i) cha Sheria ya Vyama vya Kisiasa Namba ya 5 ya 1992 (iliyorekebishwa mwaka 1992).

Ikilinanishwa na taarifa zangu zilizopita inaonekana kuna ongezeko la vyama kutoka Vyama vinne (4) mpaka tisa (9) ambavyo havikuwasilisha hesabu zao Hii inaonesha hakukuwa na hatua za kutosha zilizochukuliwa kwa wale ambao hawakuwasilisha kwa mwaka jana.

*Naendelea kuvisisitiza vyama vya siasa kuhakikisha wanazingatia kifungu na.14 (1)(i) cha Sheria ya Usajili wa Vyama vya siasa na.5 ya mwaka 1992 (Iliyorekebishwa 2015)*

*Msajili wa vyama vya siasa anashauriwa kuwa na mpango wa ufahamu na kujenga uwezo kwa vyama vya siasa juu ya umuhimu wa maandalizi na uwasilishaji wa taarifa za kifedha. zaidi,*

*ninarudia ushauri wangu kuwa Msajili lazima awawajibishe viongozi wa vyama vilivyoshindwa kuwasilisha taarifa zao za kifedha kwa lengo la ukaguzi.*

c. Kutokuwa na rejista ya mali za kudumu Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Vyama vinne (4) ambavyo ni CHADEMA Kanda ya Magharibi, NLD, Demokrasia Makini na ADC havina daftari la mali za kudumu.

Kukosa daftari la mali za kudumu ni kinyume na kifungu na.14(1)(b)(ii) cha Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa na.5 ya mwaka 1992 (Iliyorekebishwa 2015) inayovitaka vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu kuwasilisha kwa Msajili tamko la mali zote zinazomilikiwa na Chama kila mwaka.

Kushindwa kuweka daftari la mali za kudumu kunaleta ugumu wa kujua mali za chama, aina yake, gharama na sehemu ilipo, hivyo kuziacha mali za Chama kwenye hatari ya kuibiwa au kutumika vibaya.

*Ninashauri kuwa Vyama vya Siasa viwe na madaftari ya mali za kudumu ambayo yanahuishwa mara kwa mara kutokana na mununuizi au mauzo ya mali.*

d. Kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki Udhibiti wa ndani unaohusiana na usuluhishi wa salio la vitabu vya fedha na salio la benki haukutekelezwa vizuri. Ufanyaji mara kwa mara wa usuluhishi wa kibenki unagundua mapungufu mapema, hivyo kurahisha na kufanya marekebisho. Inaweza, Pia husaidia kutambua ubadhirifu au makosa.

Hata hivyo ilionekana kuwa vyama havifanyi usuluhishi wa kibenki mara kwa mara. Niliona kuwa usuluhishi kati ya salio la daftari la hesabu na salio la benki haukufanywa kwa Vyama vitano (5) vya Siasa ambavyo ni Chama cha kidemokrasia (ADC), Demokrasia Makini, Chama cha Sauti ya Umma (SAU), na NLD. Bila kufanya usuluhishi wa kibenki makosa hayawezi kugunduliwa na kurekebishwa mapema, hivyo kusababisha taarifa za fedha kuwa na makosa.

*Menejimenti ya Vyama vya Siasa ihakikishe kuwa inaweka utaratibu wa kufanya usuluhishi wa kibenki na maafisa husika wanapitia vizuri na kuhakiki miamala ya benki na vitabu vya hesabu ili kurekebisha makosa katika hatua za mwanzo.*

e. Malipo yenyne nyaraka pungufu Shilingi 735,978,559 Nimebaini vyama vya siasa vitatu (3) kati ya vyama tisa (9) vilivyokaguliwa vina malipo yenyne nyaraka pungufu zenye thamani ya Shilingi 735,978,559 ambayo ni kinyume na miongozo ya kiuhasibu pamoja na kanuni na. 86(1) na kanuni na.95 (4) ya Kanuni za fedha za Umma za mwaka 2001 ambazo zinalekeza kila malipo yawe yameambatishwa na nyaraka sahihi. Hivyo mawanda ya ukaguzi yamezuiwa; hata hivyo, uhalali wa malipo yenyne thamani ya Shilingi 735,978,559 umeshindwa kujulikana. Orodha la malipo yameonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:-

#### Jedwali Na. 89: Malipo yenyne nyaraka pungufu

Na	Chama	Malipo yenyne nyaraka pungufu kwa mwaka			
		2014/2015	2015/2016	2016/2017	Jumla
1	CHADEMA	276,795,959	128,884,000	240,163,600	520,443,559
2	SAU	0	0	639,100	639,100
3	ADC	0	58,175,900	31,320,000	89,495,900
<b>JUMLA</b>		<b>276,795,959</b>	<b>187,059,900</b>	<b>272,122,700</b>	<b>735,978,559</b>

*Chanzo:* Barua za mapungufu kwa kila Chama 2016/2017

*Navishauri vyama vya siasa kutii mahitaji ya miongozo ya fedha na kanuni na.86 (1) na kanuni na.95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kwa kuhakikisha malipo yote yana viambatisho vya kutosha.*

f. Masurufu ambayo hayakurejeshwa Shilingi 558,915,600 Nimekagua matumizi ya fedha ya CHADEMA na kubaini kuwa, masurufu kiasi cha Shilingi 400,038,600 kililipwa kwa waajiriwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za ofisi.

Nilibaini kuwa kiasi hicho cha masurufu Shilingi 400,038,600, mwaka 2014/2015 (Sh 20,900,100) na mwaka 2015/2016 (Sh 379,138,500) hakikurejeshwa wala kutambuliwa kama madai katika taarifa ya mizania ya fedha kwa mwaka tofauti na

maelekezo ya kifungu 9.3.1 mpaka kifungu 9.3.6 cha Miongozo ya kiuhasibu ya terehe 25 Aprili, 2012. Hivyo, nilishindwa kutambua kuwa malipo hayo yalitumika kwa malengo kusudiwa.

Mbali na hayo, ukaguzi wangu wa marejesho ya mikopo kwa mwaka 2014/2015 umebaini kuwa kiasi cha Shilingi 158,877,000 kilirejeshwa kutokana na mikopo iliyokuwa imetolewa kwa wafanyakazi wa Chama.

Hata hivyo, hakukuwa na mkataba wala nyaraka zinazothibitisha uhalali wa marejesho hayo, na kama yamerejeshwa kulingana na makubaliano.

*Naishauri menegimenti ya CHADEMA iendelee kusimamia na kuendana na miongozo ya fedha inayotaka urejeshwaji wa masurufu baada ya kuisha kwa shughuli tarajiwa.*

- g. Mkopo ambao haukuthibitisha mapokezi yake ndani ya Chama Shilingi 2,000,000,000

Mnamo tarehe 11 Aprili 2015, menejimenti ya CHADEMA (Mkopaji) iliingia makubaliano na mwanachama wake (mkopeshaji) kuhusu kukopeshwa kiasi cha Shilingi 2,000,000,000 kwa shughuli za Chama.

Hakuna nyaraka zinazoonesha kuwa kiasi cha mkopo walichokubaliana kilitolewa na kupokelewa na Chama husika. zaidi niliona kwamba, ankara ya kodi (tax invoice) na.201508226 ya terehe 26 Agosti 2016 ya kiasi cha Shilingi 866,600,000 ililipwa na mwanachama kwa niaba ya Chama kwa ajili ya mabango ya matangazo yaliyoletwa na mzabuni M/S Milestone International Co. Ltd. Nje ya hilo deni, kiasi cha Shilingi 715,000,000 kililipwa kwa mwanachama kama marejesho ya fedha iliyokopwa kulipia ununuza wa mabango bila ya kuambatishwa makubaliano ya kisheria. Yote hii ni kwa sababu chama hakijaandaa sera ya mikopo.

- h. Makusanyo ambayo hayakupelekwa benki Shilingi 2,302,305,500

Kwa kупingana na kifungu na.15 (1) cha Sheria ya Usajili wa Vyama vya siasa, CHADEMA kimeshindwa kupeleka makusanyo yake katika benki inayosimamiwa na wadhamini wa chama

Ukaguzi wangu wa taarifa za makusanyo ya chama umebaini kiasi chs Shilingi 2,302,305,500 (Sh 4,420,000 kwa mwaka 2014/2015 na Sh 2,297,885,500 kwa mwaka 2015/2016) zilikusanywa kutoka kwa wanachama lakini hazikupelekwa benki na matumizi yake hayakutolewa kwa ajili ya ukaguzi.

Kutokupeleka makusanyo benki kunaonesha Chama kutokuwa na mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani ambao utapelekea makusanyo kuwa katika hatari ya kutumika vibaya.

*Naishauri menejimenti ya chama ihakikishe makusanyo yote yanapelekwa benki bila kuchelewa pindi yanapokusanywa.*

- i. Manunuzi yaliyofanyika bila ushindanishi Shilingi 2,130,452,577.28

Nimebaini kuwa CHADEMA kimefanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Shilingi 24,216,625,390 ambayo yanakinzana na kifungu cha 16.2.2 cha Muongozo wa fedha za Chama ambacho kinaeleza kuwa “manunuzi yote yafanyike kwa ushindanishi baada ya kujihakikishia ubora, uzoefu na uwezo wa mzabuni na Mhasibu ahakiki na kuchukua fomu tatu za ushindanishi wa bei kutoka kwa wazabuni tofautitofauti.

Kushindwa kuchukua fomu za ushindanishi wa bei, kunakiingiza chama katika hatari ya kutumia vyanzo vyake vibaya.

*Naishauri menejimenti ya Chama ihakikishe inazingatia Miongozo ya fedha ili kuhamasisha ushindani na uwazi katika manunuzi kwa ajili ya kupata thamani ya fedha ya bidhaa au huduma inayonunuliwa.*

- j. Mikopo ya Maendeleo kwa makampuni isiyo na faida Shilingi 12,011,038,049.

Ukaguzi wangu wa taarifa za fedha ulibainisha kuwa CCM iliendelea kuwekeza katika makampuni 4 mikopo ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi 12,011,038,049.61. Hata hivyo, tumejifunza kwamba mikopo hiyo haina faida yoyote iliyooonekana imeingia kwenye Chama. Pia, ilibainika kuwa, Shilingi 80,000,000 zilitambuliwa kama mapato ya uwekezaji katika taarifa za fedha kutoka kwa Jitegemee Trading Company

Limited lakini hazikuwa na kiambatisho kinachothibitisha kama ni gawio au kitu kingine.

Bila kuanzisha sera ya uwekezaji, uwekezaji wa Chama upo katika hatari ya kutumiwa vibaya na malengo yaliyowekwa yanaweza yasifikasiwe kama ilivyopangwa.

*Ninashauri menejimenti ihakikishe kuwa sera ya uwekezaji inaanzishwa kwa usimamizi sahihi wa uwekezaji wake.*

k. Mikopo ya uwekezaji haikuwa na viambatisho Sh 455,974,146,90

Fungu 14-16 ya viwango vya kimataifa vya uandaaji hesabu (IFRS 12) 'Ufafanuzi wa Maslahi katika vyombo vingine' inahitaji taasisi kufungua masharti ya mipango yoyote ya mkataba ambayo inaweza kuhitaji kampuni mama kutoa msaada wa kifedha, kiasi na malengo ya kutoa msaada wa fedha kwa matawi yake.

Hata hivyo, nilibaini kupitia ukaguzi wa taarifa za fedha za CCM kwa mwaka 2016/2017 kuwa, haina taarifa za kutosha juu ya mikataba, masharti, kiasi na sababu za kutoa msaada wa kifedha wa Shilingi 455,974,146.90 kwa Radio Uhuru kinyume na fungu 14-16 ya IFRS 12. Kwa hiyo, siwezi kuthibitisha mikopo ya maendeleo iliyօenda kwenye matawi hayo.

*Menejimenti inashauriwa kuzingatia Viwango vya kimataifa vya uandaaji hesabu (IFRS 12) kwa kuonesha mpangilio wa mkataba, masharti, kiasi na madhumuni ya msaada wa kifedha wa Sh 455,974,146.90 iliyotolewa kwa Radio Uhuru kwa mwaka.*

l. Mikopo ya ndani ambayo haikurejeshwa Sh 337,143,334

Mapitio yangu ya taarifa za kifedha yalibaini kuwa menejimenti ya CCM ilikopa na kuhamisha fedha kiasi cha Sh 337,143,334.15 kutoka akaunti ya malipo ya pensheni kwenda Akaunti ya Katibu Mkuu wa Chama na kupokelewa kwa stakabadhi namba 156424. Hata hivyo, kiasi hicho hakijarejeshwa hadi wakati huu wa ukaguzi Februari 2018; matokeo yake, madai ya wafanyakazi wastaa fu yanaweza yasilipwe kwa wakati.

### *Ukaguzi wa Vyama vya Siasa*

*Naishauri menejimenti ihakikishe kuwa kiasi kilichokopwa kinarejeshwa kwenye akaunti husika.*

*Namkumbusha Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa kushirikiana na wadau wa vyama vya siasa, kukamilisha kuandaa muundo wa uandaaji wa hesabu za vyama. Kuwa na mfumo mmoja wa muundo wa uandaaji hesabu utakaopelekea kuwa na muendelezo unaofanana na usawa kwa kuandika miamala na maandalizi ya uandaaji                wa                hesabu                za                vyama.*

Sura ya Kumi na Mibili

## SURA YA KUMI NA TATU

### 13.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 13.1 Maelezo ya jumla

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo ya jumla kwa masuala yaliyojitokeza kwenye taarifa hii ambapo yanahitaji mpango kazi na kushughulikiwa na Serikali, Bunge pamoja na Menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu. Mapendekezo haya kwa sehemu kubwa yametokana na taarifa za Ukaguzi za taasisi husika zilizowasilishwa kwa kila Afisa Masuuli wakati wa ukaguzi pamoja na maswala mengine ya muhimu ambayo umma unapaswa kuyafahamu.

#### 13.2 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya yaliyopita

Ili kuwa na Uwazi, Uwajibikaji, Utawala Bora, Usimamizi na kufuata sheria na kanuni ambazo hatimaye huhakikisha matumizi bora ya rasilimali za Umma, inakuwa muhimu sana kutekeleza mapendekezo ya CAG na maelekezo ya PAC na hivyo kufanya jukumu la CAG na uwajibikaji kwa PAC kuwa na maana.

Wakati wa ukaguzi wa hali ya utekelezaji katika mapendekezo ya CAG ya mwaka uliopita na maagizo ya PAC, nimebainisha kuwa kuna maboresho kwa kutekeleza mapendekezo yangu na maagizo yaliyotolewa na PAC. Hata hivyo, mapendekezo mengi na maagizo bado yapo katika hatua ya utekelezaji. Kwa hiyo, ninawahimiza Maafisa Masuuli husika kuhakikisha maagizo yaliyo katika hatua ya utekelezaji yanatekelezwa kikamilifu. Vivyo hivyo jitihada nyingi zinahitajika ili kuhakikisha mapendekezo na maelekezo yote yanatekelezwa.

Kwa hiyo, ninawashauri Maafisa Masuuli kuanzisha vitengo imara vya Ukaguzi ambavyo vitakuwa na wataalamu mbalimbali ili kutekeleza mapendekezo na maelekezo ipasavyo. Hii iendane na kuimarisha kwa mifumo ya Udhibiti wa Ndani ambayo ni sababu inayochangia madhaifu katika usimamizi.

### 13.3 Usimamizi Wa Fedha Za Umma

Makusanyo ya ndani ya mapato yameonyesha mwenendo mzuri kwa miaka minne mfululizo. Licha ya kuongeza matarajio ya mapato na ukusanyaji bado Serikali imeweza kupata asilimia 62.50 tu ya bajeti iliyoidhinishwa mwaka 2016/17 ambapo mwaka 2015/16 Serikali iliweza kutoa asilimia 62.58 ya bajeti yake. Hii inaonyesha kwamba, makadirio yote kwa jumla ya makusanyo na matumizi yameongezeka lakini mapato kutoka kwenye kodi kwa ajili ya kugharamia bajeti bado ni sawa licha ya hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuongeza mapato ya kodi.

Kukopa haswa mikopo ya ndani ina athari kubwa kwenye uchumi katika mambo yafuatayo: Kwa Serikali ina athari kwenye riba ambayo itatakiwa kulipwa na vile vile ina athari katika kiwango cha kukopesha kutoka katika mabenki ya kibiashara. Katika mwaka huu wa ukaguzi, Serikali imekopa kutoka vyanzo vyatatu kwa asilimia 10.08 zaidi ya bajeti iliyopitishwa. Riba inayotakiwa kulipwa kwenye amana za muda mfupi kwa ajili ya kugharamia kwa mwaka huu ni asilimia 11.51 na amana za muda mrefu ni asilimia 30.25 ambayo ni tofauti ya thamani ya amana (face value) na gharama ya amana (cost value). Deni la nje huwa linaathiriwa na kiwango cha ubadilishwaji wa fedha, kwahiyiko kugharamia bajeti kwa kutumia mikopo ni gharama sana.

Serikali inahimizwa kuchunguza vyanzo vingine vyatatu kwa mapato au kutafuta njia bora ya kutumia, ushirikiano wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kama njia ya kuhamisha baadhi ya majukumu ya sekta binafsi na kupunguza gharama ya endeshaji wa bajeti kwa kutumia mikopo na Misaada. Shughuli nyingi za maendeleo zinapaswa kufanyika kwa ushirikiano wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya Umma ambayo itasababisha upatikanaji wa kazi kwa urahisi na ubora na itasaidia kuongeza kiwango cha maisha ya wananchi na kutengeneza fursa nyingi za ajira.

Katika kupitia utoaji wa leseni katika migodi iliyoko Mwanza, Kahama na Shinyanga niligundua kuwa kuna kampuni zinachenjua madini bila kuwa na leseni. Kufanya kazi bila kuwa na leseni kunaikosesha Serikali mapato ya Dola 104,400 sawa na Shilingi 231,663,600 kwa mwaka.

Kiasi cha Shilingi 14,546,473,044.63 kilikusanywa katika ofisi za Balozi 21, lakini iligundulika kuwa mapato hayakuhamishwa kwenda mfuko kuu wa Serikali hivyo kunainyima Serikali fursa ya kuzitumia na pia kuna leta ushawishi wa kutumika vibaya.

#### **13.4 Deni la Taifa**

Mapungufu mengi yaliyojitokeza mwaka huu, yalijitokeza pia miaka iliyopita, hii inaashiria kuwa serikali imekuwa na umakini hafifu katika utekelezaji wa mapendekezo yangu. Kama nilivyoeleza awali mapungufu mengi kwenye deni la taifa yanababishwa na kukosekana kwa muundo wa kufuatilia madeni ulioimara. Mapungufu hayo ni pamoja na Kushushwa Kiwango cha Deni la Taifa, Ukuaji hafifu wa dhamana za Serikali katika soko la mtaji, Mikopo iliyosainiwa mikataba lakini haijapokelewa, Mapungufu katika utaratibu wa kuingiza kumbukumbu za mapokezi ya mikopo, Usimamizi usioridhisha wa mikataba ya mikopo iliyofaulishwa ‘on-lending contracts’

*Kwa kuzingatia hayo, napendekeza serikali ifanye yafuatayo; (i) kuharakisha utoaji dhamana isiyo ya fedha kwa mifuko ya pensheni ili kuwezesha madeni yake kuingia katika kasma ya deni la taifa,, (ii) Itenge sehemu ya mapato ya ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya deni la ndani ili kupunguza kiwango kinachohuishwa kila mwaka, (iii) kuweka utaratibu thabiti wa kufuatilia na kutathmini mapokezi na matumizi ya fedha zitokanazo na deni la taifa, (iv) kupata kutoka kwa wanufaika uhakika wa mapokezi ya fedha za mikopo kabla ya kuingiza kumbukumbu hizo katika mfumo wa kutunza kumbukumbu za madeni (CS-DRMS), (v) kuhakikisha usuluhishi wa viwango vya mikopo iliyofaulishwa ili kutunza kumbukumbu sahihi baina ya pande zote zinazohusika na utunzaji wake. na (vi) Kutekeleza*

*pendekezo langu la muda mrefu la kuanzisha ofisi ya pamoja ya kusimamia shughuli za deni la taifa.*

### **13.5 Tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala bora**

Katika kutathmini mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala bora, nilijikita zaidi kwenye tathmini ya kamati za ukaguzi, ukaguzi wa ndani, usimamizi wa vihatarishi kwenye mifumo ya TEHAMA, tathmini ya kutambua na kuzuia udanganyifu, changamoto kwenye utekelezaji wa Sheria ya utwaliwaji na upatikanaji tena wa mali pamoja na masuala ya utawala bora.

Ninashauri Serikali iendelee kufuatilia na kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani kwa kuwa na utaratibu madhubuti ambao utasaadia kuongeza ufanisi na umakini katika kupunguza mapungufu yaliyojitekeza. Pia, ninashauri menejimenti za taasisi zilizokaguliwa kuweka udhibiti makini wa kufuatilia mapungufu kwenye mfumo wa udhibiti wa ndani na kuhakikisha kuwa mapungufu hayo hayajitokezi tena.

### **13.6 Usimamizi wa raslimali watu na mishahara**

Wizara, Idara, wakala, Sekretarieti za mikoa na ofisi za balozi zimeendelea kuwa na mapungufu yaliyojitekeza kwenye kaguzi za nyuma kwenye eneo la usimamizi wa raslimali watu na mishahara. Mapungufu yaliyojirudia ni pamoja na; mapungufu kwenye usimamizi wa mishahara, malipo ya mishahara kwa watumushi ambao hawapo tena kwenye utumishi wa umma, kutowafanya tathmini ya utendaji watumishi wa umma, kuchelewesha kuwasilisha makato ya kisheria ya mishahara kwenye mifuko/taasisi husika, watumishi wa Umma kupokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria, upungufu wa watumishi kwenye taasisi nyingi na kutokufanyika kwa mikutano ya baraza la wafanyakazi.

Hivyo, nashauri Maafisa Masuuli wote kwa kushirikiana na Ofis ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhakikisha kuwa mapungufu yote yaliyojitekeza kwenye ripoti

hii yanapatiwa ufumbuzi na kuhakikisha kuwa taarifa za wafanyakazi kwenye mifumo zinapitiwa mara kwa mara na kuondoa zile ambazo hazistahili katika ngazi zote za kila taasisi. Pia kuhakikisha kuwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma pamoja na sheria na kanuni nyingine zinazohusiana na usimamizi wa rasilimali watu zinazingatiwa.

### **13.7 Ukaguzi wa Wakala Wa Serikali, Bodi za Mabonde ya Maji, Mifuko Maalaumu ya Fedha na Taasisi Nyingine**

Katika sura ya nane nimekagua Wakala wa Serikali 35, Bodi za Mabonde ya Maji 13, Mifuko Maalumu ya Fedha 17 and Taasisi nyingine za Serikali 38.

Wakala za Serikali zimeendelea kuwa tegemezi kwenye fedha za Serikali ili kujiendesha. Nashauri Wakala hawa kuboresha utoaji wa huduma zao, kuangalia upya tozo wanazotoza katika huduma zao, kutumia njia mpya za kisasa za kibiashara katika utoaji wa huduma na kubuni njia mpya za kuongeza mapato yao ili Wakala hizi ziweze kujiendesha na kupunguza wa ruzuku toka Serikalini.

Katika mapungufu yaliojitokeza katika matumizi yasiozingatia taratibu za kibajeti, manunuzi yasiofuata kanunu za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013, utekelezaji wa mikataba na matumizi yote yasiofuata Sheria ya Fedha ya umma ya mwaka 2001. Nimebaini kuwa mapungufu yote haya yamekuwa yakijirudia mara kwa mara na nimekuwa nikishauri mara kwa mara namna ya kuepukana na mapungufu haya. Nasisitiza kwa Watendaji wakuu wote wa Serikali kutekeleza shughuli zao kulingana na kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2013, Sheria ya Fedha ya Umma 2001 (iliyorejewa 2004) pamoja na Sheria za kodi, pamoja na kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani ilikudhibiti mapungufu yaliojitokeza.

Katika ukaguzi huu nimebaini upungufu wa fedha zilizotolewa na serikali kutekeleza bajeti za matumizi ya kawaida pamoja na bajeti ya maendeleo. Naishauri Serikali kutoa fedha kama ilivyoidhinishwa katika bajeti na pia naishauri serikali kuzitoa fedha hizo kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za

Serikali. Pia nazishauri Wakala na Taasisi zote za Serikali kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kilipa Madeni ya Serikali kuzuia kulipa adhabu zinazotokana na madeni hayo.

Katika Utekelezaji wa shughul za Mifuko ya fedha ya Serikali katika kutoa Mikopo, nazishauri menejimenti za Mifuko hii, kufuatilia kwa ukaribu, mikopo yote iliyotolewa kwa muda mrefu na kuhakikisha wakopaji wote wanalipa madeni yao ili fedha hizo zitumike kuwanufaisha watanzania wengine. Pia nazishauri menejimenti za mifuko hii kutimiza malengo ya Mifuko hii kama ilivyoanzishwa

Ninazishauri Bodi zote za Mabonde ya maji kutohamisha fedha kwenda wizara ya Maji na Umwagiliaji, Na zile zilizopelekwa Wizarani zirudishwe ili fedha hizo zitumike katika kutekeleza shughuli za Bodi hizo. Pia naishauri serikali kuhakikisha kuwa inatoa fedha za utekelezaji wa shughuli za Bodi za Mabonde ya Maji kwa wakati.

### **13.8 Manunuzi Na Usimamizi Wa Mikataba**

Katika mwaka huu wa ukaguzi nimeweza kukagua Manunuzi na usimamizi wa mikataba kwenye Wizara, Balozi, Wakala za Serikali, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 na Kanuni za 2013 pamoja na miogozo mbalimbali inayotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi (PPRA).

Katika ripoti hii zipo pia hoja za PPRA na Kurugenzi ya Mhakiki Mali wa Serikali.

Licha ya kuwapo kwa sheria, baadhi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Balozi bado hazizingatii kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013.

Kwa ujumla zifuatazo ni hoja zilizobainika wakati wa ukaguzi; Kuna manunuzi yaliyofanyika ambayo hayakuidhinishwa na Bodi ya Manunuzi; ilibainika kazi zimefanyika, bidhaa zimenunuliwa na huduma kutolewa bila ya kuwepo kwa mkataba wa aina

yoyote kati ya Taasisi ya Serikali na wazabuni na wakandarasi, pia ilibainika kuwa kufanyika kwa malipo kwa ajili ya Kazi mbalimbali, huduma na bidhaa kabla ya huduma kutolewa, vile vile kuna bidhaa na huduma mbalimbali ambazo zilipokelewa na Taasisi za Serikali ambazo hazikukaguliwa na Kamati inayohusika na Ukaguzi pamoja na Upokeaji wa bidhaa; kuna huduma na bidhaa mbalimbali zilinunuliwa kutoka kwa wazabuni ambao hawajasajiliwa; ilibanika baadhi ya mikataba na miradi haikutekelezwa vizuri; kuna baadhi ya mikataba na miradi ambayo imechelewa kukamilika ambayo inaleta mashaka kuwa bei yaweza kubadilika; tulibaini kuwa kuna manunuzi ya bidhaa, vifaa, kazi na huduma ambazo zilifanyika kwa fedha taslim au kwa njia ya kutumia masurufu; pia kuna manunuzi ambayo yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka; nilibaini baadhi ya manunuzi ya bidhaa na mafuta kufanyika lakini hayakuingizwa kwenye leja ya vifaa na leja ya mafuta na pia mafuta hayakuingizwa kwenye daftari la kuratibu mwenendo wa safari za gari, kwa hiyo utumiaji haukuweza kujulikana.

Manunuzi ya Umma ni nguzo muhimu ya kimkakati katika utoaji huduma Serikalini. Kutokana na Manunuzi ya Umma kutumia kiasi kikubwa cha fedha za Serikali, usimamizi wake ni muhimu katika kukuza ufanisi wa sekta ya Umma. Matukio mengi yaliyopita ya rushwa yalibaini kuwa Manunuzi ndiyo eneo hatarishi kwa rushwa na ufujaji wa fedha. Matukio ya rushwa katika manunuzi si tu kwamba husababisha hasara, bali huharibu taswira ya taasisi katika eneo la uaminifu katika kutoa huduma kwa jamii.

Kwa hiyo, kutokana na hoja nilizobaini kwenye manunuzi na usimamizi wake nazishauri Taasisi za umma kuhakikisha kwamba zinazingatia kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya 2011 na Kanuni zake za 2013 pamoja na miongozo mbalimbali inayotolewa na PPRA mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na thamani ya fedha, uwazi zaidi na thamani ya fedha iweze kupatikana katika manunuzi yanayofanyika. Pia nashauri menejimenti za Taasisi husika zizingatie kikamilifu ushiriki wa

Bodi ya Zabuni katika kuidhinisha manunuzi ili kuepuka manunuzi yasiyo kuwa na tija au mikataba isiyo kubalika kisheria.

### **13.9 Mapungufu yariojitekeza katika Matumizi ya fedha za Umma**

Licha ya mapendekezo niliyokwishayatoa mara kwa mara katika ripoti zangu za miaka ya nyuma, nimebaini kuwa, baadhi ya Wizara, Idara za Serikali, na Sekretariati za Mikoa zinaendelea kuwa na mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani usio na ufanisi juu ya usimamizi wa matumizi ambayo husababisha makosa kama ilivyoelezwa katika Sura ya kumi ya taarifa hii.

Nawashauri Afisa masuuli wa Wizara, Idara za Serikali, Balozi pamoja na Sekretariati za Mikoa kuhakikisha kuwa mifumo yao ya ndani ya uthibiti inaboreshw, ikiwa ni pamoja na kuapeleka watumishi wao katika mafunzo mbalimbali ili kuwajengea uwezo zaidi. Utunzaji wa nyaraka za matumizi unatakiwa kuboreshwa zaidi ili kuendana na matakwa ya Sheria na Kanuni za Fedha za Umma.

Ninamshauri Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wakuu wa Wizara, Sekretariati za mikoa pamoja na Benki Kuu, kuhakikisha Wahasibu wakuu wa Wizara na Sekretarieti za Mikoa wanauwezo wa kupata taarifa zao za kibenki ili kuwarahisishia Wahasibu wakuu kufanya usuluhishi wa taarifa za benki kila mwezi. Najua kuwa Wizara zote zinatumia Akaunti moja ya Amana, Akaunti ya Maendeleo na Akaunti ya Matumizi ila kuna uwezekano wa kila muamala kwenye kila Akaunti ya Benki kuwa na kifungu chake ili kuiwezesha Benki kutoa taaarifa za Kibenki kwa kila Wizara kwa sababu kila wizara itakuwa nambari yake ya utambuzi.

Kwa sasa idara ya CPO ndo inafanya usuluhishi wa taarifa za kibenki kila mwezi kwa niaba ya Taasisi zote,hii ina mapungufu mengi kwa sababu inaweza kushindwa kujua kutokukubaliana kwa taarifa kumetokea kwenye Taasisi ipi,lakini kama usuluhishi wa taarifa za kibenki ungekuwa unafanywa na wahasibu wakuu husika wangeweza kujua kwa urahisi. Pia kushindwa kufanya

usuluuhishi wa taarifa za kibenki, kunaweza kusababisha kushindwa kujua salio sahihi la fedha katika akaunti ya wizara husika ambayo imeoneshwa katika taarifa za fedha.

Pia Namshauri Mhasibu Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia upya Mfumo mzima wa EPICOR ili kuendana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Mfumo Usio wa Taslim (IPSAS-Accrual), kwa sasa Mfumo wa Epicor umezuiliwa kurekodi LPO au Hati za Madai ikiwa hakuna fedha yoyote ilioingizwa.

Pia nashauri kuwepo na upitishwaji wa makisio ya fedha zitakazotumika kulipia madeni ya miaka iliyopita na makisio hayo yapitishwe na kamati za bunge tofauti na utendaji wa sasa ambapo malipo ya madeni mbalimbali yanafanyika kwa kutumia utaratibu wa kubadili matumizi kutoka katika Fungu mbalimbali. Vilevile wakati wa ulipaji wa madeni, Afisa Masuuli kufanya malipo katika vifungu tofauti na makadirio ya mwaka husika.

### **13.10 Changamoto katika utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi usio wa taslim.**

Ripoti zangu za awali zilionyesha mapendekezo kadhaa juu ya kasi ya utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi usio wa taslim katika kutambua na kuripoti Mali za Kudumu. Mapungufu bado yanaonekana katika ripoti hii ikiwa ni pamoja na kutambua na kuripoti mali zisizoonekana, bajeti ya kitaifa inaandaliwa chini ya msingi wa taslim wakati taarifa za kifedha zinaandaliwa chini ya msingi usio wa taslim, taarifa za ardhi na majengo kama kitu kimoja, mali iliyoandikwa katika rejista bila thamani, mali kutokuwepo kwenye rejista hivyo kutoripotiwa, kutokuthaminisha ardhi, kutokuripoti uchakavu wa Mali za Kudumu kwa miaka ya nyuma, kuripoti ya Mali za Kudumu zenye thamani ya chini ya kiwango kilichoidhinishwa, mkanganyiko katika kuripoti Mali za Kudumu kwa kutumia gharama za awali na kuthaminisha pamoja na kutokuufanya Mfumo wa Epicor- IFMS kutoendana na mahitaji ya IPSAS accrual.

Ninapendekeza Serikali kuwa na mipango mzuri ya mafunzo ilioandaliwa mahsusini kwa kuwapa mafunzo wafanyakazi wanaofanya kazi ya usimamizi wa Mali za Kudumu, kutafakari upya taratibu za usimamizi wa Mali za Kudumu na kufanya kazi kwa moduli ya Mali za Kudumu iliyopo katika mfumo wa EPICOR-IFMS.

Nilibaini kwamba taasisi kushindwa kulipa madeni mbalimbali, matokeo yake madeni yameongezeka na kuadhiri makisio ya bajeti mwaka unaofuata.

Ninapendekeza kwa Menegimenti za taasisi mbalimbali kuchukua hatua muhimu ili kusimamia kwa ufanisi madeni na kuhakikisha yanalipwa kwa ukamilifu, hasa madeni ya matibabu.

### **13.11 Ukaguzi wa taarifa za fedha za vyama vyaa siasa**

Nilifanya taratibu za kupata ushahidi kwamba Vyama vyaa Siasa vianzingatia sheria zinazohusika kuhusiana na masuala ya fedha, usimamizi wa fedha na mambo mengine yanayohusiana. Sura ya kumi na mbili (12) ya ripoti hii inatoa maelezo juu ya matokeo juu ya mambo makubwa ambayo hayakuuatana na mambo maalum katika sheria husika na mapendekezo maalum.

Nilifanya ukaguzi wa taarifa za kifedha za vyama vyaa siasa na niliona udhaifu mkubwa katika vyama vingi vyaa siasa kama vile kutokuwepo kwa mfumo wa kawaida wa taarifa za kifedha; kutokufanana kwa msingi wa uhasibu na baadhi hazijaambatishwa na maelezo ya uhasibu na hivyo kupunguza upeo wa ukaguzi.

Ninaishauri menejimenti ya vyama vyaa siasa ili kuhakikisha kuwa mifumo yao ya udhibiti wa ndani inaimarishwa ili kuhakikishiwa kufikia malengo yaliyolengwa.

### **13.12 Matokeo ya ukaguzi maalum**

#### **13.12.1 Ukaguzi Maalum Ukusanyaji Maduhuli/Mapato na Ununuzi wa Kiwanja Katika Idara ya Uhamiaji**

Kuhusu ukaguzi wangu maalum niliofanya, nimejiridhisha kuwa menejimenti ya Fungu 93 kwa njia moja au nyingine walishiriki katika matumizi mabaya ya fedha za umma, usimamizi usiofaa wa nyaraka za uwajibikaji hasa katika makao makuu ya Uhamiaji, RIO Arusha na RIO Tanga kutokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani. Pia, kulikuwa na makosa katika masuala yanayohusu manunuvi ya kiwanja kilichopo Kasumulu, wilaya ya Kyela Mkoa wa Mbeya.

Menejimenti lazima ihakikishe kwamba kiasi ambacho kilitumiwa vibaya cha dola za Marekani (US\$) 127,184 sawa na shilingi za Tanzania milioni 205 zinarejeshwa na kupelekwa benki. Pia, hatua zinazofaa za kinidhamu na za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa waliohusika.

#### **13.12.2 Ukaguzi Maalum wa Chama cha Walimu (CWT)**

Ukaguzi wangu umejiridhisha bila shaka kwamba menejimenti ya Chama cha Walimu, Bodi ya Wadhamini, na menejimenti ya kampuni ya TDCL ni sehemu ya udanganyifu wa mali na fedha za Chama cha Walimu kwa kipindi cha kuanzia 2011 mpaka 2016. Mapungufu katika Mfumo wa udhibiti wa ndani ulichangia sehemu kubwa katika mfumo mbaya wa kuhifadhi kumbukumbu za kutosha za wanachama, mkanganyiko wa sheria juu ya usimamizi wa mali za Chama chini ya Bodi ya Wadhamini, uwepo wa malipo yenye nyaraka pungufu na Malipo yaliyolipwa nje ya bajeti, malipo yasiyoidhinishwa na kutokuzingatia taratibu za manunuvi.

**Kutokana na udhaifu uliotajwa hapo juu, naishauri menejimenti kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani kwa ajili ya kuthibitisha mafanikio ya malengo ya shirika.**

Mbali na kuimarisha udhibiti wa ndani kama hatua ya kukabiliana na udhaifu uliotajwa katika ukaguzi maalum, hatua za kinidhamu na kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa maafisa waliohusika kwa

kutotimiza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kusababisha hasara kwa wanachama.

### **13.12.3 Ukaguzi Maalum wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

Ukaguzi wangu ulijiridhisha kuwa menejimenti ya NIDA, BMTL na Gotham International Limited (GIL) ni sehemu ya udanganyifu wa fedha za NIDA.

Menejimenti ya NIDA inapaswa kuhakikisha kiasi kilicholipwa kwa Kampuni za BMTL (sasa inajulikana kama Copy Cat Tanzania Ltd) (Sh.402,210,885.02), Kampuni ya Gotham International Limited (Sh 167,445,671.91) na dola za Marekani (US\$) 551,500 zilizolipwa kwa Huduma za kisheria ambazo hazikutolewa zinarejeshwa.

### **13.12.4 Ukaguzi Maalum Katika Utekelezaji wa Mradi wa Vituo Vya Polisi vya Mfano Tanzania Chini ya Mpango wa STACA**

Nilifanya taratibu za kupata ushahidi wa ukaguzi husika, nilibaini kuwa menejimenti ya Jeshi la Polisi, Mratibu wa Mradi, wafanyakazi wengine na watoa huduma walihusika kwa matumizi mabaya ya fedha za DFID, matumizi ya fedha tofauti na memoranda ya makubaliano iliyosainiwa.

Pia Vituo vya Polisi vya Mfano vilivyojengwa havikumalizika kutokana na uhaba wa fedha kwa kuwa fedha zilizopokelewa zilikuwa ni ukarabati na sio ujenzi mpya.

#### **Kutokana na mapungufu yaliyojitokeza nashauri kwamba:-**

Menejimenti ya Jeshi la Polisi (TPF) inabidi kuhakikisha kwamba shughuli zote zinatekelezwa kwa kufuata mikataba au Memoranda za Makubaliano ambayo Mpango kazi na Bajeti zilipangwa. Pia kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo itahakikisha kufuata sheria na kanuni wakati wa mchakato wa manunuvi.

### **13.12.5      Ukaguzi Maalum wa Fedha za Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT)**

Ukaguzi wangu umejiridhisha kuwa Menejimenti ya Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT), Benki ya NMB, mzabuni M/S Vision Investment na wafanyakazi wengine ni washiriki wa udanyanyifu uliobainika kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2017. Pia ukaguzi ulibaini mapungufu juu ya Udhhibit wa ndani ambao ulisababisha uwepo wa udanyanyifu na matumizi yasiyo na tija kwa fedha za chama.

**Kutokana na udhaifu uliotajwa hapo juu, naishauri menejimenti kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani, kwa sababu udhaifu mkubwa uliopo ni sababu ya udhibiti wa ndani usiofaa. Pia, hatua za kinidhamu na kisheria zinapaswa kuchukuliwa kwa maafisa hao kwa kutotimiza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kusababisha hasara kwa fedha za ALAT.**

### **13.12.6      Ukaguzi Maalum wa Ujenzi wa Mtandao wa Usambazaji Umeme kwa ajili ya Mradi wa Mtwara (MEP)**

Kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi na ushahidi uliokusanywa, nilijiridhisha kwamba Serikali inatakiwa irudishiwe/Mkandarasi akatwe kiasi cha Dola za Marekani US\$ 8,426,819.33 kutoka katika madai ya kampuni Wentworth Gas Ltd (M/S Umoja Light Company Ltd) kiasi cha Dola za Marekani US\$ 8,121,058. Gharama hizo hazijakidhi matakwa ya kimkataba yaliyopo katika mikataba ya TEF na MICRA.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Na. 2.1: Orodha ya taasisi na aina ya hati zilizotolewa

Taasisi zilizopata hati inayoridhisha		Fungu	2016/17	2015/16
Na	Jina			
1	Ofisi ya Rais - Ofisi ya Ushauri Mafuta na Gesi	11	Hati inayoridhisha	Taasisi mpya
2	Ubalozi wa Tanzania nchini Kuwait	2039	Hati inayoridhisha	Taasisi mpya
3	SUMA - Makao Makuu	Mfuko	Hati inayoridhisha	Taasisi mpya
4	Baraza la Madaktari wa Afya ya Mazingira	TN	Hati inayoridhisha	Taasisi mpya
5	Bodi ya Filamu Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Taasisi mpya
6	Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzanai	Mamlaka	Hati inayoridhisha	Taasisi mpya
7	Mfuko wa Uwekeza Maji Kitaifa National Water Investment	Mfuko	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Taasisi mpya
8	Ministerial Delivery Unit	TN	Hati inayoridhisha	
9	Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale	Mfuko	Hati inayoridhisha	Haikukaguliwa
10	Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe	90	Hati inayoridhisha	Haikukaguliwa
11	Wakala wa Akiba ya Taifa ya Chakula	Wakala	Hati inayoridhisha	Haikukaguliwa
12	Mfuko wa Maendeleo ya Haki Miliki wa Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea	Mfuko	Hati inayoridhisha	Haikukaguliwa
13	Mfuko wa Bodi ya Barabara	Mfuko	Hati inayoridhisha	Haikukaguliwa
14	Mfuko wa Dhamana wa Rais wa Kujitegemea	Mfuko	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	
15	Tume ya Fedha ya Pamoja	10	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
16	Wizara ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi	43	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
17	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	78	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
18	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	81	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
19	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	85	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
20	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	87	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
21	Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma	94	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
22	Ubalozi wa Tazania nchini Cairo	2003	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
23	Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikali	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
24	Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
25	SUMA - Idara ya Kilimo na Viwanda	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
26	SUMA - Idara ya Zana za Kilimo	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
27	SUMA - Idara ya Ujenzi	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
28	Mamlaka ya Mapato Tanzania - Mapato	TRA	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
29	Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Nyasa	BBM	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
30	Shirika Hodhi la Mzinga	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
31	Mzinga Corporation	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
32	Prisons Corporation Sole	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
33	Treasury Registrar	7	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati yenye shaka
34	Tume inayosimamia matokeo makubwa sasa	6	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
35	Ubalozi wa Tazania nchini Ufaransa	2013	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
36	Ofisi ya Rais Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma	9	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
37	Tume ya Huduma ya Mahakama	12	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na	Jina	Fungu	2016/17	2015/16
38	Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha	13	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
39	Jeshi la zimamoto na Uokoaji	14	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
40	Tume ya Usululishi na Uamuzi	15	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
41	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	16	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
42	Ofisi ya Rais Ikulu	20	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
43	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	23	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
44	Tume ya Maendeleo ya Ushirika	24	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
45	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	25	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
46	Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais	26	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
47	Msajili wa Vyama vya Siasa	27	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
48	Idara ya Huduma za Magereza	29	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
49	Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	30	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
50	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka	35	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
51	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	36	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
52	Ofisi ya Waziri Mkuu	37	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
53	Jeshi la Wanachi wa Tanzania	38	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
54	Mahakama ya Tanzania	40	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
55	Bunge la Tanzania	42	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
56	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji	44	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
57	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	47	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
58	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	49	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
59	Wizara ya Fedha na Mipango	50	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
60	Wizara ya Mambo ya Ndani	51	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
61	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	55	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
62	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	56	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
63	Tume ya Kurekebisha Sheria	59	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
64	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	61	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
65	Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye ulemavu	65	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
66	Ofisi ya Rais Tume ya Mipango	66	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
67	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Utumishi wa Umma	67	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
68	Wizara ya Kazi, Uchukuzi na Mawasiliano	68	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
69	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	71	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
70	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	72	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
71	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	73	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na	Jina	Fungu	2016/17	2015/16
72	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	76	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
73	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	77	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
74	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	79	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
75	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	80	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
76	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	83	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
77	Singida Regional Secretariat	84	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
78	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam	88	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
79	Tume ya Kuzuia UKIMWI	92	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
80	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	96	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
81	Wizara ya Kazi, Uchukuzi na Mawasiliano	98	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
82	Ubalozi wa Tanzania, Addis Ababa	2001	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
83	Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani	2002	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
84	Ubalozi wa Tanzania nchini Kongo	2004	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
85	Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza	2006	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
86	Ubalozi wa Tanzania - Lusaka	2007	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
87	Ubalozi wa Tanzania nchini Urusi	2009	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
88	Ubalozi wa Tanzania nchini India	2010	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
89	Ubalozi wa Tanzania nchini Canada	2012	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
90	Ubalozi wa Tanzania nchini China	2014	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
91	Ubalozi wa Tanzania nchini Italia	2015	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
92	Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden	2016	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
93	Ubalozi wa Tanzania nchini Japani	2017	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
94	Ubalozi wa Tanzania nchini Uganda	2021	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
95	Ubalozi wa Tanzania nchini Zimbabwe	2022	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
96	Ubalozi wa Tanzania nchini Kenya	2023	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
97	Ubalozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia	2024	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
98	Tanzanian embassy in Pretoria, South Africa	2025	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
99	Ubalozi wa Tanzania nchini Rwanda	2026	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
100	Ubalozi wa Tanzania nchini Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu	2027	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
101	Ubalozi wa Tanzania nchini Burundi	2028	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
102	Tanzanian embassy in Lilongwe	2030	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
103	Ubalozi wa Tanzania nchini Brazil	2031	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
104	Ubalozi wa Tanzania nchini Malasia	2032	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
105	Ubalozi wa Tanzania nchini Uhlanzi	2033	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na	Jina	Fungu	2016/17	2015/16
106	Ubalozi wa Tanzania nchini - Comoro	2034	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
107	Wakala wa Umeme, Mitambo na UMfukTN	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
108	Wakala wa Utafiti wa Miamba	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
109	Agriculture Seeds Wakala	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
110	Wakala wa Usajili Lesseni na Biashara	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
111	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
112	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
113	Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
114	Chuo cha Maji	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
115	Chuo cha Mafunzo ya Twakwimu Afrika Mashariki.	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
116	Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
117	Chuo cha Utumishi wa Umma	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
118	Wakala wa Mbegu za Miti	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
119	Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA)	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
120	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
121	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
122	Wakala wa Maabara za Serikali	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
123	Chuo cha Mafunzo ya Mifugo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
124	Wakala wa Vipimo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
125	Wakala wa Serikali wa Mtandao	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
126	Bodi ya Bonde la Maji Ruvuma na Pwani ya Kusini	BBM	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
127	Mfuko wa Maji	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
128	Mfuko wa Pembejeo za Kilimo)	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
129	Mfuko wa Usimamizi na Uguzi wa vyama vya Ushirika.	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
130	Mfuko wa Uwezesaji Maendeleo ya Madini	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
131	Mfuko wa Hifadhi ya Wanyama Pori	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
132	Mfuko wa Taifa wa Maafa	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
133	Mamlaka ya Kuzuia Madawa ya Kulevyta	91	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
134	Shirika la SUMA	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
135	Chuo cha Kuthibitisha ubora wa Mbegu	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
136	Baraza la Manesi na Wakunga Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
137	Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
138	Bodi ya Ushauri Hospitali Binafsi	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
139	Mkakati wa Kukuza na Kuratibu Biashara Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na	Jina	Fungu	2016/17	2015/16
140	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
141	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
142	Bodi ya Maabara Binafsi za Afya	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
143	Mpango wa Kutathminiana katika nchi za Afrika	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
144	Balaza la Wataalamu wa Miyonzi na Picha	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
145	Tume ya Taifa ya Umgwiliajji	5	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
146	Wakala wa Usafiri wa Mwendoo Kasi Dar es Salaam	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
147	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji	BBM	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
148	Bodi ya Bonde la Maji Rukwa	BBM	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
149	Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Viktoria	BBM	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
150	Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Tanganyika	BBM	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
151	Mfuko wa Misitu Tanzania	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
152	Mfuko wa Mikopo ya Hazina	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
153	Mfuko wa Bodi ya Uratibu wa Taasisi Sisizo za Kiserikali	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
154	Mamlala ya Maji safi na Taka Handeni (HTM)	NWSSA	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
155	Mamlaka ya Maji ya Wanging'ombe	NWSSA	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
156	Baraza la Mifugo Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
157	Chuo cha Rasilimali Madini	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
158	Chuo cha Utafiti wa Mifugo Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
159	Chuo cha Usimamizi wa Mahakama	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
160	Chuo cha Uongozi	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
161	Baraza la Wataalamu wa Macho	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
162	Chuo cha Sayansi na Teknologia Afrika cha Nelson Mandela	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
163	Mamlaka ya Mapato Tanzania - Matumizi	TRA	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
164	Ubalozi wa Tanzania wa Kudumu UN - Geneva	2020	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
165	Ofisi ya Makamu wa Rais	31	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
166	Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	32	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
167	Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Maadili	33	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
168	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	34	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
169	Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknologia na Mafunzo ya UMfukTN	46	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
170	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	52	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
171	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	53	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
172	Wizara ya Nishati na Madini	58	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
173	Wizara ya Maliasili na Utalii	69	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

Na	Jina	Fungu	2016/17	2015/16
174	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	86	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
175	Ubalozi wa Tanzania - Abuja	2005	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
176	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
177	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
178	Chuo cha Taifa cha Utalii	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
179	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	70	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
180	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	74	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
181	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	82	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
182	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	95	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
183	Ubalozi wa kudumu wa Tanzania Marekani	2011	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
184	Ubalozi wa Tanzania - Washington	2018	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
185	Chuo cha Uhasibu Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
186	Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvvi	99	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
187	Mfuko wa Maendeleo ya Nishati Vijijini.	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
188	Shule ya Sheria Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
189	SUMA - Idara ya Ulinzi	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
190	Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake	Mfuko	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
191	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	75	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
192	Ofisi ya Rais Idara ya Usimamizi wa kumbukumbu na Nyaraka za Serikali.	4	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
193	Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)	39	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
194	Wizara ya Katiba na Sheria	41	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
195	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Msumbiji	2008	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
Na	Jina	Fungu	2016/17	2015/16
196	Nyumbu	TN	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
197	Health Laboratory Practitioners Council	TN	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha
198	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe	54	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine	Hati inayoridhisha
199	Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi	Wakala	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
200	Wakala wa Barabara Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
201	Wakala wa Majengo Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine
202	Rukwa Regional Secretariat	89	Hati inayoridhisha yenye masuala mengine	Hati isiyoridhisha
203	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	57	Hati inayoridhisha	Hati mbaya
204	Wizara ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano	62	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha



Taasisi zilizopata hati yenyeshaka		Fungu	2016/17	2015/16
Na	Jina			
1	Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala za Afya	TN	Hati yenyeshaka	Hati isiyoridhisha
2	Chama cha Demokrasia	CCS	Hati yenyeshaka	Hati mbaya
3	Baraza la Famasia	TN	Hati yenyeshaka	Haikukaguliwa
4	Chama Cha Mapinduzi	CCS	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
5	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	48	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
6	Chama cha Demokrasia na Maendeleo	CCS[2]	Hati yenyeshaka	Hati yenyeshaka
7	Idara ya Hazina	21	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
8	Idara ya Deni la Taifa	22	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
9	Jeshi la Polisi Tanzania	28	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
10	Sekretarieti ya Mkoa wa Geita	63	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
11	Idara ya Uhaniaji	93	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
12	Ubalozi wa Tanzania Muscat	2029	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
13	Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania	Wakala	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
14	Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania	Wakala	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
15	Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania	Wakala	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
16	Bodi ya Bonde la Maji Pangani	BBM[3]	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
17	Bodi ya Bonde la Manj 'Internal Drainage'	BBM	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
18	Bodi ya Bonde la Maji Wami/Ruvu	BBM	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
19	Mugango/Kiabakari/Butiama	NWSSA	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
20	Baraza la Dawa Tanganyika	TN	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
21	Ubalozi wa Tanzania Nchini Ubelligiji	2019	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo
22	Mamlaka ya Usambazaji Maji safi bonde Makonde	NWSSA	Hati yenyeshaka	Hati inayoridhisha
Taasisi zilizopata hati isiyoridhisha				
1	Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi	TN	Hati isiyoridhisha	Hati yenyeshaka
2	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	Wakala	Hati isiyoridhisha	Hati yenyeshaka
3	Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (HOMBOLO)	TN	Hati isiyoridhisha	Hati yenyeshaka
4	Hesabu Jumuifu za Taifa	N/A	Hati isiyoridhisha	Hati isiyoridhisha
Taasisi zilizopata hati mbaya				
1	Chama cha Alliance For Tanzania Farmers	CCS	Hati mbaya	Hati mbaya
2	Chama Cha Kijamii	CCS	Hati mbaya	Hati mbaya
3	Chama Cha Sauti ya Umma	CCS	Hati mbaya	Hati mbaya
4	Chama cha Alliance For Tanzania Democracy	CCS	Hati mbaya	Haikukaguliwa
5	Chama cha Tanzania Labour Party	CCS	Hati mbaya	Haikukaguliwa
6	Demokrasia Makini	CCS	Hati mbaya	Haikukaguliwa
7	Chama cha National League For Democracy	CCS	Hati mbaya	Hati mbaya
[1]	TN maana yake Taasisi Nyingine			
[2]	Chama Cha Siasa			
[3]	Bodi ya Bonde la Maji			

**Kiambatisho Na. 2.2: Taasisi zenye hati yenyé shaka na msingi wa hati hiyo**

<b>Jina la taasisi na msingi wa hati Zenye Mashaka</b>	
<b>1. Jeshi la Polisi Tanzania (Fungu 28)</b>	
<p>Jeshi la Polisi Tanzania lilipokea magari 196 yenyé thamani ya dola za Marekani 10,362,135 ambayo ni sawa na shilingi za Tanzania 23,221,544,535 (kwa kiwango cha kubadilishia fedha cha dola 1 kwa Sh 2241) kutoka kwa mzabuni M/S Ashok Leyland Limited kati ya mwezi Oktoba na Disemba 2015 na yalinza kutumika, hata hivyo magari haya hayakuingizwa katika vitabu vya fedha, hivyo kiasi cha mali za kudumu kilichoingizwa kwenye taarifa za fedha kilikuwa pungufu kwa Sh 23,221,544,535.</p>	
<b>2. Idara ya Huduma za Uhamiaji (Fungu 93)</b>	
<p>a) Mali, mitambo na vifaa vilitolewa taarifa katika taarifa za fedha kwa thamani ya Shilingi 83,288,795,818. Hata hivyo kiasi hicho hakikujumuisha jumla ya uchakavu kwa miaka ya nyuma ila kwa mwaka 2016/2017 kilitolewa taarifa, hivyo kiasi cha Mali, mitambo na vifaa kilichotambuliwa kilizidishwa na jumla ya uchakavu ilipunguzwa.</p> <p>b) Menejimenti ilitumia muundo wa kuthaminisha mali zake katika taarifa za hali ya fedha tofauti na muundo wanaoutumia wa gharama halisi, hivyo thamani baada ya kuthaminiwa zaidi kwa shilingi 50,454,255,585.06 kilitolewa taarifa kwenye mali ikionyesha ongezeko la thamani ya mali, mitambo na vifaa viliviyotolewa taarifa. Hivyo thamani ya mali, mitambo na vifaa iliyoonyeshwa katika taarifa ya hali ya mali ilizidishwa kwa kiasi hicho.</p>	
<b>3. Idara ya Hazina (Fungu 21)</b>	
<p>a) Taarifa ya hali ya mali iliyotolewa katika mikopo ya chini ya mali “on-lending loans” chini ya mali za fedha zenye thamani ya shilingi Shilingi 255,281,929,856 hata hivyo, mapitio ya viambatisho na nyaraka husika ulibaini kuwa kiasi cha deni lililobakia chini ya utaratibu huo Sh 310,098,343,856 lisisababisha kutolewa taarifa ya mali za fedha pungufu kwenye taarifa ya hali ya fedha kwa Shilingi 54,816,414,000.</p>	
<b>4. Deni la Taifa (Fungu 22)</b>	
<p>a) Taarifa ya madeni ilionyesha hali ya deni kiasi cha shilingi bilioni 46,081.43 kwa kipindi kinachoishia 30 Juni 2017, hata hivyo kiasi hicho hakikujumuisha mfuko wa pensheni kiasi cha shilingi bilioni 3,182.8 na dhamana za muda mrefu (zilizopangwa) zenye thamani ya shilingi bilioni 166.67 chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, ambayo husababisha kuwa chini ya shilingi bilioni 3,349.48</p> <p>b) Taarifa za fedha zilionyesha masharti ya pensheni kiasi cha shilingi 422,040,000,000, hata hivyo hakuna ripoti ya sasa “actuarial valuation report” kuthibitisha kiasi kilichoonyeshwa.</p>	
<b>5. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi</b>	
<p>a) Taarifa ya mtiririko wa fedha taslimu kwa mwaka 2016/2017 ilionyesha</p>	

**Jina la taasisi na msingi wa hati Zenye Mashaka**

- mapato mengine kiasi cha shilingi 85,978,598,700 wakati huo huo daftari la fedha taslimu lilionyesha kiasi cha shilingi 32,351,604,193.58 hivyo kusababisha kuripoti zaidi kwa Sh 53,626,994,507.
- b) Kodi ya ardhi iliripotiwa pungufu kwa kiasi cha Shilingi 848,065,969.27 ambayo taarifa za fedha (maelezo 31) inaonyesha kodi iliyopokelewa kiasi cha Shilingi 93,312,138,404.90 wakati huo leja kuu ilionyesha kiasi cha Shilingi 94,160,204,374.17.
  - c) Kulikuwa na malipo kiasi cha shilingi 1,980,983,456.50 kutoka mfuko wa maendeleo kwenda kwa wazabuni mbalimbali kwa ajili ya kulipa madeni ya miaka iliyopita, hata hivyo malipo kiasi cha shilingi 1,892,747,172.90 yalibadilishwa na kusababisha tofauti ya shilingi 88,236,283.60 bila maelezo.
  - d) Mpaka tarehe 30 Juni 2016, Wizara ilionyesha deni lililosalia kiasi cha shilingi 13,814,725,236.89 ambapo kipindi cha kutoa taarifa Sh. 6,845,079,161.83 ililipwa na kuacha salio la Sh.6,969,646,074.97, haya hivyo kiasi cha shilingi 6,783,700,824.89 pekee kilitolewa taarifa mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2017 ambayo ilipelekeea kutolea taarifa pungufu kwa Sh 185,945,250.08.
  - e) Wizara ilionyesha masurufu yasiyorejeshwa kiasi cha Shilingi 2,025,045,495,76 wakati huo daftari la masurufu likionyesha kiasi cha Shilingi 4,637,238,044.78, hivyo kuonyesha madai kwa pungufu ya Sh 2,612,192,549.02.
  - f) Katika mwaka wa ukaguzi, Wizara ilionyesha ongezeko la mali, mitambo na vifaa vyenye thamani ya shilingi 150,821,598.96, hata hivyo uhakiki ulibaini kuwa kati ya mali, mitambo na vifaa vilivyoongezwa, kiasi cha shilingi 70,000,000 hakipo, hivyo mali, mitambo na vifaa vilitolewa taarifa zaidi ya vilivyopo.
  - g) Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 Wizara ilifungua Akaunti maalum ya ardhi na kiasi cha Shilingi 50,000,000,000 kiliwekwa kutoka akaunti ya Serikali ya Amana kwa ajili ya malipo. Hata hivyo hakuna malipo yoyote yaliyofanyika kwenye Akaunti hiyo maalum ya ardhi na taarifa za fedha hazikuonyesha kiasi hicho kama sehemu ya amana (deni).
  - h) Hati za malipo kwa malipo kiasi cha shilingi 121,926,029.88 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo kuzuia mawanda ya ukaguzi.
  - i) Katika mwaka wa ukaguzi, kiasi cha shilingi 13,652,670 kilihamishwa kutoka akaunti ya maduhuli ya ardhi namba 2011000025 iliyopo benki ya NMB kwenda benki ya biashara ya Afrika (CBA), hata hivyo hakukuwa na nyaraka yoyote ili kuthibitisha uhalali wa muamala huo.

**6. Sekretarieti ya Mkoa Geita**

- a) Taarifa ya mizania ya fedha tarehe 30 Juni 2017 ilionyesha kuwa madeni kiasi cha Sh 364,807,178, kati ya hayo kiasi cha Sh 49,861,791 yanahusiana na bidhaa na huduma kwa miaka iliyopita lakini hayana viambatisho stahiki kuthibitisha uhalali wake na wala hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha

Jina la taasisi na msingi wa hati Zenye Mashaka
za miaka iliyopita.
b) Taarifa ya ufanisi wa fedha imeonyesha matumizi kiasi cha Sh 78,625,782, lakini hati za malipo husika hazikuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, hivyo uhalali wa malipo hayo umeshindwa kuthibitishwa.
<b>7. Wakala wa Maabara za Vetenari Tanzania</b>
a) Taarifa za mizania ya fedha mpaka tarehe 30 Juni 2017 na maelezo namba 32 inaonyesha thamani ya mali, mitambo na vifaa Sh 60,748,612,361, hata hivyo ilibainika kuwa kiasi cha uchakavu Sh 617,301,294 kilitolewa kwa mwaka huu pekee kwa mara ya kwanza hata kwa mali zilizokuwepo tokea mwaka 2012/2013 and ongezeko lilioluata ni kama zilinunuliwa tarehe 1 Julai 2016 kitu ambacho ni tofauti na fungu 71 la IPSAS 17. Hivyo ilisababisha mali, mitambo na vifaa kuripotiwa zaidi na uchakavu wa jumla kuonyeshwa kwa upungufu.
b) Sera ya mali, mitambo na vifaa haionyeshi asilimia ya uchakavu na umri wa mali hiyo imesababisha ugumu wa kuhakiki kiasi cha uchakavu kilichoonyeshwa.
c) Kulikuwa na mali isiyoshikika kiasi cha Sh 1,120,000 mpaka tarehe 30 Juni 2017 lakini haikufanyiwa uchakavu kama inavyotakiwa na fungu 117 la IPSAS 31, hivyo kupelekea kuonyeshwa mali za kudumu zaidi ya halisia yake kwa mwaka. Kiasi cha fedha za walipa kodi kilichoonyeshwa katika taarifa ya mizania ya fedha na taarifa ya mabadiliko ya mtaji kiasi cha shilingi 60,438,377,002 haikuwa na maelezo ya ziada hivyo kuzuia watumiaji wa taarifa kujua nini kilichojumuishwa.
d) Taarifa za fedha ya Wakala haijaambatishwa pamoja na taarifa ya Mkurugenzi kama matakwa ya Viwango vya Uhasibu wa Fedha Tanzania.
<b>8. Baraza la Madaktari</b>
a) Mali, mitambo na vifaa vilionyeshwa katika taarifa za fedha kwa tarehe 30 Juni 2017 katika gharama zake za awali bila ya kutoa uchakavu kwa mwaka kama inavyotakiwa na fungu 66 la IPSAS 17 ambayo inaeleza kuwa uchakavu wa mali utatengwa kwa utaratibu maalum juu ya maisha yake. Bila ya kuondoa uchakavu wa mali, mitambo na vifaa itasababisha kuonyeshwa mali hizo kwa zaidi ya thamani halisi na pia uchakavu utakuwa pungufu ya kiasi halisi.
<b>9. Baraza la Wafamasia</b>
d) Kulikuwa na kutofautiana kwenye malipo yaliyopotiwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha taslimu kiasi cha Sh.2,027,038,121 na zilizopo katika kitabu cha fedha taslimu cha Sh. 1,934,790,870. Uchunguzi wa kina juu ya taarifa iliyotolewa kwa ukaguzi, kiasi cha Sh.1, 927,757,760 kimethibitishwa kuwa malipo halisi ambayo yanafanya kiasi cha Sh. 99,280,361 kutofautiana.
a) Kulikuwa na malipo yaliyofikia kiasi cha Sh.54,989,439 hayakuwa na viambatisho vya kutosha kinyume na mahitaji ya Kanuni 86 (1) na 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. Kutokuwepo kwa nyaraka za

<b>Jina la taasisi na msingi wa hati Zenye Mashaka</b>
kutosha za kutosha, uhalali wa malipo haukuweza kujulikana.
<b>10. Baraza la tiba za asili na mbadala</b>
a) Uchakavu wa mali, mitambo na vifaa ulifanyika tu kwa mwaka 2016/17 hata kwa mali zilizoripotiwa katika hali ya ufunguzi wa mizania ya fedha tarehe 1 Julai 2012 na nyongeza zake zilizofuata bila kutambua kushuka kwa thamani yoyote iliyokusanyika inayohusiana na mali hizi katika miaka yao ambayo zilitumika,. Hivyo imesababisha kuripotiwa zaidi kwa mali hizo. b) Menejimenti imetumia mtindo wa kurekebisha uwasilishaji wa CCSE katika Taarifa ya mizania ya Fedha kinyume na mtindo wa gharama uliopitishwa, kwa hiyo ziada ya uthaminishaji kiasi cha Sh 113,677,634,93 iliripotiwa katika mtaji hivyo inaonyesha ongezeko sawa na thamani ya mali iliyoripotiwa . Hivyo thamani katika taarifa ya mizania ya fedha ilikuwa imeripotiwa zaidi kwa Sh.113,677,634.93.
<b>11. Wakala wa ndege za Serikali</b>
a) Mapitio ya taarifa za fedha Shirika la Ndege Tanzania limeonyesha kuwa, ndege mbili za thamani ya Sh. 110,690,306,309,70 zilinunuliwa njia ya shughuli zisizo za kubadilishana na zitambuliwa kama mali na mtaji badala ya mali na mapato kama inavyotakiwa na fungu 44 la IPSAS 23, na hivyo kuzidisha mitaji na kupunguza jumla ya ziada/ upungufu. b) Hakukuwa na sera ya uhasibu iliyoonyeshwa kuhusiana na ruzuku kinyume na fungu 21 ya IPSAS 1 ambayo inahitaji kutoa taarifa ya muhtasari wa sera muhimu za uhasibu zinazoongozana na taarifa za fedha.
<b>12. Wakala wa Huduma za Ajira Tanzanzia</b>
a) Serikali imechagua sera ya gharama kama sera yake ya uhasibu kama inavyotakiwa na fungu 43 la IPSAS 17; hata hivyo, shirika hilo limetumia sera ua uthaminishaji kama kipimo cha baadaye cha mali hizo ambacho kinapingana na sera ya mtindo wa gharama iliyopitishwa na serikali nzima. Kwa hiyo, ziada ya Sh.79,908,226 ilitambuliwa katika taarifa ya mizania ya fedha na taarifa ya mabadiliko ya mitaji.
<b>13. Bodi ya Bonde la Mto Pangani</b>
a) Mapato mengine yamejumuisha madai yaliyokusanya ya TZS 50,301,000 kutokana na wadaiwa wariotambulika mwaka jana. Kwahiyo mapato yamezidishwa kwa kiasi hicho. b) Mizania ya hesabu imeripoti wadaiwa kiasi cha TZS 110,527,000 wakati taarifa ya maelezo 22 salio la kufungia TZS 172,072,000 na matokeo yake kupungua kwa wadaiwa kwa TZS 61,545,000. c) Taarifa ya mabadiliko ya mtaji imejumuisha pamoja na salio la TZS 202,800,000 kutokana na ziada iliyosamanisha, kwa hali halisi hawakuthaminisha na Bodi walitumia gharama za awali. e)
<b>14. Bodi ya Bonde la Maji la Ndani</b>
a) Serikali iliamua kutumia gharama za awali kama sera ya uhasibu inavyotaka na aya 43 ya IPSAS 17; Pia,bodi ilitumia mfumo wa kuthaminishwa katika

**Jina la taasisi na msingi wa hati Zenye Mashaka**

kupima,Mali,Vifaa na Mitambo ambayo inapingana na mfumo wa sera za gherama za awali ambao umekubalika Serikalini na matokeo yake ziada na pungufu ya kuthaminisha ya TZS 2,059,514,106.96 na TZS 1,969,249,026 kama inavyofuatana zimeripotia katika mahesabu.

**15. Bodi ya Bonde la Maji la Mto Ruvu Wami**

- a) Imejumuishwa katika Mizania ya hesabu ya 30 Juni 2017 ya Mali,Vifaa na Mitambo katika taarifa ya mabadiliko ya mtaji wa TZS 465,274,567, Pia ilionesa uchaakavu wa TZS 121,626,333 ililikokotolewa kwa mwaka huu kwa mara ya kwanza tena hata mali zatangia 2012/13 na ongezeko la Mali,Vifaa na Mitambo iliyonunuliwa 1 Julai 2016 ambayo ni kinyume cha Aya 71 ya IPSAS 17. Uchakavu ulichajiwu tu kwa 2016/17 hata mali za kuanzia 2012/13 na ongezeko lilizidishwa kwa Mali,Vifaa na Mitambo lililoripotiwa na punguzo la limbikizo la uchakavu.

**16. Mamlaka ya maji safi na Maji taka Bonde la Makonde.**

- a) Menejiment ya Mamlaka wamechaji uchakavu wa Mali,Vifaa na Mitambo kwa mwaka huu kwa mara ya kwanza tena hata mmali zatangia 2012/13 na ongezeko la Mali,Vifaa na Mitambo iliyonunuliwa 1Julai, 2016ambayo ni kinyume cha Aya 71 ya IPSAS 17.Uchakavu ulichajiwu tu kwa 2016/17 hata malii za kuanzia 2012/13 na ongezeko lilizidishwa kwa Mali,Vifaa na Mitambo lililoripotiwa na Punguzo la limbikizo la uchakavu.

**17. Mugango/Kiabakari/Butiama**

- b) Imejumuisha kwenye Taarifa ya ufanisi wa fedha ambayo ni bajeti ya mwisho ya mapato yanayotoka mfuko mkuu wa Serikali TZS.193,102,665.25 badala ya mapato halisi kutoka mfuko mkuu wa Serikali ya TZS.100,289,567.78, wamezidisha mapato yaliyopotiwa kwa TZS.92,813,097.47.
- a) Katika kipindi cha mwaka ,Mamlaka walikuwa na mapato ambayo hayajakusanya ya wadaiwa TZS 66,507,585; hata hivyo kiasi hicho hakuripotiwa kwenye mizania ya hesabu kama ni wadaiwa

**18. Chama Cha Demokrasia**

- b) Mezania ya Hesabu iliyokaguliwa haikuwa na viambatanisho vya taarifa ya maelezo kasoro mchango wa mwenyekiti(note 4)
- a) Chama kimerithi mfumo wa aandaji wa hesabu kwa mfumo wa taslimu, pia kimeripoti hasara ya TZS 12,873,500 kwa 2015/16 na TZS 17,660 kwa 2016/17.

**19. CHADEMA**

CHADEMA imeripoti ardhi na majengo katika mizani ya hesabu kama zote sawa katika kundi moja kwa TZS 198,036,917.15 ambayo ni kinyume na Aya 74 ya IPSAS 17 inataka ardhi na majengo kutofautishwa hata kama vinanunuliwa kwa pamoja.Bila ya kuvitofautisha thamani ya ardhi na majengo,kiasi cha uchakavu wa ardhi na majengo pia kitaigawia ardhi ambayo haihusiki na uchakavu hivyo kupunguza thamani ya ardhi na ziada kwa mwaka.

Jina la taasisi na msingi wa hati Zenye Mashaka
<b>20. Ubalozi wa Tanzania Brussels, Belgium</b>
Menejiment walitumia mfumo wa kuthaminisha Mali,Vifaa na Mitambo na kuzionyesha katika mizania za hesabu ambayo ni kinyume na mfumo wa gharama za awal,hivyo ziada ya kuthaminisha ya TZS 630,989,752 iliripotiwa kwenye taarifa ya mbadiliko ya mtaji ni sawa na ongezeko la thamani ya Ardhii,Majengo na Mitambo.Hivyo salio lililobakia linaziidi kwa TZS. 630,989,752.
<b>21. Ubalozi wa Tanzania Muscat</b>
Taarifa za maelezo (Note 59) (na gharama zingine) zimejumuisha TZS 72,524,673 zinazohusiana na malipo ya mkopo.Katika kupitia tumeona kuwa mkopo ulikuwa unahusiana na gari ndani ya mwaka 2015/2016 katika mizania ya hesabu.Kutokana na hivyo gharama zitakuwa zimeongezeka kwa mwaka 2016/17
<b>22. Chama Cha Mapinduzi</b>
Chama akija tofautisha thamani ya ardhi na majengo ,zimeripotiwa kwa pamoja kwa kiasi cha TZS 7,626,465,206 ambayo ni kinyume na Aya 74 ya IPSAS 17.which is contrary to the requirements of paragraph Para 74 of IPSAS 17. Bila ya kuvitofautisha thamani ya ardhi na majengo,kiasi cha uchakavu wa ardhi na majengo pia kitaigawia ardhi ambayo haihusiki na uchakavu hivyo kupunguza thamani ya ardhi na ziada kwa mwaka. .

### Kiambatisho Na. 2.3: Sababu zilizosababisha Taasisi kupata Hati Isiyoridhisha

**Jina La Taasisi na Sababu zilizopeleke taasisi hizo kupata Hati Isiyoridhisha.**

- 1. Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania**
  - a) Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslimu (IPSAS) namba 17 Aya ya 74 inazitaka taasisi kutenganisha thamani ya ardhi na thamani ya majengo hata kama viwili hivyo vimenunuliwa pamoja. Bila kutenganisha ardhi na nyumba, thamani halisi ya vitu hivi itakuwa sio sahihi kwa sababu Nyumba inashuka thamani na wakati Ardhi haishuki thamani. Wakala huyu ameonyesha thamani ya Ardhi na Nyumba kwa jumla ya Shilingi 369,580,000. Kufanya hivi ni kukiuka viwango vya kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma. Athari ya kufanya hivi ni kuongeza gharama ya uchakavu na kupunguza ziada katika taarifa ya Ufanisi wa fedha.
  - b) Taasisi hii imetoa taarifaa ya masurufu katika taarifa ya mizania ya hesabu kuwa ni shilingi 150,635,350. Taarifa sahihi ya masurufu iliyotakiwa kuonyeshwa katika mizania ya hesabu ni shilingi 407,993,568 hivyo mizani ya hesabu imepunguzwa kwa shilingi 265,065,017 katika taarifa ya masurufu.
  - c) Nyaraka za malipo yenye thamani ya shilingi 21,752,000 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Pia Nyaraka za malipo zenye thamani ya Shilingi 70,612,052

hazikuwa na nyaraka za viambatisho vya kutosha hivyo nimeshindwa kujua uhalali wa malipo hayo. Kwa ujumla malipo haya yenyе nyaraka pungufu na malipo ambayo nyaraka zake hazikuwasilishwa kabisa ni shilingi 92,364,051

- d) Katika taarifa ya mabadiriko ya Mtaji ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2017, inaonesha kuwa kuna marekebiso ya mtaji yenyе mabadiriko ya shilingi 837,249,326. Wakati wa ukaguzi niliomba Kupata viambatanisho na nyaraka zinazothibitisha marekebiso haya, menejimenti haikuweza kuwasilisa viambatanisho hivyo. Nimeshindwa kuthibitisha usahihi wa marekebiso ya mtaji.
- e) Makusanyo ya mapato kutoka katika vyanzo vya ndani yameonyeshwa katika taarifa ya ufanisi wa fedha kwa Upungufu wa shilingi 31,298,928 ambayo ilikuwa ni kodi ya ardhi iliyolpwa na wamiliki wa ardhi katika mwezi wa oktoba 2016.

f)

### 2. Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (Hombolo)

- a) Viwango vya Uandaaji wa hesabu kimataifa vinataka taarifa za hesabu ziwe za ulinganisho. Pia inasisitiza kuwa kiasi kilichokaguliwa mwaka jana kionekane hivyo hivyo wakati wa ulinganif katika taarifa ya fedha ya mwaka huu. Katika kulinganisha mapato yam waka jana nimebaini kuwa kuna tofauti ya shilingi 387,185,243 ambayo ni Zaidi ya mapato yalioonyeswhwa mwaka jana katika ulinganifu. Pia kiasi cha shilingi 2,927,102,913 kinaonekana kuongezeka katika linganisho wa matumizi ya mwaka jana. Hii inaonyesha kwa taarifa za taasisi hii hazina ulingano
- b) Sera za uandaaji wa taarifa za fedha za taasisi ya mafunzo ya serikali za mitaa Hombolo ni ya kutumia Gharama halisi katika kuonesha thamani ya mali zake. Katika hesabu za mwaka huu taasisi haijatumia sera hii ya gharama halisi, na badala yake imetumia grahama iliyorekebishesha na hivyo kusababisha kutoa taarifa ya ogezeko la thamani ya mali kwa jula ya shilingi 1,281,365,745 ambayo sio sahihi.
- c) Kuna malipo yaliofanyika bila ya kuwa na viambatanisho na nyaraka za kutosha yenyе jula ya shilingi 118,250,895. Katika malipo haya sikuweza kuthibitha uhalali wa kufanyika kwa malipo haya

### 3. Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori-Pasiansi

- a) Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslimu (IPSAS) namba 17 Aya ya 74 inazitaka taasisi kutenganisha thamani ya ardhi na thamani ya majengo hata kama viwili hivyo vimenunuliwa pamoja. Bila kutenganisha ardhi na nyumba, thamani halisi ya vitu hivi itakuwa sio sahihi kwa sababu Nyumba inashuka thamani na wakati Ardhi haishuki thamani. Wakala huyu ameonyesha thamani ya Ardhi na Nyumba kwa jumla ya Shilingi 1,474, 469,292. Kufanya hivi ni kukiuka viwango vya kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma. Athari ya kufanya hivi ni kuongeza gharama ya uchakavu na kupunguza ziada katika taarifa ya Ufanisi wa fedha.
- b) Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslimu (IPSAS) namba 17 Aya ya 66 inaelekeza kuwa mali zote

kupunguzwa thamani yake kila mwaka kutokana na uchakavu katika kipindi chote cha maisha ya mali hizo. Katika kaguzi huu, nilibaini kuwa Mali za Taasisi hii zenyne thamani ya shilingi 2,656,559,887 hazikupunguzwa kwa kiwango cha uchakavu katika mwaka husika. Hii imesababisha kuongeza thamani ya ziada kwa kupunguza ghamama za uendeshaji wa taasisi. Hii ni kinyume na Aya 66 ya IPSAS

- c) Kuna tofauti ya shilingi 15,776,592 kati ya mataji ulioonyeshwa katika taarifa ya Mizania ya hesabu na taarifa ya Mabadiriko ya Mtaji. Taarifa ya Mizania ya hesabu imeonyesha mtaji wa shilingi 2,640,783,295 wakati taarifa ya Mabadiriko ya Mtaji inaonyesha kuwa kuna mtaji wa shilingi 2,656,559,887. Hii inaonyesha utofauti wa taarifa. Pia katika maelezo ya ziada namba 32 katika taarifa ya fedha inaonyesha kuna mtaji wa shilingi 2,648,142,446 taarifa hizi zote tatu zinaonyesha thamani tofauti za mtaji mmoja.
- d) Anzio la Limbikizo la ziada kwa tarehe 01 Julai 2016 ni shilingi 15,109,490 wakati fungio la limbikizo la ziada kwa tarehe 30 Juni 2016 ni shilingi 104,337,321. Taarfa hii la limbikizo la ziada halijaonyesha uhalisia kwa utofauti wa shilingi 89,227,830.91
- e) Kuna taarifa zinazokinzana katika kiasi kinacho onyeshwa katika maelezo ya ziada ya taarifa za fedha na kiasi kile kinacho onyeshwa katika sura a taarifa ya fedha kaa inavyoonekana hapo chini;
  - Taarifa za ziada namba 12, 13 and 14 inaonyesha kiasi cha mapato yenye thamani ya shilingi 2,412,326,255 wakati katika uso wa taarifa ya ufanisi wa fedha inaonyesha mapato ya shilingi 2,748,594.009,
  - Taarifa za ziada namba 15 inayohusu taarifa ya mishahara na stahiki za watumishi inaonyesha kiasi cha shilingi 838,310,296 kimetumika kulipa mishahara, wakati katika taarifa ya ufanisi w fedha inaonyesha mishahara iliyolipwa ni shilingi 832,295,296,
  - Taarifa za ziada namba 16 inaonyesha taarifa yamanunuvi ya vifaa vya matumizi ya ofisini ya kiasicha shilingi 1,294,978,332 wakati katika uso wa taarifa ye ufanisi wa fedha inaonyesha taarifa ya ununuvi wa vifaa hivi kuwa ni shilini Tzs 1,580,030,959
  - Taarifa ya ufanisi wa fedha inaonyesha kuwa matumizi mengine yaliofanyika katika mwaka huu ni shilingi 327,850,342. Kiasi hiki hakija onyeshwa katika taarifa ya zaida ambayo inatakiwa kupambanua kisai hiki kinatokana na vitu gani.
  - Katika taarifa ya Ufanisi wa fedha inaonyesha kiasi cha shilingi 279,037,627 klitumika katika matengenezo ya vifaa vya taasisi. Kiasi hiki hakina mchanganuo kuitia taarifa ya Zaidi ya hesabu.
- f) Kiasi cha Ruzuku ya shilingi 15,109,490 ilichopokelewa hakijaonyeshwa katika taarifa ya mizania ya hesabu.

#### 4. Hesabu Jumuifu za taifa

- a) Taasisi 13 zilizojumuishwa na zenyne uwekezaji wa mitaji kibiashara wenye thamani ya shilingi 549,199,224,690; ulibainisha kuwa, uwekezaji huo ulithaminishwa kwa bei za awali kinyume na matakwa ya aya ya 48 ya IPSAS 29 ambayo inahitaji mali za kibiashara (financial assets) baada ya kutambua

- thamani ya uwekezaji kwa mara ya kwanza; kuthaminishwa kwa bei ya soko la wakati husika bila kuondoa ghamama za miamala inayoweza kuhusika wakati wa kuuza mali hiyo. Kwa hiyo, msingi wa thamani wa uwekezaji uliotaarifiwa haukuweza kuthibitishwa.
- b) Maelezo ya ziada (Note) 77 yanayohusiana na uwekezaji katika Mashirika (associate) na Mipango ya pamoja (joint ventures) imebainishwa uwekezaji hasi katika Mashirika na Mipango ya pamoja (Joint Ventures) wa shilingi 405,349,237,000 kwa mwaka 2016/2017 na shilingi 362,241,134,000 kwa mwaka 2015/2016. Hii ni kinyume na Aya ya 41 &42 ya IPSAS 36 inayohitaji mwekezaji kuacha kutambua sehemu yake ya upungufu/hasi alikowekeza mara tu uwekezaji huo unapokuwwa umepungua hadi kufikia sifuri. Baada ya hapo, kunahitajika kutaja/kuonesha (Disclose) upungufu wa thamani (impairment) wa mali husika.
  - c) Mapitio ya hesabu jumuifu yalibainisha uondoshwaji (Elimination) wa matumizi kiasi cha shilingi 63,781,917,503,000 dhidi ya mapato ya shilingi 63,482,869,159,000 baina ya taasisi zinazojumuishwa hivyo kusababisha kushusha/kupandisha matumizi na mapato kwa kiasi cha Shilingi 299,048,344,000. Pia nitigundua serikali ilichangia shilingi 967,593,029,717 kwa mifuko ya LAPF, NHIF na PSPF lakini mifuko hiyo ilikiri kupokea Shilingi 907,634,511,096 na hivyo kulipelekea uondoshwaji wa kuzidi kwa shilingi 59,958,518,622 kutoka mapato ya mifuko husika.
  - d) Mapitio ya hesabu jumuifu yalibainisha kuwa shilingi 15,094,949,741,000 zilionyeshwa kwenye hesabu jumuifu kama mapato ya kodi iliyokusanywa na TRA. Kiasi hiki kinajumuisha kodi iliyokusanywa na TRA kwa niaba ya taasisi nyingine shilingi 2,165,273,630,236 .
  - e) Kati ya kiasi cha shilingi 2,165,273,630,236 jumla ya shilingi 1,478,502,889,386 kiliripotiwa na taasisi husika. Hata hivyo, ni kiasi cha shilling 1,153,194,135,886 kilichoripotiwa na taasisi husika kama ruzuku ya serikali na ada ya mafuta, kiliondoshwa (elimination) katika hesabu jumuifu ipasavyo. Kiasi kilichobaki cha shilling 325,308,753,499.97 kilichoripotiwa na taasisi husika kama mapato na ada mbalimbali hakikuondoshwa na hivyo kusabaibisha kiasi hicho kuhesabiwa mara mbili katika hesabu jumuifu. Katika hali hiyo, mapato yaliyopotiwa katika hesabu jumuifu yanapotosha watumiaji kwa kiasi cha shilingi 325,308,753,499.97 kwa kuripotiwa mara mbili.
  - f) Kati ya hesabu 23 za mashirika na Mipango ya pamoja zilizojumuishwa, 20 (Sawa na 87%) zilikuwa na tarehe za kufunga hesabu tofauti na hesabu Jumuifu na hakukuwa na marekebisho kinyume na aya 36 ya IPSAS 36. Taasisi moja ilifunga hesabu tarehe 31 Desemba 2015, taasisi 18 zilifunga hesabu tarehe 31 Desemba 2016 na taasisi nyingine ilifunga hesabu tarehe 31 Machi 2017.

#### Kiambatisho Na. 2.4: Taasisi na Mambo yaliyopelekea Kupata Hati mbaya

**Taasisi na Mambo yaliyopelekea Kupata Hati mbaya**

**1. Chama cha Wakulima (AFP)**

- a) AFP haikuanda taarifa za fedha kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wahesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslimu (IPSAS accrual), iliandaa taarifa ya ufanisi wa fedha na taarifa ya mapokezi ya fedha na malipo.
- b) Taaifa ya mapokezi ya fedha na malipo haikuwa na viambatanisho vyovyote kama vile kitabu cha fedha taslimu, risiti za mapokezi ya fedha na hati za malipo.

## **2. Demokrasia Makini**

Demokrasia Makini haitunzi vitabu sahihi vya uhasibu kama vile hesabu za majoribio, kitabu cha fedha taslim na leja kuu za hesabu kama inavyotakiwa na kifungu namba 14(1) cha sheria ya vyama vya siasa namba 5 ya 1992, hivyo taarifa za fedha hazina viambatanisho vya chanzo cha taarifa ambayo inasababisha kukwamisha ukaguzi.

## **3. Chama cha Kijamii (CCK)**

- a) Menejimenti ya CCK haikuzingatia mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha na hakuna sera za kihasibu zilizointongoza uandaaji wa hesabu. Hivyo tumeshindwa kujua msingi wa uandaaji wa hesabu.
- b) CCK haitunzi vitabu vya uhasibu kama vile vitabu vya risiti, kitabu cha fedha taslimu, vitabu vya leja, majoribia ya hesabu na kitabu cha mali za kudumu kwa ajili ya usimamizi na kuandaa ripoti za fedha, kinyume na kifungu namba 14(1) cha sheria ya vyama vya siasa namba 5 ya 1992 (iliyorekebishwa mwaka 2015). Matokeo yake risiti kiasi cha Shilingi 3,200,000 na malipo kiasi cha Shilingi 3,200,000 hayakuungizwa katika vitabu vya kihasibu. Hali hii inazuia mawanda ya ukaguzi.

## **4. Chama cha National League For Democracy (NLD)**

- a) Chama hakijaanda hesabu kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslimu (IPSAS Accrual), taarifa ya mapato na matumizi tu ndo ilioandalialiwa, vile vile hakuna misingi wala sera za uandaaji wa hesabu zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha.
- b) Hakuna utunzaji wa vitabu vya uhasibu kama vile majoribia ya hesabu, leja na kitabu cha mali za kudumu ambavyo vingesaidia katika uandaaji wa taarifa za fedha.
- c) Matumizi ya Shilingi 470,000 hayakuweza kukaguliwa kwasababu hakukuwa na hati za malipo na viambatanisho vyake.

## **5. Chama cha Sauti ya Umma**

- a) Menejimenti haikuzingatia mfumo wa uandaaji katika uandaaji wa taarifa za fedha na hakuna sera ya kihasibu ilioanzishwa ili kuongoza uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha, kwahiyoo hatukuweza kupata misingi iliyotumika katika uandaaji wa taarifa za fedha.
- b) Taarifa ya mapato na matumizi tu ndo ilioandalialiwa ambapo ni kinyume na viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslimu (IPSAS Accrual).

## **6. Chama cha Tanzania Labour Party (TLP)**

- a) Misingi iliyotumika katika uandaaji wa taarifa za fedha haikuonyeshwa, hivyo

taarifa za fedha zilizowasilishwa hazikuzingatia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslim (IPSAS Accrual).

- b) Madeni kiasi cha Shilingi 112,890,102 hayakuwa na viambatanisho hivyo uhalali wake haukuweza kupatikana.
- c) Ardhi na nyumba hazikutenganishwa katika taarifa za fedha kama inavyotakiwa na kifungu namba 74 cha viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslim (IPSAS Accrual), hivyo thamani kamili ya mali za kudumu iliyoripotiwa imejumuishwa kiasi cha uchakavu wa ardhi.

#### **7. Chama cha Alliance For Tanzania Democratic Change (ADC)**

- a) ADC haitunzi vitabu sahihi vya uhasibu ambavyo ni: kitabu cha fedha taslim, leja na kitabu cha mali za kudumu ili kusaidia katika uandaaji wa taarifa za fedha hivyo kukwamisha hatua za ukaguzi.
- b) Menejimenti haikuzingatia na kuonyesha mfumo iliyotumika katika uandaaji wa taarifa za fedha.
- c) Taarifa ya mapato na matumizi tu ndo iliyoandaliwa kinyume na matakwa ya viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma visivyo vya misingi ya taslim (IPSAS Accrual) ambavyo Menijimenti ilitakiwa kuvitumia.
- d) Hati za malipo kiasi cha Shilingi 31,320,000 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi hivyo imekwamisha taratibu za ukaguzi katika kuhakikisha uhalali wake.

**Kiambatisho Na. 3.1: Ufuartiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita katika Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa CAG**

Na	Mapendekezo ya CAG	Majibu ya PMG	Maoni ya Ukaguzi kwa Majibu ya PMG
<b>2006/2007</b>			
1	<b>Mapungufu katika usimamizi wa dhamana za serikali</b>  Wizara inashauriwa kupitia Sheria na Kanuni kwa kufanya marekebisho kwenye sheria ya dhamana na Kanuni zake ili kuendana na hali ya sasa	Marekebisho yamefanyika kwenye Sera ya madeni na Mikopo ya Serikali na Sheria ya dhamana na mikopo Na. 30 ya 1974. Marekebisho hayo yataapelekwa bungeni kwa uidhinishaji hivi karibuni. Mkakati wa madai umerekebishiwa	<b>Iko katika utekelezaji</b>  Marekebisho ya sheria ya mikopo ya Serikali, dhamana na ruzuku Na.3 ya mwaka 1974 (iliyorekebishiwa 2004) na mapitio ya Mkakati wa Deni la Taifa (NDS) yanashubiriwa
2	<b>Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo hazijarudishwa Serikalini</b>  Tunaendelea kusisitiza kwamba Wizara ifanye juhudhi ikishirikiana na mkusanyaji wa madeni ya Serikali kusisitiza makusanyo ya kiasi kilichobaki cha JPY 16,699,499,858 na kuwasilisha maendeleo yaliyofikiwa kwa ajili ya ukaguzi.	Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali iliizungu Serikali kutochukua hatua yoyote mpaka pale maelekezo juu ya suala hili yatakapo tolewa.	<b>Haijatekelezwa</b>
<b>2008/2009</b>			
3	Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa	Makubaliano hayo yaliyofikiwa baina ya	<b>Iko katika utekelezaji</b>

	<b>na serikali kama dhamana</b>  Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilisha makubaliano hayo yaliyofikiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Makampuni hayo ya maua, ratiba ya ulipaji mikopo pamoja na vielelezo vingine vinavyoonyesha kuanza kulipwa kwa mkopo.	Serikali na Makampuni ya maua pamoja na vielelezo vingine vya msingi vitawasilishwa ofisi ya ukaguzi kwa ajili ya uhakiki.	
<b>2011/2012</b>			
4	<b>Deni la Shirika la ndege (ATCL)</b>  Ninapendekeza hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya waliohusika katika kuingiza serikali katika biashara zisizozaa matunda, na ambazo zimesababisha serikali kudaiwa limbikizo la deni la dola za Marekani 41,466,177.16 kuanzia 26/10/2012; na  Kuanzia tarehe 26/10/2012 deni limekuwa likiongezeka mpaka kufikia dola za Marekani 41,466,177.16 kutoka dola 39,000,000 .Serikali inapaswa kujadili hili deni na kampuni ya Wallis kama kuna uwezekano wa kulifuta kwa vigezo kwamba serikali haikufaidika na biashara hiyo.	Suala hili liko katika uchunguzi na TAKUKURU. Uongozi utawasiliana na Wakaguzi juu ya hatua zilizo chukuliwa baada ya TAKUKURU kukamilisha uchunguzi. Taarifa inayoonesha gharama za uendeshaji wakati ndege inafanya kazi na baada ya kutofanya kazi iko tayari na itawasilishwa kwa Wakaguzi kwa ajili ya uhakiki. Andiko linaandalowiwa kwa ajili ya kupitisha na Baraza la Mawaziri. Kwa sasa kamati ndogo ya IMTC inajadiliana na wadai wa ATCL ili wapunguze deni kabla ya kuomba kibali cha baraza la Mawaziri	<b>Iko katika utekelezaji</b>  Suala hili bado liko katika uchunguzi na TAKUKURU. Hata hivyo tunasisitiza kuwa Mlipaji mkuu wa Serikali afanye majadiliano na kampuni ya kibashara ya Wallis juu ya suala hili
<b>2012/2013</b>			
5	<b>Kutofanyiwa kazi kwa changamoto ya upungufu wa nguvu kazi katika Wizara na</b>	Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Managementi ya Utumishi wa Umma ilitoa miongozo kwa	<b>Iko katika utekelezaji</b>  Utekelezaji hauko katika

	<p><b>Sekretarieti za Mikoa</b></p> <p>Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa wa wafanyakazi ikilinganishwa na ikama ya watumishi katika taasisi. Kwa hiyo, ninapendekeza:</p> <p>Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM) ipitie upya ikama za Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa na kuja na mapendekezo halisi ya idadi ya watumishi wanaohitajika.</p> <p>Maafisa Masuhuli wa Wizara, Idara za Serikali na Tawala za Mikoa wanapaswa kuhakikisha kwamba wana idadi ya kutosha ya watumishi wenye sifa stahiki. Uhaba wa watumishi unapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM).</p>	<p>waajiri juu ya mishahara ya Watumishi kwa mwaka wa fedha 2014/15 kwa kuendelea kuomba nguvukazi kulingana na mahitaji. Kwa kipindi cha kati year wa fedha 2008/09 na 2013/15 nafasi mpya 373,280 zilitolewa kwa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na halmashauri .</p>	<p>kiwango kinachotakiwa</p>
6	<p><b>Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa</b></p> <p>Ili kuepuka upotevu kama huu katika siku zijazo, Maafisa Masuhuli katika Wizara, Idara na Mikoa husika wanapaswa kuangalia taarifa za mishahara ya watumishi wao mara kwa mara na kuthibitisha uhalali wa watumishi wote kabla ya malipo. Mawasiliano pia lazima yaimarishwe ili kuhakikisha kwamba</p>	<p>Serikali imanzishwa Mfumo wa kusimamia Taarifa za Watumishi .Hii imewezesha jumla ya wafanyakazi 61,136 kufutwa kutoka kwenye orodha ya mishahara kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kifo na kustaafu,</p>	<p><b>Iko katika utekelezaji</b></p> <p>Kazi ya kuondoa watumishi hewa linapaswa kuwa endelevu</p>

	<p>majina ya wastaafu, watoro/walioacha kazi au walioachishwa kazi yanafutwa katika taarifa za wafanyakazi mara moja.</p> <p>Mbali na hayo, Maafisa Masuhuli wanatakiwa kuhakikisha mishahara isiyolipwa kwa watumishi ambao muda wao wa utumishi umekoma kwa sababu moja au nyingine inarudishwa Hazina kwa wakati kulingana na maagizo.</p> <p>Zaidi ya hayo, Maafisa Masuhuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa kutunza taarifa za watumishi (HCMIS-LAWSON) unafanya kazi na unatumika kikamilifu ili kupata thamani ya fedha tarajiwa.</p>		
7	<p><b>Utendaji katika Balozi</b></p> <p>Balozi husika zikishirikiana na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa (MFAIC) zinatakiwa kusitisha malipo ya posho kwa maafisa wastaafu na kufanya utaratibu wa kuwarudisha nyumbani haraka pindi utumishi wao unapokoma. Napendekeza mamlaka husika iangalie ni jinsi gani zitakavyoweza kurudisha fedha zilizolipwa kwa maafisa wasiostahili wa Balozi.</p> <p>Menejimenti ya Balozi iwasiliane na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa</p>	<p>Uongozi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje inatathmini uwezekano wa kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kufanya diplomasia ya kiuchumi na kukuza kivutio cha utalii ambayo itategemea upatikanaji wa rasilimali</p>	<p>Iko katika utekelezaji</p>

	<p>Kimataifa kwa ajili ya kuwarejesha majumbani watumishi waliomaliza utumishi wao ambao bado wanaendelea kuishi ubalozini na wale ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu wabadilishwe. Hii itakuwa chachu katika utoaji wa huduma kwa balozi zetu.</p> <p>Menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ione uwezekano wa kuanzisha mfuko katika bajeti yake kwa ajili ya kufanya shughuli za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio nya utalii, kwa kuzingatia kwamba hii ni kazi muhimu kwa uchumi wa nchi.</p>		
8	<p><b>Uendeshaji wa Hospitali Teule na Hospitali za Rufaa</b></p> <p>Wizara ya Afya inapaswa kuhakikisha kuwa fedha zote zinapohamishwa kwenda hospitali mbalimbali zinaambatana na mchanganuo wa matumizi yake badala ya utaratibu wa sasa usioainisha malengo ya fedha hizo kama ilivyodhahirika wakati wa ukaguzi.</p> <p>Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Hazina ni muhimu waboreshe mawasiliano na menejimenti za Hospitali husika kuhakikisha kuwa watumishi hewa wanafutwa kwa wakati katika mfumo wa</p>	<p>Wizara imewasiliana na hospitali zote teule nchini kwa barua yenye kumbukumbu Na. HC.209/320/01 ya tarehe 30 Oktoba, 2013 na kuwataka kurejesha Wizara ya fedha mishahara yote haikustaili kulipwa.</p>	<p><b>Iko katika utekelezaji</b></p> <p>Ushahidi wa mishahara iliyorejeshwa kutoka hospital teule na hospitali za rufaa unapaswa kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki</p>

	<p>ajira serikalini</p> <p>Nasisitiza Hospitali teule zizingatie makubaliano ya mkataba kati yao na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii</p> <p>Ninapendekeza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na menejimenti za Hospitali husika ihakikishe ya kwamba, wanafungua akaunti ya benki inayojitegemea mahususi kwa ajili ya fedha za ruzuku za Serikali badala ya hali ya sasa ya kuchanganya fedha hizi za Serikali na fedha za matumizi mengine ya hospitali. Aidha, Menejimenti za hospitali zinapaswa kuwajibika kutoa taarifa za mara kwa mara za matumizi ya fedha hizo kwa Wizara husika.</p>		
9	<p><b>Ununuzi wa Kivuko cha Misungwi</b></p> <p>Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wa umma walishindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi. Na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mzabuni M/S Sinnautic international ambaye alishindwa kutekeleza kazi zote za kuleta vipuri vya thamani ya Euro 41,140 za kivuko cha Misungwi kwa mujibu wa mkataba.</p>	<p>Hatua zimeshachuliwa dhidi ya maafisa wa umma ambao walishindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi,</p> <p>Wizara ikishirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaangalia utaratibu wa kuchukua hatua zaidi za kisheria dhidi ya Mkandarasi</p>	<p><b>Iko katika utekelezaji</b></p> <p>Vipuri muhimu kwa ajili ya kivuko bado havijapokelewa. Taratibu za kisheria zinapaswa kufuatwa</p>

10	<p><b>Ulipaji wa kodi ya kupanga ofisi Sh. 7,895,872,337</b></p> <p>Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, nyumba na maendeleo ya makazikwa kushirikiana na Wakala wa majengo Tanzania (TBA) watafute maeneo ambayo Serikali inaweza kujenga ofisi za wizara, idara na wakala wake.</p> <p>Serikali ifanye majadiliano na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili waweze kupata mkopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali.</p> <p>Serikali pia ifanye mazungumzo na washirika wa maendeleo kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Dunia ili waweze kupata mikopo/misaada kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa ofisi hizo.</p> <p>Nia ya Serikali ya ujenzi wa majengo inapaswa pia kuelekezwa kwenye Balozi Zetu kwani ni gharama sana kupangisha ofisi na nyumba za wafanyakazi</p>	<p>Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mamlaka ya Kustawisha Mji mkuu wameanza kutenga maeneo kwa ujenzi wa majengo ya Serikali</p>	<b>Iko katika utekelezaji</b>
11	<p><b>Changamoto zinazokabili huduma ya magereza Tanzania</b></p> <p>Mahakama ya Tanzania iharakishe kutoa maamuzi juu ya kesi zilizopo. Kuna idadi kubwa ya mahabusu katika magereza ambao</p>	<p>Serikali kupitia Sheria ya Huduma za Jamii, Sheria ya kifungo mbadala (Parole act) na Magereza (Kinga ya ziada ya kifungo cha nje) Kanuni na Sheria zote hizi zinafanya kazi lakini idadi ya wafungwa ambao wanastahili ni wachache sana kutokana na</p>	<b>Iko katika utekelezaji</b>

<p>wanasubiri kesi zao kusikilizwa na haki kutolewa na mahakama. Kukamilisha kesi zinazowakabili mahabusu kutasaidia kupunguza idadi ya mahabusu katika magereza,</p> <p>Serikali inaweza kuchagua kutumia njia nyingine ya kuwaadhibu wafungwa baada ya kupatikana na hatia. Serikali inaweza kuchagua kutumia njia mbadala kama wafungwa kutumikia kifungo cha nje cha kuanzia mwaka mmoja mpaka miwili chini ya uangalizi wa mkuu wa wilaya au mkoa huku akijushughulisha na shughuli za jamii kama usafi maofisini bila malipo (<i>extra Mural labour</i>), kifungo cha nje chini ya uangalizi cha miaka minne na kuendelea kutokana na makosa madogo madogo kwa wafungwa ambao tayari wametumikia theluthi moja (1/3) ya kifungo chao gerezani huku wakishughulika na huduma za jamii bila malipo (Parole). Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi ya mahabusu na wafungwa katika magereza,</p> <p>Kwa ajili ya wahalifu wadogo na wanaokiuka sheria ni bora kulipa faini, na kama wao wakishindwa kulipa faini, wanapaswa kupelekwa kwa uongozi wa miji yao, au wilaya na kupewa kazi za jamii (<i>communal</i></p>	<p>masharti husika. Jitihada zinafanyika ili sheria zilizotajwa kufanyiwa marekebisho ili wafungwa wengi waweze kustahili. Hadi Aprili, 2015 jumla ya wafungwa 4,402 waliandikishwa chini ya kifungo mbadala (Parole)</p> <p>Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge (PAC) wataalikwa kutembelea Magereza na kuona hali halisi ili waweze kuendelea kutoa ushauri juu ya uboreshaji wa Idara ya Magereza.</p>	
---	--	--

<p><i>based labour),</i></p> <p>Kuwahudumia mahabusu na wafungwa kunasababisha gharama kubwa kwa Serikali. Kuwalisha, kuwapa mavazi na matibabu ni ghali. Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kuboresha shughuli zao za uzalishaji kama useremala, shughuli za kilimo, ushonaji, ujenzi wa nyumba na mafundi mitambo na magari. Baada ya hapo, watafute soko la bidhaa zao. Hii itawawezesha kuwa na uwezo wa kujilisha na kujinunulia mavazi wenyewe,</p> <p>Idara ya huduma ya Magereza inahamasishwa kuandika juu ya mapendekezo kadhaa ya maendeleo na kutafuta wahisani mbalimbali kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), nk ambao watatoa fedha kwa ajiri ya kupanua na kuboresha magereza,</p> <p>Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kutoa wito kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Serikali Kuu (PAC) na viongozi wengine wa Serikali kutembelea magereza na kuona hali halisi katika magereza. Hii itawasaidia kufanya maamuzi sahihi juu</p>		
---	--	--

	ya mgao wa rasilimali.		
<b>2013/2014</b>			
12	<b>Kuchelewa katika kushughulikia rufaa za kodi</b>  Naishauri Serikali kuongeza kasi ya kushughulikia hizo rufaa kwa kuzingatia umuhimu wake katika uchumi	TRA imefanikiwa kushughulikia kesi za kodi kupitia Bodi ya Rufaa ya Mapato, Baraza laUshururishi wa Mapato ya Kodi na Mahakama ya Rufaa  .Aprili 2016, Bodi ya Rufaa ya Mapato ilikuwa na kesi 117 zenyet thamani ya shilingi bilioni 116 . Katika kipindi cha Aprili na Septemba 2016 jumla ya kesi 63 zenyet thamani ya shilingi bilioni 66 zilitolea maamuzi.. TRA ilishinda kesi 50 zenyet thamani ya shilingi bilioni 58.TRA Ilisindwa Kesi 13 zenyet thamani ya shilingi bilioni 8 (sawa na 12.5%). Kwa hiyo bado kuna kesi 54 zinazosubilia maamuzi ya mahakama	<b>Iko katika utekelezaji</b>  Matokeo ya kesi ambazo hazijafanyiwa maamuzi hayawezu kujulikana kwa sasa. Hivyo tutafanya Ufutiliaji katika kaguzi zijazo
13	<b>Ukosefu wa Uwiano Sawia wa Ukomo katika Dhamana za Serikali</b>  Napenda kuishauri serikali kuongeza ushindani katika soko la ndani la dhamana za serikali na hivyo kuongeza ushawishi wa ununuzi wa dhamana za muda mrefu.	Mara kwa mara Serikali imekuwa ikichukua hatua kuboresha taratibu za ushiriki wa masoko ya dhamana za Serikali kwa kuwashawishi wawekezaji katika dhamana za Serikali za muda mrefu pamoja na kutoa misamaha ya kodi kwenye riba kutoka miaka miwili ya kuiva kwa dhamana za Serikali	<b>Iko katika utekelezaji</b>

14	<b>Usimamizi Usiotosheleza Kwenye Uwekezaji wa Serikali na Vipaumbele Vyake</b> Naishauri serikali kuandaa Mfuko wa Uwekezaji utakaowezeshwa kutoka katika makampuni amabyo inamiliki hisa chache kwenye gawio na mapato mbalimbali ili kunusuru hisa za serikali, na pia kuiwezesha serikali kuwekeza katika sekta zingine ambazo itaona zinahitaji ushiriki wake. Mwisho, naishauri serikali kuitia mara kwa mara ufanisi wa uwekezaji wake na malengo k	Utungaji wa sheria mpya ya Msajili wa Hazina uko katika hatua za mwisho. Kwa sasa andiko la Baraza la Mawaziri linapendekeza kutunga sheria ya Msajili wa Hazina linasubiri kujadiliwa na Mkutano wa Baraza la Mawaziri. Andiko limejumuisha mapendekezo yote ya IMTC	Iko katika utekelezaji
15	<b>Mapungufu katika Usimamizi wa mali kwani kasi ya kutadhimini mali, kuandaa rejista ya mali na kuweka alama za utambulisho unaonekana kukwama</b>  Mlipaji Mkuu wa Serikali aharakishe mchakato huo na ahakikishe changamoto zote zilizobainika zinashughulikiwa kabla ya mwaka 2016/2017 ambapo serikali inatakiwa iwe inatekeleza IPSAS kikamilifu,  Mlipaji Mkuu wa Serikali atoe mwongozo wa namna ya kuweka kumbukumbu katika rejista ya mali za kudumu, msisitizo uwe katika jinsi ya kutathimini mali, kiwango cha uchakavu, kuweka alama za utambulisho na uboreshaji wa taarifa mara kwa mara katika	Mshauri mwelekezi aliyeazimwa na Wizara ya Fedha kuitia Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazikwa ajili ya kuhakikisha ardhi yote inayomilikiwa na Serikali inapewa nyaraka za usimamizi wa Ardhi na si lazima hati miliki	Iko katika utekelezaji

	<p>rejista ya mali za kudumu,</p> <p>Kuzingatia matumizi ya mifumo ya kompyuta ambayo inaendana na kuingiliana na mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) kwa ajili ya kusimamia mali za serikali ili kuepuka uandaaji wa taarifa nyingi na viharishii vinavyotokana na kuhamisha taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mwengine,</p> <p>Naishauri Serikali ihakikishe taarifa za kihasibu za Maafisa Masuhuli zinatenganisha ardhi na majengo ili kupata thamani ya ardhi na kutoza uchakavu kwenye mali zinazochakaa. Pia, nashauri serikali ihakikishe Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa zinapata hati miliki ili kulinda mali zake,</p> <p>Nashauri serikali ichukue hatua stahiki kuweza kufuta ambazo zimechakaa na hazitengenezeki kwa mujibu wa kanuni za fedha za mwaka 2001.</p>		
16	<p><b>Madeni yanayotegemea Matukio (Contingent Liabilities)</b></p> <p>Maafisa Nasuuli wa kila Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa Kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wahakikishe ufuatiliaji wa karibu</p>	<p>Serikali iko hatua za mwisho za kutoa muongozo kwa Maafisa Masuhuli wote juu ya taratibu za kushughulikia kesi za kisheria ili kuwasaidia kuzifanyia kazi kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali , hasa kutoa taarifa sahihi kwa wakati ili kumsaidia Mwanasheria Mkuu wa</p>	<p><b>Iko katika utekelezaji</b></p>

	kuakikisha kesi ambazo hazijaamuliwa zinashughulikiwa mapema ili kuiondloea au kupunguza gharama zinazoweza kuotkana na kushindwa kesi	Serikali kuandaa mashtaka au kuandaa taarifa ya upande wa utetezi kadri ya kesi itakavyokuwa na kuanza mashhtaka katika mahakama husika	
17	<p><b>Ukaguzi maalum katika Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha Shilingi 252,975,000,000 za ujenzi wa barabara kutumika kulipia madeni nje ya utaratibu</b></p> <p>Bajeti inapaswa iandaliwe kwa kuzingatia mahitaji halisi.</p> <p>Serikali isaini mikataba mipy ya ujenzi wa barabara baada ya kupima uwezo ilionao wa kulipa madeni ya wakandarasi waliopo ili kuzuia kukua kwa madeni katika siku zijazo</p>	<p>Serikali inakubali mapendekezo ya Wakaguzi juu ya kuhakikisha bajeti inaandaliwa kwa kuangalia shughuli halisi zitakazotekelzwa.</p> <p>Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi itaandaa bajeti na kuanza kujenga barabara mpya kulingana na uwezo wa kifedha ili kuepusha ukuaji wa deni kwa siku za usoni</p>	<b>Iko katika utekelezaji</b>
<b>2014/2015</b>			
18	<p><b>Mapato yaliyokusanya chini ya kiwango Shilingi 1,091.27</b></p> <p>Serikali inaombwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani. Jitihada zaidi zinahitajika kwa Serikali kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kuchukua hatua juu ya limbikizo la madeni ya kodi kwa kuweka riba na adhabu, kuimarisaukaguzi wa kodi na vikosi vya uhakiki vya Mamlaka ya Mapato na idara ya uchunguzi wa Kodi kupunguza kuongezek kwa ukwepaji na mazoea ya kukwepa kodi na</p>	<p>Serikali inatambua mapendekezo ya Mdibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Kupitia uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Serikali itaendelea kuanzisha hatua za kudhibiti ili kuboresha ukusanyaji wa mapato. hatua ni pamoja na ukusanyaji wa malimbikizo ya kodi kwa nguvu, kusululisha mapingamizi ya kodi, na ufuatiliaji wa kesi za rufaa. Hatua nyingine zitajumuisha ukaguzi wa kodi na uchunguzi</p>	<b>Iko katika utekelezaji</b> Tutafanya tathimini ya utekelezaji katika kaguzi zinazofuata

	kuimarisha ukaguzi, udhibiti na mmbinu za usimmashineamizi wa mizigo na mafuta kutoka nje au ilio njiani ili kupata kaodi zote kulingana na sheria zilizopo, kuongeza wigo wa kodi, kuboresha utii na ukusanyaji wa kodi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali		
19	<p><b>Kushindwa kurejesha pesa za Mpango wa kubakiza makusanyo kiasi cha Shilingi bilioni 21.04</b></p> <p>Natoa wito kwa Wizara na Idara zilizo chini ya mpango wa kubakisha pesa kwa kukusanya mapato yasiyo ya kodi ili kufikia malengo yaliyowekwa, hii ni pamoja na kuwa na bajeti ya awali (zero budget) kwa ajili ya wale amba walikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni moja kwa mfano (Idara ya Magereza na Wizara ya Maendeleo ya Jamii chini ya CDTI).</p>	<p>Kutorejeshwa kwa shilingi bilioni 21.04 chini ya mpango wa kubakiza makusanyo ilitokana na ukweli kwamba mapato yaliyokusanya hayakutosheleza kulingana na vipaumbeli</p>	<p><b>Haijatekelezwa</b> Tutafanya tathimini katika Ugazi unaofuata</p>
20	<p><b>Kuandaa Hesabu za Majumuisho za Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa serikasli, Serikali za mitaa na Taasisi za Serikali zinazofanya biashara kwa Kutumia Mfumo Usiojiendesa</b></p> <p>Serikali inapaswa:</p> <p>Kuboresha mfumo wa Epicor unaojiendesa</p>	<p>Serikali inatambua ukweli kwamba maandalizi ya taarifa za fedha hayatokani na mfumo unojiendesa. Taarifa jumuifu za fedha za Serikali zimeandaliwa kwa kutumia TEHAMA (ICT) kwa njia excel na si kwa mfumo wa EPICOR amba ulijumuisha taasisi 553. Hata hivyo, uongozi unafanya mipango yote ili kuhakikisha kwamba</p>	<p><b>Iko katika utekelezaji</b> Tunatambua jitihada zilizofanya na Serikali. Hata wivyo mfumo unaoandaliwa unasubiliwa. Vilevile tunaishauri Serikali kuweka</p>

	<p>kujumuisha Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa na Taasisi zinazojiendesha kibiashara</p> <p>Kuungeza jitihada za kujumuisha Balozi za Tanzania katika mfumo wa ili kuungeza udhibiti wa bajeti na kuaminiwa kwa taarifa za fedha</p> <p>Kuoanisha mfumo wa kutunza taarifa(Database) wa Wizara,Idara ,Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa ili kuweza kuijendesha kutoa taarifa za fedha kutoka kwenye mfumo wa Epicor, na hatimaye, kuendeleza mfumo bora wa kujumuisha taarifa za fedha za Serikali kwa kutumia Epicor lakini mazingira ya utendaji yanasaababisha utenganisho wa mifumo ya kuhifadhi taarifa.</p>	<p>kuoanisha/kushirikiana kwa programu mbalimbali ya kutumiwa na taasisi hizi baada ya utafiti wa kina juu ya jinsi muungano unaweza kufikiwa kwa kuijendesha wenyewe. Hivi sasa, uongozi unendelea na mchakato wa kuanganisha balozi katika EPICOR kwa majoribio ya Balozi saba. Wakati huo huo, utafiti wa jinsi programu mbalimbali ya kutumiwa na Taasisi za serikali unavyoweza kuanganishwa.</p>	<p>ukomo wa mfumo unaosubiliwa</p>
21	<p><b>Kukosekana kwa vigezo vya uthaminishaji kwa ajili ya utoaji wa Pensheni za Serikali shilingi bilioni 597.4</b></p> <p>Serikali kuzingatia IPSAS 25 juu ya uhasibu wa maslai ya wafanyakazi kwa kufanya tathimini ili kujua kiasi cha madeni ya wastaifu na Watumushi wa kudumu wanaoidai Serikali.</p>	<p>Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kazi ya kutathimini PPesheni inafanyika.Kwa kufanya hivyo bajeti imetengwa katika mwaka wa fedha 2017/18</p>	<p><b>Iko katika utekelezaji</b></p> <p>Tutafanya tathimini ya utekelezaji wa wa pendekezo letu kwenye ukaguzi unaofuata</p>

22	<b>Usimamizi usiojitosheleza katika uwekezaji wa Serikali na maslahi yake</b>  Serikali kuanzisha mfuko uliotayari kusubiri uwekezaji kutoka kwenye mapato yaliyopokelewa kutoka kwenye gawio na mapato mengine ili kujenga mfuko wa uwekezaji wa mtaji ambao Serikali ina hisa ili kuwekeza tena au kushiriki katika kufungua njia nyingine za uwekezaji ambayo Serikali anataka kuwekeza. Hii inaweza kuhusisha serikali kuruhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kubakisha makusanyo yote kwa kipindi maalum (miaka minne hadi mitano)  Serikali kupitia, Wixara ya Fedha, ianzishe mpango wa kubakiza mapato kwa ajili ya Ofisi ya Msajiri wa Hazina ili kuanzisha mfuko wa uwekezaji uliopendekezwa. jMpango huu utasaidia pia kama kipimo cha ufanisi kwa Msajili wa Hazina ambacho kitawezesha Serikali kufanya tathimini uwezo wa Msajili wa Hazina kuhamasisha mapato kutoka kwenye mapato ya uwekezaji wake	Serikali kupitia Msajiri wa Hazina amependekeza uanzishwaji wa Mfuko wa Uwekezaji.lmependekezwa kuwa vyanzo vyta fedha vyta mfuko wa uwekezaji utokane na bajeti ya Serikali, Kubakiza fedha zilizokuswanya kutoka kwenye gawio na michango kutoka PSCS, Fedha za Wafadhili na vyanzo vingine.  Hatahivyo,kuanzisha kwa mfuko kutategemea kukamilika kwa sheria mpya ya Msajili wa Hazina.Kwasasa,Andiko la Balaza la Mawziri lilalopendekeza kutungwa kwa sheria ma Msajili wa Hazina linasubiliwa ili lijadiliwe na kaika mkutano wa Balaza la Mawaziri bada ya kutekelezamapendekezo ya IMTC	<b>Iko katika utekelezaji</b> Tutafanya tathimini ya utekelezaji wa mapendeleko yetu katika ukaguzi utakaofuata
23	<b>Usimamizi wa Pingamizi za kodi na kesi za pingamizi za kodi za muda mrefu ambazo hazijafanyiwa maamuzi na Mamlaka ya Mapato</b>  Usikilizaji wa rifaa za kodi unapaswa	Idara ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato inafanya kazi kwa ukaribu na mahakama ili kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi mbalimbali za Rufaa pamoa na  Tarehe 7/2/2017 siku ya Sheria, Rais wa	<b>Iko katika utekelezaji</b>

	<p>kuhakishwa na Bodi ya Rufaa, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa</p> <p>Kwa utatuzi ulioshindikana kwa muda mrefu, Napendekeza Serikari kuunda Tume huru ya Malalamiko ili kuharakisha kushughulikia rufaa</p> <p>Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania uimarishe ukaguzi na uchunguzi ili kupunguza migogoro ya kodi kati ya Mamlaka na Walipakodi.</p>	<p>Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, John Pombe Magufuli alimuagiza Jaji Mkuu, Othman Chande kuhakikisha usikilizaji wa kesi za kodi unaongezewa kasi.. Mahaakama ya Rufaa ya Tanzania imenza kusikiliza kesi ambazo hazijashughulikiwa.</p> <p>Kuanzisha Tume huru ya kushughulikia mlalamiko ni suala la sera litakaloshughulikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa maana hiyo TRA ina mradi wa majaribio katika Mkoa wa Manyara kwa kuanzisha mfumo wa utetezi wa Walipakodi (Taxpayer Advocacy System-TAS) kwa kusikiliza na kumshauri Kamishina Mkuu juu ya mapingamizi ya kodi ziliyotokea kwa Walipakodi wadogo na wakati ili kufapa sululisho la haraka la hiyo migogoro</p> <p>TRA ina taarifa za kila robo mwaka juu ya Kesi zilizoshughulikia na kutengeneza ripoti za kesi ambazo hazijashughulikiwa</p>	
24	<p><b>Kasoro zilizoonekana katika mapingamizi ya Kodi na Mifumo ya ushawishi ya ulipaji Kodi</b></p> <p>a) Kushughulikia maombi ya mapingamizi ya kodi kwa</p>	<p>Uongozi unachukua hatua stahiki za kuhakikisha maombi ya migogoro ya kodi yanashughulikiwa mapema na kujumuisha mapingamizi ya kodi ambayo muda wake wa kulipwa umefika lakini hayajalipwa Shilingi 580,718,607,384. Hizi ni pamoja na</p>	<b>Iko katika utekelezaji</b>

	<p>haraka ili kutatua hizo pingamizi. Hii inaweza kufanyika kwa kuongeza idadi wa Wafanyakazi hodari na wenyewe uzoefu na kuimarisha kitengo cha ufundi. Pia, kuimarisha mchakato wa kutathmini ili kupunguza idadi ya mapingamizi yaliyoweza kujitokeza</p> <p>b) Kuchunguza mahitaji ya sheria ya Kukusanya juu ya theludhi mona ya kodi iliyotathaminiwa au kiasi ambacho hakiko katika mgogoro kabla ya kupokea pingamizi la kodi na Kuokoa amana kutoka kodi iliyotathminiwa katika pingamizi</p>	<p>hatua za muda mfupi kwa kuongeza muda wa kufanya kazi na hatua za muda mrefu zinajumuisha kutafuta wafanyakazi wenye ujuzi ili kuimarisha timu ya kushughulikia pingamizi .</p>	
25	<p><b>Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizohifadhiwa katika maghala kabla ya kulipiwa ushuru wa forodha</b></p> <p>Serikali ichukue hatua za haraka kuuza bidhaa zilizokaa kwenye maghala kwa muda mrefu kwa njia ya mnada ili kuepusha kushuka kwa thamani na kuharibika kwa bidhaa zilizokaa muda mrefu na kuisababishia Serikali hasara ya mapato</p> <p>Serikali iongeze usimamizi na mbinu za</p>	<p>Kati ya Kiasi kilichohojiwa, shilingi 77,872,535,125 (71%) zilihusiana na bidhaa zilizoingizwa kwenye Ukanda wa kuuza Bidhaa nje (Export Processing Zone), Kutengeneza bidhaa chini ya dhamana, maduka yaliyosamehewa ushuru, maghala yaliyo ya ushuru wa kodi na wauaji wa magari mapya ambayo hayahusiki chini ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya</p>	<b>Iko katika utekelezaji</b>

